شرح ثلاثة الأصول

# *Sharh Thalaathat-il-Usuwl*

*[Ufafanuzi wa misingi mitatu]*

الامام محمد بن صالح العثيمين

**Imaam Muhammad bin Swaalih al-´Uthaymiyn**

*Mfasiri:*

**Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush**

***www.firqatunnajia.com***

01- Maana ya Basmalah ... 4
02- Tambua – Allaah Akurehemu ... 6
03- Ujuzi juu ya Allaah, Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) na Uislamu ... 8
04- Matendo kwa elimu ... 12
05- Kulingania kwa elimu ... 13
06- Subira kwa maudhi ... 16
07- Subira kwa maudhi II ... 19
08- Elimu kabla ya kauli na matendo ... 21
09 – Dalili ya kwamba Allaah ndiye Ametuumba ... 23
10- Dalili ya kwamba Allaah ndio Ameturuzuku ... 26
11- Dalili ya kwamba Allaah Hakutuacha bure pasina malengo yoyote ... 28
12- Dalili kuwa Allaah Ametutumia Mtume ... 29
13- Dalili ya kuwa mwenye kumtii Mtume (صلى الله عليه وسلم) ataingia Peponi ... 31
14- Dalili ya kuwa mwenye kumuasi Mtume (صلى الله عليه وسلم) ataingia Motoni ... 33
15- Allaah Haridhii kushirikishwa na yeyote ... 35
16- Haijuzu kufanya urafiki na wale wanaompinga Allaah na Mtume Wake ... 37
17- Haniyfiyyah ndio Dini ya Ibraahiym (صلى الله عليه وسلم) ... 40
18- Lengo la kuumbwa ... 42
19- Aina mbili za ´Ibaadah ... 43
20- Tawhiyd ndio jambo kubwa Aliloamrisha Allaah ... 44
21- Shirki ndio jambo kubwa Alilokataza Allaah ... 47
22- Misingi mitatu – Ujuzi wa kumjua Mola ... 50
23- Ujuzi wa kuijua Dini ... 53
24- Ujuzi wa kumjua Mtume ... 54
25- Ni nani Mola Wako ... 55
26- Dalili ya kwamba Allaah ndio Mola wa walimwengu ... 57
27- Kila kisichokuwa Allaah kimeumbwa ... 58
28- Vipi umemjua Mola Wako? ... 59
29- Alama za Allaah ... 60
30- Dalili ya alama za Allaah ... 62
31- Mola ndiye Mwabudiwa ... 64
32- Muumbaji wa vitu hivi ndiye Mwenye kustahiki kuabudiwa ... 67
33- Mfano wa aina za ´Ibaadah ambazo Allaah Ameamrisha ... 68
34- Dalili ya ´Ibaadah ... 70
35- Dalili ya khofu ... 72
36- Dalili ya matarajio ... 74
37- Dalili ya utegemeaji ... 75
38- Dalili ya shauku, woga na unyenyekeaji ... 78
39- Dalili ya tisho ... 80
40- Dalili ya kurejea ... 81
41- Dalili ya kutaka msaada ... 83
42- Dalili ya kutaka kinga ... 86
43- Dalili ya kutaka kuokolewa ... 90
44- Dalili ya kuchinja ... 92
45- Dalili ya nadhiri ... 94
46- Msingi wa pili ni kuijua Dini ya Kiislamu ... 96

47- Daraja za Dini ni: Uislamu, Imani na Ihsaan ........ 98
48- Dalili ya Shahaadah ........ 99
49- Maana ya Shahaadah ........ 101
50- Tafsiri inayoweka wazi maana ya Shahaadah ........ 103
51- Tafsiri inayoweka wazi maana ya Shahaadah II ........ 105
52- Dalili ya kushuhudia kuwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ni Mtume wa Allaah ........ 106
53- Maana ya kwamba Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ni Mtume wa Allaah ........ 108
54- Dalili ya Swalah na Zakaah na na tafsiri ya Tawhiyd ........ 110
55- Dalili ya Swawm ........ 112
56- Dalili ya Hajj ........ 114
57- Daraja za Imani ........ 116
58- Kumuamini Allaah ........ 118
59- Kuamini Malaika ........ 131
60- Kuamini Vitabu ........ 136
61- Kuamini Mitume ........ 138
62- Kuamini siku ya mwisho ........ 145
63- Kuamini Qadar ........ 160
64- Dalili ya nguzo sita za Imani ........ 169
65- Ihsaan na nguzo yake ........ 170
66- Dalili ya nguzo za Uislamu, Imani na Ihsaan ........ 173
67- Msingi wa tatu ni kumjua Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ........ 175
68- Mtume (صلى الله عليه وسلم) Ametumwa ili kutahadharisha shirki na kulingania katika Tawhiyd ........ 178
69- Safari ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kupandishwa mbinguni ........ 179
70- Hijrah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kutoka Makkah na kwenda al-Madiynah ........ 182
71- Hijrah ni kutoka katika mji wa kikafiri na kwenda wa Kiislamu ........ 185
72- Uwajibu wa Hijrah ........ 186
73- Hijrah itaendelea kuwepo mpaka siku ya Qiyaamah ........ 188
74- Hukumu ya kusafiri kwenda katika miji ya kikafiri ........ 189
75- Shari´ah zilizowekwa al-Madiynah ........ 196
76- Kifo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) ........ 198
77- Viumbe wote ni wajibu kumfuata Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ........ 200
78- Allaah Ameikamilisha Dini kupitia Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ........ 201
79- Dalili ya kufa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ........ 203
80- Baada ya kufufuliwa watu watahesabiwa na kulipwa ........ 205
81- Yule mwenye kukanusha kufufuliwa anakufuru ........ 207
82- Mitume wametumwa wakiwa ni wenye kutoa bishara njema na wenye kuonya ........ 213
83- Kazi kubwa ya Mitume ........ 215
84- Mitume wote wametumwa kwa kazi moja ........ 217
85- Maana ya Twaaghuut ........ 218
86- Twawaaghiyt wakubwa watano ........ 221
87- Ni wajibu kuhukumu kwa Aliyoteremsha Allaah ........ 229
88- Kichwa cha mambo ni Uislamu ........ 231
89- Mwisho wa kitabu ........ 232

# 01- Maana ya Basmalah

*Kwa Jina la Allaah, Mwingi wa rehma, Mwenye kurehemu*

**Allaah –** Ni Jina la Allaah (Jalla wa ´Alaa) Pekee ambalo linafuatiwa na Majina mengine yote. Allaah (Ta´ala) Amesema:

الر ۚ كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِ رَبِّهِمْ إِلَىٰ صِرَاطِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ اللَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَوَيْلٌ لِّلْكَافِرِينَ مِنْ عَذَابٍ شَدِيدٍ

**“*Alif Laam Raa.* Kitabu Tumekiteremsha kwako ili uwatoe watu katika viza kuwaingiza katika Nuru kwa Idhini ya Mola wao, waelekee katika njia ya *Al-‘Aziyzil-Hamiyd* (Mwenye enzi ya nguvuAsiyeshindika daima - Mwenye kustahiki kuhimidiwa kwa yote daima). Allaah Ambaye ni Vyake Pekee (vyote) viliyomo katika mbingu na katika ardhi. Na ole kwa makafiri kutokana na adhabu kali.” (Ibraahiym 14 : 01-02)**

Hatusemi kuwa neno la kitukufu ”Allaah” ni sifa, isipokuwa hali ya kubainisha. Neno la kitukufu linakuwa na maana ya sifa yenye kufuata kwa kile kinachosifiwa.

**Jina –** Mwandishi wa kitabu (Rahimahu Allaah) ameanza kitabu chake kwa Jina la Allaah kwa kuiga Kitabu cha Allaah (´Azza wa Jalla) kilichoanzwa kwa Basmalah. Kadhalika amefanya hivo kwa kufuata Hadiyth:

**”Kila jambo lililo na umuhimu lisiloanzwa kwa Jina la Allaah limeondolewa baraka.”**

Vilevile amemuiga Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambaye alikuwa siku zote akianza barua zake kwa Jina la Allaah.

**Mwingi wa rehma [ar-Rahmaan] –** Mwingi wa rehma ni katika Majina maalum ya Allaah (´Azza wa Jalla) na hivyo haliitwi mtu mwingine. Mwingi wa rehma maana yake ni Yule Mwenye kusifika na rehma kunjufu.

**Mwenye kurehemu [ar-Rahiym] –** Ni jina ambalo huitwa Allaah (´Azza wa Jalla) na wengineo. Maana yake ni mwenye rehma zenye kuendelea. Pale ambapo Mwingi wa rehma, ambaye rehma zake ni kunjufu, na Mwenye kurehemu, ambaye ni mwenye rehma zenye kuendelea, yanakuwa pamoja, maana yake inakuwa "Mwingi wa rehma anayemfikishia rehma Zake kwa yule anayemtaka katika waja Wake". Allaah (Ta´ala) Amesema:

يُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ وَيَرْحَمُ مَن يَشَاءُ ۖ وَإِلَيْهِ تُقْلَبُونَ

**"Anamuadhibu Amtakaye na Anamrehemu Amtakaye; na Kwake mtarudishwa." (al-´Ankabuut 29 : 21)**

# 02- Tambua – Allaah Akurehemu

*Tambua – Allaah Akurehemu – ya kwamba ni wajibu juu yetu kujifunza masuala mane:*

**Ujuzi –** Kuwa na utambuzi wa kitu kama jinsi kilivyo kikweli. Utambuzi huu una daraja sita:

**Ya kwanza:** Ujuzi, wa kukitambua kitu kama jinsi kilivyo kikweli kwa njia ya kihakika.

**Ya pili:** Ujinga mwepesi, wa kutokuwa na utambuzi kabisa.

**Ya tatu:** Ujinga wa kutokujitambua, nao ni kule kukitambua kitu kwa njia inayoenda kinyume na uhakika wake.

**Ya nne:** Ufikiriaji, ambao ni wa kukitambua kitu wakati kinyume chake pengine ndio ikawa sahihi zaidi.

**Ya tano:** Mashaka, ambayo ni kule kukitambua kitu pamoja na uwezekano wa kuwepo kitu kingine kinachoweza kuwa kama kile.

**Ya sita:** Dhana, ambayo ni kule kukitambua kitu na wakati huo huo kuna uwezekano kikawa ni sahihi zaidi kuliko kile kinachoenda kinyume.

Ujuzi umegawanyika sehemu mbili; ya kidharurah na kinadhari.

Kuhusu ujuzi wa kidharurah, ni ule ambao kuyatambua mambo kidharurah ni jambo la wajibu kwa njia ya kwamba mtu hahitajii kufanya utafiti wala dalili. Mfano wa hilo ni mtu kujua kuwa moto unachoma.

Kuhusiana na ujuzi wa aina ya kinadhari, ni ule ambao unahitajia nadhariya na dalili. Katika mfano wa ujuzi huu ni kama mtu kujua kwamba ni wajibu kutia nia katika Wudhuu.

**Allaah Akurehemu –** Allaah Akumiminie rehema Zake ambazo unafikia malengo yako na kukuokoa na yawezayo kukudhuru. Maana ya hilo ni Allaah Akusamehe yaliyopita katika madhambi yako na Akuwafikishe na Kukuhifadhi na yaliyo huko mbeleni. Maana hii ni pale endapo rehema

inapotajwa peke yake. Ama pale ambapo inapoambatanishwa pamoja na msamaha, msamaha unakuwa kwa yale madhambi yaliyopita, wakati rehema na Tawfiyq inakuwa katika kheri na kusalimika na madhambi siku za mbeleni.

Kitendo cha mwandishi (Rahimahu Allaah) kinatolea dalili kuonesha jinsi anavyomtilia umuhimu, kumuonea huruma yule anayemzungumzisha na kumtakia kheri zote.

Masuala haya ambayo mwandishi (Rahimahu Allaah) ameyataja yanaizunguka Dini yote. Kwa hiyo, yanatakiwa kutiliwa umuhimu mkubwa kutokana na manufaa yake makubwa.

# 03- Ujuzi juu ya Allaah, Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) na Uislamu

*Suala la kwanza: Ujuzi, nao ni ujuzi wa kumjua Allaah, ujuzi wa kumjua Mtume Wake na ujuzi wa kuijua Dini ya Kiislamu kwa dalili.*

**Ujuzi –** Nao ni kumjua Allaah (´Azza wa Jalla) kwa moyo kwa njia ambayo italazimisha mtu kuyakubali yale Aliyoweka katika Shari´ah, kujisalimisha nayo na kuhukumu kwa Shari´ah Yake ambayo imekuja na Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mja huwa ni mwenye kumjua Mola Wake kwa kutazama alama za Kishari´ah katika Kitabu cha Allaah (´Azza wa Jalla) na Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kama jinsi anavyotazama alama za kilimwengu ambazo ni viumbe. Hakika ya mwanaadamu kila pale atapotazama ishara hizi, basi ujuzi wake kuhusu Mola Wake huzidi na Yule anayemwabudu. Allaah (´Azza wa Jalla) Amesema:

وَفِي الْأَرْضِ آيَاتٌ لِّلْمُوقِنِينَ وَفِي أَنفُسِكُمْ ۚ أَفَلَا تُبْصِرُونَ

**"Na katika ardhi (kuna) alama kwa wenye yakini. Na katika nafsi zenu (kuna alama) je hamuoni?" (adh-Dhaariyaat 51 : 20-21)**

**Ujuzi wa kumjua Mtume Wake –** Nao ni kumjua Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa utambuzi ambao utalazimisha kukubali uongofu na Dini ya haki aliyokuja nayo, kumsadikisha kwa yale aliyoelezea, kujisalimisha katika yale aliyoamrisha, kujiepusha na yale aliyokataza, kuhukumu kwa Shari´ah yake na kuridhika kwa hukumu yake. Allaah (´Azza wa Jalla) Amesema:

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

**"Basi Naapa kwa Mola wako, hawatoamini mpaka wakufanye wewe ni hakimu (mwamuzi) katika yale wanayozozana baina yao, kisha wasione katika nyoyo zao uzito katika yale uliyohukumu na wajisalimishe kwa unyenyekevu." (an-Nisaa 04 : 65)**

إِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ أَن يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا ۚ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

**"Hakika kauli ya Waumini (wa kweli) wanapoitwa kwa Allaah na Mtume Wake ili Awahakumu baina yao; husema: "Tumesikia na Tumetii." Na hao ndio wenye kufaulu." (an-Nuur 24 : 51)**

فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا

**"Mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Allaah na Mtume mkiwa mnamwamini Allaah na Siku ya Mwisho. Hivyo ni (njia) bora na matokeo mazuri zaidi." (an-Nisaa 04 : 59)**

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

**"Basi watahadhari wale wanaokhalifu amri yake, isije kuwasibu *fitnah* au ikawasibu adhabu iumizayo." (an-Nuur 24 : 63)**

Imaam Ahmad (Rahimahu Allaah) amesema:

"Unajua ni nini fitnah? Fitnah ni shirki. Huenda ataporudisha kitu katika maneno yake akatumbukiwa na upotevu katika moyo wake ambao unasababisha maangamivu."

**Kuijua Dini ya Kiislamu –** Uislamu, kwa maana ya jumla, ni kumuabudu Allaah kwa yale Aliyoweka katika Shari´ah tangu pale Alipotuma Mitume mpaka pale Qiyaamah kitaposimama. Hili Allaah (´Azza wa Jalla) Amelitaja katika Aayah nyingi ambazo zinatolea dalili kuonesha kuwa Shari´ah zote zilizotangulia zilikuwa zimejengeka juu ya kujisalimisha kwa Allaah (´Azza wa Jalla). Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu Ibraahiym:

رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَا ۖ إِنَّكَ أَنتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ

**"Mola wetu, Tujaalie tuwe wenye kujisalimisha Kwako pamoja na *kizazi chetu* wawe ummah wenye kujisalimisha Kwako na Tuonyeshe *manaasik* (taratibu za 'ibaadah) zetu na Pokea tawbah zetu, hakika Wewe ni *at-Tawwaabur-Rahiym* (Mwingi wa kupokea tawbah - Mwenye kurehemu)." (al-Baqarah 02 : 128)**

Kuhusu Uislamu kwa maana maalum baada ya kutumwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), inakuwa ni maalum kwa yale Aliyotumwa nayo Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwa sababu yale Aliyotumwa nayo Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) yamefuta dini zote zilizotangulia na kwa ajili hiyo ikawa yule anayemfuata ndio Muislamu, tofauti na yule asiyemfuata sio Muislamu. Kwa njia hiyo wafuasi wa Mitume wote ni Waislamu katika zama za Mitume wao. Mayahudi walikuwa ni Waislamu katika zama za Muusa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kama jinsi Manaswara walikuwa pia ni Waislamu katika zama za ´Iysaa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ama pale Alipotumwa Mtume Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), hawakumwani na kwa ajili hiyo wakazingatiwa kuwa sio Waislamu.

Dini hii ya Kiislamu ndio Dini pekee yenye kukubaliwa mbele ya Allaah na itakayomnufaisha yule anayeifuata. Allaah (´Azza wa Jalla) Amesema:

إِنَّ الدِّينَ عِندَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ ۗ وَمَا اخْتَلَفَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَّا مِن بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ ۗ وَمَن يَكْفُرْ بِآيَاتِ اللَّهِ فَإِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ

**"Hakika Dini mbele ya Allaah ni Uislamu. Na hawakukhitilafiana waliopewa Kitabu ila baada ya kuwajia elimu (ikawa) ni chuki baina yao. Na atakayekanusha alama za Allaah basi hakika Allaah ni Mwepesi wa kuhesabu." (al-´Imraan 03 : 19)**

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ

**"Na yeyote anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitokubaliwa kwake; naye katika Aakhirah atakuwa miongoni mwa waliokhasirika." (al-´Imraan 03 : 85)**

Uislamu huu ndio ule Uislamu ambao Allaah Amemtukuza kwao Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Ummah wake. Allaah (Ta´ala) Amesema:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

**"Leo Nimekukamilishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni neema Yangu, na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe (ndio) Dini**

**yenu." (al-Maaidah 05 : 03)**

**Kwa dalili –** Dalili ni kile kinachoelekeza katika malengo. Dalili zinazoelekeza katika hilo ni za kiungu na za kiakili. Dalil za kiungu ni zile zilizothibiti kwa Wahyi, nacho ni Kitabu na Sunnah. Ni Aayah ngapi Allaah Hakutaja ndani yake kwamba kadhaa na kadhaa ni katika Aayah Zake? Kwa hivyo, mfuatano wa zile dalili za kiakili zikaonesha kuwepo kwa Allaah (Subhanaahu wa Ta´ala).

Ama kuhusu kumjua Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa dalili za kiungu, mfano wake ni Kauli Yake (Ta´ala):

مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ اللَّهِ

**"Muhammad ni Mtume wa Allaah." (al-Fath 48 : 29)**

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ الرُّسُلُ

**"Na Muhammad si yeyote isipokuwa ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake Mitume." (al-´Imraan 03 : 144)**

Wakati huo huo mtu akajisaidia kwa dalili za kiakili na kufanya utafiti na kuzingatia khabari zilizo wazi alizokuja nazo. Kubwa zaidi katika hizo ni Kitabu cha Allaah (´Azz wa Jalla) mbacho ndani yake mna maelezo mengi na yenye manufaa na hukumu zenye kutengeneza na ambazo ni adilifu. Nyinginezo ni ile miujiza aliyofanya, mambo yenye kufichikana aliyoelezea ambayo hayawezi kujulikana isipokuwa kwa njia ya Wahyi na ukweli wake ni yale yaliyotokea.

# 04- Matendo kwa elimu

## *Suala la pili: Kuifanyia kazi*

**Kuifanyia kazi –** Matendo yanayohitajia ujuzi huu. Ikiwa ni pamoja na kumwamini Allaah, kusimama kwa kumtii, kutekeleza maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake katika aina za ´ibaadah maalum na aina elekezi ya ´ibaadah. ´Ibaadah ambazo ni maalum ni mfano wa Swalah, Swawm na Hajj. ´Ibaadah ambazo ni elekezi ni mfano wa kuamrisha mema, kukataza maovu, kupigana Jihaad katika njia ya Allaah na mfano wa hayo.

Matendo kwa hakika ndio matunda ya ujuzi. Yule mwenye kutenda pasina ujuzi, basi amejishabihisha na manaswara, wakati yule mwenye ujuzi na asitende, basi amejishabihisha na mayahudi.

# 05- Kulingania kwa elimu

*Suala la tatu: Kuilingania*

Ina maana ya kulingania katika Shari´ah ya Allaah (Ta´ala) iliyokuja na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutokana na daraja zake tatu au nne ambazo Amezitaja Allaah (´Azza wa Jalla) katika Kauli Yake:

ادْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ

**"Waite (watu) katika Njia ya Mola wako kwa hikmah na mawaidha mazuri." (an-Nahl 16 : 125)**

وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ

**"Na wala msijadiliane na watu wa kitabu isipokuwa kwa yale ambayo ni mazuri zaidi; isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao." (al-´Ankabuut 29 : 46)**

Ni lazima katika Da´wah hii iwe imefungamana na elimu kuhusu Shari´ah ya Allaah (´Azza wa Jalla) ili iweze kuwa imejengeka juu ya ujuzi na umaizi. Allaah (Ta´ala) Amesema:

قُلْ هَٰذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي ۖ وَسُبْحَانَ اللَّهِ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ

**"Sema: "Hii ndio njia yangu nalingania kwa Allaah, juu ya *baswiyrah* (ujuzi, umaizi) mimi na anayenifuata. Na *Subhaana-Allaah* (Utakasifu ni wa Allaah), nami si miongoni mwa washirikina." (Yuusuf 12 : 108)**

Umaizi ina maana mlinganizi awe ni mjuzi wa hukumu ya Kishari´ah, namna ya kulingania na hali ya yule anayemlingania.

Da´wah inaweza kuwa kwa njia na nyanja mbali mbali. Miongoni mwazo ni kulingania katika Dini ya Allaah kwa khutbah, mawaidha, makala, mizunguko ya kielimu, kutunga vitabu na vikao binafsi. Kwa mfano mtu

akikaa katika mizunguko ya kielimu ambapo kunalinganiwa katika Dini ya Allaah, inahesabika kuwa ni uwanja ambapo kunalinganiwa katika Dini ya Allaah (´Azza wa Jalla). Lakini hata hivyo inatakiwa iwe kwa njia isiyokuwa ndani yake na uchovu wala uzito. Hili hupatikana pale ambapo mlinganizi anapotoa masuala ya kielimu kwa wale waliokaa pale halafu baada ya hapo likaanza kujadiliwa. Ni jambo lenye kujulikana ya kwamba majadiliano na maswali na majibu ni jambo lililo na umuhimu mkubwa katika kufahamu yale Aliyoteremsha Allaah kwa Mtume Wake na kuwafanya wengine wakafahamu. Kadhalika njia hii inaweza kuwa na taathira kubwa kuliko khutbah au muhadhara, kama inavyojulikana.

Kulingania katika Dini ya Allaah (´Azza wa Jalla) ndio kazi ya Mitume wote (´alayhimus-Swalaat was-Salaam) na wafuasi wao. Pindi mtu Anaponeemeshwa na Allaah kumjua ni nani Mola Wake, ni nani Mtume Wake na ni ipi Dini yake, anachotakiwa ni kufanya bidii kuwaokoa ndugu zake kwa kuwalingania katika Dini ya Allaah (´Azza wa Jalla) na kuwabashiria kheri. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisema kumwambia ´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anhu) siku ya Khaybar:

**"Nenda mpaka utapofika katika mji wao. Halafu uwalinganie katika Uislamu na uwaeleze kuhusu haki za Allaah (Ta´ala) zilizo juu yao. Ninaapa kwa Allah! Lau Allaah Atamwongoza mtu mmoja kupitia wewe ni kheri kwako kuliko kupata ngamia mwekundu."**[1]

Wameafikiana juu ya usahihi wake.

Muslim amepokea pia kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Anayelingania katika uongofu basi anapata sawa na ujira wa yule atakayemfuata pasina chochote katika ujira wao kupungua. Na anayelingania katika upotevu basi anapata sawa na madhambi ya yule atakayemfuata pasina chochote katika madhambi yao kupungua."**[2]

[1] al-Bukhaariy (2942), Muslim (2407) na Abu ´Awaanah (4/279).

[2] Muslim (2674), Abu Daawuud (4609), at-Tirmidhiy (2764), Ibn Maajah (206), Ahmad (2/397), ad-Daarimiy (513), Ibn Hibbaan (112), Abu Ya´laa (6458) na Abu ´Awaanah (5823).

Vilevile amepokea Muslim kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**“Anayeelekeza katika kheri anapata sawa wa ujira wa yule mwenye kuitenda.”**[3]

[3] Muslim (1893), at-Tirmidhiy (2809), Abu Daawuud (5139), Ahmad (4/120), Ibn Hibbaan (289) na Abu ´Awaanah (6/3).

# 06- Subira kwa maudhi

*Suala la nne: Kusubiri juu ya maudhi yatakayompata mtu ndani yake.*

Subira ni kuifunga nafsi katika kumtii Allaah, kuiweka mbali na kumuasi Allaah na kutokukasirika na Qadar ya Allaah. Kwa njia ya kwamba mtu akaifunga nafsi kutokana na ghadhabu, dhiki na kuchoka na badala yake siku zote akawa ni mchangamfu katika kulingania katika Uislamu hata kama atakumbana na kuudhiwa. Kwa sababu kuwaudhi wale wanaolingania katika kheri ni katika maumbile ya mwanaadamu isipokuwa yule Aliyeongozwa na Allaah. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ فَصَبَرُوا عَلَىٰ مَا كُذِّبُوا وَأُوذُوا حَتَّىٰ أَتَاهُمْ نَصْرُنَا

**"Na kwa yakini walikadhibishwa Mitume kabla yako, wakasubiri juu ya yale waliyokadhibishwa; na wakaudhiwa hata ilipowafikia Nusura Yetu." (al-An´aam 06 : 34)**

Kila pale ambapo maudhi yatazidi kuwa mazito, nusura inakaribia. Hata hivyo nusura haikuwekewa mpaka kwa mtu kunusuriwa katika maisha haya tu na akaona athari ya Da´wah yake, bali nusura inaweza kuja pia baada ya kufa. Hili linapitika kwa njia ya kwamba Allaah Anawafanya watu kukubali yale ambayo siku moja alikuwa akiwalingania kwayo kwa kuyachukua na kushikamana nayo bara bara. Hili pia huzingatiwa kuwa ni nusura kwa mlinganizi huyu hata kama atakuwa ameshakufa. Kwa ajili hiyo ni lazima kwa mlinganizi awe ni mvumilivu katika Da´wah yake na mwenye kuendelea kulingania katika Dini ya Allaah (´Azza wa Jalla). Kadhalika ni lazima awe na uvumilivu kwa vile vipingamizi ambavyo vitajitokeza na maudhi yatakayompata. Hata Mitume (´alayhimus-Swalaat was-Salaam) walifanyiwa maudhi kwa maneno na matendo. Allaah (Ta´ala) Amesema:

كَذَٰلِكَ مَا أَتَى الَّذِينَ مِن قَبْلِهِم مِّن رَّسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ

**"Ndio kama hivyo, hawakuwafikia wale wa kabla yao Mtume yeyote (yule) isipokuwa walisema: "Mchawi au mwendawazimu." (adh-Dhaariyaat 51 : 52)**

Vilevile Amesema (´Azza wa Jalla):

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا مِّنَ الْمُجْرِمِينَ ۗ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ هَادِيًا وَنَصِيرًا

**“Na hivyo ndivyo Tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wahalifu. Na Mola wako Anatosheleza kuwa ni Mwenye kuongoa na Mwenye kunusuru.” (al-Furqaan 25 : 31)**

Lakini hata hivyo inatakiwa kwa mlinganizi apambane na hayo kwa subira. Tazama Kauli ya Allaah (´Azza wa Jalla) kwa Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ تَنزِيلًا

**“Hakika Sisi Tumekuteremshia Qur-aan uteremsho wa hatua kwa hatua.” (al-Insaan 76 : 23)**

Hapa pengine matarajio ilikuwa kusemwe:

“Shukuru neema ya Mola Wako.”

Lakini badala yake Allaah (´Azza wa Jalla) Akasema:

فَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تُطِعْ مِنْهُمْ آثِمًا أَوْ كَفُورًا

**“Basi subiri hukumu ya Mola wako, na wala usimtii miongoni mwao atendaye dhambi au mwenye kukufuru.” (al-Insaan 76 : 24)**

Hapa kuna ishara ya kuwa kila atakayesimama kwa Qur-aan basi ni lazima yampate yeye yale yanayohitajia subira. Tazama hali ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wakati walipompiga watu wake na wakamtoa damu na huku anafuta damu usoni mwake na wakati huo huo anasema:

**“Ee Allaah, wasamehe watu wangu! Kwani hakika hawajui.”**[4]

Kwa ajili hiyo ni lazima kwa mlinganizi awe ni mwenye subira na mwenye kutaraji malipo.

Subira imegawanyika sehemu tatu:

[4] al-Bukhaariy (3477), Muslim (1792), Ibn Maajah (4025), Ahmad (1/380), Ibn Hibbaan (969) na Abu ´Awaanah (4/313).

**Ya kwanza:** Subira katika kumtii Allaah.

**Ya pili:** Subira kwa kujitenga na yale Aliyoharamisha Allaah.

**Ya tatu:** Subira juu ya Qadar ya Allaah ambayo inapitika ima pasina chumo na taathira ya mja, au ambayo Allaah Anayafanya kupitia mikono ya baadhi ya waja katika maudhi na mashambulizi.

# 07- Subira kwa maudhi II

*Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَالْعَصْرِ إِنَّ الْإِنسَانَ لَفِي خُسْرٍ إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ

*"Naapa kwa Al-'Aswr (zama). Hakika ya mwanaadamu bila shaka yumo katika khasara. Isipokuwa wale walioamini na wakatenda mema na wakausiana kwa (kufuata) haki na wakausiana (kuwa na) subira." (al-´Aswr 103 : 01-03)*

**Dalili –** Bi maana dalili ya masuala haya mane ni Kauli Yake (Ta´ala):

"Naapa kwa al-´Aswr"

Katika Suurah hii Allaah (´Azza wa Jalla) Anaapa kwa alasiri ambayo ni zama ambapo ndani yake kunatokea matukio ya kheri na shari. Allaah (´Azza wa Jalla) Ameapa kwa zama ya kwamba kila mwanaadamu yumo katika khasara, isipokuwa wale wanaosifika na sifa hizi nne; imani, matendo mema, kuusiana kwa haki na kuusiana kwa subira. Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah) amesema:

"Kupigana vita na nafsi kuna daraja nne;

**Ya kwanza:** Kupigana nayo vita kwa kuifunza uongofu na Dini ya haki ambayo ndio njia ya kufaulu na furaha.

**Ya pili:** Kupigana nayo vita kwa kutenda kazi kwa mujibu wa elimu.

**Ya tatu:** Kupigana nayo vita kwa kulingania katika Dini ya haki na kuwafundisha wale wasiokuwa na elimu juu yake.

**Ya nne:** Kupigana nayo vita kwa kuwa na subira kwa ajili ya Allaah kwa yale matatizo na maudhi ya viumbe pindi inapolingania katika Dini ya Allaah.

Sifa hizi nne zinapokusanyika kwa mtu, basi anakuwa katika wale wanaoishi kwa mfumo wa kiungu."

Allaah (´Azza wa Jalla) Ameapa katika Suurah hii ya kwamba kila mwanaadamu yumo katika khasara pasina kujali ni mali na watoto kiasi gani alionayo na pasina kujali ni heshima au cheo kiasi gani alio nacho. Isipokuwa yule mtu ambaye anasifika kwa sifa hizi nne;

**Ya kwanza –** Imani, ina maana ya kila I´tiqaad sahihi na elimu yenye manufaa inayomkurubisha mtu kwa Allaah (Ta´ala).

**Ya pili -** Tendo jema, ambayo ni kila kauli na tendo ambalo linamkurubisha mtu kwa Allaah, kwa sharti mtendaji awe anafanya kwa kumtakasia Allaah na ni mwenye kumfuata Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

**Ya tatu –** Kuusiana kwa haki, nayo ina maana ya mtu kuitana na kuhimizana katika matendo mema.

**Ya nne –** Kuusiana kuwa na subira kwa baadhi kuwausia wengine kuwa na subira ya kutekeleza maamrisho ya Allaah (Ta´ala), kujiepusha na makatazo ya Allaah na kuwa na subira ya makadirio ya Allaah.

Kuusiana kwa haki na subira ni pamoja na kuamrishana mema na kukatazana maovu. Mambo haya mawili ndio msingi wa Dini na sababu ya mafanikio yake na nusura na kufikia heshima na fadhila:

كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ

**"Mmekuwa Ummah bora kabisa uliotolewa (mfano) kwa watu; mnaamrisha mema na mnakataza maovu na mnamwamini Allaah." (al-´Imraan 03 : 110)**

# 08- Elimu kabla ya kauli na matendo

*ash-Shaafi´iy (Rahimahu Allaah) amesema:*

*"Lau Allaah Asingeliteremsha hoja yoyote kwa viumbe Wake isipokuwa Suurah hii, basi ingeliwatosheleza."*

*al-Bukhaariy (amesema):*

*"Mlango: Elimu kabla ya kauli na kitendo. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا اللَّهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنبِكَ

*"Basi elewa kwamba laa ilaaha illa-Allaah (hapana mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki ila Allaah), na omba msamaha kwa dhambi zako." (Muhammad 47 : 19)*

*Akawa ameanza kwa elimu kabla ya kauli na kitendo."*

**ash-Shaafi´iy –** Alikuwa ni Abu ´Abdillaah Muhammad bin Idriys bin al-´Abbaas bin ´Uthmaan bin Shaafiy´ al-Haashimiy al-Qurayshiy. Alizaliwa Ghazza mwaka wa 150 na alifariki Misri mwaka 204. Ni mmoja katika maimamu wane – Rehema za Allaah (Ta´ala) ziwe juu yao wote!

Makusudio yake (Rahimahu Allaha) ni kwamba Suurah hii ni yenye kumtosheleza kiumbe kwa kumhimiza katika kushikamana bara bara na Dini kwa imani, tendo jema, kulingania katika Dini ya Allaah na kuwa na subira kwa hilo. Anachokusudia si kwamba Suurah hii inawatosheleza viumbe katika Shari´ah zote.

Mtu mwenye busara na uoni wa mbali pindi anaposikia au kusoma Suurah hii, ni lazima akimbilie kujikwamua na khasara hii. Hili linapitika ikiwa tu atasifika na sifa hizi nne; imani, tendo jema, kuusiana kwa haki na kuusiana kwa subira.

**al-Bukhaariy –** Alikuwa ni Abu ´Abdillaah Muhammad bin Ismaa´iyl bin Ibraahiym bin al-Mughiyrah al-Bukhaariy. Alizaliwa Bukhaaraa katika mwezi wa Shawwaal mwaka wa 194 na alikulia akiwa ni yatima na mama yake. Alifariki (Rahimahu Allaah) katika usiku wa kuamkia ´Iyd-ul-Fitwr mwaka wa 256 Khartank mji ambao uko maili mbili tatu kutoka Samarkand.

al-Bukhaariy (Rahimahu Allaah) ametumia dalili kwa Aayah hii juu ya kuonesha kwamba ni wajibu kuanza kwa elimu kabla ya kauli na kitendo. Dalili hii ya mapokezi inaonesha ya kwamba mwanaadamu anatakiwa kwanza kujifunza baada ya hapo ndio atende. Vilevile kuna dalili za kiakili zinazoonesha kuwa elimu inakuja kabla ya kauli na kitendo. Hilo ni kwa sababu kauli au kitendo hakiwezi kuwa cha sawa sawa na chenye kukubalika isipokuwa mpaka kiwe kimeafikiana na Shari´ah. Wakati huo huo haiwezekani kwa mtu akajua ya kwamba kitendo chake kimeafikiana na Shari´ah bila ya elimu. Hata hivyo kuna mambo ambayo mtu anayajua kwa maumbile. Mfano wa elimu hiyo ni kama mtu kujua ya kwamba hakika ya Allaah ni mungu Mmoja. Maumbile haya mja ameumbiwa nayo na kwa hivyo mtu hahitajii kutia nguvu nyingi katika masomo kama hayo. Ama mambo yaliyoenea ya pande pande ndio ambayo yanahitajia masomo, uanzishwaji na juhudi.

# 09 – Dalili ya kwamba Allaah ndiye Ametuumba

*Tambua – Allaah Akurehemu – kwamba ni wajibu kwa kila Muislamu mwanaume na mwanamke, kujifunza masuala haya matatu na kuyatendea kazi:*

*La kwanza: Allaah Ametuumba...*

Dalili za kiungu na za kiakili zinazothibitisha kuwa Allaah Ametuumba ni hizi zifuatazo:

**Za kiungu:** Dalili hizi ni nyingi na miongoni mwazo ni Kauli Yake (Ta´ala):

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُم مِّن طِينٍ ثُمَّ قَضَىٰ أَجَلًا ۖ وَأَجَلٌ مُّسَمًّى عِندَهُ ۖ ثُمَّ أَنتُمْ تَمْتَرُونَ

**"Yeye Ndiye Ambaye Amekuumbeni kutokana na udongo kisha Akakidhia muda (wa ajali ya kila kiumbe); na muda maalumu (uliowekwa kuondoka ulimwengu) uko Kwake; kisha (juu ya haya) nyinyi mnafanya shaka." (al-An´aam 06 : 02)**

وَلَقَدْ خَلَقْنَاكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَاكُمْ

**"Na kwa yakini Tumekuumbeni kisha Tukakutieni sura." (al-A´raaf 07 : 11)**

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ مِن صَلْصَالٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ

**"Na kwa yakini Tumemuumba mwanaadamu kutokana na udongo wa mfinyanzi unaotoa sauti, unaotokana na tope nyeusi iliyotaghayari (iliyofinyangwa)." (al-Hijr 15 : 26)**

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَكُم مِّن تُرَابٍ ثُمَّ إِذَا أَنتُم بَشَرٌ تَنتَشِرُونَ

**"Na katika ishara Zake ni kwamba Amekuumbeni kutokana na mchanga; tahamaki mmekuwa watu mnaotawanyika**

**(ulimwenguni)." (ar-Ruum 30 : 20)**

خَلَقَ الْإِنسَانَ مِن صَلْصَالٍ كَالْفَخَّارِ

**"Amemuumba mwanaadamu kutokana na udongo wa mfinyanzi unaotoa sauti kama wa vyungu uliookwa moto." (ar-Rahmaan 55 : 14)**

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ

**"Allaah ni *Khaaliq* (Muumbaji) wa kila kitu." (az-Zumar 39 : 62)**

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ

**"Na Allaah Amekuumbeni na yale (yote) mnayoyafanya?" (asw-Swaaffaat 37 : 96)**

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

**"Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu." (adh-Dhaariyaat 51 : 56)**

**Za kiakili:** Ishara yake imetajwa katika Kauli Yake (Ta´ala):

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ

**"Au wameumbwa pasipo na kitu chochote, au wao (wenyewe) ndio waumbaji?" (atw-Twuur 52 : 35)**

Hakika ya mwanaadamu hakujiumba mwenyewe kwa sababu hapo kabla hakuwepo, na kitu kisichokuwepo hakiwezi kuumba. Kitu kisichokuwepo hakiwezi kuumba kitu kilichopo. Hakuumbwa na wazazi wake wala kiumbe yeyote na vilevile hakuja patupu bila ya muumbaji. Kila kitendo ni lazima awepo mtendaji. Kuwepo kwa viumbe hivi kumejengwa kwa ubora na kwa mpangilio na nidhamu, jambo ambalo haliwezekani kabisa wakawa wametoka patupu. Uwepo wa patupu asli hauumbwi kwa nidhamu yoyote na kwa hivyo kubaki kwake na maendeleo yake hayawezi pia kuwa hivo. Hii inakuwa ni sababu ya wazi inayoonesha kuwa Muumbaji ni Allaah Pekee –

hakuna Muumbaji yeyote wala Muamrishaji isipokuwa Allaah. Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ

**“Tanabahi! Ni Vyake Pekee Uumbaji na Amri.” (al-A´raaf 07 : 54)**

Haijulikani kwamba kuna kiumbe yeyote aliyekanusha uola wa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) isipokuwa kwa kiburi, kama alivofanya Fir´awn. Siku moja Jubayr bin Mutw´im alisikia jinsi Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anavyosoma Suurat-utw-Twuur na Aayah:

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ أَمْ خَلَقُوا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ ۚ بَل لَّا يُوقِنُونَ أَمْ عِندَهُمْ خَزَائِنُ رَبِّكَ أَمْ هُمُ الْمُصَيْطِرُونَ

**“Au wameumbwa pasipo na kitu chochote, au wao (wenyewe) ndio waumbaji? Au wameumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini. Au wanazo hazina za Mola wako, au wao ndio wenye mamlaka (nayo)?” (atw-Twuur 52 : 35-37)**

Wakati huo Jubayr bin Mutw´im alikuwa ni mshirikina na akawa amesema:

**“Moyo wangu ulikuwa unakaribia kuruka na hapo ndio ilikuwa mara ya kwanza imani kuingia kwenye moyo wangu.”**[5]

[5] al-Bukhaariy (4853), Muslim (463), Abu Daawuud (806), an-Nasaa’iy (986), Ibn Maajah (832), Maalik (167), ash-Shaafi´iy (uk. 214), ad-Daarimiy (1295), Ibn Khuzaymah (514), at-Twahaawiy (1/211-212), Abu ´Awaanah (1766) na Ibn Hibbaan (1831).

## 10- Dalili ya kwamba Allaah ndio Ameturuzuku

*... akaturuzuku...*

Dalili ya jambo hili ni nyingi katika Kitabu, Sunnah na akili. Ama kuhusu Kitabu, Allaah (Ta´ala) Anasema:

إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ

**"Hakika Allaah Ndiye *Ar-Razzaaq* (Mwenye kuruzuku vyote daima) Mwenye nguvu kali madhubuti." (adh-Dhaariyaat 51 : 58)**

قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ قُلِ اللَّهُ

**"Sema: "Nani yule anayekuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini?" Sema: "Ni Allaah!" (Sabaa´ 34 : 24)**

قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ وَمَن يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَن يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۚ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ ۚ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ

**"Sema: "Nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini. Au nani anayemiliki kusikia na kuona, na nani anayemtoa (aliye) hai kutoka maiti, na anayemtoa maiti kutoka (aliye) uhai na nani anayeendesha mambo (yote)? Watasema: "Ni Allaah"; basi sema: "Je, basi kwa nini hamchi?" (Yuunus 10 : 31)**

Ama kuhusu Sunnah, ikiwa ni pamoja na alivyosema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwamba kuna Malaika anayetumwa kwa mtoto alietumboni na anaamrishwa mambo mane; riziki yake, umri wake, kitendo chake na kama atakuwa asiye na furaha au mwenye furaha.

Kuhusu dalili ya kiakili juu ya kwamba Allaah Ameturuzuku, ni kuwa hatuwezi kuishi bila ya chakula na kinywaji ambavyo vimeumbwa na Allaah (´Azza wa Jalla). Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَفَرَأَيْتُم مَّا تَحْرُثُونَ أَأَنتُمْ تَزْرَعُونَهُ أَمْ نَحْنُ الزَّارِعُونَ لَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَاهُ حُطَامًا فَظَلْتُمْ تَفَكَّهُونَ إِنَّا لَمُغْرَمُونَ بَلْ نَحْنُ مَحْرُومُونَ

أَفَرَأَيْتُمُ الْمَاءَ الَّذِي تَشْرَبُونَ أَأَنتُمْ أَنزَلْتُمُوهُ مِنَ الْمُزْنِ أَمْ نَحْنُ الْمُنزِلُونَ لَوْ نَشَاءُ جَعَلْنَاهُ أُجَاجًا فَلَوْلَا تَشْكُرُونَ

**"Je, mnaona (mimea) mnayopanda? Je, ni nyinyi ndio mlioiotesha au Sisi ndio Tulioiotesha? Lau Tungelitaka, Tungeliifanya mapepe (haizai), mkabakia mnanung'unika (mnajuta). (Mkisema): "Hakika sisi tumegharimika. "Bali sisi tumenyimwa." Je, mnaona maji ambayo mnakunywa? Je, ni nyinyi ndio mliyoyateremsha mawinguni au Sisi ndio Wateremshaji?" Lau Tungelitaka, Tungeliyafanya machungu basi kwa nini hamshukuru?" (al-Waaqi´ah 56 : 63-70)**

Katika Aayah hizi kumebainishwa ya kwamba chakula chetu na kinywaji vinatoka kwa Allaah (´Azza wa Jalla).

## 11- Dalili ya kwamba Allaah Hakutuacha bure pasina malengo yoyote

*... na Hakutuacha bure tu bila ya malengo...*

Huu ndio uhakika wa mambo ambao unathibitishwa na dalili za kiungu na dalili za kiakili. Kuhusiana na za kiungu, miongoni mwazo Anasema (Ta´ala):

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ فَتَعَالَى اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ ۖ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ

**"Je, mlidhania kwamba Sisi Tulikuumbeni bila kusudio na kwamba nyinyi Kwetu hamtorejeshwa? Basi Ametukuka Allaah Mfalme wa haki. Hapana *ilaaha* (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ila Yeye. Mola wa *'Arshi* tukufu." (al-Muuminuun 23 : 115-116)**

أَيَحْسَبُ الْإِنسَانُ أَن يُتْرَكَ سُدًى أَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِّن مَّنِيٍّ يُمْنَىٰ ثُمَّ كَانَ عَلَقَةً فَخَلَقَ فَسَوَّىٰ فَجَعَلَ مِنْهُ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ أَلَيْسَ ذَٰلِكَ بِقَادِرٍ عَلَىٰ أَن يُحْيِيَ الْمَوْتَىٰ

**"Je, anadhani mwanaadamu ataachwa bila ya lengo (bure)? Kwani hakuwa tone kutokana na manii lilotonwa? Kisha akawa pande la damu, (Allaah) Akamuumba na Akamsawazisha? Akamjaalia jozi; dume na jike. Je, hivyo Hakuwa (Huyo Muumbaji) *Qaadir* (Muweza) wa kuhuisha wafu?" (al-Qiyaamah 75 : 36-40)**

Kuhusu dalili za kiakili, haistahiki kwa Hekima ya Allaah (´Azza wa Jalla) mwanaadamu akaishi na kustarehe kama wanyama wanavyostarehe, halafu hatimae akafa pasina kufufuliwa wala kuhesabiwa. Ni upuuzi wa kihakika. Ni jambo lisiloingia akilini Allaah Akaumba kiumbe hichi, Akakitumia Mtume na Akatuhalalishia damu kwa kupigana na wale wapinzani na wanaoenda kinyume na Mitume wa Allaah, kisha natija isiwe ni chochote. Hili ni jambo lisilowezekana kutokana na Hekima ya Allaah (´Azza wa Jalla).

## 12- Dalili kuwa Allaah Ametutumia Mtume

*... bali Amewatumia Mtume...*

Allaah (´Azza wa Jalla) Ametutumia Mtume, Ummah wetu huu wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Mtume mwenye kutusomea Aayah za Mola Wetu, kututakasa na kutufunza Kitabu na hekima kama jinsi Alivyowatuma wale waliokuwa kabla yetu. Allaah (Tabaaraka wa Ta´ala) Amesema:

وَإِن مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ

**"Na hakuna Ummah wowote (ule) isipokuwa amepita humo mwonyaji." (Faatwir 35 : 24)**

Ni lazima kwa Allaah Kuwatumia viumbe Mitume ili hoja iweze kuwasimamia na wapate kumuabudu Allaah kwa yale Anayoyapenda na kuyaridhia. Allaah (Tabaaraka wa Ta´ala) Amesema:

إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَىٰ نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِن بَعْدِهِ ۚ وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ وَعِيسَىٰ وَأَيُّوبَ وَيُونُسَ وَهَارُونَ وَسُلَيْمَانَ ۚ وَآتَيْنَا دَاوُودَ زَبُورًا وَرُسُلًا قَدْ قَصَصْنَاهُمْ عَلَيْكَ مِن قَبْلُ وَرُسُلًا لَّمْ نَقْصُصْهُمْ عَلَيْكَ ۚ وَكَلَّمَ اللَّهُ مُوسَىٰ تَكْلِيمًا رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۚ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

**"Hakika Tumekuletea *Wahy* kama Tulivyomletea Nuwh na Manabii baada yake. Na Tumemletea Ibraahiym na Ismaa'iyl na Is-haaq na Ya'quwb na *Al-Asbaatw* (vizazi) na 'Iysaa na Ayyuwb na Yuwnus na Haaruwn na Sulaymaan. Na Tumempa Daawuwd Zabuwr. Na (Tuliwapelekea *Wahy*) Mitume Tuliokwishakusimulia (habari zao) kabla; na Mitume (wengine) Hatukukusimulia (habari zao). Na bila shaka Allaah Alimsemesha Muwsaa maneno moja kwa moja. Mitume ni wabashiriaji na waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya (kuletwa) Mitume. Na Allaah ni *'Aziyzan-Hakiymaa* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika**

**daima - Mwenye hikmah wa yote daima).” (an-Nisaa 04 : 163-165)**

Hatuwezi kumuabudu Allaah kwa njia Anayoiridhia isipokuwa kwa uongofu wa Mitume (´alayhim-us-Swalaat was-Salaam). Kwa sababu wao ndio ambao wametubainishia yale Anayopenda Allaah na kuyaridhia na yale yanayotukurubisha kwa Allaah (´Azza wa Jalla). Kwa ajili hiyo ni katika Hekima ya Allaah kutuma wajumbe wenye kutoa bishara njema na maonyo kwa watu. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):

إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ رَسُولًا فَعَصَىٰ فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيلًا

**“Hakika Sisi Tumekutumieni Mtume (awe) shahidi juu yenu, kama Tulivyotuma kwa Fir’awn Mtume. (Lakini) Fir’awn alimuasi (huyo) Mtume, Tukamchukuwa mchukuo wa kuangamiza.” (al-Muzzammil 73 : 15-16)**

# 13- Dalili ya kuwa mwenye kumtii Mtume (صلى الله عليه وسلم) ataingia Peponi

*... mwenye kumtii, ataingia Peponi...*

Hili ni haki na limechukuliwa kutoka katika Kauli Yake (Ta´ala):

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ وَسَارِعُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَاوَاتُ وَالْأَرْضُ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ

**"Na mtiini Allaah na Mtume mpate kurehemewa. Na kimbilieni msamaha kutoka kwa Mola wenu na Pepo upana wake ni wa mbingu na ardhi imeandaliwa kwa wacha Mungu. " (al-´Imraan 03 : 132-133)**

وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ وَذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

**"Na yeyote atakayemtii Allaah na Mtume Wake Atamuingiza Pepo zipitazo chini yake mito, ni wenye kudumu humo, na huko ndiko kufuzu kukubwa." (an-Nisaa 04 : 13)**

مَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَخْشَ اللَّهَ وَيَتَّقْهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ

**"Na yeyote yule atakayemtii Allaah na Mtume Wake, na akamkhofu Allaah na akamcha; basi hao ndio wenye kufuzu." (an-Nuur 24 : 52)**

وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَٰئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِم مِّنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ ۚ وَحَسُنَ أُولَٰئِكَ رَفِيقًا

**"Na atakayemtii Allaah na Mtume, basi hao watakuwa pamoja na wale ambao Allaah Amewaneemesha miongoni mwa Manabii, wa kweli na Mashahidi na (waja) wema, na uzuri ulioje hao kuwa ni rafiki (zake)." (an-Nisaa 04 : 69)**

وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا

**“Na anayemtii Allaah na Mtume Wake, basi kwa yakini amefanikiwa mafaniko makubwa.” (al-Ahzaab 33 : 71)**

Aayah mfano wa hizi ni nyingi. Vilevile kauli yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**“Ummah wangu wote utaingia Peponi isipokuwa yule atakayekataa.” Kukasemwa: “Ee Mtume wa Allaah, ni nani atayekataa?” Akasema: “Yule atayenitii ataingia Peponi, na yule atayeniasi ataingia Motoni.”**[6]

Ameipokea al-Bukhaariy.

[6] al-Bukhaariy (7280) na Ahmad (2/361).

## 14- Dalili ya kuwa mwenye kumuasi Mtume (صلى الله عليه وسلم) ataingia Motoni

*... na yule mwenye kumuasi, ataingia Motoni. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ رَسُولًا فَعَصَىٰ فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيلًا

*"Hakika Sisi Tumekutumieni Mtume (awe) shahidi juu yenu, kama Tulivyotuma kwa Fir'awn Mtume. (Lakini) Fir'awn alimuasi (huyo) Mtume, Tukamchukuwa mchukuo wa kuangamiza."*
*(al-Muzzammil 73 : 15-16)*

Hili pia ni haki na limechukuliwa kutoka katika Kauli Yake (Ta´ala):

وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَتَعَدَّ حُدُودَهُ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيهَا وَلَهُ عَذَابٌ مُّهِينٌ

**"Na yeyote atakayemuasi Allaah na Mtume Wake na akapindukia mipaka Yake Atamuingiza Motoni, ni mwenye kudumu humo na atapata adhabu inayodhalilisha." (an-Nisaa 04 : 14)**

وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا

**"Na anayemuasi Allaah na Mtume Wake, basi kwa yakini amepotea upotofu bayana." (al-Ahzaab 33 : 36)**

وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا

**"Na yeyote yule atakayemwasi Allaah na Mtume Wake, basi hakika atapata Moto wa *Jahannam,* ni wenye kudumu humo milele." (al-Jinn 72 : 23)**

Vilevile amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika Hadiyth iliyotangulia:

**"… na yule atayeniasi ataingia Motoni."**

## 15- Allaah Haridhii kushirikishwa na yeyote

*La pili: Hakika Allaah Haridhii kushirikishwa pamoja Naye yeyote katika ´ibaadah Yake; si Malaika aliyekaribu wala Mtume aliyetumwa. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَأَنَّ الْمَسَاجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا

*"Na kwamba Misikiti ni (kwa ajili) ya Allaah, basi msiombe (msimuabudu) yeyote pamoja na Allaah." (al-Jinn 72 : 18)*

Suala la pili ni wajibu kwetu kujua kwamba Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) haridhii kushirikishwa pamoja Naye katika ´ibaadah Yake na yeyote. Bali Yeye Pekee ndiye mwenye kustahiki kuabudiwa. Dalili ya hilo ni ile aliyoitaja mwandishi (Rahimahu Allaah) katika Kauli Yake (Ta´ala):

وَأَنَّ الْمَسَاجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا

**"Na kwamba Misikiti ni (kwa ajili) ya Allaah, basi msiombe (msimuabudu) yeyote pamoja na Allaah." (al-Jinn 72 : 18)**

Allaah (Ta´ala) Amekataza mtu kumuomba yeyote badala ya Allaah na Allaah Hakatazi kitu isipokuwa Hakiridhii (Subhaanahu wa Ta´ala). Allaah (´Azza wa Jalla) Amesema:

إِن تَكْفُرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنكُمْ ۖ وَلَا يَرْضَىٰ لِعِبَادِهِ الْكُفْرَ ۖ وَإِن تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ

**"Mkikufuru, basi (eleweni kuwa) hakika Allaah ni *Ghaniyyun* (Mkwasi) kwenu na wala Haridhii kufuru kwa waja Wake. Na mkishukuru (Yeye) Huridhika nanyi." (az-Zumar 39 : 07)**

فَإِن تَرْضَوْا عَنْهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَرْضَىٰ عَنِ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ

**"Mkiwaridhia, basi hakika Allaah Haridhii watu mafasiki." (at-**

**Tawbah 09 : 96)**

Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) Haridhii shirki na kufuru. Bali Ametuma Mitume na Kuteremsha Vitabu ili kupiga vita kufuru na shirki na kuvitokomeza. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ

**"Na piganeni nao mpaka kusiwekofu fitna na Dini yote iwe kwa ajili ya Allaah." (al-Anfaal 08 : 39)**

Ikiwa Allaah Haridhii kufuru na shirki, basi lililo la wajibu kwa muumini ni kutofanya hivo pia. Kwa sababu muumini anatakiwa kupenda na kuchukia kwa mujibu wa kupenda na kuchukia kwa Allaah. Hivyo Akasirike kwa yale yanayomkasirikisha Allaah na Aridhike na yale yanayomridhisha Allaah (´Azza wa Jalla). Ikiwa Allaah Haridhii kufuru na shirki, basi haijuzu kwa muumini kuyaridhia.

Shirki ni jambo kubwa na la khatari. Allaah (´Azza wa Jalla) Amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

**"Hakika Allaah Hasamehi kushirikishwa; lakini Anasamehe yasiyokuwa hayo kwa Amtakae." (an-Nisaa 04 : 48)**

إِنَّهُ مَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ ۖ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ أَنصَارٍ

**"Hakika mwenye kumshirikisha Allaah bila shaka Allaah Atamharamishia Pepo na makazi yake yatakuwa ni Motoni. Na madhalimu hawatopata mwenye kunusuru yeyote." (al-Maaidah 05 : 72)**

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mwenye kukutana na Allaah bila ya kumshirikisha na chochote, ataingia Peponi, na mwenye kukutana na Allaah ilihali ni mwenye kumshirikisha na chochote, ataingia Motoni."**

## 16- Haijuzu kufanya urafiki na wale wanaompinga Allaah na Mtume Wake

*La tatu: Mwenye kumtii Mtume na akampwekesha Allaah Mmoja, basi haijuzu kwake kufanya urafiki na wale wanaompinga Allaah na Mtume Wake, hata kama itakuwa ni jamaa wa karibu. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

لَّا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ ۚ أُولَٰئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ ۖ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ۚ أُولَٰئِكَ حِزْبُ اللَّهِ ۚ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

*"Hutokuta watu wanaomuamini Allaah na Siku ya Mwisho (kuwa) wanawapenda wale wanaopinzana na Allaah na Mtume Wake, japo wakiwa (ni) baba zao, watoto wao, ndugu zao au jamaa zao. Hao (Allaah) Amewaandikia katika nyoyo zao iymaan, na Akawatia nguvu kwa Roho kutoka Kwake, na Atawaingiza Pepo zipitazo chini yake mito ni wenye kudumu humo. Allaah Ameridhika nao, nao wameridhika Naye. Hao ndio kundi la Allaah. Tanabahi! Hakika kundi la Allaah ndio lenye kufaulu."*
*(al-Mujaadalah 58 : 22)*

Suala la tatu ambalo ni wajibu juu yetu kulijua kuhusu kupenda na kuchukia. Kupenda na kuchukia ni msingi mkubwa uliotajwa na maandiko mengi. Allaah (´Azza wa Jalla) Amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا بِطَانَةً مِّن دُونِكُمْ لَا يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُّوا مَا عَنِتُّمْ

**"Enyi mlioamini! Msichukue rafiki mwandani (msiri wenu) wasiokuwa nyinyi. Hawatoacha kukuharibieni. Wanatamani kama mngetaabika." (al-´Imraan 03 : 118)**

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ ۘ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

**"Enyi mlioamini! Msiwachukuwe Mayahudi na Manaswara (kuwa ndio) marafiki walinzi. Wao kwa wao ni marafiki walinzi. Na yeyote atakayewafanya marafiki; basi hakika yeye ni miongoni mwao. Hakika Allaah Haongoi watu madhalimu." (al-Maaidah 05 : 51)**

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَكُمْ هُزُوًا وَلَعِبًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَالْكُفَّارَ أَوْلِيَاءَ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ

**"Enyi mlioamini! Msiwafanye (kuwa ndio) marafiki walinzi wale ambao wameifanyia Dini yenu mzaha na mchezo miongoni mwa wale waliopewa Kitabu kabla yenu na makafiri. Na mcheni Allaah, kama nyinyi ni Waumini." (al-Maaidah 05 : 57)**

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا آبَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ أَوْلِيَاءَ إِنِ اسْتَحَبُّوا الْكُفْرَ عَلَى الْإِيمَانِ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ قُلْ إِن كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِنُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُم مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

**"Enyi mlioamini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu wandani (wenu) ikiwa wanapendelea ukafiri badala ya Iymaan. Na yeyote miongoni mwenu atakayewafanya vipenzi, basi hao ndio madhalimu. Sema: "Ikiwa baba zenu, watoto wenu, ndugu zenu, wake (au waume) zenu, jamaa zenu mali mliyoichuma, biashara mnayoikhofia kuharibika kwake na majumba mnayoridhika nayo ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Allaah na Mtume Wake na kufanya jihaad katika njia Yake; basi ngojeeni mpaka Allaah Alete Amri Yake (ya adhabu). Na Allaah Haongoi watu mafasiki." (at-Tawbah 09 : 23-24)**

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا

**"Kwa yakini mna kigezo (ruwaza) kizuri kwa Mtume wa Allaah kwa mwenye kumtaraji Allaah na Siku ya Mwisho na**

**akamdhukuru Allaah kwa wingi.” (al-Ahzaab 33 : 21)**

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَآءُ مِنكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةُ وَالْبَغْضَاءُ أَبَدًا حَتَّىٰ تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَحْدَهُ

**“Kwa yakini mna kigezo kizuri kwa Ibraahiym na wale walio pamoja naye, walipowaambia watu wao: “Hakika sisi tumejitenga mbali nanyi na yale (yote) mnayoyaabudu badala ya Allaah, tunakukanusheni, na umedhihirika baina yetu na baina yenu uadui na bughudha daima mpaka mumuamini Allaah Pekee.” (al-Mumtahinan 60 : 04)**

Kuwapenda na kuwa na urafiki na wale wanaompinga Allaah, inaonesha kuwa imani ni dhaifu katika kumuamini Allaah na Mtume Wake. Kwa kuwa sio jambo linaoingia akilini mwanaadamu akampenda mtu ambaye ni adui wa yule anayempenda.

Kufanya urafiki na makafiri ina maana ya kuwanusuru na kuwasaidia pamoja na ile kufuru na upotevu waliyomo. Kuhusu kuwapenda, ina maana ya kufanya matendo ambayo yana kuwapenda. Kwa ajili hiyo utamuona mtu anafanya kila aliwezalo ili apate mapenzi yao. Hili halina shaka kwamba linaondosha imani kabisa au ukamilifu wake. Kwa hivyo ni wajibu kwa muumini kumchukia, kumbughudhi na kujitenga mbali na wale wanaompinga Allaah na Mtume Wake, hata kama itakuwa ni jamaa wa karibu. Lakini hata hivyo hili halizuii kumnasihi mtu na kumlingania katika haki.

## 17- Haniyfiyyah ndio Dini ya Ibraahiym (صلى الله عليه وسلم)

*Tambua – Allaah Akuongoze katika utiifu Wake – kwamba Haniyfiyyah ndio dini (mila) na njia ya Ibraahiym; nako ni kule kumuabudu Allaah Pekee na kwa kumtakasia Yeye Dini.*

Tumeshatangulia kuzungumzia kuhusu ujuzi na hivyo hakuna haja ya kukariri hilo.

**Uongofu –** Kushikamana na njia ya haki.

**Utiifu –** Kuafikiana na malengo kwa kufanya yaliyoamrishwa na kuacha yaliyokatazwa.

**Haniyfiyyah –** Ni dini iliyojitenga mbali na shirki na iliyojengwa juu ya ´ibaadah ya ikhlaasw kwa kumfanyia Allaah (´Azza wa Jalla).

**Mila –** Ni njia yake ya kidini aliyopita juu yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

**Ibraahiym –** Ni rafiki wa karibu wa Mwingi wa rehema. Allaah (´Azza wa Jalla) Amesema:

وَاتَّخَذَ اللَّهُ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا

**"Na Allaah Amemchukua Ibraahiym kuwa ni *khaliyl* (kipenzi)." (an-Nisaa 04 : 125)**

Yeye ndiye baba wa Mitume na mfumo na njia yake imetajwa mara nyingi ili kumfanya ndio kiigizo chema.

**Nako ni kule kumuabudu Allaah Pekee –** Neno ´ibaadah kwa ufahamu wa jumla, ina maana ya kumdhalilikia Allaah kwa mapenzi na kumuadhimisha kwa kutekeleza maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake kwa njia ambayo imekuja katika Shari´ah Yake.

Kuhusu ufahamu maalum na ufafanuzi wa neno ´ibaadah, Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

"´Ibaadah ni neno lililokusanya kila Anachokipenda Allaah na Kukiridhia, katika maneno na matendo, yaliyodhahiri na yaliyojificha. Kama mfano wa khofu, woga, kutegemea, kuswali, kufunga, zakaah na mengineyo katika Shari´ah za Kiislamu."

**Kwa kumtakasia Yeye Dini –** Ikhlaasw. Maana yake ni kule mtu kukusudia kwa ´ibaadah Yake (anayofanya) thawabu kutoka kwa Allaah na kujaribu kufika katika Nyumba Yake ya furaha kwa njia ambayo hamuabudu yeyote pamoja Naye, si Malaika aliyekaribu wala Mtume aliyetumwa. Allaah (Ta´ala) Amesema:

ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنِ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۖ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

**"Kisha Tukakuletea *Wahy* kwamba fuata mila (dini) ya Ibraahim *haniyfaa* na hakuwa miongoni mwa washirikina." (an-Nahl 16 : 123)**

وَمَن يَرْغَبُ عَن مِّلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَن سَفِهَ نَفْسَهُ ۚ وَلَقَدِ اصْطَفَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا ۖ وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمْ ۖ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمُ بَنِيهِ وَيَعْقُوبُ يَا بَنِيَّ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ لَكُمُ الدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ

**"Na nani atakayejitenga na mila (dini) ya Ibraahiym isipokuwa anayeitia nafsi yake upumbavu? Na kwa yakini Tumemchagua duniani, naye Aakhirah ni miongoni mwa (waja) wema. Mola wake Alipomwambia: "Jisalimishe." (Ibraahiym) Akasema: "Nimejisalimisha kwa Mola wa walimwengu." Na Ibraahiym akawausia hayo wanawe na (kadhalika) Ya'quwb (akawaambia): "Enyi wanangu! Hakika Allaah Amekuchagulieni nyinyi Dini; basi msife isipokuwa nyinyi ni Waislamu." (al-Baqarah 02 : 130-132)**

# 18- Lengo la kuumbwa

*Hilo Allaah Amewaamrisha watu wote na Amewaumba kwa lengo hilo. Allaah (Ta´ala) Amesema:*

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

*"Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu." (adh-Dhaariyaat 51 : 56)*

**Hilo... –** Bi maana kwa Hanafiyyah ambayo maana yake ni kumuabudu Allaah kwa kumtakasia Yeye Dini. Allaah Amewaamrisha watu wote na Akawaumba kwa lengo hilo. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ

**"Na Hatukutuma kabla yako Mtume yeyote isipokuwa Tulimpelekea *Wahy* ya kwamba: "Hakika hapana ilaaha (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ila Mimi; basi Niabuduni." (al-Anbiyaa 21 : 25)**

Allaah (´Azza wa Jalla) Amebainisha katika Kitabu Chake kuwa viumbe wameumbwa kwa lengo hili tu. Amesema (Ta´ala):

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

**"Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu." (adh-Dhaariyaat 51 : 56)**

# 19- Aina mbili za ´Ibaadah

*Maana ya waniabudu ni wanipwekeshe.*

Tambua kwamba kuna aina mbili ya ´ibaadah:

**´Ibaadah ya kilimwengu.** Aina hii maana yake ni kule kunyenyekea kwa maamrisho ya Allaah ya kilimwengu na hii imeenea kwa viumbe vyote pasina yeyote kutoka ndani yake. Allaah (Ta´ala) Amesema:

إِن كُلُّ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتِي الرَّحْمَٰنِ عَبْدًا

**"Hakuna yeyote (yule aliyomo) katika mbingu na ardhi isipokuwa (Siku ya kufufuliwa) atamfikia *Ar-Rahmaan* (Mwingi wa Rahmah) kuwa ni mja." (Maryam 19 : 93)**

Hii imeenea kwa muumini na kafiri, mwema na muovu.

**Ibaadah ya Kishari´ah.** Aina hii maana yake ni kule kunyenyekea kwa maamrisho ya Allaah (Ta´ala) ya Kishari´ah na ´ibaadah hii ni maalum kwa yule anayemtii Allaah (Ta´ala) na akafuata yale waliyokuja nayo Mitume. Mfano wa hii ni Kauli Yake (Ta´ala):

وَعِبَادُ الرَّحْمَٰنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا

**"Na waja wa *Ar-Rahmaan* (Mwingi wa Rahmah) ni wale wanaotembea katika ardhi kwa unyenyekevu, na wajinga wanapowasemesha, wao husema (maneno ya) salama." (al-Furqaan 25 : 63)**

Aina ya kwanza mtu hasifiwi nayo, kwa sababu sio mja yeye anayesimama kwa kitendo. Lakini huenda akasifiwa akionesha shukurani wakati wa raha na subira wakati wa majanga. Kuhusiana na aina ya pili, inasifiwa.

# 20- Tawhiyd ndio jambo kubwa Aliloamrisha Allaah

*Kubwa Aliloamrisha Allaah ni Tawhiyd, nayo ni kumpwekesha Allaah kwa ´ibaadah.*

Chimbuko la neno "Tawhiyd" kilugha ina maana ya amepwekesha, anapwekesha na kukifanya kitu kuwa kimoja. Hili halihakikishwi isipokuwa kwa kukanusha na kuthibitisha; mtu akakanusha hukumu isiyokuwa kwa yule anayepwekeshwa, na wakati huo huo kumthibitishia nayo Yeye. Mfano wa hilo ni Tawhiyd ya mtu haikamiliki isipokuwa mpaka ashuhudie kwamba hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah. Hivyo anakuwa amekanusha uungu wote unaonasibishwa kwa wengine asiyekuwa Allaah (Ta´ala), na wakati huo huo authibitishe kwa Allaah Pekee.

Kwa mujibu wa istilahi, mwandishi ameifasiri kwa kusema:

"Tawhiyd, ni kumpwekesha Allaah kwa ´ibaadah."

Maana ya hili ni kumuabudu Allaah Mmoja asiyekuwa na mshirika. Usimshirikishi Yeye na chochote; usimshirikishi Yeye na Nabii yeyote aliyetumwa, Malaika aliyekaribu, raisi, mfalme wala yeyote katika viumbe. Bali mpwekeshe Yeye Peke Yake kwa mapenzi, uadhimisho, shauku na khofu. Shaykh (Rahimahu Allaah) anachokusudia ni aina ya Tawhiyd ambayo Mitume walitumwa kwayo ili kuja kuisimamisha. Licha ya kwamba aina hii ndio sababu ya kupatikana mizozo kati ya wao na watu wao.

Vilevile kuna tafsiri nyingine ya ujumla ya Tawhiyd, nayo ni:

"Ni kumpwekesha Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) kwa yale ambayo ni maalum Kwake."

Kuna aina tatu za Tawhiyd:

**Ya kwanza:** Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah. Maana yake ni kuamini kwamba Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) yuko Peke Yake katika kuumba, ufalme na uendeshaji wa mambo. Allaah (Ta´ala) Amesema:

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ

**"Allaah ni *Khaaliq* (Muumbaji) wa kila kitu." (az-Zumar 39 : 62)**

هَلْ مِنْ خَالِقٍ غَيْرُ اللَّهِ يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۚ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ

**"Je, kuna muumbaji yeyote (yule) badala ya Allaah Anayekuruzukuni kutoka mbinguni na (kwenye) ardhi? Hapana *ilaaha* (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ila Yeye." (Faatwir 35 : 03)**

تَبَارَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**"Amebarikika Ambaye Mkononi Mwake umo ufalme Naye juu ya kila kitu ni *Qadiyr* (Muweza)." (al-Mulk 67 : 01)**

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Tanabahi! Ni Vyake Pekee Uumbaji na Amri. Amebarikika Allaah Mola wa walimwengu." (al-A´raaf 07 : 54)**

**Ya pili:** Tawhiyd-ul-Uluuhiyyah. Maana yake ni kumpwekesha Allaah (Subhaanayu wa Ta´ala) kwa ´ibaadah pasina kumfanyia yeyote pamoja na Allaah kwa kumuabudu na kujikurubisha Kwake kama jinsi anavyomuabudu Allaah na kujikurubisha Kwake.

**Ya tatu:** Tawhiyd al-Asmaa´ was-Swifaat. Maana yake ni kuamini kuwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) yuko Peke Yake katika Majina Aliyojiita Yeye Mwenyewe na Sifa Alizojisifu Mwenyewe au kupitia ulimi wa Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hili linakuwa kwa kuthibitisha yale Aliyojithibitishia Mwenyewe na kukanusha yale Aliyojikanushia, bila ya *Tahriyf,* kuharibu, *Ta´twiyl,* kukanusha, *Takfiyf,* kuziwekea namna na *Tamthiyl,* kufananisha.

Aina anayokusudia hapa mwandishi ni Tawhiyd-ul-Uluuhiyyah. Aina hii ndio ambayo washirikina wamepotea na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akawapiga vita. Vilevile akahalalisha damu zao na mali zao na ardhi zao na majumba yao na wakati huo huo akachukua mateka wanawake wao na vizazi vyao. Aina hii ya Tawhiyd ndio ambayo kwa kiasi kikubwa Mitume wanawatunza watu wao. Amesema (Ta´ala):

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ

**“Na kwa yakini Tulituma katika kila ummah Mtume (awaamrishe watu wake) kwamba: “Mwabuduni Allaah.” (an-Nahl 16 : 36)**

´Ibaadah haisihi isipokuwa ikifanywa kwa Allaah (´Azza wa Jalla) Pekee. Yule mwenye kukosea katika aina hii ya Tawhiyd ni mshirikina kafiri hata kama atakubali Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah na Tawhiyd al-Asmaa´ was-Swifaat. Lau tutachukulia mfano mtu anakiri kikamilifu Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah na Tawhiyd al-Asmaa´ was-Swifaat, lakini mtu huyu anaenda kwenye kaburi na kumuabudu mtu mwenye kaburi hilo au kumuwekea nadhiri ili ajikurubishe kwake, mtu huyu anazingatiwa kuwa ni mshirikina kafiri ambaye atadumishwa Motoni milele. Allaah (Ta´ala) Amesema:

إِنَّهُ مَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ ۖ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ أَنصَارٍ

**“Hakika mwenye kumshirikisha Allaah bila shaka Allaah Atamharamishia Pepo na makazi yake yatakuwa ni Motoni. Na madhalimu hawatopata mwenye kunusuru yeyote.” (al-Maaidah 05 : 72)**

Sababu ya Tawhiyd kuwa ni jambo kubwa Aliloamrisha Allaah, ni kwa sababu ndio msingi ambao Dini yote imejengwa juu yake. Kwa ajili hiyo ndio maana Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alianza ulinganizi wake kwayo katika kulingania katika Dini ya Allaah na akaamrisha wajumbe wake waanze kwayo.

## 21- Shirki ndio jambo kubwa Alilokataza Allaah

*Kubwa Alilokataza Allaah ni Shirki, nako ni kuomba wengine pamoja Naye. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا

*"Na mwabuduni Allaah na wala msimshirikishe na chochote." (an-Nisaa 04 : 36)*

Kubwa Alilokataza Allaah ni shirki na hilo ni kwa sababu haki iliokubwa ni haki ya Allaah (´Azza wa Jalla). Yule mwenye kufanya upungufu katika suala hili, basi amefanya upungufu katika haki iliokubwa, nayo ni kumuabudu Allaah (´Azza wa Jalla) Pekee. Allaah (Ta´ala) Amesema:

إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ

**"Hakika shirki ni dhulma kubwa mno!" (Luqmaan 31 : 13)**

وَمَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَىٰ إِثْمًا عَظِيمًا

**"Na yeyote atakayemshirikisha Allaah basi kwa yakini amebuni dhambi kuu." (an-Nisaa 04 : 48)**

وَمَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا بَعِيدًا

**"Na yeyote atakayemshirikisha Allaah basi kwa yakini amepotoka upotofu wa mbali." (an-Nisaa 04 : 116)**

وَمَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَىٰ إِثْمًا عَظِيمًا

**"Na yeyote atakayemshirikisha Allaah basi kwa yakini amebuni dhambi kuu." (al-Maaidah 05 : 72)**

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

**"Hakika Allaah Hasamehi kushirikishwa; lakini Anasamehe yasiyokuwa hayo kwa Amtakae." (an-Nisaa 04 : 48)**

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Dhambi kubwa ni kumfanyia Allaah mshirikina ilihali Yeye ndiye Amekuumba."**[7]

Amesema (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) katika Hadiyth ambayo Muslim amepokea kutoka kwa Jubayr (Radhiya Allaahu ´anhu):

**"Atayekutana na Allaah pasina kumshirikisha Yeye na chochote, ataingia Peponi, na atayekutana na Allaah ilihali ni mwenye kumshirikisha na chochote, ataingia Motoni."**[8]

Vilevile Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Mwenye kufa na yeye anaomba mshirikina badala ya Allaah, ataingia Motoni."**[9]

Ameipokea al-Bukhaariy.

Kutolea dalili kwamba Allaah (Ta´ala) Ameamrisha Tawhiyd na Kukataza shirki, mwandishi (Rahimahu Allaah) ametumia dalili Kauli Yake (´Azza wa Jalla):

وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا

**"Na mwabuduni Allaah na wala msimshirikishe na chochote." (an-Nisaa 04 : 36)**

Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) Ameamrisha kumuabudu Yeye na Amekataza kumshirikisha. Hili linapelekea kuthibitisha ya kuwa ´ibaadah Anafanyiwa Yeye Pekee. Yule asiyemuabudu Allaah ni kafiri na ni mwenye kiburi, yule mwenye kumuabudu Allaah pamoja na wengine ni kafiri mshirikina na yule mwenye kumuabudu Allaah Peke Yake ni Muislamu mwenye kumtakasia nia.

[7] al-Bukhaariy (7520), Muslim (141), Abu Daawuud (2308), at-Tirmidhiy (3396), an-Nasaa´iy (4024), Ahmad (1/380) na Ibn Hibbaan (4397).

[8] Muslim (152), Ibn Maajah (2618) na Ahmad (2/362).

[9] al-Bukhaariy (4497) na Ahmad (1/402).

Kuna aina mbili za shirki:

Shirki kubwa.

Shirki ndogo.

**Aina ya kwanza:** Shirki kubwa. Hii ni kila kitu ambacho Shari´ah imeita kuwa ni "shirki" na ikawa inamtoa mtu katika Dini.

**Aina ya pili:** Shirki ndogo. Hii ni kila kauli na kila kitendo ambacho Shari´ah imeeleza kuwa ni shirki pasina kumtoa mwenye nayo katika Dini.

Ni wajibu kwa mtu kutahadhari na aina zote za shirki, sawa ikiwa ni kubwa au ndogo. Amesema (Ta´ala):

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ

**"Hakika Allaah Hasamehi kushirikishwa." (an-Nisaa 04 : 48)**

## 22- Misingi mitatu – Ujuzi wa kumjua Mola

*Ukiambiwa: "Ni misingi ipi mitatu ambayo ni wajibu kwa mtu kuijua?" sema: "Mja kumjua Mola Wake...*

Misingi ni wingi wa "msingi". Msingi ni kitu ambacho mtu anajengea juu yake. Miongoni mwa hili ni mfano wa msingi wa ukuta na mizizi ya mti ambao matawi yanakulia. Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ أَصْلُهَا ثَابِتٌ وَفَرْعُهَا فِي السَّمَاءِ

**"Je, huoni vipi Allaah Amepiga mfano wa neno twayyibah (zuri) kama mti mzuri asili yake (yaani mizizi yake) ni thabiti (imethibitika iko imara) na matawi yake (yanafikia) mbinguni?" (Ibraahiym 14 : 24)**

Misingi hii mitatu ambayo mwandishi (Rahimahu Allaah) ametaja, ni misingi ambayo mtu ataulizwa ndani ya kaburi: Ni nani Mola Wako? Ni ipi Dini yako? Ni nani Mtume wako?

Mwandishi (Rahimahu Allaah) ametaja misingi hii mitatu kwa njia ya swali ili amzindue mtu nayo. Hili linaonesha kuwa ni suala kubwa na misingi mikubwa. Amesema kuwa hii ni misingi mitatu ambayo ni wajibu kwa mtu kuijua, kwa sababu ni misingi hii mitatu ndio ambayo mtu ataulizwa ndani ya kaburi. Wakati ndugu na jamaa zake watakapomzika na kumwacha, atajiwa na Malaika wawili ambao watamkaza na kumuuliza:

"Ni nani Mola Wako? Ni ipi Dini yako? Ni nani Mtume wako?"

Muumini atajibu:

"Mola Wangu ni Allaah, Uislamu ndio Dini yangu na Muhammad ndio Mtume wangu."

Ama mwenye mashaka na mnafiki, watasema:

"Haa, haa. Sijui. Nilisikia watu wanasema kitu, hivyo na mimi nikasema kadhalika."

Ujuzi wa kumjua Allaah inakuwa kwa njia tofauti. Miongoni mwazo ni kutazama na kuzingatia viumbe vya Allaah (´Azza wa Jalla). Hilo linapelekea kuweza kumjua na kujua nguvu Zake kubwa na ukamilifu wa uwezo na hekima Yake. Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَوَلَمْ يَنظُرُوا فِي مَلَكُوتِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا خَلَقَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ

**"Je, hawatazami ufalme wa mbingu na ardhi na vitu Alivyoviumba Allaah." (al-A´raaf 07 : 185)**

قُلْ إِنَّمَا أَعِظُكُم بِوَاحِدَةٍ ۖ أَن تَقُومُوا لِلَّهِ مَثْنَىٰ وَفُرَادَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا

**"Sema: "Hakika nakuwaidhini kwa (jambo) moja tu: msimame kwa ajili ya Allaah wawili wawili, au mmoja mmoja (kutafuta haki), kisha mtafakari." (Sabaa´ 34 : 46)**

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ

**"Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitilafiana (kubadilika) usiku na mchana; bila shaka ni alama kwa wenye akili." (al-´Imraan 03 : 190)**

إِنَّ فِي اخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَمَا خَلَقَ اللَّهُ فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَّقُونَ

**"Hakika katika mabadiliko (ya mfuatano) ya usiku na mchana na Alivyoviumba Allaah katika mbingu na ardhi, bila shaka ni alama kwa wanaomcha Allaah." (Yuunus 10 : 06)**

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنفَعُ النَّاسَ وَمَا أَنزَلَ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِن مَّاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيهَا مِن كُلِّ دَابَّةٍ وَتَصْرِيفِ الرِّيَاحِ وَالسَّحَابِ الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ

**"Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitilafiana usiku na mchana na merikebu zipitazo katika bahari viwafaavyo watu na Aliyoteremsha Allaah kutoka mbinguni katika maji Akahuisha kwayo ardhi baada ya kufa kwake na Akaeneza humo**

**kila aina ya mnyama na mgeuko wa pepo na mawingu yanayotiishwa baina ya mbingu na ardhi ni Ayaat kwa watu wenye akili." (al-Baqarah 02 : 164)**

Njia nyingine ambayo mja anaweza kumjua Mola Wake, ni kwa kufikiria alama Zake za Kishari´ah. Alama Zake za Kishari´ah ni Wahyi ambao Mitume (´alayhim-us-Swalaat was-Salaam) waliokuja nao. Mtu anatakiwa kutazama alama hizi manufaa makubwa ilionazo. Manufaa haya viumbe hawawezi kujitosheleza nazo, si duniani wala Aakhirah. Pindi mtu atakapozitazama, kuzizingatia na elimu na hekima ilionazo na kupata nidhamu yake na kuafikiana kwake na maslahi ya mja, basi kwa hilo mtu atapata kumjua Mola Wake (´Azza wa Jalla). Allaah (´Azza wa Jalla) Amesema:

أَفَلَا يَتَدَبَّرُونَ الْقُرْآنَ ۚ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِندِ غَيْرِ اللَّهِ لَوَجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا كَثِيرًا

**"Je, hawaizingatii Qur-aan? Na lau ingelikuwa imetoka kwa asiyekuwa Allaah, bila shaka wangelikuta ndani yake tofauti nyingi." (an-Nisaa 04 : 82)**

Njia nyingine ni Allaah (´Azza wa Jalla) Aingize ujuzi Wake Yeye Mwenyewe (Subhanaahu wa Ta´ala) ndani ya moyo wa muumini, kana kwamba anamuona Mola Wake na macho yake. Mtume (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) amesema wakati walipoulizwa na Jibriyl: "Ni nini Ihsaan?":

**"Ni kumuabudu Allaah kama vile unamuona. Ikiwa wewe humuoni, basi Yeye Anakuona."**[10]

[10] al-Bukhaariy (4777), Muslim (8), Abu Daawuud (4681), at-Tirmidhiy (2738), Ibn Maajah (63) na Ahmad (1/27).

## 23- Ujuzi wa kuijua Dini

*... Dini yake...*

Kujua msingi wa Dini ambao ni Dini yake ambayo amekalifishwa kuitendea kazi na ina hekima na rehema na manufaa yote ambayo inamwelekeza kiumbe kwayo na madhara yote ambayo inamkinga nayo.

Yule mwenye kuzingatia juu ya Dini ya Uislamu kwa njia ya usawa kujengea katika Kitabu na Sunnah, basi ataona kuwa Uislamu ndio Dini ya haki ambayo viumbe hawawezi kujitosheleza nayo ili kuweza kufikia manufaa. Hata hivyo haitakikani kulinganisha Uislamu na hali ya Waislamu wa leo. Hakika ya Waislamu wamepuuza mambo mengi na kujiingiza katika madhambi makubwa. Katika baadhi ya miji yule anayeishi baina yao kana kwamba anaishi katika jamii isiyokuwa ya Kiislamu.

Dini ya Uislamu – himdi zote ni Zake Allaah – ina manufaa yote ambayo dini zilizotangulia ilikuwa nayo. Kile ambacho Uislamu unatofautiana nazo, ni kwamba ni nzuri na inatumika katika kila zama, mahala na watu. Ina maana ya kwamba manufaa ya watu hayatoweki ikiwa mtu atashikamana nayo pasina kujali zamani, mahala na watu. Uislamu unaita katika kila tendo jema na kukataza kila tendo baya. Inaita katika kila tabia nzuri na kukataza kila tabia mbaya.

# 24- Ujuzi wa kumjua Mtume

… *na Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).*"

Msingi wa tatu ni mtu kumjua Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hili linapatikana kwa mtu kusoma maisha ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), ´ibaadah zake, tabia, kulingania katika Dini ya Allaah (´Azza wa Jalla), kupigana Jihaad katika njia Yake na kadhalika. Kwa ajili hii inampasa kila mtu ambaye anataka kuzidisha maarifa kuhusu Mtume wake na imani yenye nguvu, asome historia yake kiasi na atakavyoweza. Kisomo kihusiane na hali yake katika vita na usalama, wakati wa raha na wakati wa shida na hali zake zingine zote. Tunamuomba Allaah (´Azza wa Jalla) Atujaalie katika wale wenye kumfuata Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kwa ndani na nje, na Atufishe katika hali hiyo – hakika Yeye ni Muweza wa hilo.

# 25- Ni nani Mola Wako

### Msingi wa kwanza – ujuzi wa kumjua Mola

*Kukisemwa: "Ni nani Mola Wako?" Jibu: "Mola Wangu ni Allaah ambaye Amenilea na Akawalea walimwengu wote kwa neema Zake. Yeye ndiye ninayemwabudu na sina mwabudiwa mwingine asiyekuwa Yeye."*

**Mola –** Bi maana ni nani Mola wako aliyekuumba, akakusaidia na akakuruzuku.

**Malezi –** Ni ibara ya uchungaji ambayo malezi ya mlelewa hujengeka juu yake. Maneno ya mwandishi yanaashiria kuwa neno "Mola" [Rabb] limechukuliwa kutoka katika neno "malezi" [Tarbiyah], kwa sababu amesema:

"Mola Wangu ni Allaah ambaye Amenilea na Akawalea walimwengu wote kwa neema Zake."

Allaah Amewalea viumbe wote kwa neema Zake, Akawaandaa kwa lile waliloumbiwa kwa ajili yake na Akawaruzuku kwa riziki Yake. Allaah (Tabaaraka wa Ta´ala) amesema kuhusu mdahalo kati ya Muusa na Fir´awn:

فَمَن رَّبُّكُمَا يَا مُوسَىٰ قَالَ رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَىٰ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَىٰ

**"Basi nani (huyo) Mola wenu (Aliyekutumeni), ewe Muwsaa?" (Muwsaa) Akasema: "Mola wetu ni Yule Aliyekipa kila kitu umbo lake, kisha Akakiongoza." (Twaaha 20 : 49-50)**

Kwa njia hiyo viumbe vyote vimelelewa na neema za Allaah (´Azza wa Jalla). Neema za Allaah (´Azza wa Jalla) kwa viumbe Vyake ni nyingi na haziwezi kuhesabika. Allaah (Tabaaraka wa Ta´ala) Amesema:

وَإِن تَعُدُّوا نِعْمَةَ اللَّهِ لَا تُحْصُوهَا

**"Na mkihesabu neema za Allaah hamtoweza kuzihesabu." (an-**

**Nahl 16 : 18)**

Allaah ndiye ambaye Amekuumba, Akakuandaa, Akakusaidia na Akakuruzuku na Yeye Peke Yake ndio mwenye kustahiki kuabudiwa.

**Yeye ndiye ninayemwabudu na sina mwabudiwa mwingine asiyekuwa Yeye –** Yeye ndiye ninayemwabudu na kujisalimisha Kwake kwa kumnyenyekea, kumpenda na kumuadhimisha. Ninafanya yale Aliyoniamrisha na kuacha yale Aliyonikataza. Sina mwingine ninayemuabudu asiyekuwa Allaah (´Azza wa Jalla). Allaah (Tabaaraka wa Ta´ala) Amesema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ

**"Na Hatukutuma kabla yako Mtume yeyote isipokuwa Tulimpelekea *Wahy* ya kwamba: "Hakika hapana ilaaha (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ila Mimi; basi Niabuduni." (al-Anbiyaa 21 : 25)**

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ ۚ وَذَٰلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ

**"Na hawakuamrishwa (chochote kile) isipokuwa wamwabudu Allaah kwa kusafisha na kumtakasia Yeye Dini, na wasimamishe Swalaah na watoe Zakaah; na hiyo ndiyo Dini iliyosimama imara." (al-Bayyinah 98 : 05)**

# 26- Dalili ya kwamba Allaah ndio Mola wa walimwengu

*Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

*"Sifa njema zote ni za Allaah Mola wa walimwengu."*
*(al-Faatihah 01 : 02)*

Ili kuthibitisha ya kuwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) ndiye mlezi wa viumbe wote, mwandishi (Rahimahu Allaah) Ametumia Kauli Yake (Ta´ala):

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**"Sifa njema zote ni za Allaah Mola wa walimwengu." (al-Faatihah 01 : 02)**

Hapa kuna Sifa ya ukamilifu, utukufu na ukubwa inayoelezwa kwa Allaah (Ta´ala) Pekee.

"Mola wa walimwengu" ni Yule Aliyewalea kwa neema, Amewaumba, Amewamiliki na kuyaendesha mambo yao kama Anavyotaka (´Azza wa Jalla).

## 27- Kila kisichokuwa Allaah kimeumbwa

*Kila kisichokuwa Allaah ni walimwengu [kimeumbwa] na mimi ni mmoja katika walimwengu hao.*

Walimwengu ni kila kisichokuwa Allaah. Wamepata jina hili kwa sababu wao ni alama ya Mola Wao, Mmiliki Wao na Anayewaendesha. Katika kila kitu kuna alama inayoonesha kuwa Yeye ni Mmoja.

Mimi ni mmoja katika walimwengu na ikiwa Yeye ndiye Mola Wangu, ni wajibu kwangu kumwabudu Yeye peke Yake.

# 28- Vipi umemjua Mola Wako?

*Kukisemwa: "Vipi umemjua Mola Wako?"...*

**Kukisemwa... –** Bi maana ni kwa njia ipi umemjua Mola Wako (´Azza wa Jalla)? Jibu ya swali hili ni:

"Nimemjua kwa alama Zake na viumbe Vyake."

## 29- Alama za Allaah

*... jibu: "Kwa alama Zake na viumbe Vyake. Miongoni mwa alama Zake ni usiku, mchana, jua na mwezi. Miongoni mwa viumbe Vyake ni mbingu saba na ardhi saba, vilivyomo ndani yake na vilivyomo kati yake."*

Alama ni athari ya kitu chenye kujulisha alama hiyo na kuibainisha.

Alama za Allaah ni aina mbili; za kilimwengu na za Kishari´ah. Alama za kilimwengu ni viumbe na alama za Kishari´ah ni Wahyi ambao Allaah Amewateremshia Mitume Wake. Tukifasiri maandiko kama za kilimwengu na za Kishari´ah, maneno ya mwandishi (Rahimahu Allaah) "Kwa alama Zake na viumbe Vyake" yanaonesha kwamba zile maalum ni ushirikiano wa zile za jumla. Tukikhusisha *Aayaat* [alama] kwa *Aayaat* za Kishari´ah, itakuwa ni ushirikiano unaofanya tofauti na upambanuzi. Hali vovyote ilivyo, Allaah (´Azza wa Jalla) Anajulikana kwa alama Zake za kilimwengu ambavyo ni vile viumbe Vyake vikubwa na yale mambo ya ajabu na hekima ya hali ya juu inayopatikana ndani yake. Kadhalika Anajulikana kwa *Aayaat* Zake za Kishari´ah na yaliyomo ndani yake katika uadilifu na manufaa na kuzuia madhara.

*Katika kila kitu Ana alama*

*Inayoonesha kuwa Yeye ni Mmoja*

Alama zote za Allaah zinaonesha uwezo wa kikamilifu, hekima na rehema. Jua ni moja katika alama za Allaah (´Azza wa Jalla) kwa sababu linaenda kwa nidhamu na njia ya kipekee tangu Allaah (´Azza wa Jalla) Alipoliumba na litaendelea kufanya hivo mpaka pale Allaah (Ta´ala) Atapotoa idhini ya ulimwengu kuharibika. Kwa ajili hiyo jua linaenda mpaka katika kikomo chake. Amesema (Ta´ala):

وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَّهَا ۚ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ

**"Na jua linatembea kwa muda wake (uliopangwa) wa kutulia (kituoni) kwake. Hayo ni makadirio ya *Al-'Aziyzil-'Aliym* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima - Mjuzi wa**

**yote daima)." (Yaasiyn 36 : 38)**

Vilevile ni katika alama za Allaah (Ta´ala) kwa sababu ya ukubwa na athari yake. Ama ukubwa wake, ni likubwa, na kuhusu athari yake, linanufaisha miili, miti, mito, bahari na mengineyo. Tukilitazama jua ambalo ni alama kubwa na ule umbali mkubwa kati yetu sisi na lenyewe, pamoja na hayo tunapata ukali wake mkubwa. Kisha litazame tena na uone ni kitu gani mwangaza wake mkubwa unachangia unapowafanya watu kuhifadhi kiasi kikubwa cha pesa. Wakati wa mchana mtu hana haja ya mwangaza mwingine na kwa hivyo ananufaika kwa kuhifadhi pesa zake. Hili ni katika moja ya alama Zake ambazo sisi hatuzifahamu isipokuwa kitu kidogo tu.

Kadhalika mwezi ni katika alama za Allaah (´Azza wa Jalla). Ameuwekea vituo na kila usiku una kituo chake:

وَالْقَمَرَ قَدَّرْنَاهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَالْعُرْجُونِ الْقَدِيمِ

**"Na mwezi (pia) Tumeukadiria vituo (unatembea) mpaka unarudi (kudhihirika mwembamba) kama kwamba ni shina la mtende lilopinda la zamani." (Yaasiyn 36 : 39)**

Huanza hali ya kuwa ni mdogo kisha unakuwa kidogo kidogo mpaka ukakamilika kuwa mkubwa. Halafu baada ya hapo ukarudi kuwa mdogo. Unafanana na mwanaadamu ambaye anaumbwa akiwa ni mdhaifu. Baada ya hapo anakuwa na nguvu kidogo kidogo mpaka siku moja anarudi kuwa ni mdhaifu tena – Ametukuka Allaah, mbora wa waumbaji.

# 30- Dalili ya alama za Allaah

*Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ ۚ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ

*"Na katika alama Zake ni usiku na mchana, jua na mwezi. (Basi) Msisujudie jua na wala (msisujudie) mwezi; bali msujudieni Allaah Ambaye Aliyeviumba (hivyo) ikiwa Yeye Pekee mnamwabudu." (Fuswswilat 41 : 37)*

*Vile vile Amesema (Ta´ala):*

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ

*"Hakika Mola wenu ni Allaah Ambaye Ameumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha Akalingana juu ya 'Arshi." (al-A´raaf 07 : 54)*

**Dalili –** Dalili ya kwamba mchana na usiku, jua na mwezi, ni katika alama za Allaah (´Azza wa Jalla), ni Kauli Yake (Ta´ala):

وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ

## "Na katika alama Zake ni usiku na mchana... " (Fuswswilat 41 : 37)

Miongoni mwa alama za wazi na bainifu ni usiku na mchana katika dhati yake na katika kutofautiana kwake. Vilevile Allaah Amevifanya kuwanufaisha viumbe na kubadilisha hali zao. Kadhalika jua na mwezi katika dhati yake, kwenda kwake na nidhamu zake; vinachangia katika manufaa ya viumbe na kuwakinga na madhara yake.

Kisha Allaah (Ta´ala) Akawakataza kusujudia jua na mwezi, hata kama vina nafasi kubwa kwao. Kwa sababu vitu hivi havistahiki kuabudiwa kwa kuwa

vimeumbwa. Yule anayestahiki kuabudiwa ni Allaah (Ta´ala) ambaye ameviumba.

**Vile vile Amesema... –** Katika dalili kwamba Allaah Ameumba mbingu na ardhi, ni Kauli Yake (Ta´ala):

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ

**"Hakika Mola wenu ni Allaah Ambaye Ameumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha Akalingana juu ya 'Arshi." (al-A´raaf 07 : 54)**

Ndani yake mna alama za Allaah:

**Ya kwanza:** Allaah Ameumba viumbe hivi vikubwa katika siku sita na kama Angelitaka Angeliviumba kwa dakika. Badala yake Amefungamanisha sababu kwa sababu zake zile zile, kutokana na hekima Yake.

**Ya pili:** Amelingana juu ya ´Arshiy kwa kuweko juu ambao ni maalum na unaolingana na utukufu na ukubwa Wake. Hili linaonesha ukamilifu wa nguvu na ufalme.

**Ya tatu:** Anaufanya usiku kuufunika mchana kama nguo inavyofunika mwangaza wa mchana.

**Ya nne:** Allaah Amefanya jua, mwezi na nyota kudhalilikia amri Zake na Anaviamrisha yale Anayoyataka, kwa maslahi ya viumbe.

**Ya tano:** Kuenea kwa nguvu Zake na ufalme kamilifu kwa kule Kuumba na Kuamrisha ni Kwake Yeye Pekee.

**Ya sita:** Kuenea kwa uola Wake kwa walimwengu wote.

## 31- Mola ndiye Mwabudiwa

*Mola ndiye Mwabudiwa. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۖ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

*"Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu Ambae Amekuumbeni na wale wa kabla yenu mpate kuwa na ucha Mungu. Ambaye Amewafanyieni ardhi kuwa ni tandiko na mbingu kuwa ni paa, na Akateremsha kutoka mbinguni maji, Akawatolea kwayo matunda kuwa ni riziki zenu. Basi msimuwekee Allaah waliolingana naye (washirika) na hali ya kuwa nyinyi mnajua (kuwa Allaah Hana Anayelingana nae)." (al-Baqarah 02 : 21-22)*

Mwandishi (Rahimahu Allaah) analenga Kauli ya Allaah (´Azza wa Jalla):

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Hakika Mola wenu ni Allaah Ambaye Ameumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha Akalingana juu ya 'Arshi; Anafunika usiku kwa mchana, unaufuatia upesi upesi na (Ameumba) jua na mwezi na nyota (vyote) vimetiishwa kwa Amri Yake. Tanabahi! Ni Vyake Pekee Uumbaji na Amri. Amebarikika Allaah Mola wa walimwengu." (al-A´raaf 07 : 54)**

Mola ndiye Mwabudiwa, bi maana ndiye ambaye anastahiki kuabudiwa, au Yeye ndiye mwenye kuabudiwa kwa sababu Anastahiki kuabudiwa. Haina maana kila mwenye kuabudiwa ni mola. Ile miungu inayoabudiwa badala ya Allaah na ikafanywa kuwa ni miungu badala ya Allaah, sio miungu ya kweli. Mola ni Muumbaji na Mfalme na Mwenye kuendesha mambo yote.

**Dalili –** Bi maana dalili juu ya kwamba Mola ndiye mwenye kustahiki kuabudiwa.

**Watu! –** Wito unawaelekea watu wote. Allaah (´Azza wa Jalla) Amewaamrisha watu kumuabudu Yeye Peke Yake bila ya kumshirikisha na kumfanyia washirika. Halafu Amebainisha kwamba Yeye Pekee ndiye Anastahiki kuabudiwa kwa sababu Yeye Mmoja ndiye Muumbaji, asiyekuwa na mshirika.

**... Ambae Amekuumbeni... –** Hii ni sifa ya wazi inayoeleza yaliyotangulia. Mwabuduni Allaah, kwa kuwa Yeye ndiye Mola Wenu Aliyekuumbeni. Kwa vile Yeye ndiye Mola na Muumbaji, inawalazimu kwenu nyinyi kumuabudu. Kwa ajili hii tunasema kila aliyekubali uola wa Allaah, amuabudu Allaah Pekee ili asitumbukie katika kujigonga.

**... ili mpate kuwa na ucha Mungu –** Bi maana ili muwe na ucha Mungu. Taqwa ni kuchukua kinga kutokana na adhabu ya Allaah (´Azza wa Jalla) kwa kufuata maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake.

**Ambaye Amewafanyieni ardhi kuwa ni tandiko –** Ameifanya kuwa ni tandiko na godoro. Tunastarehe juu yake bila ya matatizo wala tabu kama jinsi mtu anavyolala kwenye kitanda chake.

**... na mbingu kuwa ni paa –** Bi maana juu yetu, kwa sababu ya paa, ambayo ni paa juu ya wakazi wa ardhi, iko juu ya mbingu na ni sakafu iliyohifadhiwa. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَجَعَلْنَا السَّمَاءَ سَقْفًا مَّحْفُوظًا ۖ وَهُمْ عَنْ آيَاتِهَا مُعْرِضُونَ

**“Na Tukajaalia mbingu kuwa ni sakafu ilohifadhiwa. Lakini wao wanazikengeuka ishara zake.” (al-Anbiyaa 21 : 32)**

**... na Akateremsha kutoka mbinguni maji... –** Ameteremsha maji masafi kutoka juu mbinguni. Amesema (Ta´ala):

لَّكُم مِّنْهُ شَرَابٌ وَمِنْهُ شَجَرٌ فِيهِ تُسِيمُونَ

**“... katika hayo mnapata kinywaji na kwa hayo (inatoa) miti ambayo humo mnalisha (wanyama).” (an-Nahl 16 : 10)**

**... Akawatolea kwayo matunda kuwa ni riziki zenu –** Kipao kwenu. Katika Aayah nyingine:

مَتَاعًا لَّكُمْ وَلِأَنْعَامِكُمْ

**”Ni manufaa kwenu na kwa wanyama wenu wa mifugo.” (an-Naazi´aat 79 : 33)**

**Basi msimuwekee Allaah washirika... –** Msimuwekee washirika Yule Aliyekuumbeni nyinyi na wale waliokuwa kabla yenu, Akawafanyieni ardhi kuwa ni tandiko na mbingu kuwa paa, Akawateremshieni maji kutoka mbinguni, Akawatolea kwayo matunda kuwa ni riziki zenu. Msimfanyie washirika ambao mnawaabudu au kuwapenda kama jinsi mnavyomuabudu au kumpenda Allaah. Hili haliwafai kwenu nyinyi, si kiakili wala kidini.

**... na hali ya kuwa nyinyi mnajua... –** Nyinyi mnajua kuwa Hana mshirika yeyote na Kuumba kuko Mikononi Mwake, riziki na uendeshaji wa mambo. Hivyo basi, usimuabudu yeyote mwingine badala Yake.

## 32- Muumbaji wa vitu hivi ndiye Mwenye kustahiki kuabudiwa

*Ibn Kathiyr (Rahimahu Allaah) amesema:*

*"Muumbaji wa vitu hivi ndiye Mwenye kustahiki kuabudiwa."*

**Ibn Kathiyr –** Imaad-ud-Diyn Abul-Fidaa´ Ismaa´iyl bin ´Umar al-Qurashiy ad-Dimashqiy. Muhifadhi anayejulikana, mwandishi wa "at-Tafsiyr" na "at-Taariykh" na mmoja katika wanafunzi wa Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah. Alikufa mwaka wa 774.

## 33- Mfano wa aina za ´Ibaadah ambazo Allaah Ameamrisha

*Mfano wa aina za ´ibaadah ambazo Allaah Ameamrisha ni Uislamu, Imani na Ihsaan. Miongoni mwa hizo ni Du´aa pia, khofu, matarajio, utegemeaji, shauku [raghbah] na woga [rahbah], unyenyekeaji, tisho, kurejea (Inaabah), kutaka msaada, kutaka kinga, kutaka kuokolewa, kuchinja, kuweka nadhiri na aina nyinginezo zote miongoni mwa aina za ´ibaadah ambazo Allaah Ameamrisha. Zote ziwe kwa ajili ya Allaah Pekee.*

Baada ya mwandishi (Rahimahu Allaah) kubainisha kwamba ni wajibu kwetu kumuabudu Allaah Peke Yake asiyekuwa na mshirika, amebainisha vilevile baadhi ya aina za ´ibaadah kama Uislamu, Imani na Ihsaan.

Sampuli tatu hizi, Uislamu, Imani na Ihsaan, ndio Dini yenyewe. Imepokelewa na Muslim kutoka katika Hadiyth ya ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anhu) ambaye amesema:

**“Siku moja tulipokuwa tumekaa na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitutokea mtu ambaye nguo zake zilikuwa nyeupe pepe na nywele zake zilikuwa nyeusi sana. Hakuwa na alama ya kuonesha kuwa ni msafiri na wala hapakuwa na hata mmoja katika sisi aliyemtambua. Alienda akakaa karibu na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akaweka magoti yake karibu na mago yake na akaweka viganja vyake juu ya mapaja yake[11].” Akasema: “Ee Muhammad, nieleze kuhusu Uislamu!” Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: “Uislamu ni kushuhudia kuwa hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na Muhammad ni Mtume wa Allaah, kusimamisha Swalah, kutoa Zakaah, kufunga Ramadhaan na kwenda kuhiji ukiweza.” Akasema: “Umesema kweli.”**

[11] Ibn ´Uthaymiyn (Rahimahu Allaah) amesema:

”Bi maana kwenye mapaja yake na sio juu ya mapaja ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).” (Sharh al-Arbaa´iyn an-Nawawiyyah, uk. 21)

**Tukashangazwa kwa kumuuliza kwake Mtume na kumsadikisha. Kisha akasema: "Nieleze kuhusu imani!" Akasema: "Ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake na siku ya Mwisho na kuamini Qadar; kheri na shari yake." Akasema: "Umesema kweli!" Akasema: "Nielezee kuhusu Ihsaan!" Akasema: "Ni kumuabudu Allaah kama vile unamuona. Ikiwa wewe humuoni, basi Yeye Anakuona." Akasema: "Nieleze kuhusu Qiyaamah." Akasema: "Muulizwaji si mjuzi kama asivyo vilevile muulizaji." Akasema: "Nieleze kuhusu alama zake!" Akasema: "Kijakazi kumzaa bibi yake na utaona wachunga wanaenda miguu chini, uchi na mafukara wakishindana kujenga majumba marefu." Amesema: "Kisha akaondoka na tukatulia muda mrefu. Halafu akasema (Swallla Allaahu ´alayhi wa sallam): "Ee 'Umar! Je, unamjua ni nani yule aliyekuwa akiuliza?" Nikajibu: "Allaah na Mtume Wake ndio wanajua zaidi." Akasema Mtume: "Ilikuwa ni Jibriyl ambaye amekuja kuwafundisha Dini yenu.""**

Hivyo akafanya (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) mambo haya kuwa ndio Dini kwa sababu yameizunguka Dini yote.

**... na aina nyinginezo zote miongoni mwa aina za ´ibaadah ambazo Allaah Ameamrisha. Zote ziwe kwa ajili ya Allaah Pekee –** Bi maana aina zote za ´ibaadah zilizotajwa na nyinginezo ni kwa ajili ya Allaah Pekee na si mwingine. Kwa hivyo, haijuzu kumfanyia yeyote katika hizo asiyekuwa Allaah (Ta´ala).

## 34- Dalili ya ´Ibaadah

*Katika Hadiyth imekuja:*

*"Du´aa ndio kiini cha ´ibaadah."*

*Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

*"Na Mola wenu Amesema: "Niombeni, Nitakuitikieni. Hakika wale wanaotakabari na'Ibaadah Yangu, watauingika (Moto wa) Jahanam wadhalilike." (Ghaafir 40 : 60)*

Hapa ndipo mwandishi (Rahimahu Allaah) anaanza kutaja dalili ya aina za ´ibaadah ambazo amezitaja hapo nyuma. Ameanza (Rahimahu Allaah) kutaja dalili ya Du´aa. Kuhusu ufafanuzi wa dalili ya Uislamu, Imani na Ihsaan, zitakuja hapo mbeleni – Allaah Akitaka.

Mwandishi (Rahimahu Allaah) ametumia yaliyopokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambaye amesema:

**"Du´aa ndio kiini cha ´ibaadah."**

Vilevile ametumia dalili kwa Kauli Yake (Ta´ala):

وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

**"Na Mola wenu Amesema: "Niombeni, Nitakuitikieni. Hakika wale wanaotakabari na 'Ibaadah Yangu, watauingika (Moto wa) *Jahanam* wadhalilike." (Ghaafir 40 : 60)**

Aayah hii tukufu ikatoa dalili kwamba Du´aa ni miongoni mwa ´ibaadah. Lau isingelikuwa hivo, isingelikuwa sahihi kusema:

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

**“Hakika wale wanaotakabari na ‘Ibaadah Yangu, watauingika (Moto wa) *Jahanam* wadhalilike.” (Ghaafir 40 : 60)**

Hivyo basi, yule mwenye kumuomba asiyekuwa Allaah kwa kitu ambacho hakiwezi yeyote isipokuwa Allaah (´Azza wa Jalla), ni mshirikina kafiri. Pasina kujali sawa ikiwa huyu mwenye kuombwa bado yuhai au ameshakufa. Hata hivyo, mwenye kumuomba mtu ambaye yuhai kwa kitu ambacho anakiweza, kwa mfano akamuomba chakula au kinywaji, hakuna neno juu yake. Mwenye kumuomba maiti au mtu asiyekuwepo kwa mfano wa kitu [chakula na kinywaji], mtu huyu anazingatiwa kuwa ni mshirikina. Kwa sababu maiti au mtu asiyekuwepo hawezi akafanya kitu kama hichi. Kwa ajili hiyo maombi yake kwa watu hao ni dalili inayoonesha kuwa anaamini ya kwamba wanauendesha ulimwengu – na hili linamfanya kuwa ni mshirikina!

Tambua ya kwamba kuna aina mbili za Du´aa; Du´aa ya kuomba na Du´aa ya ´ibaadah.

Du´aa ya kuomba inahusiana na kuomba kitu, mtu kuomba haja zake. Aina hii inazingatiwa kuwa ni ya ´ibaadah ikiwa mja anamuomba Mola Wake. Kwa kuwa kitendo hichi kinaonesha udhalili kwa Allaah (Ta´ala) na kumtegemea Yeye. Kadhalika kinaonesha kwamba anaonelea kuwa Allaah ni Muweza na Mtoaji na Mwenye fadhila na rehema kunjufu. Vilevile inajuzu Du´aa kama hii mja akamuomba kiumbe mwenzake, maadamu muombwaji huu anafahamu maombi haya na akawa na uwezo wa yale anayoombwa, kama ilivyotangulia kusema mtu akamuomba mwengine chakula.

Kuhusu Du´aa ya ´ibaadah, inahusiana na kumuabudu yule anayeombwa, kwa kutarajia thawabu zake na kuogopa adhabu zake. Hii haisihi kufanyiwa asiyekuwa Allaah. Kumfanyia aina hii asiyekuwa Allaah ni shirki kubwa [Shirk Akbar] inayomtoa mtu katika Uislamu. Vilevile anaingia katika matishio ya Kauli Yake (Ta´ala):

وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

**“Na Mola wenu Amesema: “Niombeni, Nitakuitikieni. Hakika wale wanaotakabari na ‘Ibaadah Yangu, watauingika (Moto wa) *Jahanam* wadhalilike.” (Ghaafir 40 : 60)**

## 35- Dalili ya khofu

*Dalili ya khofu ni Kauli Yake (Ta´ala):*

فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ

*"Basi msiwakhofu na nikhofuni Mimi mkiwa ni Waumini."*
*(al-´Imraan 03 : 175)*

Khofu ni kule kufadhaika kimatendo kunakopatikana wakati mtu anapoogopa kifo, madhara au maudhiko. Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) Amekataza kuwaogopa wapenzi wa Shaytwaan na badala yake Akaamrisha kumuogopa Yeye Peke Yake.

Khofu imegawanyika aina tatu:

**Ya kwanza:** Khofu ya kimaumbile. Mfano wa hilo ni mtu kuogopa wanyama wakali, moto na kuzama. Khofu kama hii mja halaumiwi kwayo. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu Muusa (´alayhis-Swalaat was-Salaam):

فَأَصْبَحَ فِي الْمَدِينَةِ خَائِفًا يَتَرَقَّبُ

**"Akapambaukiwa kuwa mwenye khofu katika mji ule anaangaza." (al-Qaswasw 28 : 18)**

Lakini endapo khofu kama hii itakuwa ni sababu ya kuacha jambo la wajibu au kufanya kitu cha haramu, kama alivyosema Shaykh (Rahimahu Allaah), [khofu hii] inakuwa ni haramu. Kila ambacho ni sababu ya kuacha kitu cha wajibu au kufanya jambo la haramu, inakuwa ni haramu. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):

فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ

**"Basi msiwakhofu, na nikhofuni Mimi mkiwa ni Waumini." (al-´Imraan 03 : 175)**

Khofu ya kumuogopa Allaah (Ta´ala) hata hivyo inaweza kuwa yenye kusifiwa na yenye kulaumiwa.

Kuhusiana na aina inayosifiwa, ni ile ambayo ikiwa lengo ni kutomuasi Allaah. Inapitika kwa kukufanya kutenda mambo ya wajibu na kuacha mambo ya haramu. Lengo hili likitimizwa, moyo hutulia na utazidiwa na furaha kwa neema za Allaah na kutaraji thawabu Zake.

Ama kuhusiana na aina isiyosifika, ni ile inayomfanya mja kukata tamaa na reheme za Allaah. Katika hali hii mja hudhurika na kupata khasara. Vilevile huenda kutokana na ile nguvu ya kukata kwake tamaa ikampelekea kuzidi kuingia katika maasi zaidi.

**Ya pili:** Khofu ya ´ibaadah. Hili linapitika kwa mtu kufanya ´ibaadah kwa khofu. Aina hii hafanyiwi yeyote isipokuwa Allaah, kumfanyia asiyekuwa Allaah (Ta´ala) ni shirki kubwa.

**Ya tatu:** Khofu ya siri. Kwa mfano mtu akamuogopa alie ndani ya kaburi au walii alie mbali na yeye. Hata kama hawezi kumfanya lolote, pamoja na hivyo akawa anamuogopa kwa khofu ya siri. Wanachuoni wamesema kuwa hii ni shirki.

## 36- Dalili ya matarajio

*Dalili ya matarajio ni Kauli Yake (Ta´ala):*

فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا

*"Hivyo anayetaraji kukutana na Mola wake, na atende 'amali njema na wala asishirikishe katika 'ibaadah za Mola wake yeyote." (al-Kahf 18 : 110)*

Matarajio ni mtu kuwa na matarajio kwa kitu kilicho karibu kupatikana. Vilevile inaweza kuwa inahusiana na kitu kilicho mbali, lakini kwa fikira zake kikawa karibu.

Matarajio yanayoambatana na udhalilifu na unyenyekevu hayafanyiwi yeyote isipokuwa Allaah (´Azza wa Jalla). Kufanyiwa yeyote asiyekuwa Allaah (Ta´ala), huzingatiwa ima ni shirki ndogo au kubwa kutegemea na kilichomo ndani ya moyo wa mwenye kutaraji. Mwandishi ametumia dalili Kauli Yake (Ta´ala):

فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا

**"Hivyo anayetaraji kukutana na Mola wake, na atende 'amali njema na wala asishirikishe katika 'ibaadah za Mola wake yeyote." (al-Kahf 18 : 110)**

Tambua kuwa matarajio yenye kusifiwa hayawi isipokuwa kwa yule mwenye kumtii Allaah na huku akitarajia thawabu za Allaah au ametubu kwa madhambi yake na huku akatarajia kukubaliwa Tawbah yake. Ama matarajio pasina matendo, ni kudanganyika na matarajio batili na yenye kulaumika.

## 37- Dalili ya utegemeaji

*Dalili ya utegemeaji ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ

*"Na kwa Allaah Pekee tawakalini ikiwa nyinyi ni Waumini."*
*(al-Maaidah 05 : 23)*

وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ

*"Na yeyote (yule) atakayemtegemea Allaah, basi Yeye Humtosheleza."*
*(at-Twalaaq 65 : 03)*

Kutegemea kitu ni kule kukiamini na kukiegemea. Kumtegemea Allaah (Ta´ala) ina maana ya kumtegemea Allaah (Ta´ala) Pekee ili kujiletea manufaa na kujikinga na madhara. Kitendo hichi ni katika kukamilika na dalili ya imani. Amesema (Ta´ala):

وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ

**"Na kwa Allaah Pekee tegemeeni ikiwa nyinyi ni Waumini." (al-Maaidah 05 : 23)**

Mja akiwa mkweli katika kumtegemea Kwake Allaah (Ta´ala), basi Atamtosheleza (Ta´ala) kwa kile anachohitajia. Amesema (Ta´ala):

وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ

**"Na yeyote (yule) atakayemtegemea Allaah." (at-Twalaaq 65 : 03)**

yaani Atamtosheleza yeye. Halafu Akamtuliza yule mtegemeaji na kusema:

إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ

**"Hakika Allaah Anatimiza amri Yake." (at-Twalaaq 65 : 03)**

bi maana Hashindwi na kitu chochote Anachokitaka.

Tambua kwamba utegemeaji umegawanyika sampuli mbali mbali:

**Ya kwanza:** Kumtegemea Allaah (Ta´ala) ambako ni katika ukamilifu wa imani na alama ya ukweli wake. Hii ni wajibu na imani haitimii isipokuwa kwayo. Kumeshatangulia dalili juu ya hili.

**Ya pili:** Kutegemea kwa siri ambako kunamfanya mtu akamtegemea maiti ili kufikia manufaa au kuzuia madhara. Hii ni shirki kubwa, kwa sababu haitokei isipokuwa kwa yule mwenye kuitakidi kwamba maiti huyu ana uendeshaji wa siri wa ulimwengu. Vilevile hakuna tofauti ikiwa maiti huyo atakuwa ni maiti, walii au adui wa Allaah (Ta´ala).

**Ya tatu:** Kumtegemea mwengine kwa kitu anachokiweza, pamoja na kuonelewa kuwa ana hadhi ya juu na wakati yeye mwenyewe anaonelea kuwa ana hadhi ya chini. Mfano wa hilo akawa anamtegemea katika kupata riziki na mfano wa hayo. Hii ni aina ya shirki kubwa kutokana na nguvu ya moyo wake kufungamana na jambo hilo na kumtegemea.

Ama ikiwa utegemeaji wake kwake hauvuki zaidi ya kumuonelea kuwa yeye ni sababu tu na Allaah (Ta´ala) ndiye Amempa uwezo wa kawaida au hadhi hiyo, itakuwa sio shirki ikiwa mtegemewaji huyo anaweza kufanya hivo kwa njia sahihi.

**Ya nne:** Kumtegemea mwengine kwa kitu anachokipitisha yeye, kwa njia ya kwamba anamuwakilisha mtu mwengine afanye kitu katika nafasi yake midhali kitendo hicho kinajuzu. Hili halina neno kutokana na dalili ya Kitabu, Sunnah na Ijmaa´. Ya´quub alisema kuwaambia wanawe:

يَا بَنِيَّ اذْهَبُوا فَتَحَسَّسُوا مِن يُوسُفَ وَأَخِيهِ

**"Ee wanangu! Nendeni mkamtafute Yuwsuf na ndugu yake." (Yuusuf 12 : 87)**

Vilevile Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwawakilisha watu kukusanya Zakaah na kuihifadhi. Kadhalika aliwawakilisha watu katika kusimamisha adhabu. Alimuwakilisha ´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anhu) katika Hajj ya kuaga kuchinja nafasi yake na akamwambia atoe Swadaqah ngozi ya kichinjwa na nyama. Akamuamrisha kuchinja ngamia mia waliobakia baada ya yeye mwenyewe (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuchinja sitini na tatu.

Ama kuhusu Ijmaa´, inajulikana kwa jumla.

# 38- Dalili ya shauku, woga na unyenyekeaji

*Dalili ya shauku, woga na unyenyekeaji ni Kauli Yake (Ta´ala):*

إِنَّهُمْ كَانُوا يُسَارِعُونَ فِي الْخَيْرَاتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا ۖ وَكَانُوا لَنَا خَاشِعِينَ

*"Hakika wao walikuwa wakikimbilia katika mambo ya kheri, na (walikuwa) wakituomba kwa matumaini na khofu, na walikuwa Kwetu wenye kunyenyekea." (al-Anbiyaa 21 : 90)*

Shauku (Raghbah) ni mapenzi yenye kumfikisha mtu katika jambo linalopendwa.

Woga (Rahbah) ni khofu inayopelekea katika kumkimbia yule anayeogopwa. Nayo inahusiana na khofu iliyoambatana na kitendo.

Unyenyekeaji (Khushuu´) ni udhalilifu na unyonge kwa Utukufu wa Allaah kwa njia ya mtu kujisalimisha na hukumu Zake za ulimwengu na za Kishari´ah.

Katika Aayah hii tukufu Allaah (Ta´ala) Amewasifu waja Wake wa kweli ya kwamba wanamuomba Allaah (Ta´ala) kwa shauku, woga pamoja na kumyenyenyekea. Katika maana hii imekusanya Du´aa ya ´ibaadah na Du´aa ya maombi. Wanamuomba Allaah ilihali wakiwa na shauku kwa yale Alionayo na thawabu Zake, pamoja na kuogopa adhabu Zake na athari ya madhambi yake. Muumini katika juhudi zake kwa Allaah (Ta´ala) anatakiwa kuwa baina ya khofu na matarajio. Matarajio yawe na nguvu kipindi cha wakati wa ´ibaadah, ili apate uchangamfu na kutaraji yakubaliwe, khofu yake iwe na nguvu endapo atapotaka kufanya maasi ili aweze kukimbia yale maasi na kuokoka na adhabu yake.

Baadhi ya wanachuoni wamesema upande wa matarajio uwe na nguvu katika hali ya ugonjwa na khofu iwe na nguvu katika hali ya afya njema. Kwa sababu mgonjwa ni mdhaifu na huenda kifo chake kiko karibu na akafa hali ya kuwa ni mwenye kumdhania vizuri Allaah (´Azza wa Jalla). Na katika hali ya afya njema, anakuwa ni mchangamfu na anatarajia kubaki maisha mrefu. Kwa ajili hiyo hilo linamfanya kutenda madhambi na kuwa na kiburi. Kwa hivyo upande wa khofu unatakiwa kuwa na nguvu ili aweze kuokoka na yote hayo.

Vilevile imesemekana kwamba matarajio na khofu yawe katika daraja moja ili matarajio yasimpelekei akahisi kusalimika na adhabu ya Allaah, kama jinsi khofu pia isimfanye akakata tamaa na rehema za Allaah. Yote mawili ni sifa mbaya zinazomwangamizi mwenye nazo.

# 39- Dalili ya tisho

*Dalili ya tisho ni Kauli Yake (Ta´ala):*

فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ

*"Basi msiwakhofu, na nikhofuni Mimi mkiwa ni Waumini." (al-´Imraan 03 : 175)*

Tisho (Khashyah) ni khofu iliyojengwa juu ya ujuzi wa kumtukuza yule mwenye kuogopwa na ukamilifu wa nguvu zake. Allaah (Ta´ala) Amesema

إِنَّمَا يَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ

**"Hakika wanaomuogopa Allaah (kikweli kweli) miongoni mwa waja Wake ni wanachuoni." Faatwir 35 : 28**

Bi maana wanachuoni ambao wana ujuzi juu ya Ukubwa Wake na Ukamilifu wa nguvu Zake. Tisho (Khashyah) ni aina maalum zaidi kuliko khofu (Khawf). Tofauti kati ya hayo mawili inaweza kubainika kwa mfano. Ikiwa unamuogopa mtu ambaye hujui aweza kukushinda au hapana, hii huhesabiwa kuwa ni khofu (Khawf). Ikiwa unamuogopa mtu ambaye unajua aweza kukushinda, hii inahesabiwa kuwa ni tisho (Khashyah).

Husemwa juu ya vigawanyo mbali mbali vya tisho, yale yale yanayosemwa kuhusu khofu.

# 40- Dalili ya kurejea

*Dalili ya kurejea ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَأَنِيبُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ

*"Na rejeeni (kutubu) kwa Mola wenu na jisalimisheni Kwake." (az-Zumar 39 : 54)*

Kurejea (Inaabah) ni kule kurudi kwa Allaah (Ta´ala) kwa kumtii na kujiepusha kumuasi, na ni tamko liko karibu na maana ya Tawbah. Tofauti iliyopo tu ni kuwa tamko hili ni lepesi zaidi kutokana na kule kumtegemea Allaah.

Hafanyiwi yeyote isipokuwa Allaah (Ta´ala) na dalili ya hilo ni Kauli Yake (Ta´ala):

وَأَنِيبُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ

**"Na rejeeni (kutubu) kwa Mola wenu na jisalimisheni Kwake." (az-Zumar 39 : 54)**

Makusudio ya "... na mjisalimishe Kwake" ni ule Uislamu wa Kishari´ah ambao una maana ya kujisalimisha kwa hukumu za Allaah za Kishari´ah, kwa sababu mtu anaweza kujisalimisha kwa Allaah kwa njia mbili:

**Ya kwanza:** Kujisalimisha kilimwengu. Ina maana mtu akajisalimisha na hukumu Zake za kilimwengu. Hili limeenea na kukizunguka kila kilichoko ndani ya mbingu na ardhi, muumini, kafiri, mwema na muovu. Haiwezekani kwa yeyote kuwa na kiburi kwa aina hii ya ujisalimishaji. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):

وَلَهُ أَسْلَمَ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ

**"... na hali Kwake amejisalimisha kila aliye katika mbingu na katika ardhi akipenda asipende na Kwake watarejeshwa." (al-´Imraan 03 : 83)**

**Ya pili:** Kujisalimisha Kishari´ah. Kujisalimisha huku ina maana mtu akajisalimisha na hukumu Zake za Kishari´ah. Aina hii ni maalum kwa wale Mitume na wafuasi wao wanaomtii. Kuna dalili nyingi ya hilo katika Qur-aan na moja wapo ni Aayah hii iliyotajwa na mwandishi (Rahimahu Allaah).

## 41- Dalili ya kutaka msaada

*Dalili ya kutaka msaada ni Kauli Yake (Ta´ala):*

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

*"Wewe Pekee tunakuabudu na Wewe Pekee tunakuomba msaada."*
*(al-Faatihah 01 : 05)*

*Katika Hadiyth pia imekuja:*

*"Unapotaka msaada, basi mtake msaada Allaah."*

Isti´aanan ni kutaka msaada na kuna aina mbali mbali:

**Ya kwanza:** Kumtaka msaada Allaah, ambako kumefungamana na mja kumdhalilikia Mola Wake kikamilifu, kumwachia mambo yake Yeye na kuamini kuwa Anatosheleza. Hili hafanyiwi yeyote isipokuwa Allaah (Ta´ala). Dalili ya hilo ni Kauli Yake (Ta´ala):

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

**"Wewe Pekee tunakuabudu na Wewe Pekee tunakuomba msaada." (al-Faatihah 01 : 05)**

Uanisho huu umekuja katika neno "iyyaaka" na kutokana na hilo inazingatiwa kuwa ni shirki kubwa inayomtoa mtu katika Uislamu akimfanyia mwingine asiyekuwa Allaah (Ta´ala).

**Ya pili:** Kumtaka msaada kiumbe kwa kitu anachokiweza. Hili linatokana na msaada unao-ombwa; ikiwa ni jambo jema, inazingatiwa kuwa inajuzu kwa yule anayetakwa msaada na limewekwa Kishari´ah kwa yule mwenye kusaidia. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ

**"Saidianeni katika wema na ucha Mungu." (al-Maaidah 05 : 02)**

Ikiwa kitendo hicho kina madhambi, itakuwa ni haramu kwa yule mwenye kutaka na mwenye kutakwa msaada. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ

**"... na wala msisaidiane katika dhambi na uadui." (al-Maaidah 05 : 02)**

Ikiwa kitendo kinaruhusiwa [Mubaah], inajuzu kwa yule mwenye kutaka msaada na mwenye kutakwa. Lakini hata hivyo yule mwenye kusaidia anaweza kulipwa thawabu kwa kitendo chake kizuri kumfanyia mwingine. Kwa njia hiyo kitendo hicho kwa haki kinakuwa kimewekwa katika Shari´ah. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَأَحْسِنُوا ۛ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ

**"Na fanyeni wema. Hakika Allaah Anapenda watendao wema." (al-Baqarah 02 : 195)**

**Ya tatu:** Kumtaka msaada kiumbe ambaye yuko hai na anapatikana kwa kitu asichokiweza. Kitendo hichi ni upuuzi. Mfano wa kitendo kama hicho ni mtu kumtaka msaada mtu dhaifu kubeba kitu kizito.

**Ya nne:** Kuwataka msaada maiti au kuwaomba viumbe wasiokuwepo na waliohai kitu wasichoweza kufanya kikapatikana. Hili linazingatiwa kuwa ni shirki na linafanywa tu na mtu ambaye anaamini kuwa watu hawa wana uendeshaji wa siri juu ya ulimwengu.

**Ya tano:** Kutaka msaada kupitia matendo na hali zinazopendwa kwa Allaah (Ta´ala). Hichi ni kitendo kilichowekwa katika Shari´ah ambacho kimeamrishwa na Allaah (Ta´ala) katika Kauli Yake:

اسْتَعِينُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَاةِ

**"Tafuteni msaada kwa subira na Swalaah." (al-Baqarah 02 : 153)**

Kuhusiana na aina ya kwanza, mwandishi (Rahimahu Allaah) ametumia dalili Kauli Yake (Ta´ala):

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

**"Wewe Pekee tunakuabudu na Wewe Pekee tunakuomba msaada." (al-Faatihah 01 : 05)**

Amefanya kadhalika kwa Hadiyth:

**"Unapotaka msaada, basi mtake msaada Allaah."**

## 42- Dalili ya kutaka kinga

*Dalili ya kutaka kinga ni Kauli Yake (Ta´ala):*

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ

*"Sema: "Najikinga na Mola wa watu." (an-Naas 114 : 01)*

Isti´aadhah ni kutaka msaada kutokana na kitu kinachotahadhariwa na ina aina mbali mbali:

**Ya kwanza:** Kumuomba Allaah (Ta´ala) kinga. Imefungamana na ukamilifu wa kujidhalilisha Kwake, kutafuta nguvu Kwake na kuamini kutosheleza Kwake na kwamba Yeye ndiye mwenye kulinda kikamilifu na kila kitu, sawa ikiwa ni kwa hivi sasa au huko mbeleni, kidogo au kikibwa, mwanaadamu au asiyekuwa mwanaadamu. Dalili Yake ni Kauli Yake (Ta´ala):

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ مِن شَرِّ مَا خَلَقَ

**"Sema: "Najikinga na Mola wa mapambazuko. Kutokana na shari ya Alivyoviumba"." (al-Falaq 113 : 01-02)**

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ لِكِ النَّاسِ إِلَهِ النَّاسِ مِن شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ

**"Sema: "Najikinga na Mola wa watu. Maliki (Mfalme) wa watu. *Ilaah* (Mungu Anayestahiki kuabudiwa kwa haki) na watu. Kutokana na shari za anayetia wasiwasi *Al-Khannaas* (mwenye kurejea nyuma akinyemelea). Ambaye anayetia wasiwasi vifuani mwa watu"." (an-Naas 114 : 01-05)**

**Ya pili:** Kuomba kinga kwa Sifa Zake kama Maneno Yake, Ukubwa Wake, Utukufu Wake na mfano wa hayo. Dalili ya hilo ni kauli (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**“Najilinda kwa Maneno ya Allaah yaliyotimia kwa shari ya Alichokiumba.”**[12]

**“Ee Allaah! Ninaomba kinga kwa Ukubwa Wako kuuliwa chini yangu.”**[13]

Amesema katika Du´aa ya maumivu:

**“Najilinda kwa Utukufu wa Allaah na Uwezo Wake kutokana na shari ninayopata na ninatahadhari nacho.”**[14]

**“Najilinda kwa Radhi Zako kutokana na Khasira Zako.”**[15]

Pindi kulipoteremka Kauli Yake (Ta´ala):

قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَىٰ أَن يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّن فَوْقِكُمْ

**“Sema: “Yeye ni *Al-Qaadir* (Muweza) wa Kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu.” (al-An´aam 06 : 65)**

akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**“Najilinda kwa Uso Wako.”**[16]

---

[12] Muslim (2708), Abu Daawuud (3898), at-Tirmidhiy (2663), Ibn Maajah (3547), ad-Daarimiy (2680), Maalik (1832), Ahmad (6/377), Ibn Khuzaymah (2566) na Ibn Hibbaan (2689). Ibn Hajar ameiandika Hadiyth pia katika ”al-Mustakhraj” ya Abu ´Awaanah”. Tazama ”Ittihaaf-ul-Maharah” (16/927).

13 al-Bukhaariy katika ”at-Taariykh al-Kabiyr” (2278), Ahmad (2/25), Abu Daawuud (5074), an-Nasaa´iy (5544), Ibn Maajah (3871), al-Haakim (1/517) na Ibn Hibbaan (957). al-Haakim amesema:

> ”Isnadi ni Swahiyh na si al-Bukhaariy wala Muslim hawakuipokea.”
>
> adh-Dhahabiy amesema:
>
> ”Swahiyh.” (Talkhiys-ul-Mustadrak (1/517))
>
> al-Albaaniy amesema:
>
> ”Swahiyh.” (at-Ta´liyqaat al-Hisaan (2/290))

14 Muslim (2202), Ahmad (4/217), Abu Daawuud (3891), at-Tirmidhiy (2080), Ibn Maajah (2522) na Maalik (4/309) na al-Qabas.

[15] Muslim (222), Ahmad (1/96), Abu Daawuud (874), at-Tirmidhiy (3726), an-Nasaa´iy (1099), Ibn Maajah (3841) na at-Twahaawiy (1/234).

**Ya tatu:** Kuwaomba maiti kinga, au waliohai na viumbe wasiokuwepo wasioweza kukulinda. Kitendo hichi ni shirki na miongoni mwa hayo ni Kauli Yake (Ta´ala):

وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ الْإِنسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِّنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا

**"Na kwamba walikuwa wanaume miongoni mwa wanaadamu wanajikinga na wanaume miongoni mwa majini, basi wakawazidishia mzigo (wa madhambi na kufru)." (al-Jinn 72 : 06)**

**Ya nne:** Kuwaomba viumbe kinga kwa vitu wanavyoviweza. Kwa mfano ya watu, mahala na mfano wa hayo. Aina hii inajuzu kutokana na kauli yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wakati alipokuwa anataja fitina:

**"Mwenye kuielekea, na yenyewe itamwelekea, na mwenye kupata upenyo au kinga, ajikinge napo."**[17]

Wameafikiana kwayo.

Amebainisha (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) marejeo haya na kinga hii na kusema:

**"Yule alie na ngamia aende naye."**[18]

Hadiyth ameipokea Muslim. Vilevile katika "as-Swahiyh" yake kuna Hadiyth ambayo imepokelewa na Jaabir (Radhiya Allaahu ´anhu) ya kwamba kuna mwanamke aliyeiba. Wakati Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipoamrisha aletwe, akaomba kinga kwa Ummu Salamah. Katika "as-Swahiyh" yake kwamba Ummu Salamah (Radhiya Allaahu ´anha) ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mtu atajilinda katika Nyumba wakati atapotumiwa kikosi."**[19]

---

[16] al-Bukhaariy (7313), Ahmad (3/309), at-Tirmidhiy (3261), Ibn Hibbaan (7176) na Ibn Khuzaymah katika "Kitaab-ut-Tawhiyd" (1/28).

[17] al-Bukhaariy (7082), Muslim (2886) na al-Aajurriy katika "ash-Shari´ah" (68).

[18] Muslim (2887).

[19] Muslim (2882).

Endapo mtu ataomba kinga kujilinda na shari ya dhalimu, ni wajibu kumkinga kiasi cha mtu atakavyoweza. Hata hivyo ni haramu kumlinda iwapo anataka kufikia kitu kilichokatazwa au kuacha kitu kilichowajibishwa.

## 43- Dalili ya kutaka kuokolewa

*Dalili ya kutaka kuokolewa ni Kauli Yake (Ta´ala):*

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ

*"Na (kumbukeni) pale mlipomuomba uokozi Mola wenu Naye Akakujibuni." (al-Anfaal 08 : 09)*

Istighaathah ni kule kutaka uokozi kutokana na matatizo na maangamivu. Ina aina mbali mbali:

**Ya kwanza:** Kumuomba uokozi Allaah (´Azza wa Jalla), jambo ambalo ni katika matendo bora zaidi na kamilifu. Ni katika sifa za Mitume na wafuasi wao ya siku zote. Dalili ya hilo ni yale aliyosema Shaykh (Rahimahu Allaah):

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ أَنِّي مُمِدُّكُم بِأَلْفٍ مِّنَ الْمَلَائِكَةِ مُرْدِفِينَ

**"Na (kumbukeni) pale mlipomuomba uokozi Mola wenu Naye Akakujibuni kuwa: "Hakika Mimi Nitakusaidieni kwa Malaika elfu wafuatanao mfululizo." (al-Anfaal 08 : 09)**

Hili lilikuwa katika vita vya Badr wakati Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipowaangalia washirikina waliokuwa elfu moja wakati Maswahabah zake walikuwa juu kidogo tu ya mia tatu na ishirini. Akaingia ndani ya kibanda chake, akimlilia Mola Wake hali ya kuwa amenyanyua mikono akielekea Qiblah na akisema:

**"Ee Allaah, nitekelezee yale Uliyoniahidi. Ee Allaah, Ukiangamiza kipote hichi cha Kiislamu, hutoabudiwa tena katika ardhi."**

Hakuacha kumtaka uokozi Mola Wake hali ya kuwa amenyanyua mikono yake mpaka kikanzu chake cha juu kikaanguka kutoka kwenye mabega yake. Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anhu) akawa amekichukua na kukiweka kwenye mabega yake. Halafu akakaa nyuma yake na kusema:

**"Ee Mtume wa Allaah, umemuomba Allaah vyakutosha. Hakika Atakutekelezea yale Aliyokuahidi."**[20]

Hapo ndipo Allaah Alipoteremsha Aayah hii.

**Ya pili:** Kuwaomba uokozi maiti au waliohai na viumbe wasiokuwepo wasiokuwa na uwezo wa kuokoa. Kitendo hichi ni shirki, kwa kuwa hili linafanywa tu na mtu anayeamini ya kwamba watu hawa wana uendeshaji wa kisiri juu ya ulimwengu na kwa ajili hiyo anakuwa amewapa sehemu katika uola wa Allaah. Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَمَّن يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ ۗ أَإِلَٰهٌ مَّعَ اللَّهِ ۚ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ

**"Au Yule Anayemuitika aliyedhikika anapomwomba, Akamuondoshea dhiki na Akakufanyeni makhalifa wa ardhi? Je, yuko mungu (mwengine) pamoja na Allaah? Ni machache (mno) mnayokumbuka." (an-Naml 27 : 62)**

**Ya tatu:** Kuwaomba uokozi waliohai, wajuzi na wana uwezo juu ya kusaidia. Kitendo hichi kinajuzu kama jinsi inavyojuzu kuwaomba msaada. Allaah (Ta´ala) Amesema:

فَاسْتَغَاثَهُ الَّذِي مِن شِيعَتِهِ عَلَى الَّذِي مِنْ عَدُوِّهِ فَوَكَزَهُ مُوسَىٰ فَقَضَىٰ عَلَيْهِ

**"Akamsaidia yule ambaye ni katika kundi lake dhidi ya yule ambaye ni katika adui wake, Muwsaa akampiga ngumi, akammaliza (kumuua pale pale)." (al-Qaswasw 28 : 15)**

**Ya nne:** Ni kuomba uokozi kiumbe aliehai asiyekuwa na uwezo wa kuokoa bila ya kuamini ya kwamba ana uwezo wa siri. Kwa mfano mtu yuko katika hali ya kuzama na akamuomba uokozi mtu ambaye amepooza. Hili ni upuuzi, bali ni mchezo pia kwa yule aliyepooza, jambo ambalo ndio sababu ya kukatazwa. Sababu nyingine ni kwamba yule mjeruhiwa [mzamaji] huenda akamdanganya mtu mwingine aliyepo pale ya kwamba mpoozaji huyu ana nguvu za kisiri anazotumia kuoa katika hali ya shida.

[20] Muslim (1763) na at-Tirmidhiy (3276).

## 44- Dalili ya kuchinja

*Dalili ya kuchinja ni Kauli Yake (Ta´ala):*

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ لَا شَرِيكَ لَهُ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ

*"Sema: "Hakika Swalaah yangu, kichinjwa changu, uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allaah (Pekee) Mola wa walimwengu." Hana mshirika, na kwa hayo ndio nimeamrishwa, nami ni Muislamu wa kwanza (waliojisilimisha kwa Allaah)." (al-An´aam 06 : 162-163)*

*na katika Sunnah:*

*"Allaah Amemlaani yule mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allaah."*[21]

Kuchinja ni kule kuizima roho kwa kumwaga damu kwa njia maalum. Hili linakuwa kwa njia mbali mbali:

**Ya kwanza:** Kuchinja kwa ´ibaadah na kukusudia kuadhimisha kile kinachochinjiwa na kujidhalilisha kwacho na kujikurubisha kwacho. Hili haliwi isipokuwa Allaah (Ta´ala) Pekee, kwa njia ambayo imewekwa na Allaah (Ta´ala). Aina hii kumfanyia asiyekuwa Allaah, inazingatiwa kuwa ni shirki kubwa. Dalili ya hilo ni yale aliyosema Shaykh (Rahimahu Allaah), nayo ni Kauli Yake (Ta´ala):

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ لَا شَرِيكَ لَهُ

**"Sema: "Hakika Swalaah yangu, kichinjwa changu, uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allaah (Pekee) Mola wa walimwengu." Hana mshirika." (al-An´aam 06 : 162-163)**

**Ya pili:** Mtu kufanya hivo [kuchinja] katika mnasaba wa kumkirimu mgeni, walima wa harusi na mfano wa hayo. Hili limeamrishwa na inaweza kuwa

[21] Muslim (1978), Ahmad (1/108) na an-Nasaa´iy (4434).

ima wajibu au imependekezwa. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**“Yule anayemwamini Allaah na siku ya Mwisho, basi amkirimu mgeni wake.”**[22]

Vilevile amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kumwambia ´Abdur-Rahmaan bin ´Awf:

**“Fanya walima, hata kama itakuwa mbuzi.”**[23]

**Ya tatu:** Mtu kufanya hivo kwa ajili ya kujistarehesha na kibiashara na mfano wa hayo. Hili ni katika kigawanyo cha yenye kujuzu kutokana na Kauli Yake (Ta´ala):

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا خَلَقْنَا لَهُم مِّمَّا عَمِلَتْ أَيْدِينَا أَنْعَامًا فَهُمْ لَهَا مَالِكُونَ وَذَلَّلْنَاهَا لَهُمْ فَمِنْهَا رَكُوبُهُمْ وَمِنْهَا يَأْكُلُونَ

**“Je, hawaoni kwamba Sisi Tumewaumbia kutokana na yale iliyofanya Mikono Yetu (Tumewaumbia) wanyama wa mifugo basi wao wanawamiliki? Na Tumewadhalilisha kwao, basi baadhi yao humo wanawapanda, na wengine humo wanawala?” (Yaasiyn 36 : 71-72)**

Aina hii inaweza kuwa yenye kutakikana au kukatazwa, kutokana na ni kwa kitu gani itatumiwa.

---

[22] al-Bukhaariy (6019), Muslim (48), Ahmad (2/174), Ibn Maajah (3672), ad-Daarimiy (2035) na Maalik (4/22) na al-Qabas.

[23] al-Bukhaariy (3781), Muslim (1427), Ahmad (3/165), Abu Daawuud (2109), at-Tirmidhiy (1100), Ibn Maajah (1907), ad-Daarimiy (2204) na Maalik (3/85) na al-Qabas. Tazama ”Aadaab-uz-Zafaaf”, uk. 149 ya al-Albaaniy.

## 45- Dalili ya nadhiri

*Dalili ya nadhiri ni Kauli Yake (Ta´ala):*

يُوفُونَ بِالنَّذْرِ وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ مُسْتَطِيرًا

*"(Ambao) Wanatimiza nadhiri (zao), na wanaiogopa siku ambayo shari yake ni yenye kuenea." (al-Insaan 76 : 07)*

Dalili ya kuonesha kuwa nadhiri ni katika ´ibaadah:

يُوفُونَ بِالنَّذْرِ وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ مُسْتَطِيرًا

**"(Ambao) Wanatimiza nadhiri (zao), na wanaiogopa siku ambayo shari yake ni yenye kuenea." (al-Insaan 76 : 07)**

Pwenti katika Aayah ni kwamba Allaah Amewasifu kwa kutekeleza kwao nadhiri, jambo ambalo ni dalili ya kuonesha kuwa Allaah Anapenda kitendo hicho. Na kila kitendo ambacho kinapendwa na Allaah huzingatiwa kuwa ni ´ibaadah. Hilo linatiliwa nguvu zaidi na Kauli Yake (Ta´ala):

وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ مُسْتَطِيرًا

**"... na wanaiogopa siku ambayo shari yake ni yenye kuenea." (al-Insaan 76 : 07)**

Tambua kuwa aina mbali mbali za nadhiri ambazo Allaah (Ta´ala) Amewasifu nazo watu hawa wenye kuzitekeleza, ni zile aina za ´ibaadah ambazo Allaah (´Azza wa Jalla) Amezifaradhisha. Mtu akianza kufanya kitendo cha wajibu, basi akitimize. Dalili ya hilo ni Kauli Yake (Ta´ala):

ثُمَّ لْيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلْيُوفُوا نُذُورَهُمْ وَلْيَطَّوَّفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ

**"Kisha waondoshe takataka zao (nywele, makucha), watimize nadhiri zao na watufu kwenye *Baytil-'Atiyq*." (al-Hajj 22 : 29)**

Kuhusiana na nadhiri ambayo mtu anajilazimisha nayo kwa jambo fulani au kumtii Allaah, lisilokuwa la wajibu, imechukizwa. Baadhi ya wanachuoni wamesema pia ya kwamba ni haramu kwa sababu ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekataza mtu kuweka nadhiri na kusema:

**"Hakika haileti kheri, isipokuwa tu inatoka kwa mtu bakhili."**[24]

Pamoja na hivyo mtu akiweka nadhiri ya kumtii Allaah, basi itakuwa ni wajibu kuitekeleza. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Yule mwenye kuweka nadhiri ya kumtii Allaah, basi amtii."**[25]

Kwa jumla ´ibaadah zote ambazo ni faradhi huitwa "nadhiri". Kuhusiana na nadhiri maalum, ni ile ambayo mtu anailazimisha nafsi yake kwa jambo kwa ajili ya Allaah (´Azza wa Jalla). Wanachuoni wameigawanya nadhiri maalum katika vipengele vingi na imetajwa katika vitabu vya Fiqh.

[24] al-Bukhaari (6608), Muslim (1639), Ahmad (2/61), Abu Daawuud (3277), at-Tirmidhiy (1578), an-Nasaa´iy (3810), Ibn Maajah (2122) na ad-Daarimiy (2340).

[25] al-Bukhaariy (6696) na (6670), Ahmad (6/36), Abu Daawuud (3279), at-Tirmidhiy (1564), an-Nasaa´iy (3816) och (3817), Ibn Maajah (2126) na Maalik (983).

# 46- Msingi wa pili ni kuijua Dini ya Kiislamu

*Msingi wa pili ni kuijua Dini ya Kiislamu kwa dalili. Nako ni kujisalimisha kwa Allaah kwa Tawhiyd, kunyenyekea Kwake kwa kumtii na kujitenga na Shirki na watu wake.*

Miongoni mwa misingi mitatu ni kuijua Dini ya Kiislamu kwa dalili, jambo ambalo ina maana mtu aijue Dini ya Kiislamu kwa dalili kutoka katika Kitabu na Sunnah.

Dini ya Kiislamu inaweza pia kufasiriwa kuwa ni kujisalimisha kwa Allaah kwa Tawhiyd, kunyenyekea Kwake kwa kumtii na kujitenga na Shirki na watu wake. Kwa nji hii imekusanya mambo matatu.

Ya kwamba mja ajisalimishe kwa Mola Wake maana yake ni kujisalimisha Kishari´ah. Huko inakuwa kwa kumpwekesha Allaah (´Azza wa Jalla) na kumuabudu Yeye Peke Yake. Aina hii ndio ambayo mtu anasifiwa nayo na kulipwa nayo. Ama kuhusiana na ujisalimishaji wa kilimwengu, hauna thawabu yoyote ndani yake, kwa sababu mwanaadamu hawezi kuepuka hilo. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَلَهُ أَسْلَمَ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ

**"... na hali Kwake amejisalimisha kila aliye katika mbingu na katika ardhi akipenda asipende na Kwake watarejeshwa." (al-´Imraan 03 : 83)**

**Kunyenyekea Kwake kwa kumtii –** Huko inakuwa kwa kutekeleza maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake. Utiifu maana yake ni kutekeleza maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake.

**Kujitenga na Shirki na watu wake –** Maana yake ni mtu ajiweke mbali na shirki na ajiepushe nayo, jambo ambalo linalazimu vilevile kujiweka mbali na watu wake. Allaah (Ta´ala) Amesema:

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَآءُ مِنكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ

وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةُ وَالْبَغْضَاءُ أَبَدًا حَتَّىٰ تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَحْدَهُ

**"Kwa yakini mna kigezo kizuri kwa Ibraahiym na wale walio pamoja naye, walipowaambia watu wao: "Hakika sisi tumejitenga mbali nanyi na yale (yote) mnayoyaabudu badala ya Allaah, tunakukanusheni, na umedhihirika baina yetu na baina yenu uadui na bughudha milele mpaka mumuamini Allaah Pekee." (al-Mumtahinah 60 : 04)**

## 47- Daraja za Dini ni: Uislamu, Imani na Ihsaan

*Hili lina daraja tatu: Uislamu, Imani na Ihsaan. Kila daraja ina nguzo zake.*

*Nguzo za Uislamu ni tano: Kushuhudia ya kwamba hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah, kusimamisha Swalah, kutoa Zakaah, kufunga Ramadhaan na kuhiji Nyumba ya Allaah takarifu.*

Mwandishi (Rahimahu Allaah) amebainisha kwamba Dini ya Kiislamu ina daraja tatu na baadhi yake ziko juu kuliko zingine. Daraja hizi ni Uislamu, Imani na Ihsaan.

Dalili ya hilo ipo katika kauli yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika Hadiyth ambayo imepokewa na kiongozi wa waumini ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anhu) wakati Jibriyl alipokuja na kumuuliza Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuhusu Uislamu, Imani na Ihsaan. Akabainisha hilo (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kusema:

**"Ilikuwa ni Jibriyl ambaye amewajia ili kuwafunza Dini yenu."**

**Nguzo za Uislamu ni tano –** Dalili ya hilo ni Hadiyth ya Ibn ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa) katika Hadiyth ambapo ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Uislamu umejengwa kwa matano: Kushuhudia ya kwamba hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah, kusimamisha Swalah, kutoa Zakaah, kufunga Ramadhaan na kuhiji Nyumba ya Allaah takatifu."**[26]

[26] al-Bukhaariy (08), Muslim (16), at-Tirmidhiy (2736), an-Nasaaiy (5016), Ahmad (2/120) na al-Bayhaqiy (7322) kutoka kwa Ibn ´Umar.

## 48- Dalili ya Shahaadah

*Dalili ya Shahaadah ni Kauli Yake (Ta´ala):*

شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ ۚ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

*"Allaah Ameshuhudia kwamba hapana ilaaha (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ila Yeye, Malaika na wenye elimu (wote wameshuhudia kwamba Yeye) ni Mwenye kusimamisha (uumbaji Wake) kwa uadilifu. Hapana mungu wa haki ila Yeye Al-'Aziyzul-Hakiym (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima – Mwenye hikmah wa yote daima)." (al-´Imraan 03 : 18)*

Kushuhudia ya kwamba hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na Muhammad ni Mtume wa Allaah ni nguzo moja. Hata kama ni sentisi mbili pamoja na hivyo ni nguzo moja kwa kuwa ´ibaadah zimejengeka juu ya kuhakikisha hayo mawili kwa pamoja. ´Ibaadah haikubaliwi isipokuwa kwa kumtakasia Dini Allaah (´Azza wa Jalla), jambo ambalo limefungamana na kushuhudia ya kwamba hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah, na kumfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), jambo ambalo limefungamana pia na kushuhudia ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah.

Katika Aayah tukufu Allaah Anajitolea ushahidi Mwenyewe na ushahidi wa Malaika na ushahidi wa wanachuoni ya kuwa hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye na kwamba ni Mwenye kusimamisha kwa uadilifu. Halafu Akakariri hilo kwa Kauli Yake:

لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

**"Hapana mungu wa haki ila Yeye *Al-'Aziyzul-Hakiym* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima - Mwenye hikmah wa yote daima)." (al-´Imraan 03 : 18)**

Katika Aayah hii kuna ngazi kubwa kwa wanachuoni pindi Aliposema kwamba wanachuoni wanashuhudia pamoja na Yeye na Malaika. Makusudio

ya wanachuoni hapa ni wale walio na elimu katika Shari´ah na wanaoanza kuingia hapa kwanza ni Mitume Wake.

Shahaadah hii ni Shahaadah kubwa kutokana na ukubwa wa mwenye kushuhudia na mwenye kushuhudiwa. Wenye kushuhudia ni Allaah, Malaika Wake na wanachuoni, wakati mwenye kushuhudiwa ni kupwekeka kwa Allaah katika kuwa na haki ya kuabudiwa. Kitu ambacho kinathibitisha hilo ni:

لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

**“Hapana mungu wa haki ila Yeye *Al-‘Aziyzul-Hakiym* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima - Mwenye hikmah wa yote daima).” (al-´Imraan 03 : 18)**

## 49- Maana ya Shahaadah

*Maana yake ni kwamba hapana mola mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah. "Hapana mola" ni kukanusha kila kinachoabudiwa badala ya Allaah, wakati "isipokuwa Allaah" ni kuthibitisha ya kwamba ´ibaadah afanyiwa Allaah Pekee. Hana mshirika katika ´ibaadah Yake, kama ambavyo Hana mshirika katika Ufalma Wake.*

Maana ya Shahaadah ni "hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah". Shahaadah hii ni mtu atambue kwa ulimi wake na moyo wake ya kwamba hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah (´Azza wa Jalla). Neno "hakuna mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah" limekusanya ukanushaji na uthibitishaji.

Neno "hapana mola" kuna ukanushaji wakati uthibitishaji upo katika neno "isipokuwa Allaah". Kwa msaada wa maelezo ya maunganisho haya [kule kuweka "kwa haki"] kutakuwa kumebainika jawabu kwa mtu juu ya utatizi wa suala "Vipi mtu atasema ya kwamba hapana mola anayeabudiwa isipokuwa Allaah, wakati kuna miungu mingi inayoabudiwa badala ya Allaah na sivyo tu, bali Allaah ameipa jina la "miungu" na wale wenye kuiabudu? Allaah (Tabaaraka wa Ta´ala) Amesema:

فَمَا أَغْنَتْ عَنْهُمْ آلِهَتُهُمُ الَّتِي يَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مِن شَيْءٍ لَّمَّا جَاءَ أَمْرُ رَبِّكَ

**"Basi hawakuwafaa kitu chochote miungu yao waliyokuwa wakiyaomba badala ya Allaah ilipokuja amri ya Mola wako." (Huud 11 : 101)**

Na vipi tunaweza kuthibitisha uungu wa mtu mwingine, mbali na uungu wa Allaah, wakati Mitume wamesema kuwaambia watu wao:

يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُ

**"Enyi watu wangu! Mwabuduni Allaah (kwani nyinyi) hamna *ilaah* (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) badala Yake. (al-A´raaf 07 : 59)?"**

Jibu juu ya utatizi huu linapatikana kwa kule kuyakadiria maelezo katika "hapana mola mwenye kuabudiwa isipokuwa Allaah". Miungu hii inayoabudiwa badala ya Allaah ni miungu ya batili. Sio miungu ya kikweli na haina haki yoyote ya kuabudiwa. Dalili ya hilo ni Kauli Yake (Ta´ala):

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ هُوَ الْبَاطِلُ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

**"Hivyo ni kwa kuwa Allaah Ndiye *Al-Haqq* (Mungu wa kweli Anayestahiki kuabudiwa), na kwamba vile wanavyoomba (makafiri) badala Yake ndiyo batili; na kwamba Allaah Ndiye *Al-'Aliyyul-Kabiyr* (Mwenye 'Uluwa Yuko juu ya vyote - Mkubwa wa dhati, vitendo na sifa)." (al-Hajj 22 : 62)**

Dalili nyingine ni Kauli Yake (Ta´ala):

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ أَلَكُمُ الذَّكَرُ وَلَهُ الْأُنثَىٰ تِلْكَ إِذًا قِسْمَةٌ ضِيزَىٰ إِنْ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمَّيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَآبَاؤُكُم مَّا أَنزَلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطَانٍ ۚ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَمَا تَهْوَى الْأَنفُسُ ۖ وَلَقَدْ جَاءَهُم مِّن رَّبِّهِمُ الْهُدَىٰ

**"Je, mmeona *Laata* na *'Uzzaa* (masanamu miongoni mwa miungu ya makafiri)? Na *Manaata* (sanamu) mwengine wa tatu? Je, nyinyi mna wana wa kiume Naye (Allaah) Ana wana wa kike? Huo ni mgawanyo si wa uadilifu. Hayo si chochote isipokuwa ni majina mmeyaita (hayo masanamu) nyinyi na baba zenu, wala Allaah Hakuyateremshia madaraka yoyote. Hawafuati isipokuwa dhana na yale yanayotamani nafsi (zao), na hali imekwishawajia kutoka kwa Mola wao uongofu." (an-Najm 53 : 19-23)**

Amesema (Ta´ala) ya kwamba Yuusuf (´alayhis-Salaam) amesema:

مَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِهِ إِلَّا أَسْمَاءً سَمَّيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَآبَاؤُكُم مَّا أَنزَلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطَانٍ

**"Hamuabudu pasi Naye (Allaah) isipokuwa majina (ya masanamu) mmeyaita nyinyi na baba zenu, Hakuyateremshia Allaah kwayo mamlaka (amri) yoyote." (Yuusuf 12 : 40)**

Kwa hivyo "hakuna mola mwenye kuabudiwa isipokuwa Allaah" maana yake ni hapana mola mwenye kuabudiwa *kwa haki* isipokuwa Allaah (´Azza wa Jalla). Ama kuhusiana na vingine vyote vinavyoabudiwa badala ya Allaah, uungu wao unaodaiwa ni wa batili. Bi maana uungu wa batili.

# 50- Tafsiri inayoweka wazi maana ya Shahaadah

*Tafsiri inayoweka wazi haya, ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقِبِهِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

*"Na (taja pale) Ibraahiym alipomwambia baba yake na watu wake: "Hakika mimi najitenga mbali na yale mnayoyaabudu. "Isipokuwa Yule Aliyeniumba, basi hakika Yeye Ataniongoa." Na akalifanya neno (la ilaaha illaa-Allaah) lenye kubakia katika kizazi chake ili wapate kurejea." (az-Zukhruf 43 : 26-28)*

**Ibraahiym –** Ibraahiym ni rafiki wa karibu wa Allaah kiongozi wa wapwekeshaji. Yeye ndiye Mtume bora baada ya Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Baba yake ni Aazar.

**Najitenga mbali –** Ni kitenzi cha "kujiweka mbali". Kauli yake "Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayoyaabudu" inaafikiana na "hapana mola... ".

**Isipokuwa Yule Aliyeniumba –** Kuniumba kwa maumbile ya mwanzo. Kauli Yake "isipokuwa Yule Aliyeniumba" inaafikiana na "... isipokuwa Allaah". Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) Hana mshirika katika uungu Wake, kama jinsi Hana mshirika katika ufalme Wake. Dalili ya hilo ni Kauli Yake (Ta´ala):

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Tanabahi! Ni Vyake Pekee Uumbaji na Amri. Amebarikika Allaah Mola wa walimwengu." (al-A´raaf 07 : 54)**

Katika Aayah hii kumewekewa kikomo Kuumba na Amri kwa Allaah Pekee, Mola wa walimwengu. Uumbaji wa ulimwengu na wa Kishari´ah na maamrisho ya ulimwengu na ya Kishari´ah ni Kwake Yeye.

**Hakika Yeye Ataniongoza –** Ataniongoza katika haki na kuniwafikisha nayo kuifuata.

**Na akalifanya neno –** Bi maana kujitenga mbali na kila kinachoabudiwa badala ya Allaah.

**Lenye kubakia katika dhuriya yake –** Bi maana katika kizazi chake.

**Ili wapate kurejea –** Kupata njia ya kurejea kwalo, kutoka katika shirki.

# 51- Tafsiri inayoweka wazi maana ya Shahaadah II

*Na Kauli Yake (Ta´ala):*

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ ۚ فَإِن تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ

*"Sema: "Enyi watu wa Kitabu! Njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu, kwamba tusiabudu isipokuwa Allaah Pekee, wala tusimshirikishe na chochote, wala wasichukue baadhi yetu wengine (kuwa) waungu badala ya Allaah." Wakikengeuka; basi semeni: "Shuhudieni kwamba sisi ni Waislamu." (al-´Imraan 03 : 64)*

**Sema –** Aambiwae hapa ni Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ili ajadiliane na watu wa Kitabu, mayahudi na manaswara.

**Njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu –** Neno hili "kwamba tusiabudu isipokuwa Allaah Pekee na wala tusimshirikishe na chochote na wala tusichukue baadhi yetu wengine (kuwa) waungu badala ya Allaah". Tusiabudu yeyote isipokuwa Allaah, ndio maana ya "hapana mola mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah". "Neno lililo sawa baina yetu na baina yenu" maana yake ni kwamba na sisi pia hali kadhalika.

**Wakikengeuka –** Wakiyapa mgongo yale mliyowaita kwayo.

**Shuhudieni, kwamba ´sisi ni Waislamu´ -** Watangazieni na washuhudisheni ya kwamba nyinyi ni wenye kujisalimisha kwa Allaah na mmejitenga mbali na yale waliyomo na kuipa (kwao) nyongo neno hili likubwa "hapana mola mwenye haki ya kuabudiwa badala ya Allaah".

## 52- Dalili ya kushuhudia kuwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ni Mtume wa Allaah

*Dalili ya kushuhudia ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah, ni Kauli Yake (Ta´ala):*

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

*"Kwa yakini amekujieni Mtume anayetokana na nyinyi wenyewe, ni magumu juu yake (yanamhuzunisha) yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni (kwa kukujalini), mwenye huruma kwa Waumini ni rauwfur-rahiym (mwenye huruma mno - mwenye rehma)." (at-Tawbah 09 : 128)*

**Anayetokana na nyinyi wenyewe –** Bi maana jinsia yenu, bali ni kati yenu nyinyi. Allaah (Ta´ala) Amesema:

هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِن كَانُوا مِن قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ

**"Yeye Ndiye Aliyepeleka Mtume kwa *Al-Ummiyyiyn* (watu wasiojua kusoma wala kuandika) miongoni mwao anawasomea *Aayaat* Zake na Anawatakasa, na Anawafunza Kitabu (Qur-aan) na Hikmah (Sunnah), na japo walikuwa kabla katika upotofu bayana." (al-Jumu´ah 62 : 02)**

**Ni magumu juu yake –** Yale yanayowatia uzito nyinyi, yanamtia uzito yeye.

**Anakuhangaikieni –** Kwa manufaa yenu na kuwazuia na madhara.

**Mwenye huruma kwa Waumini –** Ana huruma na hisia mno kwa waumini. Amelifanya maalum kwa waumini kwa sababu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameamrishwa kuwapiga vita makafiri na wanafiki na kuwa mali kwao. Sifa hizi ambazo amesifiwa nazo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) zinatolea dalili kuonesha ya kwamba ni Mtume wa Allaah wa haki, kama ilivyotolea dalili juu ya hilo Kauli Yake Yake (Ta´ala):

مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ اللَّهِ

**“Muhammad ni Mtume wa Allaah.” (Muhammad 48 : 29)**

Vilevile Kauli Yake (Ta´ala):

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

**“Sema: “Hakika mimi ni Mtume wa Allaah kwenu nyinyi nyote.” (al-A´raaf 07 : 158)**

Aayah kuhusiana na maana hii zinazoonesha ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah wa haki ni nyingi sana.

## 53- Maana ya kwamba Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ni Mtume wa Allaah

*Kushuhudia ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah maana yake ni kumtii katika yale aliyoamrisha, kumsadikisha kwa yale aliyoeleza, kujiepusha yale aliyokataza na kuyakemea na asiabudiwe Allaah isipokuwa kwa yale Aliyoyawekea Shari´ah.*

Maana ya kushuhudia kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah ni kukiri kwa ulimi na kuamini kwa moyo ya kwamba Muhammad bin ´Abdillaah al-Qurashiy al-Haashimiy ni Mtume wa Allaah (´Azza wa Jalla) kwa viumbe vyote, kati ya majini na watu. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

**"Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu." (adh-Dhaariyaat 51 : 56)**

Hata hivyo, hakuna ´ibaadah ilio sahihi kwa Allaah (Ta´ala) ikiwa haiafikiani na Wahyi uliyokuja na Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Amesema (Ta´ala):

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا

**"Amebarikika Yule (Ambaye) Ameteremsha *Al-Furqaan* (Pambanuzi ya haki na batili) kwa mja Wake ili awe muonyaji kwa walimwengu (wote)." (al-Furqaan 25 : 01)**

Ushuhudiaji huu unahitajia kumsadikisha Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa yale aliyoyaeleza, kutekeleza amri zake kwa yale aliyoamrisha, kujiepusha na yale aliyokataza na kuyakemea na asiabudiwe Allaah isipokuwa kwa yale aliyoyawekea Shari´ah. Kitu kingine ushuhudiaji huu unahitajia, ni mtu kutoamini kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ana sehemu ya haki katika uola, kitu katika kuuendesha ulimwengu au sehemu ya haki katika ´ibaadah. Bali (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni mja asiyeabudiwa na ni Mtume asiyekadhibishwa. Hamiliki

chochote, manufaa wala madhara, juu ya nafsi yake yeye wala nafsi ya mtu mwengine isipokuwa kwa yale Anayotaka Allaah. Allaah (Ta´ala) Amesema:

قُل لَّا أَقُولُ لَكُمْ عِندِي خَزَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ الْغَيْبَ وَلَا أَقُولُ لَكُمْ إِنِّي مَلَكٌ ۖ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ

**"Sema: "Sikuambieni kuwa mimi nina hazina ya Allaah; na (sikuambieni) kwamba naelewa (mambo ya) ghayb na wala sikuambieni kuwa mimi ni Malaika. Sifuati ila yale niloletewa *Wahy*"." (al-An´aam 06 : 50)**

# 54- Dalili ya Swalah na Zakaah na na tafsiri ya Tawhiyd

*Dalili ya Swalah na Zakaah na tafsiri ya Tawhiyd, ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ ۚ وَذَٰلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ

*"Na hawakuamrishwa (chochote kile) isipokuwa wamwabudu Allaah kwa kusafisha na kumtakasia Yeye Dini, na wasimamishe Swalaah na watoe Zakaah; na hiyo ndiyo Dini iliyosimama imara." (al-Bayyinah 98 : 05)*

**Dalili ya Swalah na Zakaah –** Bi maana dalili ya kwamba Swalah na Zakaah ni katika Dini:

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ ۚ وَذَٰلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ

**"Na hawakuamrishwa (chochote kile) isipokuwa wamwabudu Allaah kwa kusafisha na kumtakasia Yeye Dini, na wasimamishe Swalaah na watoe Zakaah; na hiyo ndiyo Dini iliyosimama imara." (al-Bayyinah 98 : 05)**

Aayah hii ni jumla na imekusanya aina zote za ´ibaadah. Hivyo ni lazima kwa mwanaadamu amuabudu Allaah (´Azza wa Jalla) kwa kumtakasia ´ibaadah na kufuata Shari´ah Yake.

**Swalah na Zakaah –** Kusimamisha Swalah na kutoa Zakaah ni katika Dini, lakini Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) Amevigusia kutokana na umuhimu wake mkubwa ulionavyo. Swalah ni ´ibaadah ya kimwili, wakati Zakaah ni ´ibaadah ya kimali. Vimetajwa vikiwa sambamba katika Kitabu cha Allaah (´Azza wa Jalla).

**Na hiyo ndio –** Bi maana kumuabudu Allaah Peke Yake kwa kumtakasia Yeye tu Dini, kusimamisha Swalah na kutoa Zakaah.

**Dini iliyosimama –** Hiyo ndio Dini iliyosimama na ya kweli, kwa kuwa ni Dini ya Allaah (´Azza wa Jalla) na Dini ya Allaah ni yenye kunyooka. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَأَنَّ هَٰذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ

**“Na kwamba hii njia Yangu iliyonyooka, basi ifuateni. Na wala msifuate vijia (vinginevyo) vitakufarikisheni na njia Yake.” (al-An´aam 06 : 153)**

Kama jinsi Aayah hii tukufu imetaja ´ibaadah na Swalah na Zakaah, kadhalika imetaja uhakika wa Tawhiyd, nako ni kumwabudu Allaah kwa kumtakasia ´ibaadah Yeye Peke Yake Allaah (´Azza wa Jalla) na kujiweka mbali na shirki. Yule asiyemwabudu Allaah kwa kumtakasia Yeye Dini hazingatiwi kuwa ni mpwekeshaji. Yule mwenye kumfanyia ´ibaadah asiyekuwa Allaah hazingatiwi pia kuwa ni mpwekeshaji.

# 55- Dalili ya Swawm

*Dalili ya Swawm ni Kauli Yake (Ta´ala):*

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

*"Enyi mlioamini! Mmeandikiwa Swawm kama ilivyoandikwa kwa walio kabla yenu mpate kuwa na ucha Mungu." (al-Baqarah 02 : 183)*

Dalili ya kuonesha uwajibu wa Swawm ni Kauli Yake (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

**"Enyi mlioamini! Mmeandikiwa *Swawm* kama ilivyoandikwa kwa walio kabla yenu mpate kuwa na ucha Mungu." (al-Baqarah 02 : 183)**

Katika Kauli Yake "kama ilivyoandikwa kwa wale walio kabla yenu" kuna faida:

**Ya kwanza:** Umuhimu wa Swawm kwa kule Allaah (´Azza wa Jalla) Kuifaradhisha kwa Ummah zilizokuwa kabla yetu. Hii ni dalili inayoonesha mapenzi ya Allaah (´Azza wa Jalla) juu yake na kwamba ni lazima kwa kila Ummah.

**Ya pili:** Uwepesi kwa Ummah huu, kwa kutofaradhishiwa Swawm wao wenyewe, jambo ambalo linaweza kuwa na ugumu kwa nafsi na viwiliwili.

**Ya tatu:** Kuna ishara juu ya kwamba Allaah (Ta´ala) Amekamilisha Dini kwa Ummah huu, wakati Alikamilisha fadhila Zake ambazo wengine walitangulia kuwa nazo.

**Mpate kuwa na ucha Mungu –** Allaah (´Azza wa Jalla) katika Aayah hii Amebainisha hekima ya Swawm:

لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

**"... mpate kuwa na ucha Mungu." (al-Baqarah 02 : 183)**

Maana yake ni kwamba ili mumche Allaah kwa Swawm zenu na yanayopelekea katika kuifikia Taqwa. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameashiria faida hii na kusema:

**"Asiyeacha uongo na kuufanyia kazi, basi Allaah hana haja kwa kuacha chakula na kinywaji chake."**[27]

[27] al-Bukhaariy (1903) na (6057), Abu Daawuud (2362), at-Tirmidhiy (707), Ibn Maajah (1689) na Ahmad (2/354).

# 56- Dalili ya Hajj

*Dalili ya Hajj ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ

*"Na kwa ajili ya Allaah ni wajibu kwa watu watekeleze Hajj katika Nyumba hiyo kwa mwenye uwezo. Na atakayekanusha, basi hakika Allaah ni* Ghaniyy *(Mkwasi) kwa walimwengu." (al-´Imraan 03 : 97)*

Dalili ya kuonesha kuwa ni wajibu ni Kauli Yake (Ta´ala):

وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ

**"Na kwa ajili ya Allaah ni wajibu kwa watu watekeleze Hajj katika Nyumba hiyo... " (al-´Imraan 03 : 97)**

Aayah hii iliteremka mwaka wa tisa baada ya Hijrah na hapo ndipo Hajj ilifaradhishwa. Hata hivyo Allaah (´Azza wa Jalla) Anasema:

مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا

**"... kwa mwenye uwezo." (al-´Imraan 03 : 97)**

Hapa kuna dalili kuwa yule asiyekuwa na uwezo wa kuitekeleza haimuwajibikii.

وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ

**"Na atakayekanusha, basi hakika Allaah ni *Ghaniyy* (Mkwasi) kwa walimwengu." (al-´Imraan 03 : 97)**

Hapa kuna dalili ya kuwa ni kufuru kwa yule mwenye uwezo. Hata hivyo ni kufuru isiyomtoa mtu katika Uislamu kwa mujibu wa kauli ya wanachuoni wengi. ´Abdullaah bin Shaqiyq amesema:

**"Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakuna kitu katika matendo walikuwa wakionelea kukiacha ni kufuru isipokuwa Swalah."**[28]

[28] at-Tirmidhiy (2757). al-Albaaniy amesema:

"Swahiyh." (Swahiyh Sunan at-Tirmidhiy (3/44))

## 57- Daraja za Imani

*Daraja ya pili ni Imani na imegawanyika zaidi ya sehemu sabini. Ya juu yake ni neno "hapana mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah" na ya chini yake ni kuondosha kitu chenye kudhuru katika njia. Hayaa ni sehemu katika imani.*

**Daraja ya pili –** Yaani katika daraja za Dini.

**Imani –** Imani kilugha ni "kusadikisha". Kishari´ah ni "kuamini ndani ya moyo, kutamka kwa ulimi na kutenda kwa viungo vya mwili". Imegawanyika zaidi ya tanzu sabini.

**Zaidi –** Ni idadi kutoka tatu mpaka tisa.

**Sehemu –** Ni sehemu ya kitu.

**Kuondosha kitu chenye kudhuru katika njia –** Bi maana kuondosha kitu chenye kudhuru ambacho kinawadhuru wapitaji. Kwa mfano mawe, miba, uchafu, taka, vitu vyenye harufu mbaya na mfano wa hayo.

**Hayaa –** Kukereketa ambako kunatokea wakati wa aibu na kunamzuia mtu na kufanya kitu ambacho kinaenda kinyume na murua.

Maneno ya mwandishi (Rahimahu Allaah) kuhusiana na kwamba imani ni zaidi ya sehemu sabini na kuwa imani nguzo zake ni sita, yanajumuishwa ifuatavyo:

Imani ambayo ni ´Aqiydah misingi yake ni sita na ndio ile iliyotajwa katika Hadiyth ya Jibriyl (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) wakati Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipomuuliza juu yake. Akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake na siku ya Mwisho na kuamini Qadar; kheri na shari yake."**

Ama kuhusiana na imani ambayo imekusanya ndani yake matendo na aina na jinsi yake, ni zaidi ya sehemu sabini. Kwa ajili hii ndio maana Allaah (Ta´ala) Ameiita Swalah kuwa ni "Imani":

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ

**"Na Allaah Hakuwa Mwenye kupoteza *iymaan* zenu, hakika Allaah kwa watu ni *Rauwfur-Rahiym* (Mwenye huruma mno - Mwenye kurehemu)." (al-Baqarah 02 : 143)**

Wafasiri wa Qur-aan wamefasiri "Imani zenu" yaani "Swalah zenu kuelekea Jerusalemu". Kwa kuwa Maswahabah kabla ya kuamrishwa kuelekea Ka´bah, walikuwa wakiswali kwa kuelekea Jerusalemu.

## 58- Kumuamini Allaah

*Nguzo zake ni sita: Kumuamini Allaah...*

Kumuamini Allaah ndani yake kuna mambo mane:

**La kwanza –** Kuamini kuwepo kwa Allaah. Mambo yanayotolea dalili ya kuthibitisha uwepo wa Allaah ni vitu vine:

1. Maumbile.

2. Akili.

3. Shari´ah.

4. Hisia.

**Kuhusiana na dalili za kimaumbile**, zinathibitisha kuwepo Kwake kwa njia ifuatayo:

Kila kiumbe ameumbwa kwa umbile la kumuamini Mola Wake, pasina kutanguliwa na kufikiri au kujifunza. Hakuna mwingine isipokuwa yule tu mwenye kupata kitu katika upotevu ndani ya moyo wake ndio huenda kinyume na maumbile haya. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Hakuna mtoto yoyote isipokuwa huzaliwa juu ya maumbile. Baadaye ni wazazi wake ndio humfanya kuwa myahudi, mnaswara au mwabudu moto."**[29]

**Ama kuhusiana na dalili ya kiakili inayothibitisha kuwepo kwa Allaah (Ta´ala)**, ni jambo lenye kujulikana kwamba viumbe vyote vilivyotangulia na kuja nyuma ni lazima viwe na Muumbaji. Haiwezekani kitu kikajileta chenyewe. Wala haiwezekani pia ikawa vimejileta patupu.

Ni jambo lisilowezekana kitu kikajileta chenyewe, kwa kuwa hakuna kitu kinachoweza kujiumba chenyewe. Vipi kitu ambacho hakikuwepo kiumbe?

[29] al-Bukhaariy (1358) na (1359), Muslim (2658) na Ahmad (2/315).

Vilevile hakuna kitu chochote kinachoweza kujileta patupu. Kila chenye kutokea ni lazima kiwe na mtu mwenye kukileta. Uwepo wake katika nidhamu hii ya kiajabu, mfumo huu wa kuambatana na mafungamano ya kisawasawa, ni dalili inayoonesha kuwa ni jambo lisilowezekana ikawa ni kitu cha patupu. Kwa sababu kitu kilichokuja ghafla patupu hakiwi hata na uwepo wake katika nidhamu, tusemeje juu ya kubaki kwake na maendeleo yake.

Ikiwa viumbe hivi haviwezi kuwa vimejileta vyenyewe wala kupatikana patupu, inalazimisha kuwa ni lazima viwe na Muumbaji Wake, na si mwingine isipokuwa ni Allaah, Mola wa walimwengu.

Allaah (Ta´ala) Ametaja dalili hii ya kiakili na hoja za kimaumbile katika Suurat-utw-Twuur". Amesema:

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ

**"Au wameumbwa pasipo na kitu chochote, au wao (wenyewe) ndio waumbaji?" (atw-Twuur 52 : 35)**

Ina maana ya kwamba hawakuumbwa pasina Muumba na wala sio wao wenyewe waliojiumba. Hili linawajibisha ya kwamba Allaah (Tabaaraka wa Ta´ala) ndio Muumbaji wao. Kwa ajili hii Jubayr bin Mutw´im (Radhiya Allaahu ´anhu) alisema pindi alipomsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akisoma Suurat-utw-Twuur na akafikia Aayah hii:

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ أَمْ خَلَقُوا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ ۚ بَل لَّا يُوقِنُونَ أَمْ عِندَهُمْ خَزَائِنُ رَبِّكَ أَمْ هُمُ الْمُصَيْطِرُونَ

**"Au wameumbwa pasipo na kitu chochote, au wao (wenyewe) ndio waumbaji? Au wameumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini. Au wanazo hazina za Mola wako, au wao ndio wenye mamlaka (nayo)?" (atw-Twuur 52 : 35-37)**

**"Moyo wangu ulikaribia kuruka. Hapo ndio ilikuwa mara ya kwanza kuingiwa na imani kwenye moyo wangu."**[30]

Wakati huo Jubayr alikuwa bado ni mshirikina.

Imepokelewa na al-Bukhaariy.

[30] al-Bukhaariy (4854).

Hebu tupige mfano. Lau mtu atakueleza kuhusu palasi ndefu lililojengwa na limezungukwa na mabustani na ambalo mito inapita kati yake. Limejazwa magodoro na vitanda na limepambwa kwa kila aina ya mapambo. Baada ya hapo mtu huyu akakwambia ya kwamba palasi hii na yote yaliyo ndani yake vimejileta vyenyewe au vimetoka patupu, papo hapo ungelikanusha hilo, kumkadhibisha na kuchukulia maneno yake hayana maana yoyote. Je, inawezekanaje kwa ulimwengu huu mpana kwa ardhi zake, mbingu zake, nyota zake na nidhamu zake na hali zake zenye kusifika iwe kwamba umejileta wenyewe au patupu na pasina Muumbaji?

**Ama kuhusiana na dalili za Kishari´ah zenye kuthibitisha kuwepo kwa Allaah**, yapo katika Vitabu vyote vilivyoteremshwa. Vyote hivo na hukumu ilizonavyo zilizo na manufaa kwa viumbe ni dalili inayoonesha kuwa zinatoka kwa Mola wa hekima ambaye ni mjuzi wa viumbe Wake. Khabari juu ya viumbe zimetolea ushahidi na uhakika wa mambo yalivo leo, jambo ambalo linatolea dalili kuonesha kuwa ni kutoka kwa Mola ambaye ni Muweza wa kuumba yale aliyoyatolea khabari.

**Ama dalili za kihisia zenye kuthibitisha kuwepo kwa Allaah**, ni kwa njia mbili:

**Ya kwanza:** Sisi tunasikia na tunaona jinsi zinavojibiwa Du´aa za wenye kuomba na wenye shida wanavosaidiwa. Hii ni dalili ya wazi ya kuonesha uwepo kwa Allaah (Ta´ala). Amesema:

وَنُوحًا إِذْ نَادَىٰ مِن قَبْلُ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ

**"Na Nuwh alipoita kabla (kutuomba); Tukamuitikia." (al-Anbiyaa 21 : 76)**

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ

**"Na (kumbukeni) pale mlipomuomba uokozi Mola wenu Naye Akakujibuni." (al-Anfaal 08 : 09)**

Katika "Swahiyh al-Bukhaariy" imepokelewa kutoka kwa Anas bin Maalik (Radhiya Allaahu ´anhu) ambaye amesema:

**"Kuna bedui mmoja aliingia siku ya Ijumaa na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) yuko anatoa Khutbah na akasema: "Ee Mtume wa Allaah! Mali zimeangamia na familia zimekuwa na**

**njaa. Tuombee kwa Allaah." Akanyanyua mikono yake na akaomba. Ghafla mawingu yajikusanya kama mfano wa jibali. Hakuwahi kuteremka kwenye minbari yake, kabla ya mvua kuteremka kwenye ndevu zake. Katika Ijumaa ya pili akaja bedui yule yule, au mwingine, na kusema: "Ee Mtume wa Allaah! Nyumba zimebomoka na mali imeangamia. Tuombee kwa Allaah." Akanyanyua mikono yake na kuomba: "Ee Allaah! Pembezoni mwetu na si juu yetu!" Hakuashiria katika upande wowote, isipokuwa kulisita."**[31]

Mpaka hivi leo kujibiwa Du´aa za wenye kuomba ni jambo linaloshuhudiwa kwa yule mwenye kurejea kwa Allaah (Ta´ala) kikweli na akatimiza masharti ya kujibiwa.

**Ya pili:** Alama za Mitume, ambazo zinaitwa pia "miujiza", ambazo watu wameziona na kuzisikia, ni dalili za wazi kwamba Yuko Yule Aliyewatuma. Na ni Allaah (Ta´ala). Mambo haya ni yenye kutoka nje ya uwezo wa mwanaadamu. Allaah (Ta´ala) Anayapitisha ili kuwapa nguvu na nusura Mitume Wake.

Mfano wa hilo ni miujiza ya Muusa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Allaah (Ta´ala) Alimuamrisha kupiga fimbo yake kwenye bahari. Wakati alipofanya hivo, bahari ikagawanyika njia kumi na mbili na maji kati yakawa kama mfano wa kuta. Allaah (Ta´ala) Amesema:

فَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنِ اضْرِب بِّعَصَاكَ الْبَحْرَ ۖ فَانفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرْقٍ كَالطَّوْدِ الْعَظِيمِ

**"Tukampelekea *Wahy* Muwsaa kwamba: "Piga kwa fimbo yako (hiyo) bahari." Basi ikatengana ikawa kila sehemu (ya maji ya bahari) kama jabali kubwa mno." (ash-Shu´araa 26 : 63)**

Mfano wa pili ni miujiza ya ´Iysaa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Alikuwa akiwahuisha maiti na akiwatoa kwenye makaburi yao kwa idhini ya Allaah. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَأُحْيِي الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِ اللَّهِ

**"Na nahuisha maiti kwa Idhini ya Allaah." (al-´Imraan 03 : 49)**

[31] al-Bukhaariy (1016) na Muslim (897).

وَإِذْ تُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِي

**"... na ulipowatoa maiti (kutoka makaburini mwao) kwa idhini Yangu." (al-Maaidah 05 : 110)**

Mfano wa tatu ni miujiza ya Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wakati Quraysh walipomtaka aoneshe alama, akaashiria mwezi na ukagawanyika sehemu mbili. Haya yalionwa na watu. Kuhusiana na hilo Amesema (Ta´ala):

اقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَانشَقَّ الْقَمَرُ وَإِن يَرَوْا آيَةً يُعْرِضُوا وَيَقُولُوا سِحْرٌ مُّسْتَمِرٌّ

**"Saa (Qiyaamah) imekaribia na mwezi umekatika. Na wanapoona *Aayah* hukengeuka na husema: "Uchawi unaoendelea" (al-Qamar 54 : 01-02)**

Alama hizi za kihisia ambazo Allaah (Ta´ala) Huzipitisha ili kuwapa nguvu na nusura Mitume Wake, ni dalili ya wazi juu ya uwepo Wake (Ta´ala).

**Ya pili –** Kuamini uola Wake. Hii ina maana kuamini ya kwamba Yeye ndiye Mola Pekee asiyekuwa na mshirika wala msaidizi.

Mola ni Yule mwenye kuendesha viumbe, ufalme na amri. Hakuna Muumbaji mwingine asiyekuwaiAllaah. Hakuna mfalme mwingine isipokuwa Yeye. Hakuna mwamrishaji isipokuwa Allaah. Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ

**"Tanabahi! Ni Vyake Pekee Uumbaji na Amri." (al-A´raaf 07 : 54)**

ذَٰلِكُمُ اللَّهُ رَبُّكُمْ لَهُ الْمُلْكُ ۚ وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ

**"Huyo (basi) Ndiye Allaah Mola wenu, ufalme ni Wake Pekee. Na wale mnaowaomba badala Yake hawamiliki (hata) kijiwavu cha kokwa ya tende." (Faatwir 35 : 13)**

Haijulikani kwamba kuna kiumbe yeyote aliyekanusha uola wa Allaah (Subhaanahu). Isipokuwa mtu mkaidi tu asiyeamini ayasemayo. Kama ilivompitikia Fir´awn. Aliwaambia watu wake:

أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَىٰ

**"Mimi ni mola wenu mkuu." (an-Naazi´aat 79 : 24)**

يَا أَيُّهَا الْمَلَأُ مَا عَلِمْتُ لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرِي

**"Enyi wakuu! Sijui kama mnaye mungu badala yangu." (al-Qaswasw 28 : 38)**

Hata hivyo hakuwa ni mwenye kuamini hilo. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا

**"Wakazikanusha na hali kuwa nafsi zao zimeziyakinisha; kwa dhulma na majivuno." (an-Naml 27 : 14)**

Allaah Ameeleza kuwa Muusa alisema kumwambia Fir´awn:

لَقَدْ عَلِمْتَ مَا أَنزَلَ هَٰؤُلَاءِ إِلَّا رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ بَصَائِرَ وَإِنِّي لَأَظُنُّكَ يَا فِرْعَوْنُ مَثْبُورًا

**"Kwa yakini umekwishajua kwamba hakuna Aliyeteremsha haya isipokuwa Mola wa mbingu na ardhi kuwa ni dalili za kuonekana dhahiri, na hakika mimi nakuona ewe Fir'awn kuwa ni mwenye kuangamizwa." (al-Israa´ 17 : 102)**

Kwa ajili hii washirikina walikuwa wakikubali uola wa Allaah (Ta´ala), pamoja na kuabudu wengine asiyekuwa Yeye. Allaah (Ta´ala) Amesema:

قُل لِّمَنِ الْأَرْضُ وَمَن فِيهَا إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ سَيَقُولُونَ لِلَّهِ ۚ قُلْ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ قُلْ مَن رَّبُّ السَّمَاوَاتِ السَّبْعِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ يَقُولُونَ لِلَّهِ ۚ قُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ قُلْ مَن بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ يُجِيرُ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ سَيَقُولُونَ لِلَّهِ ۚ قُلْ فَأَنَّىٰ تُسْحَرُونَ

**"Sema: "Ni ya nani ardhi na wale waliokuwemo humo, mkiwa mnaelewa?" Watasema: "Ni ya Allaah Pekee" Sema: "Je, basi hamkumbuki" (mkawaidhika)? Sema: "Nani Mola wa mbingu saba na Mola wa *'Arsh*i tukufu?" Watesema: "Ni ya Allaah Pekee" Sema: "Je, basi kwa nini hamwogopi? Sema: "Nani katika mikono Yake uko ufalme wa kila kitu, Naye Ndiye Alindae na wala**

**hakilindwi chochote dhidi Yake, ikiwa mnaelewa?" Watasema: "Ni Allaah Pekee" Sema: "Basi vipi mnazugwa (akili zenu kukanusha haki)?" (al-Muuminuun 23 : 84-89)**

وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ خَلَقَهُنَّ الْعَزِيزُ الْعَلِيمُ

**"Na ukiwauliza: "Ni nani yule aliyeumba mbingu na ardhi?" Bila shaka watasema: "Ameziumba *Al-Aziyzul-'Aliym* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima - Mjuzi wa yote daima)." az-Zukhruf 43 : 09)**

Amri ya Mola (Subhaanahu) imeyazunguka mambo ya kilimwengu na ya Kishari´ah. Kama jinsi Yeye ndiye mwenye kuendesha ulimwengu na anahukumu ndani yake kwa lile Analolitaka kwa mujibu wa Hekima Yake, kadhalika Yeye ndiye mwenye kuhukumu kwa Shari´ah ya ´ibaadah na hukumu za mu´amala [maisha ya kijamii] kwa mujibu wa Hekima Yake. Yule mwenye kufanya mtunga Shari´ah mwingine katika ´ibaadah badala ya Allaah, au hakimu mwingine katika mambo ya mu´amala badala ya Allaah, atakuwa amemshirikisha na hakuhakikisha imani.

**Ya tatu:** Kuamini uungu wa Allaah. Hii ina maana ya kwamba Yeye ndiye *Ilaah,* Mungu wa haki mmoja asiyekuwa na mshirika. "Mungu" ni yule mwenye kuabudiwa kwa mapenzi na kuadhimishwa. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَإِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ ۖ لَّا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَٰنُ الرَّحِيمُ

**"Na *Ilaah* wenu (Mungu Anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ni *Ilaahun-Waahid* (Mungu Mmmoja) hapana *ilaaha* ila Yeye. (*Ar-Rahmaanur-Rahiym* (Mwingi wa Rahmah - Mwenye kurehemu)." (al-Baqarah 02 : 163)**

شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ ۚ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

**"Allaah Ameshuhudia kwamba hapana ilaaha (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ila Yeye, Malaika na wenye elimu (wote wameshuhudia kwamba Yeye) ni Mwenye kusimamisha (uumbaji Wake) kwa uadilifu. Hapana mungu wa haki ila Yeye Al-'Aziyzul-Hakiym (Mwenye enzi ya**

**nguvu Asiyeshindika daima - Mwenye hikmah wa yote daima)." (al-´Imraan 03 : 18)**

Kila kinachoabudiwa nafasi ya Allaah ni batili. Allaah (Ta´ala) Amesema:

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ هُوَ الْبَاطِلُ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

**"Hivyo ni kwa kuwa Allaah Ndiye *Al-Haqq* (Mungu wa kweli Anayestahiki kuabudiwa), na kwamba vile wanavyoomba (makafiri) badala Yake ndiyo batili; na kwamba Allaah Ndiye *Al-'Aliyyul-Kabiyr* (Mwenye 'Uluwa Yuko juu ya vyote - Mkubwa wa dhati, vitendo na sifa)." (al-Hajj 22 : 62)**

Kule kuitwa kwao "miungu", haina maana wana haki ya kuabudiwa. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu al-Laat, al-´Uzzaa na Manaat:

إِنْ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمَّيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَآبَاؤُكُم مَّا أَنزَلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطَانٍ

**"Hayo si chochote isipokuwa ni majina mmeyaita (hayo masanamu) nyinyi na baba zenu, wala Allaah Hakuyateremshia madaraka yoyote." (an-Najm 53 : 23)**

Ameeleza kuwa Huud amesema kuwaambia watu wake:

أَتُجَادِلُونَنِي فِي أَسْمَاءٍ سَمَّيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَآبَاؤُكُم مَّا نَزَّلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطَانٍ

**"Je, mnanijadili katika majina mliyoyaita (masanamu) nyinyi na baba zenu (ambayo) Allaah Hakuyateremshia kwayo dalili?" (al-A´raaf 07 : 71)**

Ameeleza kuwa Yuusuf amesema kuwaambia maswahibu zake:

أَأَرْبَابٌ مُّتَفَرِّقُونَ خَيْرٌ أَمِ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ مَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِهِ إِلَّا أَسْمَاءً سَمَّيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَآبَاؤُكُم مَّا أَنزَلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطَانٍ

**"Je, waungu wengi wanaofarikiana ni bora (kuabudiwa) au Allaah (ambaye ni) *Al-Waahidul-Qahhaar* (Mmoja Pekee - Mshindi Mwenye kudhibiti na kudhalilisha."). Hamuabudu pasi Naye (Allaah) isipokuwa majina (ya masanamu) mmeyaita nyinyi**

**na baba zenu, Hakuyateremshia Allaah kwayo mamlaka (amri) yoyote." (Yuusuf 12 : 39-40)**

Kwa ajili hii Mitume (´alayhim-us-Swalaat was-Salaam) walikuwa wakiwaambia watu wao:

يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُ

**"Enyi watu wangu! Mwabuduni Allaah (kwani nyinyi) hamna *ilaah* (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) badala Yake." (al-A´raaf 07 : 59)**

Hili washirikina walikataa kulifanya. Badala yake wakaabudu wengine badala ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) na kuwaomba nusura na msaada. Allaah (Ta´ala) Amebatilisha shirki ya washirikina kwa aina ya dalili mbili za kiakili:

**Ya kwanza:** Hakuna yeyote katika miungu hii ambaye ana kitu katika sifa ya kiungu. Imeumbwa na haiumbi. Haiwezi kuwaletea manufaa wale wenye kuiabudu na haiwezi kuwazuia na madhara. Haimiliki juu yao uhai wala mauti. Haimiliki kitu katika mbingu na wala hawana ushirika wowote. Allaah (Ta´ala) Amesema

وَاتَّخَذُوا مِن دُونِهِ آلِهَةً لَّا يَخْلُقُونَ شَيْئًا وَهُمْ يُخْلَقُونَ وَلَا يَمْلِكُونَ لِأَنفُسِهِمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا وَلَا يَمْلِكُونَ مَوْتًا وَلَا حَيَاةً وَلَا نُشُورًا

**"Na wakachukua pasi Naye (Allaah) miungu (ambayo) haiumbi chochote na hali wao wanaumbwa wala hawamiliki kwa ajili ya nafsi zao (kujiondoshea) dhara wala (kujipatia) manufaa wala hawamiliki (kufisha) mauti wala (kutoa) uhai wala kufufuliwa." (al-Furqaan 25 : 03)**

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُم مِّن دُونِ اللَّهِ ۖ لَا يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ وَمَا لَهُمْ فِيهِمَا مِن شِرْكٍ وَمَا لَهُ مِنْهُم مِّن ظَهِيرٍ وَلَا تَنفَعُ الشَّفَاعَةُ عِندَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ

**"Sema: "Ombeni wale mnaodai (kuwa ni miungu) badala ya Allaah, hawamiliki uzito wa atomu (au sisimizi) mbinguni wala ardhini, na wala (wao) hawana humo ushirika (Naye), na wala (Allaah) Hana msaidizi miongoni mwao." Na wala haitofaa *ash-shafaa'ah* (uombezi) mbele Yake isipokuwa kwa yule Aliyempa**

**idhini." (Sabaa´ 34 : 22-23)**

أَيُشْرِكُونَ مَا لَا يَخْلُقُ شَيْئًا وَهُمْ يُخْلَقُونَ وَلَا يَسْتَطِيعُونَ لَهُمْ نَصْرًا وَلَا أَنفُسَهُمْ يَنصُرُونَ

**"Je, wanawashirikisha (na Allaah) wale ambao hawaumbi kitu na hali wao wameumbwa? Na wala hawawezi kuwanusuru na wala hawawezi kujinusuru nafsi zao." (al-A´raaf 07 : 191-192)**

Ikiwa hali ya miungu ni kama hii, ni upumbavu mkubwa na batili kubwa kuiabudu.

**Ya pili:** Washirikina hawa walikuwa wakikubali kwamba Allaah (Ta´ala) Peke Yake ndio Mola na Muumba ambaye Mikononi Mwake ndio mna ufalme wa kila kitu na ndiye mwenye kulinda na hakuna yeyote anayeweza kumlinda. Hili linalazimisha kwa wao kumuabudu Yeye Pekee kama jinsi walivokuwa wakionelea kuwa ni Mmoja katika uola. Amesema (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۖ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

**"Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu Ambae Amekuumbeni na wale wa kabla yenu mpate kuwa na ucha Mungu. Ambaye Amewafanyieni ardhi kuwa ni tandiko na mbingu kuwa ni paa, na Akateremsha kutoka mbinguni maji, Akawatolea kwayo matunda kuwa ni riziki zenu. Basi msimuwekee Allaah waliolingana naye (washirika) na hali ya kuwa nyinyi mnajua (kuwa Allaah Hana Anayelingana nae)." (al-Baqarah 02 : 21-22)**

وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ ۖ فَأَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ

**"Na ukiwauliza: Ni nani kawaumba? Bila shaka watasema: "Allaah." Basi vipi mnageuzwa (mbali na kumwabudu Allaah Pekee bila ya kumshirikisha)?" (az-Zukhruf 43 : 87)**

قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ وَمَن يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَن يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۚ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ ۚ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ فَذَٰلِكُمُ اللَّهُ رَبُّكُمُ الْحَقُّ ۖ فَمَاذَا بَعْدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ ۖ فَأَنَّىٰ تُصْرَفُونَ

**“Sema: “Nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini. Au nani anayemiliki kusikia na kuona; na nani anayemtoa (aliye) hai kutoka maiti, na anayemtoa maiti kutoka (aliye) uhai; na nani anayeendesha mambo (yote)? Watasema: “Ni Allaah”; basi sema: “Je, basi kwa nini hamchi?” Basi Huyo Ndiye Allaah, Mola wenu wa haki. Na kuna nini baada ya haki ila upotofu? Basi vipi mnageuzwa (kutoka kumwabudu Yeye kuelekea kumwabudu mwengine)?” (Yuunus 10 : 31-32)**

**Ya nne –** Kuamini Majina na Sifa Zake. Hii ina maana ya mtu kuthibitisha Majina na Sifa ambazo Allaah Amejithibitishia Yeye Mwenyewe katika Kitabu Chake au Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa njia inayolingana na Yeye. Hivyo Majina na Sifa hizi zifahamike pasina *Tahriyf, Ta´twiyl, Takyiyf* na *Tamthiyl.* Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا ۖ وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ ۚ سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

**”Na Allaah Ana Majina Mazuri kabisa, basi muombeni kwayo. Na waacheni wale wanaopotoa katika Majina Yake, watalipwa yale waliyokuwa wakiyatenda.” (al-A´raaf 07 : 180)**

وَلَهُ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

**“Naye Ana mifano ya juu katika mbingu na ardhi. Naye Ndiye *Al-’Aziyzul-Hakiym* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima - Mwenye hikmah wa yote daima).” (ar-Ruum 30 : 27)**

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**“Hakuna chochote kinachofanana Naye, Naye Ndiye *As-Samiy’ul-Baswiyr* (Mwenye kusikia yote daima, Mwenye kuona yote daima).” (ash-Shuuraa 42 : 11)**

Katika suala hili makundi mawili yamepotoka:

**Kundi la kwanza:** Mu´attwilah. Wanakanusha ima Majina na Sifa zote au baadhi yake. Wanadai kuwa kule kuyathibitisha kunalazimisha kumfananisha Allaah (Ta´ala) na viumbe Wake. Madai haya sio ya kweli kwa njia nyingi:

**Ya kwanza:** Nadharia yao inalazimisha malazimisho ya batili. Moja ya batili hii ni kugongana kwa Maneno ya Allaah (Subhaanahu). Allaah (Ta´ala) Amejithibitishia Yeye Mwenyewe Majina na Sifa kama jinsi Amekanusha kuwepo kwa kitu kinachofanana na Yeye. Lau kuthibitisha Majina na Sifa kungelikuwa kunalazimisha kumfananisha Allaah na viumbe, kungelilazimisha vilevile kuwepo mgongano katika Maneno ya Allaah na baadhi yakakadhibisha mengine.

**Ya pili:** Vitu viwili kuafikiana katika majina na sifa hakulazimishi viwe vinafanana. Mfano wa hilo ni watu wawili. Wote ni wanaadamu wanaosikia, wanaona na kuzungumza. Hata hivyo hilo halilazimishi kwamba wanafanana katika maana ya ubinaadamu, usikizi, uoni na maneno. Mfano mwingine ni minyama. Wana mikono, miguu na macho. Lakini pamoja na hivyo haina maana mikono yao, miguu yao na macho yao vinafanana. Ikiwa tofauti kati ya viumbe, ambao wana majina na sifa moja, iko wazi na bainifu, basi tofauti kati ya Muumba na viumbe iko wazi na bainifu zaidi.

**Kundi la pili:** Mushabbihah. Wamethibitisha Majina na Sifa pamoja na kumfananisha Allaah (Ta´ala) na viumbe Wake. Wanadai kuwa nadharia yao ndio inaendana na maandiko, kwa kuwa Allaah (Ta´ala) Amewazungumzisha waja tu kwa njia ile wanayoifahamu. Madai haya ni batili kwa njia nyingi:

**Ya kwanza:** Kumfananisha Allaah (Ta´ala) na viumbe Wake ni jambo la batili ambalo linakataliwa na akili na Shari´ah. Haiwezekani maandiko ya Kitabu na Sunnah kupelekea katika kitu batili.

**Ya pili:** Ni kweli kwamba Allaah (Ta´ala) Amewazungumzisha waja kwa njia ile wanayoifahamu, lakini hili linahusiana tu na msingi wa maana ya Dhati na Sifa Zake. Ama kuhusiana na uhakika wake na namna yake ambayo inaashiria maana hiyo, ni katika Elimu ya Allaah (Ta´ala) ambayo Anaijua Yeye Mwenyewe na hakuna mwingine yeyoye anayeijua.

Allaah Akijithibitishia juu ya Nafsi Yake kwamba ni Mwenye kusikia, Usikizi huu unajulikana tu kutokana na asli ya maana, nako ni "kufikia sauti". Lakini hata hivyo namna ya Usikizi wa Allaah (Ta´ala) haujulikani. Hata baina ya viumbe kuna tofauti kati ya namna ya usikizi wao, basi kunapatikana tofauti kubwa kati ya Muumba na viumbe.

Allaah (Ta´ala) Anapojielezea Mwenyewe kwamba Amelingana juu ya ´Arshiy, maana ya kulingana inajulikana kutokamana na asli ya maana. Lakini hata hivyo kulingana kwa Allaah juu ya ´Arshiy hakujulikani kuhusiana na namna. Namna ya kulingana kwa viumbe kunatofautiana kwa kiumbe huyu

na huyu. Kulingana (kuwa juu) ya kiti sio kama kulingana juu ya ngamia mwenye ugumu wa kuondoka. Kukibainika tofauti hii kati ya viumbe, basi tofauti ni kubwa zaidi kati ya Muumba na viumbe.

Kumuamini Allaah (Ta´ala) kutokana na yale tuliyoyataja kunampa muumini matunda yafuatayo:

**Ya kwanza:** Kumuabudu Allaah (Ta´ala) Peke Yake kwa njia ya kwamba mtu haweki matumaini yake kwa mwingine asiyekuwa Allaah, kumuogopa mwingine asiyekuwa Allaah, kumuabudu mwingine asiyekuwa Allaah na kadhalika.

**Ya pili:** Kukamilika kwa mapenzi ya kumpenda Allaah (Ta´ala) na kumuadhimisha kutokamana na Majina Yake Mazuri na Sifa Zake kuu.

**Ya tatu:** Kumuabudu Allaah Peke Yake kwa kutekeleza maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake.

# 59- Kuamini Malaika

*... Malaika Wake...*

Malaika ni viumbe visivyoonekana wanaomuabudu Allaah (Ta´ala). Hawana kitu chochote katika uola wala uungu. Allaah (Ta´ala) Amewaumba kwa nuru. Akawapa unyenyekevu mkamilifu kwa maamrisho Yake pamoja na nguvu za kuyatekeleza. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَمَنْ عِندَهُ لَا يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِ وَلَا يَسْتَحْسِرُونَ يُسَبِّحُونَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لَا يَفْتُرُونَ

**"Na wale walio Kwake (Malaika) hawatakabari na 'ibaadah Yake na wala hawachoki. Wanasabihi usiku na mchana, wala hawazembei." (al-Anbiyaa 21 : 19-20)**

Wako katika idadi kubwa na hakuna anayeijua isipokuwa Allaah (Ta´ala) tu. Imethibiti katika "Swahiyh mbili" kutoka katika Hadiyth ya Anas (Radhiya Allaahu ´anhu) kuhusiana na kisa cha Mi´raaj:

**"Nyumba iliyojaa ilinyanyuliwa kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ndani yake kila siku wanaswali Malaika 70.000. Pindi wanapotoka, hawarudi tena."**[32]

Kuamini Malaika kunakusanya mambo mane:

**La kwanza:** Kuamini kuwepo kwao.

**La pili:** Kuamini wale tunaowajua kwa majina yao. Kwa mfano wa Jibriyl. Kuhusiana na wale tusiowajua, tunawaamini kwa ujumla.

**La tatu:** Kuamini sifa zao tunazozijua. Kwa mfano sifa ya Jibriyl. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameeleza ya kwamba amemuona katika umbile lake la kihakika na alikuwa na mbawa mia sita zinazofunika ukingo.

Kutokana na amri ya Allaah Malaika anaweza kujigeuza katika umbile la mtu. Mfano wa hilo ni pale ambapo Alimtuma (Ta´ala) Jibriyl kwa Maryam katika

[32] al-Bukhaariy (3207), Muslim (259) na an-Nasaa'iy (447).

umbile la mtu mkamilifu. Mfano mwingine ni pale alipoenda kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hali ya kuwa alikuwa amekaa na Maswahabah zake. Alikuja katika umbile la mtu ambaye alikuwa amevaa mavazi meupe mno na nywele nyeusi mno. Hakuna kilichokuwa kinaashiria kuwa alikuwa ni msafiri na hakuna yeyote katika Maswahabah aliyekuwa akimjua. Akakaa kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na akaweka magoti yake karibu na magoti yake na akaweka vitanga vyake juu ya mapaja yake. Halafu akamuuliza Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuhusu Uislamu, Imani na Ihsaan, Qiyaamah na alama zake. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamjibu na kisha akaenda. Baada ya hapo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema:

**"Ilikuwa ni Jibriyl amewajia ili akufunzeni Dini yenu."**[33]

Imepokelewa na Muslim.

Kadhalika inahusiana na Malaika ambao walitumwa na Allaah (Ta´ala) kwa Ibraahiym na Luutw. Na wao pia walikuwa katika umbile la wanaume.

**Ya nne:** Kaumini kazi zao tunazozijua. Kazi hizi wanazifanya kwa maamrisho ya Allaah (Ta´ala). Mfano wa hayo ni kwamba wanamsibihi na wanamuabudu usiku na mchana pasina uvivu wala kuchoka. Baadhi yao wana kazi maalum tu.

Kazi ya Jibriyl mwaminifu ni kufikisha Wahyi wa Allaah (Ta´ala) kwa Manabii na Mitume.

Kazi ya Mikaaiyl amewakilishwa kwa ajili ya mvua na uoto.

Kazi ya Israafiyl amewakilishwa kupuliza parapanda wakati Qiyaamah kitaposimama na kufufuliwa.

Kazi ya Malaika wa mauti amewakilishwa kutoa roho wakati wa kufa.

Kazi ya Maalik amewakilishwa kuchunga Moto.

Kuna Malaika pia ambao wamewakilishwa kuwahudumia watoto waliomo kwenye matumbo. Mtoto anapofikisha miezi mine tumboni mwa mama yake, Allaah Humtumia Malaika na kumuamrisha kuandika riziki yake, umri wake, matendo yake na kama mtoto atakuja kupata mwisho usiokuwa na furaha au wa furaha.

[33] Muslim (08).

Kuna Malaika ambao kazi yao wamewakilishwa kuyadhibiti na kuyaandika matendo ya mwanaadamu. Ni Malaika wawili; mmoja yuko kuliani na mwingine kushotoni.

Kuna Malaika ambao kazi yao wamewakilishwa kumhoji maiti. Pindi anapowekwa maiti kwenye kaburi, anajiwa na Malaika wawili na kumuuliza kuhusu Mola Wake, Dini Yake na Mtume Wake.

Kuamini Malaika kutokana na tuliyotaja, kunaleta matunda yafuatayo:

**Kwanza:** Ujuzi juu ya Ukubwa wa Allaah (Ta´ala), nguvu Zake na ufalme Wake. Ukubwa wa viumbe unaashiria ukubwa wa Muumba.

**Pili:** Kumshukuru Allaah (Ta´ala) kwa kumtunza mwanaadamu kwa kule kumuwakilishia yeye Malaika hawa ambao wanamuhifadhi, kuandika matendo yao na mfano wa manufaa kama hayo.

**Tatu:** Mapenzi kuwapenda Malaika kwa ile ´ibaadah wanayomfanyia Allaah (Ta´ala).

Watu wapotevu wamekanusha Malaika kuwa na miili. Badala yake wanasema kuwa wao ni ibara ya nguvu ilio nyuma ya wema uliojificha kwa viumbe. Nadharia hii inakadhibisha Kitabu cha Allaah (Ta´ala), Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na maafikiano ya Waislamu. Allaah (Ta´ala) Anasema:

الْحَمْدُ لِلَّهِ فَاطِرِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ جَاعِلِ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا أُولِي أَجْنِحَةٍ مَّثْنَىٰ وَثُلَاثَ وَرُبَاعَ

**“Sifa njema zote ni za Allaah Muanzilishi wa mbingu na ardhi, Mwenye kuwafanya Malaika kuwa (ni) wajumbe wenye mbawa mbili-mbili, na tatu-tatu na nne-nne.” (Faatwir 35 : 01)**

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ يَتَوَفَّى الَّذِينَ كَفَرُوا ۙ الْمَلَائِكَةُ يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَدْبَارَهُمْ وَذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ

**“Na lau ungeliona pale Malaika wanapowafisha wale waliokufuru wanawapiga nyuso zao na migongo yao na (wanawaambia): “Onjeni adhabu iunguzayo.” (al-Anfaal 08 : 50)**

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمَرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُو أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنفُسَكُمُ

**“Na lau ungeliwaona madhalimu pale wakiwa katika**

**mahangaiko ya mauti, na Malaika wamenyosha mikono yao (wakiwaambia): “Zitoeni nafsi zenu!” (al-An´aam 06 : 93)**

حَتَّىٰ إِذَا فُزِّعَ عَن قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ ۖ قَالُوا الْحَقَّ ۖ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

**“Mpaka litakapoondolewa tisho nyoyoni mwao; watasema: “Amesema nini Mola wenu?” Watasema: (Amesema): “Ya haki”; Naye ni *Al-’Aliyyul-Kabiyr* (Mwenye ‘uluwa Yuko juu ya vyote - Mkubwa wa dhati vitendo na sifa).” (Sabaa´ 34 : 23)**

جَنَّاتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا وَمَن صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ ۖ وَالْمَلَائِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِم مِّن كُلِّ بَابٍ سَلَامٌ عَلَيْكُم بِمَا صَبَرْتُمْ ۚ فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ

**“Mabustani ya milele wataingia pamoja na walio wema miongoni mwa baba zao, wake zao na kizazi chao. Na Malaika wanawaingilia katika kila milango. (Wanasema) “*Salaamun ‘Alaykum*” (Amani iwe juu yenu) kwa yale mliyosubiri. Basi uzuri ulioje hatima (nzuri) ya nyumba (ya Aakhirah).” (ar-Ra´d 13 : 23-24)**

Katika “as-Swahiyh al-Bukhaariy” imepokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anhu) kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**“Wakati Allaah Anapompenda mja, Humwita Jibriyl: “Hakika Allaah Anampenda mtu fulani; hivyo na wewe mpende.” Jibriyl akaanza kumpenda na halafu akanadi kwa watu wa mbinguni: “Allaah Anampenda mtu fulani; hivyo nanyi mpendeni.” Basi hupendwa na watu wa mbinguni na halafu baada ya hapo akakubaliwa katika ardhi.”**[34]

Vilevile imepokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

[34] al-Bukhaariy (3209), Muslim (2637), at-Tirmidhiy (3372), Maalik (1778) na Ahmad (2/267).

**“Kila Ijumaa katika kila mlango wa Ijumaa kunakuwa Malaika wanaoandika wale wa mwanzo wanaohudhuria. Baada ya imamu kukaa, wanafunga vitabu vyao na kusikiliza ukumbusho.”**[35]

Maandiko haya yanaonesha wazi kabisa kwamba Malaika wana miili ya kikweli na sio ibara ya nguvu fulani, kama wanavyosema baadhi ya wapotevu. Haya ndiyo yanayosemwa na maandiko na maafikiano ya Waislamu.

[35] al-Bukhaariy (3211), Muslim (850), an-Nasaa´iy (1384), Ibn Maajah (1092), ad-Daarimiy (1544) na Ahmad (2/239).

# 60- Kuamini Vitabu

*...Vitabu Vyake...*

Vitabu ni wingi wa "kitabu". Makusudio ya vitabu hivi, ni vile ambavyo Allaah (Ta´ala) Ameviteremsha kwa Mitume Wake kama rehema na uongofu kwa viumbe. Lengo yavyo ni ili waweze kufikia furaha katika dunia na Aakhirah.

Kuamini vitabu kunakusanya mambo mane:

**La kwanza:** Kuamini kwamba ni kweli vimeteremka kutoka kwa Allaah.

**La pili:** Kuamini vile vitabu ambavyo tumevijua majina yake. Mfano wa hivyo ni Qur-aan ambacho kimeteremshwa kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Tawrat ambayo imeteremshwa kwa Muusa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Injiyl ambayo imeteremshwa kwa ´Iysaa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Zabuur ambayo imeteremshwa kwa Daawuud (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kuhusiana na vile tusivovijua majina yake, tunaviamini kwa ujumla.

**La tatu:** Kuamini yale maelezo sahihi, kama maelezo ya Qur-aan, na yale maelezo ambayo hayakubadilishwa wala kugeuzwa katika vile vitabu vilivyotangulia.

**La nne:** Kutendea kazi hukumu zile ambazo hazikufutwa na kuridhia na kujisalimisha nazo pasina kujali ikiwa tumefahamu hekima yake au hatukuifahamu. Vitabu vyote vilivyotangulia vimefutwa kwa Qur-aan Tukufu. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ

**"Na Tumekuteremshia Kitabu kwa haki kinachosadikisha yale (yaliyokuja katika) Vitabu vilivyokuwa kabla yake na chenye kuvidhibiti." (al-Maaidah 05 : 48)**

Bi maana kuhukumu juu yavyo. Kutokana na hili haijuzu kutendea kazi kwa mujibu wa hukumu za hivyo vitabu vilivyotangulia ikiwa sio sahihi au kukubaliwa na Qur-aan.

Kuamini vitabu kutokana na tuliyoyataja, kunatoa matunda yafuatayo:

**Kwanza:** Ujuzi juu ya kwamba Allaah (Ta´ala) Anawatunza waja Wake, kwa kule kuwatumia kila watu kitabu.

**Pili:** Ujuzi juu ya hekima ya Allaah (Ta´ala) katika Shari´ah Yake, kwa kule kuwawekea Shari´ah kila watu kulingana na yale yanayoendana na hali zao. Allaah (Ta´ala) Amesema:

لِكُلٍّ جَعَلْنَا مِنكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَاجًا

**"Kwa kila (Ummah) katika nyinyi Tumeujaalia Shari'ah na mfumo (wake). (al-Maaidah 05 : 48)**

## 61- Kuamini Mitume

*... Mitume Wake ...*

Mitume ni wingi wa "Mtume" na maana yake "mjumbe kufikisha kitu". Makusudio hapa ya Mtume maana yake inakuwa "mtu aliyepewa Wahyi na akaamrisha kuufikisha".

Mtume wa kwanza alikuwa ni Nuuh na Mtume wa mwisho alikuwa ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Allaah (Ta´ala) Amesema:

إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَىٰ نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِن بَعْدِهِ

**"Hakika Tumekuletea *Wahy* kama Tulivyomletea Nuwh na Manabii baada yake." (an-Nisaa 04 : 163)**

Katika "Swahiyh al-Bukhaariy" kumepokelewa katika Hadiyth ya Anas bin Maalik (Radhiya Allaahu ´anhu) kuhusu Hadiyth ya uombezi:

**"Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ametaja ya kwamba watu watamwendea Aadam ili awaombee. Atawaomba udhuru na kusema: "Nendeni kwa Nuuh. Yeye ndiye Mtume wa kwanza Aliyetumwa na Allaah.""**[36]

Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ

**"Hakuwa Muhammad baba wa mmoja yeyote miongoni mwa wanaume wenu, lakini ni Mtume wa Allaah na ni mwisho wa Manabii." (al-Ahzaab 33 : 40)**

[36] al-Bukhaariy (4712), Muslim (194), Ahmad (9589), at-Tirmidhiy (2551) na Ibn Khuzaymah katika "Kitaab-ut-Tawhiyd" (347).

Hakuna Ummah wowote isipokuwa Allaah Aliutumia Mtume na Shari´ah maalum, au Nabii ambaye anateremshiwa Wahyi ili aweze kuhuisha Shari´ah iliyokuwa kabla yake. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

**"Na kwa yakini Tulituma katika kila ummah Mtume (awaamrishe watu wake) kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na *twaaghuwt* (miungu ya uongo)." (an-Nahl 16 : 36)**

وَإِن مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ

**"Na hakuna Ummah wowote (ule) isipokuwa amepita humo mwonyaji." (Faatwir 35 : 24)**

إِنَّا أَنزَلْنَا التَّوْرَاةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ ۚ يَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا

**"Hakika Tumeteremsha Tawraat humo mna Hidaaya na Nuru; ambayo kwayo walihukumu Manabii waliyojisalimisha." (al-Maaidah 05 : 44)**

Mitume ni watu walioumbwa na hawana sehemu yoyote katika uola wala uungu. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), ambaye ndio kiongozi wa Mitume na mwenye hadhi ya juu kwa Allaah:

قُل لَّا أَمْلِكُ لِنَفْسِي نَفْعًا وَلَا ضَرًّا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ ۚ وَلَوْ كُنتُ أَعْلَمُ الْغَيْبَ لَاسْتَكْثَرْتُ مِنَ الْخَيْرِ وَمَا مَسَّنِيَ السُّوءُ ۚ إِنْ أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ وَبَشِيرٌ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ

**"Sema: "Siimilikii nafsi yangu manufaa yoyote wala dhara yoyote isipokuwa Apendavyo Allaah. Na lau ningekuwa naelewa ya ghayb, bila shaka ningelijijikithirishia ya kheri na wala lisingelinigusa ovu. Mimi si chochote isipokuwa ni mwonyaji na mbashiriaji kwa watu wanaoamini." (al-A´raaf 07 : 188)**

قُلْ إِنِّي لَا أَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا رَشَدًا قُلْ إِنِّي لَن يُجِيرَنِي مِنَ اللَّهِ أَحَدٌ وَلَنْ أَجِدَ مِن دُونِهِ مُلْتَحَدًا

**"Sema: "Hakika mimi sikumilikieni dhara na wala uongofu." Sema: "Hakika hakuna yeyote awezaye kunilinda na Allaah (ikiwa nitamuasi) na wala sitoweza kupata mahali pa kukimbilia." (al-Jinn 72 : 21-22)**

Wana sifa kama hizo kama ambazo wanaadamu wengine wote wako nazo, kama maradhi, mauti, kiu na mfano wa hayo. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu Ibraahiym (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) wakati alipokuwa anamsifu Mola Wake:

وَالَّذِي هُوَ يُطْعِمُنِي وَيَسْقِينِوَإِذَا مَرِضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ وَالَّذِي يُمِيتُنِي ثُمَّ يُحْيِينِ

**"Na Ambaye Ndiye Anayenilisha na Kuninywesha (Anayenipatia riziki). Na ninapokuwa mgonjwa, basi Yeye Huniponyesha. Na Ambaye Atanifisha kisha Atanihuisha." (ash-Shua´raa´ 26 : 79-81)**

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninasahau kama mnavyosahau. Ninaposahau, nikumbusheni."**[37]

Allaah (Ta´ala) Amewasifu kama waja Wake pindi Anapotaja nafasi zao na Akawasifia. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu Nuuh:

إِنَّهُ كَانَ عَبْدًا شَكُورًا

**"Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukurani." (al-Israa 17 : 03)**

Vilevile Amesema kuhusu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا

**"Amebarikika Yule (Ambaye) Ameteremsha *Al-Furqaan* (Pambanuzi ya haki na batili) kwa mja Wake ili awe muonyaji kwa walimwengu (wote)." (al-Furqaan 25 : 01)**

Amesema kuhusu Ibraahiym, Ishaaq na Ya´quub (Swalla Allaahu ´alayhim wa salaam):

[37] al-Bukhaariy (401), Muslim (572), an-Nasaa´iy (1241) na al-Bayhaqiy (3904).

وَاذْكُرْ عِبَادَنَا إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ أُولِي الْأَيْدِي وَالْأَبْصَارِ إِنَّا أَخْلَصْنَاهُم بِخَالِصَةٍ ذِكْرَى الدَّارِ وَإِنَّهُمْ عِندَنَا لَمِنَ الْمُصْطَفَيْنَ الْأَخْيَارِ

**"Na (taja) waja Wetu; Ibraahiym, Is-haaq na Ya'quwb, wenye nguvu na utambuzi (busara). Hakika Sisi Tumewachagua kwa kuwapa sifa khalisi ya ukumbusho wa nyumba (ya Aakhirah). Na hakika wao Kwetu bila shaka ni miongoni mwa walioteuliwa walio bora kabisa." (Swaad 38 : 45-47)**

Amesema kuhusu ´Iysaa bin Maryam (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

إِنْ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ

**"Yeye (Nabiii 'Iysaa) si chochote isipokuwa ni mja Tuliyemneemesha na Tukamjaalia (kuwa ni) mfano kwa wana wa Israaiyl." (az-Zukhruf 43 : 59)**

Kuamini Mitume kunakusanya mambo mane:

**La kwanza:** Kuamini kwamba ujumbe wao kutoka kwa Allaah (Ta´ala) ni haki. Mwenye kukanusha ujumbe wa mmoja wao, basi atakuwa amewakanusha wote. Allaah (Ta´ala) Amesema:

كَذَّبَتْ قَوْمُ نُوحٍ الْمُرْسَلِينَ

**"Watu wa Nuwh walikadhibisha Mitume." (ash-Shu´araa´ 26 : 105)**

Allaah Akawafanya ni wenye kuwakanusha Mitume wote, pamoja na kwamba alikuwepo Nuuh tu wakati walipomkadhibisha. Kutokana na hili manaswara ambao wamemkadhibisha Muhammad na hawakumfuata wamemkadhibisha pia al-Masiyh bin Maryam. Si wenye kumfuata kwa kumkadhibisha kwao Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kutomfuata na khaswa ukizingatia juu ya kwamba aliwapa bishara ya kuja kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Na maana pekee wanayopata katika bishara hii njema, ni kwamba yeye ni Mtume wao ambaye atawaokoa wao kutokana na upotevu na kuwaongoza katika njia iliyonyooka kupitia yeye.

**La pili:** Kuamini wale Mitume tunaojua majina yao. Kwa mfano Muhammad, Ibraahiym, Muusa, ´Iysaa na Nuuh (´alayhim-us-Swalaatu was-Salaam). Mitume hawa watano ndio Mitume walokuwa na azma kabisa. Allaah (Ta´ala) Amewataja sehemu mbili katika Qur-aan. Moja wapo ni katika Suurat-ul-Ahzaab:

وَإِذْ أَخَذْنَا مِنَ النَّبِيِّينَ مِيثَاقَهُمْ وَمِنكَ وَمِن نُّوحٍ وَإِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ

**"Na (kumbusha pale) Tulipochukua kutoka kwa Manabii fungamano yao na kutoka kwako, kutoka kwa Nuwh, Ibraahiym, Muwsaa, 'Iysaa mwana wa Maryam na Tukachukua kutoka kwao fungamano gumu." (al-Ahzaab 33 : 07)**

Ya pili ni katika Suurat-ush-Shuuraa:

شَرَعَ لَكُم مِّنَ الدِّينِ مَا وَصَّىٰ بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰ ۖ أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ

**"Amekuamuruni katika Dini yale Aliyomuusia kwayo Nuwh na ambayo Tumekuletea Wahy, na Tuliyomuusia kwayo Ibraahiym, Muwsaa na 'Iysaa kwamba: "Simamisheni Dini na wala msifarikiane ndani yake (mkawa makundi-makundi)." (ash-Shuuraa 42 : 13)**

Kuhusiana na wale Mitume tusiojua majina yao, tunawaamini kwa ujumla. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّن قَبْلِكَ مِنْهُم مَّن قَصَصْنَا عَلَيْكَ وَمِنْهُم مَّن لَّمْ نَقْصُصْ عَلَيْكَ

**"Na kwa yakini Tumewapeleka Mtume kabla yako; miongoni mwao wako Tuliokusimulia (habari na visa vyao) na miongoni mwao wako ambao Hatukukusimulia." (Ghaafir 40 : 78)**

**La tatu:** Kuamini maelezo yaliyosihi kutoka kwao.

**La nne:** Kufanyia kazi Shari´ah ya Mtume aliyetumwa kwetu aifikishe. Si mwingine isipokuwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Mtume wa mwisho. Ametumwa kwa watu wote. Allaah (Ta´ala) Amesema:

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

**"Basi Naapa kwa Mola wako, hawatoamini mpaka wakufanye wewe ni hakimu (mwamuzi) katika yale wanayozozana baina yao, kisha wasione katika nyoyo zao uzito katika yale uliyohukumu na wajisalimishe kwa unyenyekevu." (an-Nisaa 04 : 65)**

Kuamini Mitume kutokana na tuliyotaja, kunatoa matunda yafuatayo:

**Kwanza:** Ujuzi wa kujua rehema za Allaah (Ta´ala) kwa waja Wake na kuwatunza kwa kuwatumia Mitume. Amewatumia Mitume ili wawaongoze katika njia ya Allaah (Ta´ala) na kuwabainishia namna ya kumuabudu Allaah. Kwa kuwa akili ya mwanaadamu haiwezi kujitosheleza katika kuweza kujua hilo.

**Pili:** Kumshukuru (Ta´ala) kwa neema hii kubwa.

**Tatu:** Mapenzi na uadhmisho kwa Mitume (´alayhim-us-Swalaatu was-Salaam). Wasifiwe kwa kiasi wanachostahiki, kwa kuwa ni Mitume wa Allaah (Ta´ala) na kwa sababu wanamuabudu, wanafikisha ujumbe Wake na kuwanasihi waja Wake.

Wakaidi waliwakadhibisha Mitume na kudai kuwa Mitume wa Allaah (Ta´ala) hawawezi kuwa watu. Allaah (Ta´ala) Ametaja madai haya na kuyabatilisha kwa Kauli Yake:

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَن يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ إِلَّا أَن قَالُوا أَبَعَثَ اللَّهُ بَشَرًا رَّسُولًا قُل لَّوْ كَانَ فِي الْأَرْضِ مَلَائِكَةٌ يَمْشُونَ مُطْمَئِنِّينَ لَنَزَّلْنَا عَلَيْهِم مِّنَ السَّمَاءِ مَلَكًا رَّسُولًا

**"Na hakuna kilichowazuia watu wasiamini kulipowajia uongofu isipokuwa husema: "Je, Allaah Ametuma mtu kuwa ni Mtume?" Sema: "Lau ingelikuwa katika ardhi (kuna) Malaika wanatembea kwa utulivu; basi bila shaka Tungeliwateremshia kutoka mbinguni Malaika kuwa ni Mtume." (al-Israa´ 17 : 94-95)**

Allaah (Ta´ala) Akabatilisha madai haya kwamba Mitume ni lazima wawe wanaadamu kwa sababu wametumwa kwa watu wa ardhi ambao na wao pia ni wanaadamu. Lau watu wa ardhini wangelikuwa ni Malaika, Allaah

Angeliwateremshia kutoka mbinguni Mitume Malaika. Allaah (Ta´ala) Amewaeleza wale wenye kuwakadhibisha Mitume wamesema:

إِنْ أَنتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا تُرِيدُونَ أَن تَصُدُّونَا عَمَّا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا فَأْتُونَا بِسُلْطَانٍ مُّبِينٍ قَالَتْ لَهُمْ رُسُلُهُمْ إِن نَّحْنُ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يَمُنُّ عَلَىٰ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۖ وَمَا كَانَ لَنَا أَن نَّأْتِيَكُم بِسُلْطَانٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ

**"Nyinyi si chochote isipokuwa ni watu kama sisi, mnataka kutuzuia na yale waliyokuwa wakiabudu baba zetu. Basi tuleteeni madaraka (uthibitisho wa mnayoyasema) bayana. Mtume wao wakawajibu: "Sisi si chochote isipokuwa ni watu kama nyinyi, lakini Allaah Anamfadhilisha Amtakaye miongoni mwa waja Wake. Na haikutupasa sisi kukujieni kwa madaraka isipokuwa kwa Idhini ya Allaah." (Ibraahiym 14 : 10-11)**

## 62- Kuamini siku ya mwisho

*... kuamini siku ya Mwisho...*

Siku ya mwisho ni siku ya Qiyaamah. Siku hiyo watu watafufuliwa kwa ajili ya kufanyiwa hesabu na malipo. Imeitwa hivo kwa sababu hakuna siku nyingine baada yake. Siku hiyo watu wa Peponi watakaa katika majumba yao na watu wa Motoni katika majumba yao.

Kuamini siku ya mwisho kunakusanya mambo matatu:

**La kwanza:** Kuamini kufufuliwa. Nako ina maana ya wale maiti kurudishiwa uhai tena, baada ya kupulizwa baragumu kwa mara ya pili. Watu watasimama kwenda kwa Mola wa walimwengu. Watakuwa miguu peku, uchi na bila ya kutahiriwa. Allaah (Ta´ala) Amesema:

كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ نُّعِيدُهُ ۚ وَعْدًا عَلَيْنَا ۚ إِنَّا كُنَّا فَاعِلِينَ

**“Kama Tulivyoanza (uumbaji) umbo la awali Tutalirudisha. Ahadi juu Yetu. Hakika Sisi Tumekuwa ni Wenye kufanya (Tuyasemayo).” (al-Anbiyaa 21 : 104)**

Kufufuliwa ni jambo la haki lililothibiti kwa Kitabu, Sunnah na maafikiano ya Waislamu. Allaah (Ta´ala) Amesema:

ثُمَّ إِنَّكُم بَعْدَ ذَٰلِكَ لَمَيِّتُونَ ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ تُبْعَثُونَ

**“Kisha nyinyi baada ya hayo ni wenye kufa. Kisha hakika nyinyi Siku ya Qiyaamah mtafufuliwa.” (al-Muuminuun 23 : 15-16)**

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**“Watu watafufuliwa siku ya Qiyaamah wakiwa miguu peku na bila ya kutahiriwa.”**

Wameafikiana kwayo.

Waislamu wameafikiana juu ya kwamba kitatokea. Kadhalika ni jambo linaonesha hekima ya Allaah (Ta´ala) kuwawekea viumbe marudilio ya mwisho ambapo atakuja Kuwalipa kwa yale Aliyowafaradhishia kupitia Mitume Wake. Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ

**"Je, mlidhania kwamba Sisi Tulikuumbeni bila kusudio na kwamba nyinyi Kwetu hamtorejeshwa?" (al-Muuminuun 23 : 115)**

Amesema kumwambia Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

إِنَّ الَّذِي فَرَضَ عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لَرَادُّكَ إِلَىٰ مَعَادٍ

**"Hakika Yule Aliyekufaridhishia Qur-aan bila shaka Atakurudisha mahali pa marejeo." (al-Qaswasw 28 : 85)**

**La pili:** Kuamini hesabu na malipo. Mja atafanyiwa hesabu kwa matendo yake na atalipwa kwayo. Hilo limetolewa dalili na Kitabu, Sunnah na maafikiano ya Waislamu. Allaah (Ta´ala) Amesema:

إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُم

**"Hakika ni Kwetu (ndio) marejeo yao. Kisha bila shaka ni juu Yetu hesabu yao." (al-Ghaashiyah 88 : 25-26)**

مَن جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا ۖ وَمَن جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

**"Atakayekuja kwa jema basi atapata (thawabu) kumi mfano wa hilo. Na Atakayekuja kwa uovu, basi hatolipwa ila mfano wa hilo, nao hawatodhulumiwa." (al-An´aam 06 : 160)**

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا ۖ وَإِن كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا ۗ وَكَفَىٰ بِنَا حَاسِبِينَ

**"Na Tutaweka mizani za uadilifu Siku ya Qiyaamah; basi haitodhulumiwa nafsi yoyote (ile) kitu chochote (kile). Na japokuwa ni uzito wa mbegu ya hardali, Tutaileta. Na inatosheleza Kwetu kuwa *Haasibiyn* (Wenye kuhesabu)." (al-**

**Anbiyaa 21 : 47)**

Ibn ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa) ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Hakika Allaah Atamfanya muumini kuwa karibu [Naye]. Halafu Ataweka sitara Yake juu yake na kumfunika. Kisha Aseme: "Unatambua dhambi kadhaa? Unatambua dhambi kadhaa? Aseme: "Ndio, Mola" mpaka atapoyakubali madhambi yake yote na kuona kuwa ameangamia. Hapo ndipo Atasema: "Nilikusitiri duniani na Mimi hivi leo ninakusamehe." Baada ya hapo apewe kitabu cha mema yake. Ama kuhusu makafiri na wanafiki, wataitwa mbele ya umati: "Watu hawa ndio wale waliokuwa wakimkadhibisha Mola Wao – laana ya Allaah iwe juu ya madhalimu!""**

Wameafikiana kwayo.

Vilevile yamepokelewa mapokezi sahihi kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwamba amesema:

**"Mwenye kutaka kufanya tendo jema na akalifanya, basi Allaah Humwandikia thawabu kumi na Huziongeza mpaka mara mia saba na zaidi ya hapo. Na mwenye kutaka kufanya tendo baya na akalifanya, Allaah Humwandikia tendo baya limoja tu."**

Waislamu wameafikiana juu ya kuwepo kwa hesabu na malipo. Hekima pia inahitajia hivo. Allaah (Ta´ala) Ameteremsha vitabu, Akatuma Mitume na Akawafaradhishia waja kukubali [kupokea] yale waliyokuja nayo na kuyafanyia kazi yale ambayo ni wajibu kuyafanya. Vilevile Amefaradhisha kuwapiga vita wale wenye kumpinga Yeye na akahalalisha damu zao, vizazi vyao, wanawake wao na mali zao. Lau kungelikuwa hakuna hesabu wala malipo, yote haya yangelikuwa hayana maana, kitu ambacho Allaah Anatakasika nacho. Allaah (Ta´ala) Ameashiria hili na Kusema:

فَلَنَسْأَلَنَّ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ وَلَنَسْأَلَنَّ الْمُرْسَلِينَ فَلَنَقُصَّنَّ عَلَيْهِم بِعِلْمٍ ۖ وَمَا كُنَّا غَائِبِينَ

**"Basi kwa yakini Tutawauliza wale waliopelekea (Mitume) na bila shaka Tutawauliza Mitume (pia). Kisha Tutawasimulia kwao kwa ujuzi (kila walichokitenda) na wala Hatukukosa kuwepo."**

**(al-A´raaf 07 : 06-07)**

**La tatu:** Kuamini Pepo na Moto na kwamba ni mahala pa makazi ya milele kwa viumbe.

Pepo ni nyumba ya neema ambayo Allaah (Ta´ala) Amewaandalia waumini wenye kumcha. Watu hawa wameamini yale ambayo Allaah Amewafaradhishia kuyaamini, wakamtii Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), wakiwa ni wenye Ikhlaasw na kumfuata Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Humo kuna aina mbali mbali za neema ambazo hakuna yeyote ameshawahi kuziona, kuzisikia hata kujifikiria nazo. Allaah (Ta´ala) Amesema:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَٰئِكَ هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ جَزَاؤُهُمْ عِندَ رَبِّهِمْ

**"Hakika wale walioamini na wakatenda mema, hao ndio wema wa viumbe. *Jazaa* yao iko kwa Mola wao." (al-Bayyinah 98 : 07- 08**

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّا أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

**"Basi nafsi yoyote haijui yaliyofichiwa katika yanayoburudisha macho. Ni jazaa kwa yale waliyokuwa wakiyatenda." (as-Sajdah 32 : 17)**

Ama kuhusiana na Moto ni nyumba ya adhabu ambayo Allaah (Ta´ala) Amewaandalia makafiri madhalimu. Watu hawa wamemkanusha na wakawaasi Mitume Wake. Ndani yake mna aina mbali mbali za adhabu na mateso ambayo hakuna yeyote anaweza kujifikiria nayo. Allaah (Ta´ala) Amesema:

فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا وَلَن تَفْعَلُوا فَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِي وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ ۖ أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ

**"Msipofanya, na wala hamtaweza kufanya, basi ogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe, ulioandaliwa kwa makafiri." (al-Baqarah 02 : 24)**

إِنَّا أَعْتَدْنَا لِلظَّالِمِينَ نَارًا أَحَاطَ بِهِمْ سُرَادِقُهَا ۚ وَإِن يَسْتَغِيثُوا يُغَاثُوا بِمَاءٍ كَالْمُهْلِ يَشْوِي الْوُجُوهَ ۚ بِئْسَ الشَّرَابُ وَسَاءَتْ مُرْتَفَقًا

**"Hakika Sisi Tumewaandalia madhalimu Moto ambao kuta zake zitawazunguka. Na wakiomba msaada watasaidiwa kwa (kupewa) maji kama mafuta ya moto (au shaba iliyoyeyushwa) yanayobabua nyuso. Ubaya ulioje kinywaji hicho na uovu ulioje mahali pa kupumzikia." (al-Kahf 18 : 29)**

إِنَّ اللَّهَ لَعَنَ الْكَافِرِينَ وَأَعَدَّ لَهُمْ سَعِيرًا الدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۖ لَّا يَجِدُونَ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا يَوْمَ تُقَلَّبُ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ يَقُولُونَ يَا لَيْتَنَا أَطَعْنَا اللَّهَ وَأَطَعْنَا الرَّسُولَا

**"Hakika Allaah Amewalaani makafiri na Amewaandalia (Moto wa) *Sa'iyraa* (uwakao kwa nguvu). Ni wenye kudumu humo milele. Hawatopata mlinzi na wala mwenye kunusuru. Siku zitakapopinduliwa nyuso zao Motoni, watasema: "Laiti tungelimtii Allaah na tungelimtii Mtume." (al-Ahzaab 33 : 64-66)**

Katika kuamini siku ya Mwisho ni pamoja na kuamini kila kitakachokuwa baada ya mauti. Mfano wa hayo ni haya yafuatayo:

**Fitina ya kaburi:** Baada ya mauti kuzikwa, anahojiwa kuhusu Mola Wake, Dini yake na Mtume wake. Hapa Allaah Huwathibitisha wale waumini kwa kauli thabiti na hivyo atasema:

"Mola wangu ni Allaah, Dini yangu ni Uislamu na Mtume wangu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)."

Upande mwingine Allaah Atawafanya madhalimu kupotea. Kafiri atasema:

" Aah! Aah! Sijui."

Mnafiki na yule aliyekuwa na shaka atasema:

"Sijui. Nilisikia watu wakisema kitu na mimi nikawa nimekisema."

**Adhabu na neema za kaburi:** Adhabu itakuwa kwa madhalimu kati ya wanafiki na makafiri. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمَرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُو أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنفُسَكُمُ ۖ الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ وَكُنتُمْ عَنْ آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ

**"Na lau ungeliwaona madhalimu pale wakiwa katika**

**mahangaiko ya mauti na Malaika wamenyosha mikono yao (wakiwaambia): "Zitoeni nafsi zenu! Leo mnalipwa adhabu ya kudhalilisha kwa yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Allaah pasi na haki, na (kwa vile) mlivyokuwa mkizifanyia kiburi *Aayaat* Zake." (al-An´aam 06 : 93)**

Vilevile Amesema (Ta´ala) kuhusu Fir´awn:

النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا ۖ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ

**"Wanadhihirishiwa Moto asubuhi na jioni, na Siku itakayosimama Saa (Qiyaamah; itasemwa): "Waingizeni watu wa Fir'awn (katika) adhabu kali kabisa." (Ghaafir 40 : 46)**

Katika "Swahiyh Muslim" kumepokelewa kutoka kwa Zayd bin Thaabit kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Lau isingelikuwa ni kwa sababu msije kuanguka chini na kupoteza fahamu, basi ningelimuomba Allaah awasikilizeni adhabu ya kaburi kama jinsi mimi ninavyosikia." Kisha akatugeukia na kusema: "Ombeni kinga kwa Allaah kutokamana na adhabu ya kaburi." Wakasema: "Tunaomba kinga kwa Allaah kutokamana na adhabu ya kaburi." Akasema: "Ombeni kinga kwa Allaah kutokamana na adhabu ya kaburi." Wakasema: "Tunaomba kinga kwa Allaah kutokamana na adhabu ya kaburi." Akasema: "Ombeni kinga kwa Allaah kutokamana na fitina zenye kuonekana na zilizojificha." Wakasema: "Tunaomba kinga kwa Allaah kutokamana na fitina zenye kuonekana na zilizojificha." Akasema: "Ombeni kinga kwa Allaah kutokamana na fitina za Dajjaal." Wakasema: "Tunaomba kinga kwa Allaah kutokamana na fitina za Dajjaal."

Kuhusiana na neema za kaburi, zitawapata waumini wa kweli. Allaah (Ta´ala) Amesema:

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَبْشِرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنتُمْ تُوعَدُونَ

**"Hakika wale waliosema: "Mola wetu ni Allaah." Kisha wakanyooka; Malaika huwateremkia (wakati wa kutolewa roho kuwaambia) kwamba: "Msikhofu na wala msihuzunike, na pokeeni bishara njema ya Pepo ambayo mlikuwa mkiahidiwa**

**(kwayo)." (Fuswswilat 41 : 30)**

فَلَوْلَا إِذَا بَلَغَتِ الْحُلْقُومَ وَأَنتُمْ حِينَئِذٍ تَنظُرُونَ وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنكُمْ وَلَكِن لَّا تُبْصِرُونَ فَلَوْلَا إِن كُنتُمْ غَيْرَ مَدِينِينَ تَرْجِعُونَهَا إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ فَأَمَّا إِن كَانَ مِنَ الْمُقَرَّبِينَ فَرَوْحٌ وَرَيْحَانٌ وَجَنَّتُ نَعِيمٍ

**"Basi mbona (hamuizuii roho kutolewa) ifikapo kooni. Nanyi wakati huo mnatazama. Nasi Tuko karibu naye zaidi (anayefariki) kuliko nyinyi, lakini hamuoni. Basi kwa nini ikiwa (mnadhani kuwa) hamuwajibiki malipo? Muirudishe (hiyo roho mwilini mwake), mkiwa ni wakweli? Basi (anayefariki) ikiwa atakuwa miongoni mwa waliokurubishwa. Basi *Rawh* (mapumziko ya raha), na *rayhaan* (manukato), na Pepo yenye kudumu." (al-Waaqi´ah 56 : 83-89)**

al-Baraa´ bin ´Aazib (Radhiya Allaahu ´anhu) ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema kuhusu muumini baada ya kujibu [yale maswali matatu] Malaika wawili humjia ndani ya kaburi lake:

**"Hunadi Mwenye kunadi kutoka mbinguni: "Mja Wangu amesema kweli. Mtandikieni katika matandiko ya Peponi, mvalisheni katika mavazi ya Peponi na mfungulieni mlango katika milango ya Peponi." Azungukwe na harufu na manukato yake. Baada ya hapo kaburi lake lipanuliwe umbali wa jicho lake linapofika."**

Imepokelewa na Ahmad na Abu Daawuud kutoka kwenye Hadiyth ndefu.

Kuamini siku ya Mwisho kutokana tuliyoyataja, kunatoa matunda yafuatayo:

**Kwanza:** Shauku na pupa ya kufanya matendo mema kwa kutaraji kulipwa siku hiyo.

**Pili:** Kuogopa kufanya maasi na kuyaridhia kwa kuchelea kutokamana na adhabu ya siku hiyo.

**Tatu:** Inampa liwazo muumini kwa yale mambo atayoyakosa duniani kwa kutaraji kupata neema na thawabu za Aakhirah.

Makafiri wamepinga kufufuliwa baada ya kufa na kudai ya kwamba hilo haliwezekani. Madai haya ni batili na Shari´ah imetolea dalili ubatili wake, hisia na akili.

**Kuhusu Shari´ah,** Amesema (Ta´ala):

زَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَن لَّن يُبْعَثُوا ۚ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۚ وَذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Waliokufuru wamedai kwamba hawatofufuliwa kamwe. Sema: Bali hapana! Naapa kwa Mola wangu, bila shaka mtafufuliwa, kisha mtajulishwa kwa yale (yote) mliyoyatenda, na hayo kwa Allaah ni mepesi." (at-Taghaabuun 64 : 07)**

Jambo hili vitabu vyote vilivyoteremshwa kutoka mbinguni vimekubaliana juu yake.

**Kuhusu hisia,** Allaah Amewaonesha waja Wake jinsi Anavyohuisha maiti katika dunia. Katika Suurat-ul-Baqarah kuna mifano mitano juu ya hilo:

**Wa kwanza:** Watu wa Muusa wakati walipomwambia:

لَن نُّؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَى اللَّهَ جَهْرَةً

**"Na (kumbukeni) mliposema: "Ewe Muwsaa! Hatutakuamini mpaka tumuone Allaah waziwazi." (al-Baqarah 02 : 55)**

Allaah (Ta´ala) Akawaua kisha baada ya hapo Akawahuisha. Allaah (Ta´ala) Anasema juu ya hilo wakati alipokuwa Akiwazungumzisha Banuu Israaiyl:

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَن نُّؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَى اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْكُمُ الصَّاعِقَةُ وَأَنتُمْ تَنظُرُونَ ثُمَّ بَعَثْنَاكُم مِّن بَعْدِ مَوْتِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

**"Na (kumbukeni) mliposema: "Ewe Muwsaa! Hatutakuamini mpaka tumuone Allaah waziwazi"; ikakuchukuweni *asw-swaa'iqah* (mngurumo angamizi) nanyi mnatazama. Kisha Tukakufufueni baada ya kufa kwenu mpate kushukuru." (al-Baqarah 02 : 55-56)**

**Wa pili:** Kisa cha maiti ambaye Banuu Israaiyl waligombana juu yake. Allaah (Ta´ala) Akawaamrisha wachinje ng´ombe na halafu wapige kiungo cha

ng´ombe huo ili aweze kuwaeleza ni nani aliyemuua. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu tukio hilo:

وَإِذْ قَتَلْتُمْ نَفْسًا فَادَّارَأْتُمْ فِيهَا ۖ وَاللَّهُ مُخْرِجٌ مَّا كُنتُمْ تَكْتُمُونَ فَقُلْنَا اضْرِبُوهُ بِبَعْضِهَا ۚ كَذَٰلِكَ يُحْيِي اللَّهُ الْمَوْتَىٰ وَيُرِيكُمْ
آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ

**"Na (kumbukeni) mlipoiua nafsi, kisha mkakhitilafiana kwayo, na Allaah ni Mwenye kutoa hayo mliyokuwa mkiyaficha. Tukasema: "Mpigeni (huyo maiti) kwa baadhi ya sehemu yake (huyo ng'ombe)." Hivyo ndivyo Allaah Anavyohuisha wafu na Anakuonyesheni ishara Zake huenda mkatia akilini." (al-Baqarah 02 : 72-73)**

**Wa tatu:** Kisa cha watu waliotoka majumbani kwao wakikimbia mauti. Walikuwa ni maelfu. Allaah (Ta´ala) Akawaua kisha Akawahuisha. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu hilo:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ خَرَجُوا مِن دِيَارِهِمْ وَهُمْ أُلُوفٌ حَذَرَ الْمَوْتِ فَقَالَ لَهُمُ اللَّهُ مُوتُوا ثُمَّ أَحْيَاهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ
عَلَى النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ

**"Je, hukuwaona wale ambao walitoka kutoka majumbani mwao nao wakiwa ni maelfu wakikhofu mauti, Allaah Akawaambia: "Kufeni" kisha Akawahuisha? Hakika Allaah ni Mwenye fadhila juu ya watu lakini watu wengi hawashukuru." (al-Baqarah 02 : 243)**

**Wa nne:** Kisa cha mtu ambaye alipita katika kijiji kisichokuwa na watu na akaona kuwa ni jambo lisilowezekana Allaah (Ta´ala) kuweza kukihuisha. Hivyo basi, Allaah (Ta´ala) akamfisha kwa miaka mia moja na halafu akamuhuisha. Kuhusiana na hilo Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَوْ كَالَّذِي مَرَّ عَلَىٰ قَرْيَةٍ وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا قَالَ أَنَّىٰ يُحْيِي هَٰذِهِ اللَّهُ بَعْدَ مَوْتِهَا ۖ فَأَمَاتَهُ اللَّهُ مِائَةَ عَامٍ ثُمَّ
بَعَثَهُ ۖ قَالَ كَمْ لَبِثْتَ ۖ قَالَ لَبِثْتُ يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ۖ قَالَ بَل لَّبِثْتَ مِائَةَ عَامٍ فَانظُرْ إِلَىٰ طَعَامِكَ وَشَرَابِكَ لَمْ
يَتَسَنَّهْ ۖ وَانظُرْ إِلَىٰ حِمَارِكَ وَلِنَجْعَلَكَ آيَةً لِّلنَّاسِ ۖ وَانظُرْ إِلَى الْعِظَامِ كَيْفَ نُنشِزُهَا ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْمًا ۚ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ قَالَ
أَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**"Au (hukuzingatia mfano wa) kama yule aliyepita katika kijiji**

**nacho ni kilichoporomoka kabisa juu ya mapaa yake (kuwa gofu); akasema (kwa mshangao): "Vipi Allaah Atahuisha hiki (kijiji) baada ya kufa kwake?" Basi Allaah Alimfisha miaka mia; kisha Akamfufua. Akasema: (kwa kumuuliza) "Umekaa muda gani?" Akasema: "Nimekaa siku (moja) au sehemu ya siku". (Allaah) Akasema: "Bali umekaa miaka mia; basi kitazame chakula chako na kinywaji chako hakikuharibika. Na mtazame punda wako; na Tutakufanya (uwe) ishara kwa watu. Na itazame mifupa (ya punda) jinsi Tunavyoinyanyua, kisha Tunaivisha nyama". Basi ilipombainikia alisema: "Najua kwamba hakika Allaah juu ya kila kitu ni *Qadiyr* (Muweza)." (al-Baqarah 02 : 259)**

**Wa tano:** Kisa cha Ibraahiym wakati alipomuomba Allaah (Ta´ala) kumuonesha jinsi Anavyohuisha maiti. Allaah (Ta´ala) Akamuamrisha akachinje ndege wanne. Halafu Akamuamrisha Atenganishe vipande vya wa wale ndege pembezoni mwa majabali na halafu aviite. Basi vile vipande vikaungana na wale ndege wakaruka kurudi kwa Ibraahiym. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu hilo:

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۖ قَالَ أَوَلَمْ تُؤْمِن ۖ قَالَ بَلَىٰ وَلَـٰكِن لِّيَطْمَئِنَّ قَلْبِي ۖقَالَ فَخُذْ أَرْبَعَةً مِّنَ الطَّيْرِ فَصُرْهُنَّ إِلَيْكَ ثُمَّ اجْعَلْ عَلَىٰ كُلِّ جَبَلٍ مِّنْهُنَّ جُزْءًا ثُمَّ ادْعُهُنَّ يَأْتِينَكَ سَعْيًا ۚ وَاعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

**"Na (taja) aliposema Ibraahiym: "Mola wangu nionyeshe vipi Unahuisha wafu?" (Allaah) Akasema: "Je kwani huamini?" Akasema: "La! (Naamini) lakini (kwayo) moyo wangu upate kutulia." (Allaah) Akasema: "Basi chukua ndege wanne wazoeshe kwako, (kisha uwachinje), kisha weka juu ya kila jabali katika hao (ndege) sehemu yao; kisha waite watakujia mbio (wakiwa wameumbika upya nawe huku unawaona wanavyojiunga viungo vyao kila mmoja); na elewa kwamba hakika Allaah ni *'Aziyzun-Hakiym*** **(Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima - Mwenye hikmah wa yote daima)." (al-Baqarah 02 : 260)**

Hii ni mifano ya kihisia ya halisi inayoonesha kwamba inawezekana maiti wakafufuliwa. Vilevile kumeshatangulia ishara kwa yale Aliyoyafanya Allaah (Ta´ala) katika miujiza ya ´Iysaa bin Maryam kwa kuhuisha maiti na kuwatoa kwenye makaburi yao kwa idhini ya Allaah (Ta´ala).

**Kuhusu akili**, ni dalili kwa njia mbili:

**Ya kwanza:** Allaah (Ta´ala) Ameumba mbingu, ardhi na vile vilivyomo ndani yake. Yeye ndiye Ameviumba kutokea mwanzo. Yeye ndiye Mwenye uwezo wa kuumba mwanzo, na hashindwi kuwarudisha. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

**"Naye Ndiye Aliyeanzisha uumbaji (wa viumbe), kisha Anaurudisha, nayo ni sahali mno Kwake." (ar-Ruum 30 : 27)**

كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ نُّعِيدُهُ ۚ وَعْدًا عَلَيْنَا ۚ إِنَّا كُنَّا فَاعِلِينَ

**"Kama Tulivyoanza (uumbaji) umbo la awali Tutalirudisha. Ahadi juu Yetu. Hakika Sisi Tumekuwa ni Wenye kufanya (Tuyasemayo)." (al-Anbiyaa´ 21 : 104)**

Allaah Amesema Akiamrisha kuwaraddi wale wenye kukanusha kuhuisha mifupa baada ya kuwa imeshaoza:

قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ

**"Sema: "Ataihuisha Yule Aliyeianzisha mara ya kwanza; Naye kwa kila (namna ya) kuumba ni *'Aliym* (Mjuzi)." (Yaasiyn 36 : 79)**

**Ya pili:** Wakati fulani ardhi inakuwa ni yenye kukosa rutuba, maiti na haina miti. Inapoteremshwa mvua juu yake inaanza kuchipuka, inakuwa kijani na kuchipua kila aina ya mimea mizuri. Yule mwenye uwezo wa kuipa uhai baada ya kufa kwake, ni muweza vilevile wa kuwahuisha maiti. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنَّكَ تَرَى الْأَرْضَ خَاشِعَةً فَإِذَا أَنزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ ۚ إِنَّ الَّذِي أَحْيَاهَا لَمُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۚ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**"Na katika ishara Zake, ni kwamba utaona ardhi imedhalilika (kwa kukosa maji); basi Tunapoiteremshia maji, hutaharaki na kuumuka (iote mimea). Hakika Yule Aliyeihuisha, bila shaka ni Mwenye kuhuisha maiti, hakika Yeye juu ya kila kitu ni *Qadiyr* (Muweza)." (Fuswswilat 41 : 39)**

وَنَزَّلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً مُّبَارَكًا فَأَنبَتْنَا بِهِ جَنَّاتٍ وَحَبَّ الْحَصِيدِ وَالنَّخْلَ بَاسِقَاتٍ لَّهَا طَلْعٌ نَّضِيدٌ رِّزْقًا لِّلْعِبَادِ ۖ وَأَحْيَيْنَا بِهِ بَلْدَةً مَّيْتًا ۚ كَذَٰلِكَ الْخُرُوجُ

**"Na Tukateremsha kutoka mbinguni maji yaliyobarikiwa, kisha Tukaotesha kwayo mabustani na (kila aina za) nafaka za kuvunwa. Na mitende mirefu ya mashada ya makole yenye kupangika tabaka tabaka. (Ni) Riziki kwa waja; na Tukahuisha kwayo (maji) nchi iliyokufa, hivyo ndivyo kutoka (makaburini)." (Qaaf 50 : 09-11)**

Kuna watu waliopotea wanaokanusha adhabu na neema za ndani ya kaburi. Wanadai kuwa hilo ni jambo lisilowezekana kwa sababu linaenda kinyume na ukweli. Wanasema:

"Lau mtu atamfufua maiti ndani ya kaburi, atampata kama alivyokuwa kabla. Vilevile kaburi halikuwa pana na wala halikubana."

Madai haya ni batili kwa mujibu wa Shari´ah, hisia na akili.

**Kuhusu na Shari´ah**, yameshatajwa maandiko yanayotolea dalili juu ya kuthibiti kwa adhabu na neema za ndani ya kaburi.

Katika Swahiyh al-Bukhaariy Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amepokea yafuatayo:

**"Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitoka katika baadhi ya mabustani ya al-Madiynah na akasikia sauti za watu wawili wakiadhibiwa katika makaburi yao."**

Halafu akataja Hadiyth na ndani yake mna:

**"Mmoja wao alikuwa hajihifadhi na mkojo."**

Katika upokezi mwingine imesemekana:

**"Mmoja wao alikuwa hajihifadhi na mkojo na yule mwingine alikuwa akieneza uvumi."**

**Kuhusu hisia**, mwenye kulala wakati mwingine anaota kuwa yuko katika sehemu pakunjufu na pazuri na ananeemeka. Lakini mtu vilevile anaweza

kuota kuwa yuko sehemu penye kubana na kutisha na akahisi maumivu. Wakati mwingine pengine akafikia mpaka kuamka kutokana na ndoto. Pamoja na hivyo bado mtu anakuwa amelala kwenye kitanda hicho hicho na katika hali ile ile aliyokuwemo mwanzo. Ndoto ni ndugu wa kifo. Kwa ajili hii ndio maana Allaah (Ta´ala) ameipa jina la "kifo". Allaah (Ta´ala) Amesema:

اللَّهُ يَتَوَفَّى الْأَنفُسَ حِينَ مَوْتِهَا وَالَّتِي لَمْ تَمُتْ فِي مَنَامِهَا ۖ فَيُمْسِكُ الَّتِي قَضَىٰ عَلَيْهَا الْمَوْتَ وَيُرْسِلُ الْأُخْرَىٰ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

**"Allaah Anafisha nafsi wakati wa mauti yao; na zile zisizokufa katika usingizi wake, basi Huzizuia ambazo Amezikidhia mauti, na Huzituma nyingine mpaka muda wake maalumu uliopangwa. Hakika katika hayo bila shaka kuna alama kwa watu wanaotafakari." (az-Zumar 39 : 42)**

**Kuhusu akili**, mwenye kulala anaweza kuota ndoto ambayo baadaye ikapitika kikweli. Vilevile pengine hata mtu akamuona Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa sifa yake. Yule mwenye kumuona (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa sifa yake, basi atakuwa amemuona kikweli. Pamoja na hivyo muotaji amelala kwenye kitanda chake mbali na kile alichokiota. Ni jambo lisilowezekana Aakhirah ikiwa hili limewezekana hapa duniani?

Kuhusiana na "dalili" yao:

"Lau mtu atamfufua maiti ndani ya kaburi, atampata kama alivyokuwa kabla. Vilevile kaburi halikuwa pana na wala halikubana."

linaraddiwa kwa njia nyingi:

**Ya kwanza:** Haijuzu kupingana na yaliyokuja na Shari´ah kwa utata kama huu. Lau mtu mwenye utata kama huu angelizingatia yaliyokuja na Shari´ah kwa njia sahihi, angelijua kuwa utata huu ni batili. Kumesemwa:

*Ni wangapi wenye kukosoa kauli sahihi?*

*Sababu ya hilo ni kutokana na ufahamu mbaya*

**Ya pili:** Hali za maisha ya ndani ya kaburi ni katika mambo yaliyofichikana ambayo hisia haziwezi kuyafahamu. Lau ingelikuwa inawezekana yakafahamika kwa hisia, basi mtu angelipoteza natija ya kuamini mambo

yaliyofichikana. Vilevile ingelipelekea wale wenye kuamini mambo yenye kufichikana na wenye kuyakanusha wangelikuwa sawa.

**Ya tatu:** Adhabu, neema na makaburi mapana na yenye kubana yanafahamika na maiti tu na si mtu mwingine. Linaweza kufananishwa na mtu mwenye kulala kwenye kitanda chake na akaota ya kwamba ima yuko sehemu yenye kubana na kutisha au vilevile sehemu ambayo ni pana na pazuri. Pamoja na hivyo sehemu yake ya kulala pasibadilike tofauti na mwingine. Bado yuko kwenye chumba chake kati ya kitanda na shuka yake. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akiteremshiwa Wahyi na huku amekaa na Maswahabah wake. Akisikia Wahyi tofauti na Maswahabah wasiusikie. Wakati mwingine inatokea Malaika huja kwa umbile la binaadamu na akaongea naye. Pamoja na hivyo Maswahabah wasimuone Malaika wala kumsikia.

**Ya nne:** Fahamu za viumbe zimewekewa mpaka kwa mujibu wa fahamu ambazo Allaah (Ta´ala) Amewaamulia. Hawawezi kufahamu yote yaliyopo. Mbingu na ardhi saba na vile vilivyomo ndani yake na kila kitu kinamsabihi Allaah kwa njia ya kihakika. Wakati mwingine Allaah (Ta´ala) Anawasikilizisha wale Awatakao katika viumbe Wake. Pamoja na hivyo hili ni jambo lililofichikana kwetu. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu hilo:

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَاوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَن فِيهِنَّ ۚ وَإِن مِّن شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلَٰكِن لَّا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ

**“Zinamsabihi mbingu saba na ardhi na vilivyomo humo. Na hakuna kitu chochote isipokuwa (pia) kinasabihi kwa Sifa Zake njema, lakini hamzifahamu *tasbiyh* zao.” (al-Israa´ 17 : 44)**

Hali kadhalika Mashaytwaan na majini. Wanakwenda na kurudi katika ardhi. Majini walikuja kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), wakasikia kisomo chake na halafu wakarudi kwenda kwa watu wao ili kuwakanya. Pamoja na haya wamefichwa kwetu. Kuhusiana na hilo Allaah (Ta´ala) Amesema:

يَا بَنِي آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمُ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُم مِّنَ الْجَنَّةِ يَنزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْآتِهِمَا ۗ إِنَّهُ يَرَاكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ ۗ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ

**“Enyi wana wa Aadam! Asikufitinisheni shaytwaan kama alivyowatoa wazazi wenu (wawili) katika Pepo; akiwavua nguo zao ili awafichulie (awaonyeshe) sehemu zao za siri. Hakika yeye**

**anakuoneni yeye na kabila lake na hali ya kuwa nyinyi hamuwaoni. Hakika Sisi Tumewafanya mashaytwaan kuwa ni marafiki kwa wale wasioamini." (al-A´raaf 07 : 27)**

Kutokana na haya kuwa viumbe hawawezi kufahamu kila kilichopo, basi haijuzu kukanusha mambo yaliyothibiti katika mambo yaliyofichikana ambayo hayafahamiki na viumbe.

# 63- Kuamini Qadar

*... na uamini Qadar; kheri na shari yake.*

Qadar ni yale mambo Aliyoyakadiria Allaah (Ta´ala) kwa viumbe kulingana na Ujuzi Wake uliotangulia na kwenda kulingana na Hekima Yake.

Kuamini Qadar kunakusanya mambo mane:

**La kwanza:** Kuamini ya kwamba Allaah (Ta´ala) Alijua kila kitu milele na kwa kudumu, kwa ujumla na kwa ufafanuzi. Hili linahusiana na matendo Yake Mwenyewe na matendo ya viumbe Wake.

**La pili:** Kuamini kuwa Allaah Ameandika hayo katika ubao Uliohifadhiwa. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu haya mambo mawiali:

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ فِي كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**“Je, huelewi kwamba Allaah Anajua yale yote yaliyomo katika mbingu na ardhi? Hakika hayo yamo katika Kitabu (*Lawhum-Mahfuudhw*). Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi.” (al-Hajj 22 : 70)**

Katika Swahiyh Muslim kumepokelewa kutoka kwa ´Abdullaah bin ´Amr bin al-´Aasw (Radhiya Allaahu ´anhumaa) ambaye amesema: “Nilimsikia mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akisema:

**“Allaah Aliandika makadirio ya viumbe miaka elfu khamsini kabla ya Kuumba mbingu na ardhi.””**

**La tatu:** Kuamini kila kinachopitika, hakipitiki isipokuwa kwa matakwa ya Allaah (Ta´ala). Hili linahusiana na matendo Yake Mwenyewe na matendo ya viumbe. Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusiana na matendo Yake Mwenyewe:

وَرَبُّكَ يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ

**“Na Mola wako Anaumba Atakavyo.” (al-Qaswasw 28 : 68)**

وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ

**"Na Allaah Anafanya Atakavyo." (Ibraahiym 14 : 27)**

هُوَ الَّذِي يُصَوِّرُكُمْ فِي الْأَرْحَامِ كَيْفَ يَشَاءُ

**"Yeye Ndiye Aliyekutieni sura katika matumbo ya uzazi vile Atakavyo." (al-´Imraan 03 : 06)**

Vilevile Amesema (Ta´ala) kuhusiana na matendo ya viumbe:

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَسَلَّطَهُمْ عَلَيْكُمْ فَلَقَاتَلُوكُمْ

**"Na lau Allaah Angelitaka, Angeliwasaliti juu yenu, wakapigana nanyi." (an-Nisaa 04 : 90)**

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ ۖ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ

**"Na lau Angetaka Mola wako wasingeliyafanya (hayo). Basi waachilie mbali na wanayoyazua." (al-An´aam 06 : 112)**

**La nne:** Kuamini kuwa viumbe vyote kwa dhati yavyo, sifa zake na harakati zake yameumbwa na Allaah (Ta´ala). Allaah (Ta´ala) Amesema:

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ

**"Allaah ni *Khaaliq* (Muumbaji) wa kila kitu, Naye juu ya kila kitu ni *Wakiyl* (Mtegemewa)." (az-Zumar 39 : 62)**

الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَّرَهُ تَقْدِيرًا

**"Ambaye ni Wake Pekee ufalme wa mbingu na ardhi, na hakujichukulia mwana na wala hakuwa na mshirika katika ufalme, na Ameumba kila kitu; kisha Akakikadiria kipimo sawa sawa." (al-Furqaan 25 : 02)**

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ

**“Na Allaah Amekuumbeni na yale (yote) mnayoyafanya?” (asw-Swaaffaat 37 : 96)**

Ameeleza kuwa Mtume Ibraahiym (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) amesema kuwaambia watu wake:

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ

**“Na Allaah Amekuumbeni na yale (yote) mnayoyafanya” (asw-Swaaffaat 37 : 96)**

Kuamini Qadar, kutokana na tuliyosifu, haina maana kuwa inapingana na mja kuwa na matakwa na uwezo katika kutenda. Shari´ah na akili zinatolea dalili juu ya kuthibitisha hilo:

**Kuhusiana na Shari´ah**, Allaah (Ta´ala) Amesema kuhusu matakwa:

فَمَن شَاءَ اتَّخَذَ إِلَىٰ رَبِّهِ مَآبًا

**“... basi atakaye achukue (njia ya) marudio (kwa Mola wake).” (an-Nabaa´ 78 : 39)**

فَأْتُوا حَرْثَكُمْ أَنَّىٰ شِئْتُمْ

**”Basi ziendeeni konde zenu vyovyote mpendavyo.” (al-Baqarah 02 : 223)**

Amesema vilevile kuhusu uwezo:

فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَاسْمَعُوا وَأَطِيعُوا

**“Basi mcheni Allaah muwezavyo, na sikilizeni, na tiini.” (at-Taghaabuun 64 : 16)**

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۚ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ

**“Allaah Hakalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya uwezo wake. Itapata iliyoyachuma na ni dhidi yake iliyojichumia.” (al-**

**Baqarah 02 : 286)**

**Ama kuhusiana na akili**, kila mtu anajua kuwa ana matakwa na uwezo katika kutenda na kuacha kutenda. Anatofautisha kati ya yale anayoyafanya kwa matakwa yake, kama kutembea, na yale yanayotokea pasina matakwa yake, kama kutetemeka. Hata hivyo matakwa ya mja na uwezo wake vimefungamana na matakwa na uwezo wa Allaah (Ta´ala). Allaah (Ta´ala) Amesema:

لِمَن شَاءَ مِنكُمْ أَن يَسْتَقِيمَ وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Kwa yule atakaye miongoni mwenu anyooke (katika njia ya haki). Na hamtotaka isipokuwa Atake Allaah, Mola wa walimwengu." (at-Takwiyr 81 : 28-29)**

Vilevile ulimwengu wote ni milki ya Allaah (Ta´ala). Kwa hivyo hakukuwi lolote katika ulimwengu huu pasina Yeye kujua hilo na kutaka litokee.

Kuamini Qadar, kutokana na tuliyosifu, haina maana kuwa inampa mja hoja ya kuacha mambo ya wajibu au kufanya mambo ya maasi. Kutumia hoja kwa hilo ni jambo la batili linaloraddiwa kwa njia nyingi:

**Ya kwanza:** Kauli Yake (Ta´ala):

سَيَقُولُ الَّذِينَ أَشْرَكُوا لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكْنَا وَلَا آبَاؤُنَا وَلَا حَرَّمْنَا مِن شَيْءٍ ۚ كَذَٰلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ حَتَّىٰ ذَاقُوا بَأْسَنَا ۗ قُلْ هَلْ عِندَكُم مِّنْ عِلْمٍ فَتُخْرِجُوهُ لَنَا ۖ إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ أَنتُمْ إِلَّا تَخْرُصُونَ

**"Watasema wale walioshirikisha: "Lau Allaah Angetaka, tusingelifanya shirki, wala baba zetu (wasingelishirikisha pia); na wala tusingeliharamisha chochote." Hivyo ndivyo walivyokadhibisha wale wa kabla yao mpaka walipoonja adhabu Yetu. Sema: "Je, mna elimu yoyote mtutolee? Hamfuati isipokuwa dhana tu, nanyi si lolote ila mnabuni uongo." (al-An´aam 06 : 148)**

Lau wangelikuwa na hoja kwa kutumia Qadar, Allaah Asingeliwaadhibu.

**Ya pili:** Kauli Yake (Ta´ala):

رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۚ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

**"Mitume ni wabashiriaji na waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya (kuletwa) Mitume. Na Allaah ni *'Aziyzan-Hakiymaa* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima - Mwenye hikmah wa yote daima)." (an-Nisaa 04 : 165)**

Lau Qadar ingelikuwa ni hoja kwa waendaji kinyume, hoja isingelisita kwa kutumwa Mitume kwa sababu kwenda kwao kinyume baada ya kutumwa Mitume kunatokamana na Qadar ya Allaah (Ta´ala).

**Ya tatu:** al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kutoka kwa ´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anhu) ambaye ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Hakuna yeyote katika nyinyi isipokuwa Allaah Ameshamuandikia mahapa pake ima Motoni au Peponi." Hivyo mtu mmoja akasema: "Je, situtegemee basi hilo, ewe Mtume wa Allaah?" Akasema: "Hapana. Fanyeni ´amali, kila mmoja amefanyiwa wepesi."** Kisha akasoma:

فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَاتَّقَىٰ

**"Basi yule anayetoa na akamcha Allaah." (al-Layl 92 : 05)**

Hii ni lafdhi ya al-Bukhaariy. Lafdhi ya Muslim imekuja:

**"Kila mmoja amefanyiwa wepesi kwa yale Aliyoumbiwa."**

Kwa hiyo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akaamrisha kufanya matendo na akakataza kufanya uvivu na kutegemea Qadar.

**Ya nne:** Allaah (Ta´ala) Amemuamrisha na Kumkataza mja na hakumuwajibishia mja isipokuwa yale mambo anayoyaweza. Allaah (Ta´ala) Amesema:

فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ

**“Basi mcheni Allaah muwezavyo.” (at-Taghaabuun 64 : 16)**

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا

**“Allaah Hakalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya uwezo wake.” (al-Baqarah 02 : 286)**

Lau mja angelikuwa ametenzwa nguvu kutenda, basi angelikuwa amelazimishwa kitu asichoweza kujinasua nacho. Hili ni batili. Kwa ajili hiyo ndio maana pindi anapofanya maasi kwa ujinga, kwa kusahau au kwa kulazimishwa, anakuwa sio mwenye kupata dhambi, kwa kuwa ni mwenye kupewa udhuru.

**Ya tano:** Qadar ya Allaah (Ta´ala) ni siri iliyofichwa na haijulikani isipokuwa tu baada ya kutokea. Matakwa ya mja kwa yale anayoyafanya yametanguliwa na matendo ambayo hayatokamani na ujuzi wa Qadar ya Allaah. Kwa hivyo hakuna hoja kwa kutumia Qadar kwa sababu hakuna hoja yoyote kwa kitu ambacho mtu hakijui.

**Ya sita:** Baadhi ya watu wanafanya kila waliwezalo ili kufikia kitu chakulaumika, jambo la kidunia mpaka aweze kukifikia. Hata hivyo hawajiingizi katika matendo mazuri ili baada ya hapo mtu aseme kuwa ni katika Qadar. Kwa nini wanayapa mgongo yale yenye kuwanufaisha katika mambo ya kidini na badala yake wanafanya yale yenye kuwadhuru, halafu baada ya hapo wanailaumu Qadar? Je, haya si mambo mawili na limoja? Mfano huu unaofuata utabainisha hilo:

Hebu tuseme lau kuna mtu amesimama kwenye njia. Moja wapo inamwelekeza mtu katika nchi ya kupatwa na khatari na nyingine inamwelekeza katika nchi iliotulia na nzuri. Ni njia ipi atayochagua? Bila ya shaka atachagua ile njia ya pili ambayo inamwelekeza katika nchi iliotulia na nzuri. Haiwezekani kwa mtu mwenye akili yeyote kuchukua ile njia ya nchi ya kupatwa na khatari halafu baada ya hapo akailaumu Qadar. Kwa nini anachukua njia ya Motoni badala ya Peponi, halafu baada ya hapo akailaumu Qadar?

**Mfano mwingine** mgonjwa huamrishwa kutumia dawa na kukatazwa kula chakula chenye kumdhuru. Akatumia dawa zile na kujiepusha na kile chakula kinyume na kutaka kwake. Anafanya yote hayo ili aweze kupona. Hawezi kuacha kutumia dawa yake au kutumia chakula chenye kumdhuru halafu baada ya hapo akailaumu Qadar. Kwa nini basi mwanaadamu anaacha yale ambayo Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)

wamemuamrisha, au anafanya yale ambayo Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wamemkataza, kisha baada ya hapo anailaumu Qadar?

**Ya sita:** Lau yule mwenye kuilaumu Qadar atashambuliwa na mtu, akampora mali yake au akamvunjia heshima yake, kisha akatumia hoja Qadar ya Allaah kwa yale aliyoyafanya, yule mtu katu hatoikubali hoja yake. Vipi basi asikubali kutumiwa hoja kwa Qadar ya Allaah juu ya haki yake na badala yake akaitumia juu ya haki ya Allaah (Ta´ala) pindi inapotumiwa vibaya?

Imesemekana kuwa mwizi mmoja aliyestahiki kukatwa mkono aliletwa kwa kiongozi wa waumini ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anhu). Baada ya kuamrishwa kukatwa mkono wake, mwizi yule akasema: "Ee kiongozi wa waumini! Subiri kwanza! Nimeiba kwa Qadar ya Allaah (Ta´ala)." Hivyo naye akasema: "Na sisi tunaukata kwa Qadar ya Allaah."

Kuamini Qadar kutokana na tuliyosifu, kunatoa matunda yafuatayo:

**Ya kwanza:** Kumtegemea Allaah (Ta´ala) wakati mtu anapofanya sababu. Kwa njia ya kwamba mtu asitegemei sababu peke yake, kwa sababu kila kitu kinatokea kwa Qadar ya Allaah (Ta´ala).

**Ya pili:** Mtu asijione pindi anapofikia yale aliyokuwa anayatarajia. Kuyafikia hakutokamani na jengine isipokuwa ni neema kutoka kwa Allaah (Ta´ala) kutokana na yale Aliyoyakadiria kupitia sababu za kheri na kufaulu. Kule kujiona kunampelekea kwake kusahau neema hii.

**Ya tatu:** Raha na utulivu wa nafsi kwa yale yatayompitikia kutokana na yale ambayo Allaah (Ta´ala) Amekadiria. Hatohuzunika kwa kukosa kile anachokipenda, au kwa kupatwa na kitu chenye kuchukiza. Yote hayo yanatokamana na Qadar ya Allaah (Ta´ala) na ni Yeye ndiye mwenye ufalme wa mbinguni na ardhini. Ni jambo ambalo ni lazima litokee. Allaah (Ta´ala) Anasema juu ya hilo:

مَا أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَا ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ لِّكَيْلَا تَأْسَوْا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا بِمَا آتَاكُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ

**"Hakuna msiba wowote unaokusibuni katika ardhi au katika nafsi zenu isipokuwa umo katika Kitabu (*Lawhum-Mahfuudhw*) kabla Hatujauumba (huo msiba). Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi. Ili msisononeke juu ya yale yaliyokuondokeeni na wala**

**msifurahie kwa yale Aliyokupeni (Allaah); na Allaah Hapendi kila mwenye kujinata, anayejifakharisha." (al-Hadiyd 57 : 22-23)**

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Ni ajabu ilioje kwa sifa ya muumini. Jambo lake kila siku ni kheri. Hilo haliwi isipokuwa kwa muumini tu. Anapofikwa na kitu kizuri, hushukuru, na hilo likawa ni kheri kwake. Na akifikwa na kitu kibaya, husubiri, na hilo likawa ni kheri kwake."**

Ameipokea Muslim.[38]

Kuna makundi mawili ambayo yamepotea katika Qadar:

**La kwanza:** Jabriyyah. Wanaonelea kuwa mja ametenzwa nguvu katika kutenda na hana matakwa wala uwezo.

**La pili:** Qadariyyah. Wanaonelea kuwa mja yuko huru katika matakwa na uwezo na hivyo haathiriwi na matakwa na uwezo wa Allaah (Ta´ala).

Jabriyyah wanaraddiwa kwa Shari´ah na ukweli.

**Kuhusu Shari´ah**, Allaah (Ta´ala) Amethibitisha mja kuwa na uwezo na utashi na akategemeza kitendo kwake. Allaah (Ta´ala) Amesema:

مِنكُم مَّن يُرِيدُ الدُّنْيَا وَمِنكُم مَّن يُرِيدُ الْآخِرَةَ

**"Miongoni mwenu (wako) wenye kutaka dunia na miongoni mwenu (wako) wenye kutaka Aakhirah." (al-´Imraan 03 : 152)**

وَقُلِ الْحَقُّ مِن رَّبِّكُمْ ۖ فَمَن شَاءَ فَلْيُؤْمِن وَمَن شَاءَ فَلْيَكْفُرْ ۚ إِنَّا أَعْتَدْنَا لِلظَّالِمِينَ نَارًا أَحَاطَ بِهِمْ سُرَادِقُهَا

**"Na sema: "Hii ni Haki kutoka kwa Mola wenu. Basi anayetaka aamini na anayetaka akufuru." Hakika Sisi Tumewaandalia madhalimu Moto ambao kuta zake zitawazunguka." (al-Kahf 18 : 29)**

[38] 2999.

**Ama kuhusu ukweli**, kila mtu anajua kuwa kuna tofauti kati ya yale matendo anayoyafanya kwa matakwa yake, kama kula, kinywa na kufanya biashara, na yale yanayotokea bila ya matakwa yake, kama kutetemeka, kuwa na homa na kuanguka kutoka kwa juu. Matendo ya kwanza ni mwenye kuyafanya kwa matakwa yake pasina ulazimisho, tofauti na matendo ya pili hayafanyi kwa matakwa na kwa kupenda kwake.

Qadariyyah wanaraddiwa pia kwa Shari´ah na akili.

**Kuhusu Shari´ah**, Allaah (Ta´ala) Ameumba kila kitu. Kila kitu kinatokea kwa matakwa Yake. Allaah (Ta´ala) Amebainisha katika Kitabu Chake kuwa matendo ya waja yanatokea kwa matakwa Yake. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا اقْتَتَلَ الَّذِينَ مِن بَعْدِهِم مِّن بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمُ الْبَيِّنَاتُ وَلَٰكِنِ اخْتَلَفُوا فَمِنْهُم مَّنْ آمَنَ وَمِنْهُم مَّن كَفَرَ ۚ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا اقْتَتَلُوا وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ

**“Na lau Angelitaka Allaah wasingelipigana wale ambao (walikuja) baada yao, baada ya kuwajia hoja bayana. Lakini walikhitalifiana, basi miongoni mwao (kuna) walioamini na miongoni mwao waliokufuru. Na lau Angelitaka Allaah wasingelipigana lakini Allaah Anafanya Ayatakayo.” (al-Baqarah 02 : 253)**

وَلَوْ شِئْنَا لَآتَيْنَا كُلَّ نَفْسٍ هُدَاهَا وَلَٰكِنْ حَقَّ الْقَوْلُ مِنِّي لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ

**“Na lau Tungelitaka, (basi) Tungeliipa kila nafsi uongofu wake, lakini imethibiti Kauli kutoka Kwangu (kwamba): “Bila shaka Nitaujaza (Moto wa) *Jahannam* kwa majini na watu pamoja.” (as-Sajdah 32 : 13)**

**Ama kuhusu akili**, Allaah (Ta´ala) Anamiliki ulimwengu wote na mwanaadamu ni mmoja katika ulimwengu huo. Hii ina maana ya kwamba ni mwenye kumilikiwa na Allaah (Ta´ala). Hivyo haiwezekani kwa mwenye kumilikiwa kuwa na upelekaji katika utawala wa Mmiliki isipokuwa kwa idhini na kutaka Kwake.

# 64- Dalili ya nguzo sita za Imani

لَّيْسَ الْبِرَّ أَن تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الآخِرِ وَالْمَلاَئِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ

*"Si wema (pekee) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi lakini wema (khasa) ni mwenye kuamini Allaah na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii." (al-Baqarah 02 : 177)*

*Dalili ya Qadar ni Kauli Yake (Ta´ala):*

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ

*"Hakika sisi Tumekiumba kila kitu kwa makadirio."*
*(al-Qamar 54 : 49)*

## 65- Ihsaan na nguzo yake

*Daraja ya tatu ni Ihsaan. Ina nguzo moja, nayo ni "kumwabudu Allaah kama vile unamuona. Ikiwa wewe humuoni, basi Yeye Anakuona". Dalili ya ni Kauli Yake (Ta´ala):*

إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوا وَّالَّذِينَ هُم مُّحْسِنُونَ

*"Hakika Allaah Yu Pamoja na wenye kumcha, na wale watendao wema." (an-Nahl 16 : 128)*

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ الَّذِي يَرَاكَ حِينَ تَقُومُ وَتَقَلُّبَكَ فِي السَّاجِدِينَ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

*"Na tegemea kwa Al-'Aziyzir-Rahiym (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima – Mwenye kurehemu). Ambaye Anakuona wakati unaposimama. Na mageuko yako (ya kuinama na kusimama katika Swalaah na) katika wenye kusujudu. Hakika Yeye Ndiye As-Samiy'ul-'Aliym (Mwenye kusikia yote daima - Mjuzi wa yote daima)." (ash-Shu´araa´ 26 : 217-220)*

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُو مِنْهُ مِن قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ

*"Na hushughuliki katika jambo lolote, wala husomi humo (chochote) katika Qur-aan na wala hamtendi 'amali yoyote isipokuwa Tunakuwa Mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo." (Yuunus 10 : 61)*

Ihsaan ni kinyume cha kufanya kitu kiovu na maana yake ni kule kujitahidi kufanya mema na kujizuia na maovu. Kwa njia hiyo ina maana ya kujitahidi kuwafanyia wema waja wa Allaah kwa mali yake, nafasi yake, elimu yake na uhai wake.

**Ama mali**, inahusiana na kujitolea, kutoa Swadaqah na kutoa Zakaah. Zakaah ndio aina bora ya Ihsaan kwa sababu ni moja katika nguzo za Uislamu na misingi yake mikubwa. Uislamu wa mtu haukamiliki isipokuwa kwayo. Ni bora ya vinavyotolewa vinavyopendwa zaidi na Allaah (´Azza wa Jalla). Inafuatiwa na yale yanayomuwajibikia mume kumhudumia mke wake, wazazi wake, familia yake, ndugu zake, ami zake, wajomba zake, shangazi

zake na kadhalika. Halafu inafuatiwa na Swadaqah kuwapa masikini na wengineo wenye kustahiki kupewa Swadaqah kama kwa mfano wanafunzi.

**Ama nafasi**, pengine mtu akawa na nafasi fulani kwa mtu ambaye yuko na uongozi. Katika hali hii mtu anatakiwa kutumia nafasi yake. Kwa mfano akaja mtu kwake na kumuomba amuombee kwa mfalme. Inaweza kuhusiana na kumkinga na madhara au kumletea kheri.

**Ama elimu**, anatumia elimu yake kwa kuwafundisha waja wa Allaah katika vikao vya watu wote na watu binafsi na katika mizunguko ya elimu. Hili linahusu hata kama mtu atakuwa katika kikao cha kahawa. Ni katika kheri na wema kuwafundisha watu. Hata hivyo unatakiwa kutumia hekima katika mlango huu. Usiwatie uzito watu kwa njia ya kila unapokaa nao, kuwawaidhisha na kuzungumza nao. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akiwapa watu mawaidha pasina kukithirisha hilo. Watu huchoka. Pindi wanapochoshwa, huchoka na kudhoofika. Inaweza kufikia kiasi cha kwamba, wakaanza kuchukia kheri kwa kukithiri kwa maneno marefu na ya watu wengi.

**Ama uhai**, Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**“Ni katika Swadaqah kumsaidia mtu na mnyama wake kwa kumbeba juu yake au kumpandishia mzigo wake.”**[39]

Hapa una mtu ambaye unamsaidia kumbebea mzigo wake, kumwelekeza njia au mfano wa hayo. Yote haya ni katika Ihsaan. Haya yanahusiana na kuwafanyia waja wa Allaah Ihsaan.

Kuhusinaa na Ihsaan katika ´ibaada ya Allaah, ni kumuabudu Allaah kama vile unamuona. Hili limesemwa na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). ´Ibaadah ya kuamuabudu Allaah kama vile unamuona, ni ´ibaadah ilio na jitihada na matumaini. Wakati ´ibaadah inapokuwa na jitihada na matumaini, mtu anakuwa na moyo kwayo, kwa sababu anajitahidi kwa kitu ambacho anakipenda. Anamuabudu Allaah kama vile anamuona. Anamkusudia Yeye, anarejea Kwake na kujikurubisha Kwake (Subhanaahu).

Sentesi “ikiwa wewe humuoni, basi Yeye Anakuona” ndani yake mna kukimbia na khofu. Kwa ajili hii ndio maana ikawa daraja ya pili ya Ihsaan. Ikiwa humuabudu Allaah (´Azza wa Jalla) kama vile unamuona, kumtafuta na kuihimiza nafsi yako kumfikia, basi muabudu Allaah kama vile Yeye ndiye yuwakuona. Katika hali hii unamuabudu kwa ´ibaadah ya khofu kama vile

[39] al-Bukhaariy (2891) na Muslim (1009).

kukimbia adhabu Yake. Dajara hii kwa waja wema wenye kuabudu iko mbali kuliko ile ya kwanza.

´Ibaadah inayofanywa kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) ni kama alivyosema Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah):

*´Ibaadah anayofanyiwa Mwingi wa Rehema ni kwamba*

*Mja wake ana mapenzi na kujidhalilisha Kwake kwa hali ya juu*

*Hizi ndio nguzo mbili*

´Ibaadah imejengwa juu ya mambo haya mawili; mapenzi ya hali ya juu na kujidhalilisha kwa hali ya juu. Katika mapenzi kuna jitihada na katika kujidhalilisha kuna khofu na kukimbia. Hii ndio Ihsaan katika ´ibaadah anayofanyiwa Allaah (´Azza wa Jalla). Ikiwa mtu anamuabudu Allaah kwa njia hii, atamuabudu (´Azza wa Jalla) kwa Ikhlaasw. Kwa ´ibaadah yake kama hii hakusudii kujionyesha, kutaka kusikika wala sifa kutoka kwa watu. Hajali sawa ikiwa watu watamuona au hawamuoni. Haoni tofauti yoyote katika hali zote hizo mbili. Kwa hali yoyote ile, yeye anaifanya ´ibaadah yake kwa hali nzuri. Bali ni katika Ikhlaasw iliotimia mtu akafanya kila aliwezalo watu wasimuone na akamuabudu Mola Wake kwa siri. Isipokuwa tu ikiwa katika kufanya hilo hadharani kuna manufaa kwa Waislamu au Uislamu. Mfano wa hilo ni mtu akawa mwenye kufuatwa ambaye anachukuliwa kama kiigizo na akataka kuwabainishia watu ni vipi anavofanya ´ibaadah ili waweze kumuigiza katika kitendo hicho. Mfano mwingine ni yeye kufanya ´ibaadah hadharani ili marafiki na wenzake waweze kumuiga. Ni kitendo cha kheri. Manufaa ya kufanya kitendo hichi hadharani yanaweza kuwa ni bora kuliko manufaa ya kuficha. Kwa ajili hii Allaah (´Azza wa Jalla) Anawasifu wale wenye kuzitoa mali zao kwa siri na kwa dhahiri. Endapo ni bora, kuna manufaa, uchaji Allaah na kurejea kwa mioyo kufanya hilo kwa siri, basi mtu afanye hilo kwa siri. Na endapo kuna manufaa kwa Uislamu, kudhihirika alama zake, na Waislamu wakawa wataiga, itafanywa hadharani.

Muumini siku zote huangalia lile lililo na manufaa zaidi. Kila jinsi ´ibaadah itavokuwa na manufaa, ndivyo jinsi itavyokuwa kamilifu na bora zaidi.

## 66- Dalili ya nguzo za Uislamu, Imani na Ihsaan

*Dalili kutoka katika Sunnah ni Hadiyth ya Jibriyl inayojulikana iliyopokelewa na ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anhu) ambaye amesema:*

*"Siku moja tulipokuwa tumekaa na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitutokea mtu ambaye nguo zake zilikuwa nyeupe pepe na nywele zake zilikuwa nyeusi sana. Hakuwa na alama ya kuonesha kuwa ni msafiri na wala hapakuwa na hata mmoja katika sisi aliyemtambua. Alienda akakaa karibu na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akaweka magoti yake karibu na mago yake na akaweka viganja vyake juu ya mapaja yake." Akasema: "Ee Muhammad, nieleze kuhusu Uislamu!" Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Uislamu ni kushuhudia kuwa hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na Muhammad ni Mtume wa Allaah, kusimamisha Swalah, kutoa Zakaah, kufunga Ramadhaan na kwenda kuhiji ukiweza." Akasema: "Umesema kweli." Tukashangazwa kwa kumuuliza kwake Mtume na kumsadikisha. Kisha akasema: "Nieleze kuhusu imani!" Akasema: "Ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake na siku ya Mwisho na kuamini Qadar; kheri na shari yake." Akasema: "Umesema kweli!" Akasema: "Nielezee kuhusu Ihsaan!" Akasema: "Ni kumuabudu Allaah kama vile unamuona. Ikiwa wewe humuoni, basi Yeye Anakuona." Akasema: "Nieleze kuhusu Qiyaamah." Akasema: "Muulizwaji si mjuzi kama asivyo vilevile muulizaji." Akasema: "Nieleze kuhusu alama zake!" Akasema: "Kijakazi kumzaa bibi yake na utaona wachunga wanaenda miguu chini, uchi na mafukara wakishindana kujenga majumba marefu." Amesema: "Kisha akaondoka na tukatulia muda mrefu. Halafu akasema (Swallla Allaahu ´alayhi wa salalm): "Ee 'Umar! Je, unamjua ni nani yule aliyekuwa akiuliza?" Nikajibu: "Allaah na Mtume Wake ndio wanajua zaidi." Akasema Mtume: "Ilikuwa ni Jibriyl ambaye amekuja kuwafundisha Dini yenu."*

Imepokelewa na Muslim. Inapatikana katika kitabu Iymaan katika mlango "al-Iymaan wal-Islaam". Tumeshafafanua sehemu kubwa ya Hadiyth. Vilevile tumeifafanua katika "Majmuu´ al-Fataawaa war-Rasaail", 3/143

# 67- Msingi wa tatu ni kumjua Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم)

*Msingi wa tatu – ni kumjua Mtume wenu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)*

*Alikuwa ni Muhammad bin ´Abdillaah bin ´Abdil-Muttwalib bin Haashim. Haashim alikuwa anatokamana na [kabila la] Quraysh, Quraysh ni kutokamana na waarabu na waarabu ni kutokamana na kizazi cha Ismaa´iyl, mtoto wa Ibraahiym al-Khaliyl – baraka za juu na Salaam ziwe juu yake na kwa Mtume wetu. Aliishi kwa umri wa miaka sitini na tatu, arubaini kabla ya utume na ishirini na tatu kama Nabii na Mtume. Alipewa unabii kwa [kupewa Suurah] "Iqra´" na akapewa utume kwa "al-Muddaththir". Mji wake ni Makkah.*

**Msingi wa tatu** – Bi maana katika misingi mitatu ambayo ni wajibu kwa Muislamu kujua. Misingi hii ni mtu kumjua Mola Wake, Dini yake na Mtume Wake. Kumeshatangulia maneno juu ya mja kumjua Mola Wake na Dini yake. Kuhusiana na kumjua Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), ndani yake kunakusanyika mambo matano:

**La kwanza:** Kumjua kinasabu. Ni katika watu wenye nasabu bora zaidi. Alikuwa ni katika ukoo wa Haashim, kabila la Quraysh na kutoka katika waarabu. Anaitwa Muhammad bin ´Abdillaah bin ´Abdil-Muttwalib bin Haashim.

**La pili:** Kujua umri wake, mahala alipozaliwa na nchi aliyohamia. Haya yamebainishwa na Shaykh pale aliposema:

"Aliishi kwa umri wa miaka sitini na tatu, arubaini kabla ya utume na ishirini na tatu kama Nabii na Mtume. Alipewa unabii kwa [kupewa Suurah] "Iqra´" na akapewa utume kwa "al-Muddaththir". Mji wake ni Makkah."

Alizaliwa Makkah na akabaki huko kwa miaka khamsini na tatu. Halafu akahamia al-Madiynah ambapo aliishi miaka kumi. Akafa Rabiy´ al-Awwal miaka kumi na moja baada ya kuhama.

**La tatu:** Kujua maisha yake kama Mtume ambapo alikuwa kwa miaka ishirini na tatu. Alianza kuteremshiwa Wahyi pindi alipokuwa na miaka arubaini. Mmoja katika washairi amesema:

*Alifikisha miaka arubaini na hapo ndipo*

*Likaangaza jua la kiutume kutoka kwake katika Ramadhaan*

**La nne:** Ni kwa kitu gani alikuwa Nabii na Mtume? Alikuwa Nabii wakati alipoteremshiwa Kauli Yake (Ta´ala):

اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ خَلَقَ الْإِنسَانَ مِنْ عَلَقٍ اقْرَأْ وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ عَلَّمَ الْإِنسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ

**"Soma kwa Jina la Mola wako Aliyeumba. Amemuumba mwanaadamu kutokana na pande la damu linaloning'inia. Soma na Mola wako ni *Al-Akram* (Mkarimu kabisa). Ambaye Aliyefunza kwa kalamu. Amemfunza mwanaadamu yale asiyoyajua." (al-´Alaq 96 : 01-05)**

Alikuwa Mtume wakati alipoteremshiwa Kauli Yake (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ قُمْ فَأَنذِرْ وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ وَلَا تَمْنُن تَسْتَكْثِرُ وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ

**"Ee uliyejigubika. Simama na uonye. Na Mola wako mtukuze (kwa takbira). Na nguo zako zitwaharishe. Na *Ar-Rujz* (masanamu) epukana nayo. Na wala usifanye ihsani kwa ajili ya kutaraji kukithirishiwa (manufaa ya kidunia). Na kwa ajili ya Mola wako subiri." (al-Muddaththir 74 : 01-07)**

Akasimama (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutoka nje na kutahadharisha na kusimamisha maamrisho ya Allaah (´Azza wa Jalla).

Tofauti baina ya Mtume na Nabii, kama wanavyosema baadhi ya wanachuoni, ni kwamba Nabii ni yule mtu ambaye ameteremshiwa Wahyi kwa Shari´ah, pasina kuamrishwa kuifikisha. Ama Mtume ni yule mtu ambaye ameteremshiwa Wahyi kwa Shari´ah na akaamrishwa kuifikisha na kuyatendea kazi. Hivyo basi, kila Mtume ni Nabii na si kila Nabii ni Mtume.

**La tano:** Ametumwa kwa kitu gani na kwa nini? Ametumwa kwa kumpwekesha Allaah (Ta´ala) na Shari´ah Yake ilio na kufanya yale yaliyoamrishwa na kuacha yaliyokatazwa. Ametumwa kama rehema kwa

walimwengu. Ametumwa ili awatoe watu kutoka katika giza la shirki, kufuru na ujinga na kuwapeleka katika nuru ya elimu, imani na upwekeshaji. Yote haya ili waweze kupata msamaha na radhi za Allaah na kuokoka na adhabu na khasira Zake.

## 68- Mtume (صلى الله عليه وسلم) Ametumwa ili kutahadharisha shirki na kulingania katika Tawhiyd

*Allaah Amemtuma ili kutahadharisha shirki na kulingania katika Tawhiyd. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

يَا أَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ قُمْ فَأَنذِرْ وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ وَلَا تَمْنُن تَسْتَكْثِرُ وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ

*”Ee uliyejigubika. Simama na uonye. Na Mola wako mtukuze. Na nguo zako zitwaharishe. Na Ar-Rujz (masanamu) epukana nayo. Na wala usifanye ihsani kwa ajili ya kutaraji kukithirishiwa (manufaa ya kidunia). Na kwa ajili ya Mola wako subiri.” (al-Muddaththir 74 : 01-07)*

*“Simama na uonye” maana yake ni kutahadharisha shirki na kulingania katika Tawhiyd.*

*“na Mola Wako mtukuze” maana yake amtukuze kwa Tawhiyd.*

*“na nguo zako zitwaharishe” maana yake twahirisha matendo yako kutokana na shirki.*

*“na Masanamu epukana nayo” Masanamu. Kuyakata, ina maana ya kuyaepuka na kujitenga nayo na watu wake.*

**Allaah Amemtuma ili kutahadharisha shirki na kulingania katika Tawhiyd –** Ina maana akiwatahadharisha watu shirki na akiwalingania katika kumpwekesha Allaah (´Azza wa Jalla) katika uola Wake, uungu Wake na Majina na Sifa Zake.

**Ee uliyejigubika –** Hapa anaambiwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

**Simama na uonye –** Allaah (´Azza wa Jalla) Anamuamrisha Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) asimame kidete na kwa uchangamfu kuwatahadharisha watu na shirki. Shaykh ameshazifasiri Aayah hizi.

# 69- Safari ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kupandishwa mbinguni

*Miaka kumi alilingania katika Tawhiyd. Baada ya miaka kumi alipandishwa mbinguni na akafaradhishiwa juu yake Swalah tano kwa siku.*

**Miaka kumi alilingania katika Tawhiyd –** Bi maana alilingania (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) watu kumpwekesha Allaah (´Azza wa Jalla).

**Baada ya miaka kumi alipandishwa mbinguni na akafaradhishiwa juu yake Swalah tano –** Bi maana alinyanyuliwa juu:

تَعْرُجُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ

**“Malaika na Roho (Jibrily) wanapanda Kwake.” (al-Ma´aarij 70 : 04)**

Hili ni katika mambo makubwa maalum kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Allaah Alimfadhilisha kwa tukio hili kabla ya kuhama kutoka Makkah.

Wakati alipokuwa amelala katika chumba karibu na Ka´bah, alikuja mtu ambaye alifungua mwili wake kutoka sehemu ya chini ya shingo mpaka sehemu ya chini ya tumbo. Halafu moyo wake ukatolewa na kujazwa hekima na imani, kwa kumwandaa kwa yale atayosimama nayo. Kisha akaletewa mnyama. Alikuwa ni mdogo kuliko nyumbu na mkubwa kuliko punda na alikuwa akiitwa “al-Buraaq”. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akapanda juu yake huku akisuhubiana na mwaminifu Jibriyl. Wakasafiri mpaka walipofika Jerusalemu. Akashuka na akaswali na Mitume. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwaswalisha Mitume na Manabii wote, ili ipate kubainika fadhila na utukufu wake na kwamba yeye ndiye imaam [kiongozi] mwenye kutakiwa kufuatwa.

Kisha Jibriyl akampandisha katika mbingu ya dunia. Wakati walipofika, akaomba ifunguliwe. Kukasemwa: “Ni nani?” Akasema: “Ni Jibriyl.” Akaambiwa: “Ni nani yuko pamoja nawe?” Akasema: “Ni Muhammad.” Kukasemwa: “Ameitwa?” Akasema: “Ndio.” Hivyo kukasemwa: “Karibu! Mfikaji bora aliyoje amefika!” Hivyo akawa amefunguliwa na huko akamuona

Aadam. Jibriyl akasema: "Huyu ni baba yako Aadam. Msalimie." Akamsalimia (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na yeye akamuitikia Salaam na kusema: "Karibu mtoto mwema na Mtume mwema." Kuliani mwa Aadam kulikuwa roho zenye furaha kutoka katika kizazi chake na kushotoni mwake kulikuwa roho zisizo na furaha kutoka katika kizazi chake. Pindi anapotazama kuliani mwake, hufurahi na kucheka, na pindi anapotazama kushotoni mwake hulia. Halafu akachukuliwa na Jibriyl na kumpeleka katika mbingu ya pili. Walipofika, akaomba ifunguliwe na kadhalika. Huko akakutana na wabinamu Yahyaa na ´Iysaa (´alayhimaas-Swalaatu was-Salaam). Jibriyl akasema: "Huyu ni Yahyaa na ´Iysaa. Wasalimie." Akawasalimia na wao wakamrudishia Salaam na kusema: "Karibu ndugu mwema na Mtume mwema." Halafu akachukuliwa na Jibriyl na kumpeleka katika mbingu ya tatu. Walipofika, akaomba ifunguliwe na kadhalika. Huko akakutana na Yuusuf (´alayhis-Swalaatu was-Salaam). Jibriyl akasema: "Huyu ni Yuusuf. Msalimie." Akamsalimia na yeye akamrudishia Salaam na kusema: "Karibu ndugu mwema na Mtume mwema." Kisha akachukuliwa na Jibriyl na kumpeleka katika mbingu ya nne. Wakati walipofika, akaomba ifunguliwe na kadhalika. Huko akakutana na Idriys (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Jibriyl akasema: "Huyu ni Idriys. Msalimie." Akamsalimia na yeye akamrudishia Salaam na kusema: "Karibu ndugu mwema na Mtume mwema." Halafu akachukuliwa na Jibriyl na kumpeleka katika mbingu ya tano. Wakati walipofika, akaomba ifunguliwe na kadhalika. Huko akakutana na Haaruun bin ´Imraan (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), ndugu yake na Muusa. Jibriyl akasema: "Huyu ni Haaruun. Msalimie." Akamsalimia na yeye akamrudishia Salaam na kusema: "Karibu ndugu mwema na Mtume mwema." Kisha akachukuliwa na Jibriyl na kwenda katika mbingu ya sita. Wakati walipofika, akaomba ifunguliwe na kadhalika. Huko akakutana na Muusa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Jibriyl akasema: "Huyu ni Muusa. Msalimie." Akamsalimia na yeye akamrudishia Salaam na kusema: "Karibu ndugu mwema na Mtume mwema." Baada ya kumpita, Muusa akaanza kulia. Akaambiwa: "Ni kipi kinachokuliza?" Akasema: "Ninalia kwa kijana kutumwa baada yangu ambaye Ummah wake utakuwa na watu wengi wataoingia Peponi kuliko Ummah wangu."

Sababu ya Muusa kulia ilikuwa ni huzuni kwa fadhila ambazo Ummah wake umezikosa, na si kwa sababu ya hasadi kwa Ummah wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Kisha akachukuliwa na Jibriyl kumpeleka katika mbingu ya saba. Wakati walipofika, akaomba ifunguliwe na kadhalika. Huko akakutana na Ibraahiym (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), rafiki ya Mwingi wa rehema. Jibriyl

akasema: “Huyu ni Ibraahiym. Msalimie.” Akamsalimia na yeye akamrudishia Salaam na kusema: “Karibu mtoto mwema na Mtume mwema.”

Jibriyl alimchukua Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa Mitume hawa ili kumheshimisha na kuonesha utukufu na ubora wake. Ibraahiym alikuwa ameegemeza mgongo wake katika *Bayt-ul-Ma´muur* kwenye mbingu ya saba. Humo kila siku huingia Malaika elfu sabini kuswali na kufanya ´ibaadah. Pindi wanapotoka, hawarudi tena na siku ya kufuata huja Malaika wengine. Hakuna anayejua ni wangapi isipokuwa Allaah Pekee.

Kisha Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akapandishwa mkunazi wa mwisho. Ilikuwa imezidiwa na uzuri na pambo la Allaah kwa kiasi cha kwamba hakuna yeyote awezae kusifia uzuri na pambo lake. Halafu Allaah Akamfaradhishia Swalah khamsini kwa siku, akaridhia na akajisalimisha nalo. Alipokuwa njiani yuwarudi akakutana na Muusa na akamwambia: “Mola Wako Amewafaradhishia nini Ummah Wako?” Akasema: “Swalah khamsini kila siku.” Akasema: “Ummah wako hawatoweza hilo. Niliwajaribu watu kabla yako na nilitangamana na wana wa israel kwa ukali nilivyoweza. Rudi kwa Mola Wako na umuombe Awapunguzie Ummah wako. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: “Nikarudi na nikapunguziwa kumi.” Akaendelea kwenda kwa Mola Wake mpaka Swalah za faradhi mwishowe zikabaki kuwa tano. Akanadi mwenye kunadi: “Nimeweka faradhi Yangu na nimewawepesishia waja Wangu.”

Katika usiku huu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliingia Peponi. Huko alikutana na kuba ya lulu na udongo wa miski. Hatimae Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akashuka mpaka alipofika Makkah karibu na wakati wa alfajiri na huko akaswali Swalah ya Subh.[40]

[40] al-Bukhaariy (3207) na Muslim (162).

# 70- Hijrah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kutoka Makkah na kwenda al-Madiynah

*Aliswali Makkah kwa miaka mitatu. Baada yake akaamrishwa kufanya Hijrah kwenda al-Madiynah.*

**Aliswali Makkah kwa miaka mitatu –** Swalah ambazo ni Rakaa nne alikuwa akiziswali Rakaa mbili mpaka alipohamia al-Madiynah. Baadaye wasafiri wakaendelea kuswali kama mwanzoni na wakazi wakaanza kuswali nne.

**Baada yake akaamrishwa kufanya Hijrah kwenda al-Madiynah –** Allaah (´Azza wa Jalla) Alimuamrisha Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuhajiri kwenda al-Madiynah kwa sababu watu wa Makkah walimkataza kusimamisha Da´wah yake. Katika Rabiy´ al-Awwal miaka kumi na tatu baada ya kupewa Utume Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alifika al-Madiynah baada ya kuhajiri kutoka Makkah.

Makkah ndio ulikuwa mji wa kwanza ulioteremshiwa Wahyi na mji ambao unapendwa zaidi na Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kuhajiri kulikuwa baada ya kupewa idhini na Mola Wake. Kabla ya hapo aliishi Makkah kwa miaka kumi na tatu na anafikisha ujumbe wa Mola Wake na akilingania katika Dini Yake kwa elimu. Wakubwa wengi wa Quraysh waliikabili Da´wah yake kwa kuikataa, kuipa mgongo na kumshambulia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wale waliomuamini. Mpaka mwishowe ikafikia kiasi cha kwamba wakakusanyika ili kumuua Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wakashauriana juu ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na nini watachomfanya baada ya kuwaona Maswahabah zake wanahajiri kwenda al-Madiynah. Hii ina maana bila ya shaka ya kwamba ni lazima ataenda kujiunga nao na baada ya hapo atapata ushindi na msaada kutoka kwa Answaar ambao walimpa ahadi ya kuamini na utiifu juu ya kumzuia (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na yale wanayowazuia kwayo watoto wao na wake zao. Hili litapelekea yeye kuweza kupata ufalme wake dhidi ya Quraysh. Adui wa Allaah Abu Jahl akasema:

"Rai bora ni sisi tuchague katika kila kabila kijana mwenye nguvu. Halafu tumpe kila mmoja upanga wenye makali na waende kwa Muhammad na wamuue. Baada ya hapo tutastarehe naye. Damu yake itaenea kwa makabila mbalimbali na hapo kabila la ´Abd Manaaf – yaani nduguze Mtume (Swalla

Allaahu ´alayhi wa sallam) – hawatoweza kupigana na makabila yote. Badala yake wataridhika kupewa diya, na hapo tutawapa."

Allaah Akamweleza Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) makusudio na mipango ya washirikina na hivyo akawa amempa idhini ya kuhama.

Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anhu) tokea hapo mbele alikuwa ameshajiandaa na kuhajiri kwenda al-Madiynah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamwambia:

"Tulia. Ninatarajia kupewa idhini."

Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anhu) akaakhirisha Hijrah ili aweze kufanya na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anha) amesema:

"Siku moja pindi tulipokuwa katika nyumba ya Abu Bakr katikati ya mchana, Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akaja mlangoni. Uso wake ulikuwa umefunikwa. Abu Bakr akasema: "Ninawatoa wazazi wangu muhanga kwake! Ninaapa kwa Allaah hakuja kwa saa kama hii isipokuwa kwa kitu muhimu." Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akaingia na kumwambia: "Toa yalo kwako." Akasema: "Ni familia yako tu." Hivyo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Nimepewa idhini ya kuhajiri." Abu Bakr akasema: "Ninakuomba nisuhubiane na wewe, ewe Mtume wa Allaah." Akasema: "Ndio." Abu Bakr akasema: "Ee Mtume wa Allaah, chukua mmoja katika wanyama wangu." Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Kwa thamani."

Kisha wakatoka na wakakakaa katika pango kwenye mlima Thawr siku tatu. Katika masiku haya mtoto wa ´Abdullaah bin Abiy Bakr alilala na wao pia. Alikuwa ni kijana, mwenye akili na mwerevu. Usiku unapokaribia kumalizika, anarudi Makkah na anakuwa na Quraysh asubuhi. Hakukusemwa khabari yoyote juu ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na rafiki yake, isipokuwa anaielewa na kuihifadhi. Baada ya hapo wakati giza linapoanza kuingia, anarudi na kuwaeleza kilichosemwa. Quraysh wakaanza kumtafuta Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kila mahala na wakitumia kila njia ili waweze kumpata Mtume. Ilifikia kiasi cha kwamba, wakamuahidi kumpa ngamia mia moja, yule mwenye kuja nao, au mmoja katika wao. Lakini Allaah Alikuwa na wao na Akiwahifadhi kwa hifadhi Yake na Akiwatunza kwa ulinzi Wake. Quraysh walisimama nje ya

mlango wa pango bila ya kuwaona. Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anhu) amesema:

**“Nilimwambia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wakati tulipokuwa ndani ya pango: “Lau mmoja wao angelitazama kwenye miguu yake, wangelituona.” Akasema: “Usihuzunike. Hakika Allaah Yuko pamoja na sisi. Abu Bakr, wafikiria nini watu wawili wakati Allaah ndio watatu wao?””**[41]

Kule kuwatafuta kulipotulia kidogo, ndio wakatoka ndani ya pango lile baada ya masiku matatu na kuanza safari yao kuelekea al-Madiynah kwa njia ya pwani.

Pindi watu wa al-Madiynah miongoni mwa Muhaajiruun na Answaar waliposikia kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) yuko njiani kwenda kwao, walikuwa wakitoka kila asubuhi nje ya mji wakingojea kufika kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na rafiki yake. Wanasimama na kungojea mpaka ukali wa jua unawalazimisha kurudi. Siku ambayo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa afike, wakafanya vilevile na wakarudi majumbani mwao pindi jua lilipokuwa likali. Wakati huo kulikuwa myahudi mmoja alokuwa juu ya jengo limoja lirefu al-Madiynah na akitafuta haja yake. Pindi alipomuona Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na rafiki yake, hakuweza kustahamili kuacha kunadi kwa sauti: “Enyi kongamano la waarabu! Kumekuja zamu yenu.” Bi maana furaha na utukufu wenu mnaosubiri. Waislamu wakaondoka kwenda kumpokea Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na walikuwa na silaha ili kumuadhimisha na kumtukuza Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Lengo lingine ilikuwa kuonesha kuwa wako tayari kupigana Jihaad na kumlinda – Radhi za Allaah ziwe juu yao. Wakampokea (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwenye uwanja wa miamba. Akaendelea upande wa mashariki na akashukia kwenye kabila la ´Amr bin ´Awf Qubaa´. Huko alikaa siku kadhaa na akajenga Msikiti. Kisha akaenda al-Madiynah na wakati huo akikutana na watu njiani. Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anhu) akasema:

“Wakati tulipofika al-Madiynah, watu walitoka kwenye vijia. Watoto na wafanya kazi walisimama juu ya manyumba huku wakisema: “Allaahu Akbar, Mtume wa Allaah amekuja! Allaahu Akbar, Muhammad amekuja!”

[41] al-Bukhaariy (3653) na Muslim (2381).

## 71- Hijrah ni kutoka katika mji wa kikafiri na kwenda wa Kiislamu

*Hijrah ni kutoka katika mji wa kikafiri na kwenda katika mji wa Kiislamu.*

Hijrah kilugha maana yake ni "kukiacha kitu". Ama tafsiri ya Kishari´ah, ni kama alivyosema Shaykh:

"Hijrah ni kutoka katika mji wa kikafiri na kwenda katika mji wa Kiislamu."

Mji wa kikafiri ni ule ambao kunasimamishwa ndani yake sherehe za kikafiri na hakusimamishwi sherehe za Kiislamu kama adhaana, kuswali kwa mkusanyiko, idi na Ijumaa kwa njia ya ujumla na iliyoenea. Tumesema "kwa njia ya ujumla na iliyoenea" ili kutoa zile sherehe za Kiislamu ambazo ni kikomo zinazofanywa na Waislamu wadogo katika nchi za kikafiri. Nchi hazizingatiwi kuwa ni za Kiislamu kwa sababu tu kuna sherehe za Kiislamu ndani yake. Ama mji wa Kiislamu, ni mji ambao kunasimamishwa sherehe hizi za Kiislamu kwa njia ya ujumla na ya kuenea.

## 72- Uwajibu wa Hijrah

*Ummah huu umefaradhishiwa kufanya Hijrah kutoka katika mji wa kikafiri na kwenda katika mji wa Kiislamu na itabaki mpaka Qiyaamah kitaposimama. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ ظَالِمِي أَنفُسِهِمْ قَالُوا فِيمَ كُنتُمْ ۖ قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ ۚ قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةً فَتُهَاجِرُوا فِيهَا ۚ فَأُولَٰئِكَ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَسَاءَتْ مَصِيرًا إِلَّا الْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ لَا يَسْتَطِيعُونَ حِيلَةً وَلَا يَهْتَدُونَ سَبِيلًا فَأُولَٰئِكَ عَسَى اللَّهُ أَن يَعْفُوَ عَنْهُمْ ۚ وَكَانَ اللَّهُ عَفُوًّا غَفُورًا

*"Hakika wale ambao Malaika wamewafisha, hali wamejidhulumu nafsi zao; (Malaika) watawaambia: "Mlikuwa katika hali gani?" Watasema: "Tulikuwa tukikandamizwa katika ardhi." (Malaika) Watasema: "Je, kwani ardhi ya Allaah haikuwa pana mkahajiri? Basi hao makazi yao yatakuwa ni (Moto wa) Jahannam, na ubaya ulioje mahali pa kurejea. Isipokuwa wale waliokandamizwa kati ya wanaume na wanawake na watoto ambao hawakuweza kupata (mpango wa) hila yoyote wala hawawezi kuongoza njia. Basi hao huenda Allaah Akawasamehe. Na Allaah ni 'Afuwwan-Ghafuwraa (Mwingi wa kusamehe - Mwingi wa kughufiria)." (an-Nisaa 04 : 97-99)*

**Ummah huu umefaradhishiwa kufanya Hijrah kutoka katika mji wa kikafiri na kwenda katika mji wa Kiislamu –** Hijrah ni wajibu kwa muumini asiyeweza kudhihirisha Dini yake katika nchi ya kikafiri. Ikiwa hawezi kudhihirisha Uislamu, basi Uislamu wake unakuwa sio wenye kutimia mpaka afanye Hijrah. Jambo lolote lisilotimia isipokuwa kwa kufanya jambo hilo, basi jambo hilo litakuwa ni wajibu.

**Hakika wale ambao Malaika wamewafisha, hali wamejidhulumu nafsi zao... -** Katika Aayah hii kuna dalili kuwa wale ambao hawakuhajiri ilihali wana uwezo wa kufanya Hijrah, Malaika watawafisha. Kisha watawalaumu na kuwaambia:

أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةً فَتُهَاجِرُوا فِيهَا

**"Je, kwani ardhi ya Allaah haikuwa pana mkahajiri?" (an-Nisaa 04 : 98)**

Ama wale wasioweza na wadhaifu, Allaah Amewasamehe kwa kutoweza kwao kufanya Hijrah. Allaah Haikalifishi nafsi yoyote isipokuwa kwa uwezo wake.

# 73- Hijrah itaendelea kuwepo mpaka siku ya Qiyaamah

يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ أَرْضِي وَاسِعَةٌ فَإِيَّايَ فَاعْبُدُونِ

*"Enyi waja Wangu ambao mmeamini! Hakika ardhi Yangu ni pana, basi Mimi (Pekee) Niabuduni." (al-´Ankabuut 29 : 56)*

*al-Baghawiy (Rahimahu Allaah) amesema:*

*"Sababu ya kuteremka Aayah hii kwa baadhi ya Waislamu Makkah ambao hawakufanya Hijrah. Hivyo Allaah Amewazungumzisha kwa jina la imani."*

*Dalili juu ya Hijrah kutoka katika Sunnah, ni kauli yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):*

*"Hijrah haitosimama mpaka Tawbah isimamishwe. Na Tawbah haitosimamishwa mpaka jua lichomoze kutoka magharibi."*

**al-Baghawiy (Rahimahu Allaah) amesema... –** Ikiwa Shaykh (Rahimahu Allaah) ameleta maneno ya al-Baghawiy kutoka katika Tafsiyr yake, ni dhahiri kuwa amenukuu maneno ya al-Baghawiy kimaana na sio kilafdhi. Muundo huu hauko katika Tafiyr ya al-Baghawiy.

**"Hijrah haitosimama... –** Hili litapitika pale ambapo matendo mema yataacha kukubaliwa. Allaah (Ta´ala) Amesema:

يَوْمَ يَأْتِي بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ لَا يَنفَعُ نَفْسًا إِيمَانُهَا لَمْ تَكُنْ آمَنَتْ مِن قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِي إِيمَانِهَا خَيْرًا

**"Siku zitakapokuja baadhi za ishara za Mola wako haitoifaa nafsi iymaan yake, ikiwa haikuamini kabla au haikuchuma katika iymaan yake kheri (yoyote)." (al-An´aam 06 : 158)**

Makusudio ya "baadhi ya ishara" ni jua kuchomoza kutoka magharibi.

### *74- Hukumu ya kusafiri kwenda katika miji ya kikafiri*

Tunaonelea kuwa haijuzu kusafiri kwenda katika miji ya makafiri isipokuwa kwa masharti matatu yafuatayo:

**Ya kwanza:** Mtu awe na elimu, kiasi cha kwamba itamzuia na utata.

**Ya pili:** Mtu awe na Dini, kiasi cha kwamba itamzuia na matamanio.

**Ya tatu:** Mtu awe ni mwenye kuhitajia hilo.

Ikiwa masharti haya hayatotimizwa, itakuwa haijuzu kusafiri kwenda katika miji ya makafiri kwa sababu ya fitina, au kukhofia fitina, inayopatikana huko. Vilevile kuna kuharibu pesa. Safari hizi zina bei.

Hata hivyo ikiwa kutakuwa na haja ya kufanya hivo, kama kwenda kimatibabu au kusoma elimu ambayo haipatikani katika mji wake, na akawa na elimu na Dini kutokana na tuliyoyataja, hakuna neno mtu akifanya hivo.

Safari za utalii kwenda katika miji ya makafiri hazizingatiwi kuwa ni haja. Kadhalika kuna uwezekano akasafiri kwenda katika miji ya Kiislamu ambapo watu wake wanahifadhi mila (alama) za Kiislamu. Leo baadhi ya miji yetu ya Kiislamu – na himdi zote ni za Allaah – imekuwa ni miji ya kitalii. Ikiwa mtu ana uwezo badala yake asafiri kwenda huko na kujifurahisha na kutumia likizo yake.

Ama kuhusiana na kuishi katika miji ya makafiri, hakika khatari yake ni kubwa katika Dini, tabia, mwenendo na adabu zake. Sisi na wengine tumeshuhudia kuharibika kwa wengi wanaoishi huko na wakarudi kwa sura nyingine. Wamerudi hali ya kuwa ni watenda madhambi. Baadhi yao wamerudi hali yakuwa ni wenye kuritadi. Hawaamini si Dini yao wala nyinginezo – na tunaomba kinga kwa Allaah. Wanakanusha kila kitu na kufanyia mzaha Dini na watu wake wa zamani na wa sasa. Kwa ajili hio ndio maana ni wajibu kwa kila mmoja kujitenga na hilo na kushikamana na masharti yenye kumzuia mtu na matamanio kwa sehemu hizo za maangamizo.

Kuishi katika miji ya makafiri ni lazima kupatikane sharti mbili za kimsingi:

**Ya kwanza:** Mtu mwenye kuishi huko awe na amani na uhakika wa Dini yake, kwa njia ya kwamba awe na elimu na imani. Awe na azma yenye nguvu kuwa na thabati katika Dini yake na atahadhari na upotevu na upindaji. Vilevile awe

na chuki na bughudhi kwa makafiri. Asiwafanye kuwa ni marafiki zake au akawapenda kwa sababu kujenga nao urafiki na kuwapenda ni katika mambo yanayopingana na imani. Allaah (Ta´ala) Amesema:

لَّا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ

**"Hutokuta watu wanaomuamini Allaah na Siku ya Mwisho (kuwa) wanawapenda wale wanaopinzana na Allaah na Mtume Wake, japo wakiwa (ni) baba zao, watoto wao, ndugu zao au jamaa zao." (al-Mujaadalah 58 : 22)**

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ ۘ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ فَتَرَى الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ يُسَارِعُونَ فِيهِمْ يَقُولُونَ نَخْشَىٰ أَن تُصِيبَنَا دَائِرَةٌ ۚ فَعَسَى اللَّهُ أَن يَأْتِيَ بِالْفَتْحِ أَوْ أَمْرٍ مِّنْ عِندِهِ فَيُصْبِحُوا عَلَىٰ مَا أَسَرُّوا فِي أَنفُسِهِمْ نَادِمِينَ

**"Enyi mlioamini! Msiwachukuwe Mayahudi na Manaswara (kuwa ndio) marafiki walinzi. Wao kwa wao ni marafiki walinzi. Na yeyote atakayewafanya marafiki; basi hakika yeye ni miongoni mwao. Hakika Allaah Haongoi watu madhalimu. Basi utawaona wale ambao katika nyoyo zao mna maradhi (ya shaka na unafiki) wanakimbilia kwao (kutaka kushirikiana nao Mayahudi, Manaswara na makafiri wengine huku) wakisema: "Tunakhofu isitusibu mgeuko". Basi Huenda Allaah Akaleta ushindi au jambo (lolote jengine) litokalo Kwake; wakawa wenye kujuta kwa waliyoyaficha katika nafsi zao." ( al-Maaidah 05 : 51-52)**

Imethibiti katika Swahiyh ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mwenye kuwapenda watu basi ni katika wao. Mtu yuko pamoja na yule anayempenda."**

Kitu kinachoweza kuwa khatari kubwa kwa Muislamu, ni yeye kuwapenda maadui wa Allaah. Mapenzi yanalazimisha kukubaliana na wao na kuwafuata. Liwezalo kutokea angalau kwa uchache ni mtu kutowarudi batili zao. Kwa ajili hiyo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mtu yuko pamoja na yule anayempenda."**

**Ya pili:** Mtu awe na uwezo wa kudhihirisha Dini yake. Hili linafanywa kwa njia ya kusimamisha alama za Kiislamu bila ya kizuizi. Ikiwa kuna watu wa kutosha ili kuweza kusimamisha Swalah ya Ijumaa na Swalah za Jamaa´ah, afanye hivo bila ya kuzuiwa. Vilevile asizuiwe kutoa Zakaah, Swawm, Hajj au mengineyo katika alama za Dini. Ikiwa hawezi kufanya hayo, haijuzu kukaa katika nchi hii na hivyo itakuwa ni wajibu kufanya Hijrah. Ibn Qudaamah amesema katika "al-Mughniy´ (08/457) wakati alipokuwa anazungumzia watu sampuli mbali mbali kuhusiana na Hijrah:

"Mmoja wapo ni mtu ambaye ni wajibu kwake kufanya Hijrah. Huyu ni yule mwenye kuwa na uwezo wa kufanya hivo na hawezi kudhihirisha Dini yake. Hawezi kutekeleza ya wajibu katika Dini yake baina ya makafiri. Mtu huyu ni wajibu kwake kufanya Hijrah. Amesema (Ta´ala):

إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ ظَالِمِي أَنفُسِهِمْ قَالُوا فِيمَ كُنتُمْ ۖ قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ ۚ قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةً فَتُهَاجِرُوا فِيهَا ۚ فَأُولَٰئِكَ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَسَاءَتْ مَصِيرًا

**"Hakika wale ambao Malaika wamewafisha, hali wamejidhulumu nafsi zao; (Malaika) watawaambia: "Mlikuwa katika hali gani?" Watasema: "Tulikuwa tukikandamizwa katika ardhi." (Malaika) Watasema: "Je, kwani ardhi ya Allaah haikuwa ya wasaa mkahajiri? Basi hao makazi yao yatakuwa ni (Moto wa) *Jahannam*, na ubaya ulioje mahali pa kurejea." (an-Nisaa 04 : 97)**

Haya ni matishio makali kabisa yanayoonesha uwajibu wake. Kutekeleza wajibu wa Dini yake ni lazima kwa yule mwenye uwezo wa kufanya hivo. Na Hijrah ni katika mambo ya wajibu ya dharurah na kukamilika kwake. Jambo lolote lisilotimia isipokuwa kwa kufanya jambo hilo, basi jambo hilo litakuwa ni wajibu."

Baada ya kukamilisha masharti haya mawili ya kimsingi, kukaa katika nchi ya kikafiri kumegawanyika vigawanyo mbali mbali:

**Cha kwanza:** Akae kwa ajili ya kulingania katika Uislamu. Hii ni aina katika Jihaad na ni faradhi kwa baadhi ya Waislamu wenye uwezo wa kufanya hilo. Hata hivyo kwa sharti Da´wah iweze kufikiwa na kusikuwepo yeyote mwenye kuizuia au kukubaliwa kwake. Kwa sababu kulingania katika Uislamu ni katika mambo ya wajibu ya Dini na kadhalika ni katika mfumo wa Mitume. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameamrisha kufikisha

kutoka kwake katika kila zama na mahala. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**“Fikisheni kutoka kwangu ijapokuwa Aayah moja.”**[42]

**Cha pili:** Akae huko kwa ajili ya kuzisoma hali za makafiri na kuyajua yale mambo waliyonayo katika ´Aqiydah mbovu, ´ibaadah za batili, tabia mbaya na maumbile ya fujo ili apate kuwatahadharisha watu wasidanganyike nao na kuwabainishia wale wenye kuwapenda uhakika wa hali zao. Sampuli ya ukaaji huu pia ni aina ya Jihaad kwa sababu mtu anatadharisha kufuru na watu wake pamoja na kulingania katika Uislamu na uongofu wake. Kuharibika kwa kufuru ni dalili ya kutengemaa kwa Uislamu. Kuna mithali inayosema:

Kwa kinyume chake kinafafanua mambo.

Sharti ya hili kufanywa ni lazima mtu afikie lengo bila ya hilo kupelekea katika madhara makubwa kuliko hilo lengo. Hata hivyo ikiwa lengo halikupatikana kwa njia ya kwamba akazuiwa kuonesha yale waliyomo na kutahadharisha nao, hakuna faida yoyote ya kukaa kwake. Lakini ikiwa lengo litapatikana pamoja na madhara makubwa, kwa mfano wakakabiliana naye kwa kuutukana Uislamu, Mtume wa Uislamu na wanachuoni wa Uislamu, ni wajibu kusimamisha kazi hiyo. Amesema (Ta´ala):

وَلَا تَسُبُّوا الَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ فَيَسُبُّوا اللَّهَ عَدْوًا بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ كَذَٰلِكَ زَيَّنَّا لِكُلِّ أُمَّةٍ عَمَلَهُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِم مَّرْجِعُهُمْ فَيُنَبِّئُهُم بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

**“Na wala msiwatukane wale wanaowaomba asiyekuwa Allaah; wasije (nao) kumtukana Allaah kwa uadui bila ya kujua. Hivyo ndivyo Tumewapambia kila ummah ‘amali zao, kisha kwa Mola wao Pekee yatakuwa marejeo yao, Atawajulisha kwa yale waliyokuwa wakitenda.” (al-An´aam 06 : 108)**

Hili linafanana na kukaa katika miji ya kikafiri ili kuwapeleleza kwa ajili ya Waislamu ili apate kujua yale wanayoyapanga dhidi ya Waislamu na halafu akawatahadharisha Waislamu. Kama jinsi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa

[42] al-Bukhaariy (3461).

sallam) alivyomtuma Hudhayfah bin al-Yamaan kwenda kwa washirikina ili apate kujua khabari zao katika vita vya Khandaq.[43]

**Cha tatu:** Akae huko kwa ajili ya haja ya nchi ya Kiislamu na kupanga mafungamano yake na nchi za kikafiri. Kwa mfano mabalozi. Huyu ana hukumu moja na yule mwenye kukaa kwa ajili yake [hiyo nchi ya Kiislamu]. Kwa mfano yule mwenye kusimamia mambo ya kielimu. Akikaa katika nchi kama hiyo kwa ajili ya kusimamia masuala ya elimu, akiwatazama na kuwahimiza kushikamana na Uislamu na tabia na adabu zake, kunapatikana manufaa makubwa na wakati huo huo kunaondoka madhara makubwa.

**Cha nne:** Akae huko kwa ajili ya haja maalum na inayojuzu. Kwa mfano biashara na matibabu. Katika hali hii inajuzu kukaa huko kadiri na haja. Wanachuoni wamesema kuwa inajuzu kuingia katika miji ya makafiri kwa ajili ya biashara. Wametoa ushahidi wa hilo kutokana na baadhi ya mapokezi ya Maswahabah.

**Cha tano:** Akae huko kwa ajili ya kusoma. Aina hii inafanana na ya kabla yake. Hata hivyo aina hii ni khatari na inaharibu zaidi kwa Dini ya mtu na tabia yake. Mwanafunzi siku zote hujihisi kuwa chini ya waalimu. Hili linapelekea mtu kuwaadhimisha na kuridhia tabia zao, fikira zao na mienendo yao. Hivyo wakawafuata, isipokuwa yule ambaye Allaah Amemuhifadhi – na ni wachache.

Mwanafunzi huhisi kuwa ni mwenye haja ya mwalimu wake. Hilo linapelekea hatimae akaanza kumpenda na kumpaka mafuta katika upotevu na upindaji aliyomo.

Vilevile mwanafunzi wakati wa kozi ya masomo ana wanafunzi wenzake anaowafanya marafiki ambao anawafanya kuwa ni marafiki anaowapenda na akaathirika nao.

Kwa ajili ya khatari hii kigawanyo hichi, ni lazima kwa mtu awe macho zaidi kuliko kile cha kabla yake. Katika hayo masharti mawili ya kimsingi kumeongezwa juu yake masharti mengine mawili ya kimsingi:

**Ya kwanza:** Mwanafunzi awe na akili iliokomaa sana. Hili tukiwa na maana ya kwamba awe ni mwenye kuweza kupambanua baina ya mazuri na mabaya na awe na uoni wa mbali juu ya mambo. Ama kuwapeleka watoto wadogo na ambao hawajakomaa, ni khatari kubwa kwa Dini zao, tabia zao na mwenendo wao. Halafu isitoshe ni khatari vilevile kwa Ummah wao ambao watarudilia.

[43] Muslim (1788).

Pindi watakapowarudilia, wanaanza kueneza sumu zao ambazo wamezipata kutoka kwa wale makafiri. Hili limeshuhudiliwa na linashuhudiliwa mpaka hivi leo kutokana na hali ilivyo.

Wengi katika wanafunzi waliotumwa wamerudi wakiwa ni watu wengine. Wamerudi hali ya kuwa wamepotea katika imani zao, tabia zao na mienendo yao. Ni jambo linalojulikana kwamba mambo haya yamewadhuru watu hawa na jamii zao. Kuwatuma watu hawa katika nchi kama hizi ni kama kuitupa mbuzi kati ya mijibwa mwitu.

**Ya pili:** Mwanafunzi awe na elimu kubwa ya Kishari´ah, itayomuwezesha kuweza kupambanua baina ya haki na batili na aweze kupambana na batili kwa haki. Hili linahitajika ili asije akadanganyika na batili waliyomo na akafikiria kuwa ni haki, mambo yakamchanganya au akashindwa kuraddi batili na hivyo akawa amechanganyikiwa na kuanza kufuata batili. Kuna Du´aa iliyopokelewa inayosema:

"Ee Allaah, nioneshe haki kuwa ni haki na uniruzuku kuweza kuifuata. Nioneshe batili kuwa ni batili na uniruzuku kuweza kuiepuka."

**Ya tatu:** Mwanafunzi awe ni mtu wa Dini itayomuhifadhi na kumlinda kutokamana na kufuru na maasi. Hii ina maana ya kwamba yule mtu ambaye ana imani dhaifu hatosalimika na kukaa katika nchi kama hizo. Isipokuwa yule ambaye Allaah Atamsalimisha. Hili linatokana na kuwa mashambulizi ni yenye nguvu na mshambuliwaji ni dhaifu. Sababu za kufuru na maasi ni zenye nguvu na zimejaa katika nchi hizo. Zinapokutana na mtu ambaye nguvu za upinzani wake ni dhaifu, hufanya kazi zake.

**Ya nne:** Kuwepo haja ya elimu ambayo mwanafunzi amekaa katika nchi hiyo kwa ajili yake. Hili linahitajia ya kwamba elimu yake iwe na manufaa kwa Waislamu na masomo kama hayo hayapo katika miji ya Waislamu. Ikiwa ni elimu ambayo haina manufaa yoyote kwa Waislamu au ambayo ipo tayari katika miji ya Kiislamu, itakuwa haijuzu kukaa katika miji ya kikafiri kwa ajili yake. Sababu ya hili ni ile khatari na madhara yanayopatikana katika Dini na tabia ya mtu. Sababu nyingine ni mali nyingi inayopotea pasina faida.

**Ya tano:** Kukaa huko kwa ajili ya kuishi. Aina hii ni khatari na kubwa zaidi kuliko ya kabla yake. Hili linapelekea katika uharibifu ambao mmoja wapo ni kule kuchanganyikana kikamilifu na makafiri. Uharibifu mwingine ni kule mtu kuhisi kuwa nchi hiyo ni nchi yake na mtu anakuwa amefungamanishwa na mzalendo wake inayopelekea katika kuwapenda. Mtu anakuwa ni mwenye kuzidisha idadi ya makafiri. Familia yake inakuja kulelewa kati ya makafiri na

hivyo wanachukua tabia na ada zao. Huenda wakawafuata wao katika ´Aqiydah zao na ´ibaadah. Kuhusiana na hilo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Yule mwenye kukaa na mshirikina na akaeshi naye, ni kama yeye."**[44]

Hadiyth hii – hata kama isnadi yake ni dhaifu – ina mtazamo upande mmoja. Kule kuishi nao kunapelekea katika kuchanganyika nao. Qays bin Haazim amepokea kutoka kwa Jariyr bin ´Abdillaah (Radhiya Allaahu ´anhu) ambaye ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mimi niko mbali na kila Muislamu anayeishi kati ya washirikina." Wakasema: "Ee Mtume wa Allaah, kwa nini?" Akasema: "Moto wao hawatakuwa ni wenye kuonana."**[45]

Imepokelewa na Abu Daawuud na at-Tirmidhiy.

Wengi katika wapokezi wameipokea Hadiyth hii kupitia Qays bin Haazim kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) bila ya kutaja Swahabah yeyote katikati. at-Tirmidhiy amesema:

"Nimemsikia Muhammad – yaani. al-Bukhaariy – akisema: "Swahiyh ni Hadiyth ya Qays kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) bila ya kutaja Swahabah yeyote kati yake.""

Vipi moyo wa muumini utakuwa ni wenye furaha kwa kuishi katika mji wa kikafiri ambapo kunatangazwa ndani yake mambo ya kikafiri na hawahukumu kwa hukumu ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)? Anaona yote hayo kwa macho yake, anayasikia kwa masikio yake na akaridhia. Bali uhakika wa mambo ni kwamba anajinasibisha na nchi hiyo, anaeshi huko na mke wake na watoto wake na akahisi utulivu ndani yake, kama jinsi anavyohisi utulivu katika miji ya Kiislamu. Pamoja na khatari kubwa pia tuliyotaja inayopatikana kwake yeye, mke wake na watoto wake katika Dini na tabia zao.

Hapa ndipo tumepofikia juu ya kuishi katika nchi za kikafiri. Tunamuomba Allaah yawe yameafikiana na haki na usawa.

---

[44] Abu Daawuud (2784).

[45] Abu Daawuud (2643) na at-Tirmidhiy (1654).

## 75- Shari´ah zilizowekwa al-Madiynah

*Wakati Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipotulia al-Madiynah, Alifaradhishiwa Shari´ah zingine za Kiislamu. Kwa mfano Zakaah, Swawm, Hajj, adhaana, Jihaad, kuamrisha mema na kukataza maovu na Shari´ah zingine za Kiislamu.*

Mwandishi (Rahimahu Allaah) amesema kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) Alifaradhishiwa Shari´ah zingine za Kiislamu baada ya kutulia al-Madiynah an-Nabawiyyah. Makkah alifanya karibu miaka kumi akilingania katika Tawhiyd tu. Baada ya hapo ndio Akafaradhishiwa Swalah tano Makkah. Kisha akahajiri kwenda al-Madiynah na Hakufaradhishiwa Zakaah, Swawm, Hajj wala ´ibaadah nyinginezo katika mambo ya Kiislamu. Dhahiri ya maneno ya mwandishi (Rahimahu Allaah) yanaashiria kwamba Zakaah ilifaradhishwa al-Madiynah. Hata hivyo baadhi ya wanachuoni wamesema kuwa Zakaah ilifaradhishwa kwanza Makkah. Pamoja na hivyo viwango vya masharti yake vilikuwa havijulikani kama jinsi bidhaa inayowajibika kulipiwa pia ilikuwa haijulikani. Viwango viliwekwa al-Madiynah kwanza na bidhaa iliyo ya wajibu ikawekwa pia. Wametumia dalili ya Aayah za Suurah za Makkah zinazowajibisha Zakaah. Mfano wazo ni Kauli Yake (Ta´ala) katika Suurat-ul-An´aam:

وَآتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ

**“Na toeni haki yake (Zakaah) siku ya kuvunwa kwake.” (al-An´aam 06 : 141)**

وَالَّذِينَ فِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ

**”Na wale ambao katika mali zao (huweka) haki (sehemu) maalumu. Kwa ajili ya muombaji na aliyenyimwa (aliyepoteza makazi na mali yake akadhikika).” (al-Ma´aarij 70 : 24-25)**

Kwa hali yoyote kauli iliyo sahihi, kuwekwa kwa Zakaah, viwango vyake, bidhaa zake za wajibu na aina ya watu wanayoistahiki ilikuwa ni al-Madiynah. Kadhalika adhaana na Ijumaa. Lililo la dhahiri ni kwamba Swalah ya Jamaa´ah ilifaradhishwa pia al-Madiynah, kwa sababu adhaana inayowaita

watu katika Swalah ya Jamaa´ah ilifaradhishwa mwaka wa pili baada ya Hijrah. Ama Zakaah na Swawm vilifaradhishwa mwaka wa tatu baada ya Hijrah. Kuhusiana na Hajj ilifaradhishwa mwaka wa tisa baada ya Hijrah kutokana na kauli yenye nguvu ya wanachuoni. Hapo ilikuwa wakati ambapo Makkah ilikuwa imeshakuwa mji wa Kiislamu, baada ya kutekwa katika mwaka wa tisa baada ya Hijrah. Hali kadhalika kuamrisha mema, kukataza maovu na mengineyo katika mambo ya dhahiri yaliyoteremshwa. Yote yalifaradhishwa al-Madiynah baada ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutulia ndani yake na kusimamisha nchi ya Kiislamu.

## 76- Kifo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم)

*Aliyafanya haya kwa miaka kumi. Baada ya hapo akafa, lakini Dini yake imebaki.*

Alifanya haya (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa miaka kumi baada ya Hijrah. Wakati Allaah Alipomkamilishia Dini na Akaitimiza neema Yake kwa waumini, Allaah Alimchukua kuwa karibu na Yeye na kukutana na marafiki wa juu – Mitume, wakweli, mashahidi na watu wema.

Alianza kuuguwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) mwishoni wa mwezi wa Safar na mwanzoni wa mwezi wa Rabiy´ al-Awwal. Akawatokea watu hali ya kuwa amevaa kitambaa kwenye kichwa chake na akapanda juu ya minbari. Halafu akasoma Shahaadah na kitu cha kwanza alichoanza kutaja baada ya hapo ni kuwaombea msamaha mashahidi wa Uhud. Kisha akasema:

**"Allaah Amempa khiyari mja miongoni mwa waja Wake baina ya dunia na yaliyo Kwake. Akachagua yaliyo kwa Allaah."**

Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anhu) akafahamu anachomaanisha na akaanza kulia na kusema: "Tunawatoa muhanga baba zetu, mama zetu, watoto wetu, nafsi zetu na mali zetu kwako." Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema:

**"Taratibu, ee Abu Bakr."**

Kisha akasema:

**"Ikiwa kuna watu waliyonipa amani kwa usuhubiano na mali yake, basi ni Abu Bakr. Ningelimfanya mtu mwingine zaidi ya Mola Wangu kuwa rafiki wa karibu, basi ningelimfanya Abu Bakr. Badala yake kuwepo urafiki na mapenzi katika Uislamu."**[46]

Siku ya Jumatatu tarehe kumi na mbili Rabiy´ al-Awwal, au kumi na tatu, mwaka wa 11 baada ya Hijrah Allaah Akamchukua kwenda Kwake. Katika kitanda chake pindi mauti yalipomjia akawa anachukua mkono wake na kuuweka kwenye maji, halafu anapangusa uso wake na huku akisema:

[46] Muslim (2382).

**"Hakuna mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah. Hakika mauti yana uchungu."**

Kisha anaelekeza macho yake mbinguni na akisema:

**"Ee Allaah, rafiki wa juu."**[47]

Akafa siku hiyo. Watu wakavutana na walikuwa na haki ya kufanya hivo. Ndipo alipokuja Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anhu), akapanda juu ya minbari, akamsifu Allaah na halafu akasema:

"Yule aliyekuwa akimuabudu Muhammad, basi atambue kuwa Muhammad amekufa, na yule aliyekuwa akiamuabudu Allaah, basi atambue kuwa Allaah yuhai na hafi."

Halafu akasoma:

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ الرُّسُلُ ۚ أَفَإِن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ انقَلَبْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ

**"Na Muhammad si yeyote isipokuwa ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake Mitume. Je, akifa au akiuawa mtageuka nyuma ya visigino vyenu (mrudi katika ukafiri)?" (al-´Imraan 03 : 144)**

إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُم مَّيِّتُونَ

**"Hakika wewe ni maiti (utakufa) na wao pia ni maiti." (az-Zumar 39 : 30)**

Watu wakaanza kulia vikali na kukinaika kuwa kweli (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekufa. Akaoshwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa nguo zake kwa ajili ya kumheshimu. Kisha akavikwa sanda ya pamba kwa nguo tatu nyeupe bila ya kanzu wala kilemba. Kisha watu wakamswalia makundi makundi bila ya imamu.

Baada ya Khalifah kupewa kiapo cha utiifu na usikivu, akazikwa usiku wa kuamkia Jumatano – Swalah na salaam zimshukie yeye kutoka kwa Mola Wake.

[47] al-Bukhaariy (4449).

## 77- Viumbe wote ni wajibu kumfuata Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم)

*Hii ndio Dini yake. Hakuna kheri yoyote isipokuwa amewaonesha nayo Ummah wake, na hakuna shari yoyote isipokuwa amewatahadharisha nayo. Kheri [kubwa] Aliyowaonesha nayo ni Tawhiyd na kila Anachokipenda Allaah na Kukiridhia. Na shari [kubwa] Aliyowatahadharisha nayo ni shirki na kila Anachokichukia Allaah na kukibughudhi.*

*Allaah Amemtuma kwa watu wote na Allaah Akafaradhisha kwa viumbe wote – majini na watu – kumtii. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

*"Sema: "Hakika mimi ni Mtume wa Allaah kwenu nyinyi nyote."*
*(al-A´raaf 07 : 158)*

**Allaah Amemtuma kwa watu wote –** Bi maana Allaah Amemtumiliza kwa watu wote.

**Sema: "Hakika mimi ni Mtume wa Allaah... –** Hii ni dalili inayoonesha kuwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) Ametumwa na Allaah kwa watu wote na kwamba Aliyemtuma ni Mfalme wa mbingu na ardhi. Yule ambaye Mikononi mwake ndio mna kuhuisha na kufisha. Yeye peke Yake (Subhaanahu) ndio mwenye haki ya kupwekeshwa kwa kuabudiwa kama ambavyo Anavyopwekeshwa katika uola Wake. Mwishoni wa Aayah Akatuamrisha (Subhaanahu wa Ta´ala) kumuamini Mtume huyu asiyejua kusoma wala kuandika na kumfuata. Kufanya hivo ndio sababu ya uongofu wa kielimu na utenda kazi, nao ni uongofu wa kuonesha njia ya sawa na uongofu unaomuwafikisha mtu kuweza kuifuata. Yeye (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni Mtume kwa majini na watu.

## 78- Allaah Ameikamilisha Dini kupitia Muhammad (صلى الله عليه وسلم)

*Allaah kupitia kwake Ameikamilisha Dini. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

*"Leo Nimekukamilishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni neema Yangu, na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe (ndio) Dini yenu." (al-Maaidah 05 : 03)*

Dini yake (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) ni yenye kubakia mpaka siku ya Qiyaamah. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakufa isipokuwa baada ya kubainishia Ummah wake yale yote wanayohitajia. Abu Dharr (Radhiya Allaahu ´anhu) amesema:

**"Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakuacha hata yule ndege ambaye yuwaruka kwa mbawa zake angani, isipokuwa ametutajia kitu katika elimu yake."**[48]

Kuna mshirikina mmoja amesema kumwambia Salmaan al-Faarisiy (Radhiya Allaahu ´anhu):

**"Mtume wenu amewafundisha mpaka namna ya kukidhi haja." Akasema: "Ndio. Ametukataza kuelekea Qiblah wakati tunapofanya haja kubwa au ndogo. Ametukataza vilevile kujisafisha chini ya mawe matatu, mkono wa kulia, kinyesi au mfupa."**[49]

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amebainisha Dini yote. Amefanya hivo ima kwa kauli yake, kitendo chake, kulikubali kwake jambo au kwa kujibu kwa swali. Jambo kubwa na muhimu zaidi alichobainisha (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ilikuwa ni Tawhiyd.

48 Ahmad (5/163).

49 Muslim (262).

Kila alichokiamrisha ni kheri kwa Ummah katika Aakhirah na riziki yao. Kila alichokikataza ni shari kwa Ummah katika Aakhirah na riziki yao. Baadhi ya watu wanadai kuwa kuna ufinyu na ugumu katika Dini. Hilo linatokamana na akili yao pungufu, uchache wa subira na udhaifu wa imani. Vinginevyo kanuni ya ujumla inasema kuwa Allaah Hakutufanyia uzito wowote katika Dini na kwamba Dini yote ni nyepesi na sahali. Allaah (Ta´ala) Amesema:

يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ

**"Allaah Anakutakieni mepesi na wala Hakutakieni magumu." (al-Baqarah 02 : 185)**

وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ

**"Na Hakukufanyieni ugumu wowote (ule) katika Dini." (al-Hajj 22 : 78)**

مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ

**"Allaah Hataki kukufanyieni magumu." (al-Maaidah 05 : 06)**

Himdi zote ni Zake Allaah kwa kututimizia neema Zake na kuikamilisha Dini Yake.

# 79- Dalili ya kufa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم)

*Dalili ya kufa kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni Kauli Yake (Ta´ala):*

إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُم مَّيِّتُونَ ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عِندَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ

*"Hakika wewe ni maiti (utakufa) na wao pia ni maiti. Kisha hakika nyinyi Siku ya Qiyaamah mbele ya Mola wenu mtagombana." (az-Zumar 39 : 30-31)*

*Baada ya watu kufa, watafufuliwa. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ

*"Kutoka humo (ardhini) Tumekuumbeni, na katika hiyo (ardhi) Tutakurudisheni, na kutoka humo Tutakutoeni mara nyingine." (Twaaha 20 : 55)*

وَاللَّهُ أَنبَتَكُم مِّنَ الْأَرْضِ نَبَاتًا ثُمَّ يُعِيدُكُمْ فِيهَا وَيُخْرِجُكُمْ إِخْرَاجًا

*"Na Allaah Amekuotesheni katika ardhi muotesho (kama mimea). Kisha Atakurudisheni humo (ardhini) na Atakutoeni (tena) mtoke (kuwa hai Siku ya kufufuliwa)." (Nuuh 71 : 17-18)*

**"Hakika wewe ni maiti... –** Aayah hii inathibitisha kuwa Mtume (Swalla Allahu ´alayhi wa sallam) na wale waliotumwa watakufa. Baada ya hapo wataenda kugombana kwa Mola Wake. Hapo ndipo Allaah Atahukumu kati yao kwa haki na Allaah hakuwa ni mwenye kuwapa makafiri ushindi juu ya waumini.

**Baada ya watu kufa, watafufuliwa –** Katika sentesi hii amebainisha (Rahimahu Allaah) ya kwamba watu baada ya kufa watafufuliwa. Baada ya kufa, Allaah (´Azza wa Jalla) Atawafufua ili Awafanyie hesabu. Hii ndio natija ya kutumwa Mitume, ili mtu aweze kufanyia kazi Siku hii, siku ya kufufuliwa. Hali ya Siku hiyo na khofu yake imesifiwa na Allaah (Subhaanahu

wa Ta´ala) kwa njia ya kwamba inaufanya moyo urejee kwa Allaah (´Azza wa Jalla) na kuigopa Siku hii. Allaah (Ta´ala) Amesema:

فَكَيْفَ تَتَّقُونَ إِن كَفَرْتُمْ يَوْمًا يَجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيبًا السَّمَاءُ مُنفَطِرٌ بِهِ ۚ كَانَ وَعْدُهُ مَفْعُولًا

**“Basi vipi mtaweza kujikinga, kama mkikufuru (na adhabu ya) Siku itakayowafanya watoto kuwa wenye kutoka mvi? Mbingu zitapasuka hapo, Ahadi Yake itatimizwa.” (al-Muzzammil 73 : 17-18)**

Katika maneno haya kuna ishara ya kuamini kufufuliwa na Shaykh ametumia dalili juu ya hilo kwa Aayah mbili.

**“Kutoka humo Tumekuumbeni... –** Bi maana kutokamana na ardhi hii ndio Tumewaumba pindi Aadam (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) Alivyoumbwa kutokamana na udongo.

**... na katika hiyo (ardhi) Tutakurudisheni... –** Bi maana wakati mlipozikwa baada ya kufa.

**... na kutoka humo Tutakutoeni mara nyingine... –** Bi maana kwa kufufuliwa Siku ya Qiyaamah.

**“Na Allaah Amekuotesheni katika ardhi muotesho (kama mimea)... –** Aayah hii inaafikiana na Kauli Yake (Ta´ala):

مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ

**“Kutoka humo (ardhini) Tumekuumbeni, na katika hiyo (ardhi) Tutakurudisheni, na kutoka humo Tutakutoeni mara nyingine.” (Twaaha 20 : 55)**

Aayah kwa maana kama hii ni nyingi sana. Allaah (´Azza wa Jalla) Amefanya vitu kuishi na kufa ili baada ya hapo kuwafufua ili kuthibitisha kufufuliwa. Amefanya hivi ili watu waamini hilo, imani iweze kuzidi na kufanyia kazi Siku hiyo kubwa. Tunamuomba Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) Atujaalie kuweza kuifanyia kazi Siku hiyo na kuwa ni wenye furaha kwayo.

## 80- Baada ya kufufuliwa watu watahesabiwa na kulipwa

*Baada ya kufufuliwa watahesabiwa na watalipwa kwa matendo yao. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسَاءُوا بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَى

*"Na ni vya Allaah Pekee vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ili Awalipe (adhabu ya Moto) wale waliofanya uovu kwa yale waliyoyatenda, na (ili) Awalipe wale waliofanya wema kwa al-Husnaa (Pepo)." (an-Najm 53 : 31)*

Baada ya kufufuliwa watu watalipwa na watahesabiwa kwa matendo yao. Waliofanya kheri, watalipwa kheri, na waliofanya shari, watalipwa shari. Allaah (Tabaaraka wa Ta´ala) Amesema:

فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ

**"Basi yule atakayetenda kheri (hata kama ni) uzito wa chembe ya atomu (basi) ataiona. Na yule atakayetenda shari (hata kama ni) uzito wa chembe ya atomu (basi) ataiona." (az-Zalzalah 99 : 07-08)**

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا ۖ وَإِن كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا ۗ وَكَفَىٰ بِنَا حَاسِبِينَ

**"Na Tutaweka mizani za uadilifu Siku ya Qiyaamah; basi haitodhulumiwa nafsi yoyote (ile) kitu chochote (kile). Na japokuwa ni uzito wa mbegu ya hardali, Tutaileta. Na inatosheleza Kwetu kuwa *Haasibiyn* (Wenye kuhesabu)." (al-Anbiyaa´ 21 : 47)**

مَن جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا ۖ وَمَن جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

**"Atakayekuja kwa jema basi atapata (thawabu) kumi mfano wa hilo. Na Atakayekuja kwa uovu, basi hatolipwa ila mfano wa**

**hilo, nao hawatodhulumiwa." (al-An´aam 06 : 160)**

Kitendo kimoja kulipwa mara kumi kwenda mpaka mara mia saba na zaidi ya hapo ni fadhila na neema kutoka kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Amejifadhilisha kwanza juu ya mja kwa kitendo chema, halafu baada ya hapo Amejifadhilisha mara nyingine kwa thawabu hii iliyopana na kubwa. Ama kuhusu kitendo kiovu, kinalipwa kwa mfano wake pasina adhabu kuwa kubwa. Amesema (Ta´ala):

وَمَن جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

**"Na Atakayekuja kwa uovu, basi hatolipwa ila mfano wa hilo, nao hawatodhulumiwa." (al-An´aam 06 : 160)**

Hili ni katika ukamilifu wa fadhila na wema wa Allaah.

Shaykh ametumia dalili ya hilo kwa Kauli Yake (Ta´ala):

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسَاءُوا بِمَا عَمِلُوا

**"... ili Awalipe (adhabu ya Moto) wale waliofanya uovu kwa yale waliyoyatenda."**

Hili Hakusema juu ya wale wengine:

وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَى

**"... na (ili) Awalipe wale waliofanya wema kwa *al-Husnaa* (Pepo)." (an-Najm 53 : 31)**

## 81- Yule mwenye kukanusha kufufuliwa anakufuru

*Yule mwenye kukanusha kufufuliwa anakufuru. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

زَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَن لَّن يُبْعَثُوا ۚ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۚ وَذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

*"Waliokufuru wamedai kwamba hawatofufuliwa kamwe. Sema: Bali hapana! Naapa kwa Mola wangu, bila shaka mtafufuliwa, kisha mtajulishwa kwa yale (yote) mliyoyatenda, na hayo kwa Allaah ni mepesi." (at-Taghaabuun 64 : 07)*

Yule mwenye kupinga kufufuliwa ni kafiri. Amesema (Ta´ala):

وَقَالُوا إِنْ هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وُقِفُوا عَلَىٰ رَبِّهِمْ ۚ قَالَ أَلَيْسَ هَٰذَا بِالْحَقِّ ۚ قَالُوا بَلَىٰ وَرَبِّنَا ۚ قَالَ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنتُمْ تَكْفُرُونَ

**"Na walisema: "Haya si chochote isipokuwa ni uhai wetu wa dunia tu na wala sisi hatutofufuliwa. Na lau ungeliona (Siku ya Qiyaamah) watakaposimamishwa mbele ya Mola wao. Atasema (Allaah): "Je, haya si ya kweli?" Watasema: "Ndio, tunaapa kwa Mola wetu". Atasema (Allaah): "Basi onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyakanusha." (al-An´aam 06 : 29-30)**

وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ الَّذِينَ يُكَذِّبُونَ بِيَوْمِ الدِّينِ وَمَا يُكَذِّبُ بِهِ إِلَّا كُلُّ مُعْتَدٍ أَثِيمٍ إِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِ آيَاتُنَا قَالَ أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ كَلَّا ۖ بَلْ ۜ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُوا يَكْسِبُونَ كَلَّا إِنَّهُمْ عَن رَّبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّمَحْجُوبُونَ ثُمَّ إِنَّهُمْ لَصَالُو الْجَحِيمِ ثُمَّ يُقَالُ هَٰذَا الَّذِي كُنتُم بِهِ تُكَذِّبُونَ

**"Ole siku hiyo kwa wakadhibishaji. Ambao wanaikadhibisha siku ya Malipo. Na haikadhibishi isipokuwa kila mwenye kuruka mipaka, mtendaji dhambi. Anaposomewa *Aayaat* Zetu, husema: "Simulizi za (watu) wa kale." Hapana! Bali imefanya kutu juu ya nyoyo zao yale (maovu) waliyokuwa wakiyachuma. Hapana! Hakika wao siku hiyo watawekewa kizuizi (wasimuone) Mola wao. Kisha hakika wao bila shaka wataingizwa na waungue**

**katika (Moto wa) *Al-Jahiym*. Kisha itasemwa: "Haya ndio yale mliyokuwa mkiyakadhibisha." (al-Mutwaffifiyn 83 : 10-17)**

بَلْ كَذَّبُوا بِالسَّاعَةِ ۖ وَأَعْتَدْنَا لِمَن كَذَّبَ بِالسَّاعَةِ سَعِيرًا

**"Bali wameikadhibisha Saa (Qiyaamah). Na Tumeandaa kwa anayeikadhibisha Saa, (Moto wa) *Sa'iyraa* (uwakao kwa nguvu)." (al-Furqaan 25 : 11)**

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ وَلِقَائِهِ أُولَٰئِكَ يَئِسُوا مِن رَّحْمَتِي وَأُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

**"Na wale waliozikanusha *Aayaat* za Allaah na (pia wakakanusha) kukutana Naye, hao wamekata tamaa na Rahmah Yangu, na hao watapata adhabu iumizayo." (al-´Ankabuut 29 : 23)**

Shaykh ametumia dalili hili kwa Kauli Yake (Ta´ala):

زَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَن لَّن يُبْعَثُوا ۚ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۚ وَذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Waliokufuru wamedai kwamba hawatofufuliwa kamwe. Sema: Bali hapana! Naapa kwa Mola wangu, bila shaka mtafufuliwa, kisha mtajulishwa kwa yale (yote) mliyoyatenda, na hayo kwa Allaah ni mepesi." (at-Taghaabuun 64 : 07)**

Wakanushaji hawa wanakinaishwa kwa njia ifuatayo:

**Ya kwanza:** Kufufuliwa kumepokelewa mapokezi mengi kutoka kwa Manabii na Mitume katika vile vitabu vya kiungu na Shari´ah za kimbingu. Haya yamekubaliwa na nyumati zao. Vipi basi mnaweza kukanusha hilo wakati mnapomuamini mwanafalsafa au mwananadharia fulani? Maneno haya hayakufikia mapokezi mengi kama jinsi yalivyo ya kufufuliwa na wala hayakushuhudiliwa na uhakika wa mambo.

**Ya pili:** Kufufuliwa kumethibitishwa na akili kwa njia nyingi:

**Ya kwanza:** Hakuna anayekanusha kwamba alikuwa si mwenye kuumbwa kabla ya kuumbwa. Kwa hivyo kuna uwezekano mkubwa juu ya kwamba Yule Aliyemuumba kutoka kwenye kitu chochote, Akamuumba tena. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

**“Naye Ndiye Aliyeanzisha uumbaji (wa viumbe), kisha Anaurudisha, nayo ni sahali mno Kwake.” (ar-Ruum 30 : 27)**

كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ نُّعِيدُهُ ۚ وَعْدًا عَلَيْنَا ۚ إِنَّا كُنَّا فَاعِلِينَ

**“Kama Tulivyoanza (uumbaji) umbo la awali Tutalirudisha. Ahadi juu Yetu. Hakika Sisi Tumekuwa ni Wenye kufanya (Tuyasemayo).” (al-Anbiyaa´ 21 : 104)**

**Ya pili:** Hakuna anayepinga ukubwa na uzuri wa mbingu na ardhi. Kwa hivyo kuna uwezekano mkubwa kwa Yule Aliyeviumba kadhalika Akawaumba na Kuwarudisha watu. Allaah (Ta´ala) Amesema:

لَخَلْقُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ

**“Bila shaka uumbaji wa mbingu na ardhi ni mkubwa zaidi kuliko uumbaji wa watu.” (Ghaafir 40 : 57)**

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْيَ بِخَلْقِهِنَّ بِقَادِرٍ عَلَىٰ أَن يُحْيِيَ الْمَوْتَىٰ ۚبَلَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**“Je, hawaoni kwamba Allaah Ambaye Ameumba mbingu na ardhi na wala Hakuchoka kwa kuziumba kwake, (hawaoni) kuwa ni *Qaadir* (Muweza) wa kuwafufua maiti. Bila shaka! Hakika Yeye juu ya kila kitu ni *Qadiyr* (Muweza).” (al-Ahqaaf 46 : 33)**

أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَادِرٍ عَلَىٰ أَن يَخْلُقَ مِثْلَهُم ۚ بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّاقُ الْعَلِيمُ إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَن يَقُولَ لَهُ كُن فَيَكُونُ

**“Je, Yule Aliyeumba mbingu na ardhi (mnaona) Hana uwezo wa kuumba mfano wao? Bila shaka (Anaweza)! Naye ni *Al-Khallaaqul-‘Aliym* (Mwingi wa kuumba Atakavyo - Mjuzi wa yote daima). Hakika Amri Yake Akitaka kitu chochote (kile), hukiambia: “*Kun* (Kuwa), nacho huwa.” (Yaasiyn 36 : 81-82)**

**Ya tatu:** Kila mtu mwenye busara anaiona jinsi ardhi inavokufa [kame] na mimea yake inakauka. Wakati mvua inaponyesha juu yake, inakuwa ni yenye rutuba na ikaihuisha baada ya kuwa ni yenye kufa. Yule ambaye ni Muweza wa kuihuisha ardhi baada ya kufa kwake, kadhalika ni Muweza wa kuwahuisha maiti na kuwafufua. Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنَّكَ تَرَى الْأَرْضَ خَاشِعَةً فَإِذَا أَنزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ ۚ إِنَّ الَّذِي أَحْيَاهَا لَمُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۚ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**“Na katika alama Zake, ni kwamba utaona ardhi imedhalilika (kwa kukosa maji); basi Tunapoiteremshia maji, hutaharaki na kuumuka (iote mimea). Hakika Yule Aliyeihuisha, bila shaka ni Mwenye kuhuisha maiti, hakika Yeye juu ya kila kitu ni *Qadiyr* (Muweza).” (Fuswswilat 41 : 39)**

**Ya tatu:** Allaah (Ta´ala) Ametueleza ya kwamba hisia na uhalisia wa mambo umeshuhudilia kufufuliwa pale ambapo maiti watakapofufuliwa. Allaah (Ta´ala) Ametaja jambo hili sehemu tano katika Suurat-ul-Baqarah. Moja wapo:

أَوْ كَالَّذِي مَرَّ عَلَىٰ قَرْيَةٍ وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا قَالَ أَنَّىٰ يُحْيِي هَٰذِهِ اللَّهُ بَعْدَ مَوْتِهَا ۖ فَأَمَاتَهُ اللَّهُ مِائَةَ عَامٍ ثُمَّ بَعَثَهُ ۖ قَالَ كَمْ لَبِثْتَ ۖ قَالَ لَبِثْتُ يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ۖ قَالَ بَل لَّبِثْتَ مِائَةَ عَامٍ فَانظُرْ إِلَىٰ طَعَامِكَ وَشَرَابِكَ لَمْ يَتَسَنَّهْ ۖ وَانظُرْ إِلَىٰ حِمَارِكَ وَلِنَجْعَلَكَ آيَةً لِّلنَّاسِ ۖ وَانظُرْ إِلَى الْعِظَامِ كَيْفَ نُنشِزُهَا ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْمًا ۚ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ قَالَ أَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**"Au (hukuzingatia mfano wa) kama yule aliyepita katika kijiji nacho ni kilichoporomoka kabisa juu ya mapaa yake (kuwa gofu); akasema (kwa mshangao): “Vipi Allaah Atahuisha hiki (kijiji) baada ya kufa kwake?” Basi Allaah Alimfisha miaka mia; kisha Akamfufua. Akasema: (kwa kumuuliza) “Umekaa muda gani?” Akasema: “Nimekaa siku (moja) au sehemu ya siku”. (Allaah) Akasema: “Bali umekaa miaka mia; basi kitazame chakula chako na kinywaji chako hakikuharibika. Na mtazame punda wako; na Tutakufanya (uwe) *Aayah* kwa watu. Na itazame mifupa (ya punda) jinsi Tunavyoinyanyua, kisha Tunaivisha nyama”. Basi ilipombainikia alisema: “Najua kwamba hakika Allaah juu ya kila kitu ni *Qadiyr* (Muweza).” (al-Baqarah 02 : 259)**

**Ya nne:** Hekima inakubaliana na kufufuliwa baada ya kufa ili kila mmoja apate kulipwa kwa kile alichokichuma. Ingelikuwa si hivyo, basi ingelikuwa kuumbwa kwa watu hakuna maana, kipumbavu na pasina hekima. Vilevile kungelikuwa hakuna tofauti yoyote kati ya mwanaadamu na mnyama katika uhai huu. Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ فَتَعَالَى اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ ۖ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ

**"Je, mlidhania kwamba Sisi Tulikuumbeni bila kusudio na kwamba nyinyi Kwetu hamtorejeshwa? Basi Ametukuka Allaah Mfalme wa haki. Hapana ilaaha (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ila Yeye. Mola wa Al-'Arsh tukufu." (al-Muuminuun 23 : 115-116)**

إِنَّ السَّاعَةَ آتِيَةٌ أَكَادُ أُخْفِيهَا لِتُجْزَىٰ كُلُّ نَفْسٍ بِمَا تَسْعَىٰ

**"Hakika Saa (Qiyaamah) itafika tu; nakaribia kuificha ili kila nafsi ilipwe kwa yale iliyoyafanyia juhudi." (Twaaha 20 : 15)**

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ ۙ لَا يَبْعَثُ اللَّهُ مَن يَمُوتُ ۚ بَلَىٰ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ لِيُبَيِّنَ لَهُمُ الَّذِي يَخْتَلِفُونَ فِيهِ وَلِيَعْلَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّهُمْ كَانُوا كَاذِبِينَ إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَا أَرَدْنَاهُ أَن نَّقُولَ لَهُ كُن فَيَكُونُ

**"Na wakaapa kwa Jina la Allaah nguvu ya viapo vyao kwamba: "Allaah Hatomfufua aliyekufa." Ndio! Ahadi Yake ni haki (ya kuwa Atafufua kila kiumbe); lakini watu wengi hawajui. (Atawafufua) ili Awabainishie yale ambao wamekhitilafiana kwayo na ili wajue wale waliokufuru kwamba wao walikuwa waongo. Hakika Kauli Yetu juu ya kitu (jambo) Tunapokitaka (kiwe); Tunakiambia: *"Kun"* (Kuwa) basi kinakuwa!" (an-Nahl 16 : 38-40)**

زَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَن لَّن يُبْعَثُوا ۚ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۚ وَذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Waliokufuru wamedai kwamba hawatofufuliwa kamwe. Sema: Bali hapana! Naapa kwa Mola wangu, bila shaka mtafufuliwa, kisha mtajulishwa kwa yale (yote) mliyoyatenda, na hayo kwa Allaah ni mepesi." (at-Taghaabuun 64 : 07)**

Watakapobainishiwa dalili hizi wale wenye kupinga kufufuliwa na wakaendelea kupinga, basi watakuwa ni wenye kiburi na wakaidi.

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنقَلَبٍ يَنقَلِبُونَ

**“Na hivi karibuni watakuja kujua wale waliodhulumu mgeuko (wa aina) gani watakaogeuka.” (ash-Shu´araa´ 26 : 227)**

# 82- Mitume wametumwa wakiwa ni wenye kutoa bishara njema na wenye kuonya

*Allaah Ametuma Mitume wote wakiwa ni wenye kutoa bishara njema na kuonya. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۚ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

*"Mitume ni wabashiriaji na waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya (kuletwa) ya Mitume. Na Allaah ni 'Aziyzan-Hakiymaa (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima - Mwenye hikmah wa yote daima)." (an-Nisaa 04 : 165)*

Shaykh (Rahimahu Allaah) amebainisha kuwa Allaah Amewatuma Mitume wote ili kutoa bishara njema na kuonya. Amesema (Ta´ala):

رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۚ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

**"Mitume ni wabashiriaji na waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya (kuletwa) ya Mitume. Na Allaah ni 'Aziyzan-Hakiymaa (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima - Mwenye hikmah wa yote daima)." (an-Nisaa 04 : 165)**

Wanatoa bishara ya Pepo kwa wale wenye kuwatii na wanawaonya wale wenye kwenda kinyume na wao kwa Moto.

Kuna hekima kubwa kwa kutumwa Mitume. Muhimu zaidi ni watu wasimamiwe na hoja ili wasipate kuwa na udhuru wowote kwa Allaah baada ya kutumwa Mitume. Amesema (Ta´ala):

رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۚ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

**"Mitume ni wabashiriaji na waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya (kuletwa) Mitume. Na Allaah ni *'Aziyzan-Hakiymaa* (Mwenye enzi ya**

**nguvu Asiyeshindika daima - Mwenye hikmah wa yote daima)." (an-Nisaa 04 : 165)**

Hekima nyingine ni kutimia neema za Allaah kwa waja Wake. Akili ya mwanaadamu vovyote itakavyokuwa, haiwezi katu kuzifahamu zile haki zote kwa ufafanuzi ambazo ni za Allaah (Ta´ala). Haiwezi vilevile katu kuzifahamu Sifa kamilifu za Allaah (Ta´ala) na wala haiwezi kuyafahamu Majina Yake mazuri. Kwa ajili hiyo Allaah Akawatuma Mitume (´alayhim-us-Swalaatu was-Salaam) wakiwa ni wenye kutoa bishara njema na kuonya. Akawateremshia Vitabu kwa haki, ili wapate kuhukumu kati ya watu kwa yale waliyotofautiana baina yao.

# 83- Kazi kubwa ya Mitume

*Kikubwa ambacho Mitume walilingania kwacho, kuanzia wa mwanzo wao Nuuh (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) mpaka wa mwisho wao Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), ilikuwa ni Tawhiyd. Amesema (Ta´ala):*

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

*"Na kwa yakini Tulituma katika kila ummah Mtume (awaamrishe watu wake) kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuwt (miungu ya uongo)." (an-Nahl 16 : 36)*

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ

*"Na Hatukutuma kabla yako Mtume yeyote isipokuwa Tulimpelekea Wahy ya kwamba: "Hakika hapana ilaaha (mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ila Mimi; basi Niabuduni." (al-Anbiyaa´ 21 : 25)*

*Wa mwanzo wao alikuwa ni Nuuh (´alayhis-Salaam) na wa mwisho wao alikuwa ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Dalili juu ya kwamba wa mwanzo wao alikuwa ni Nuuh (´alayhis-Salaam) ni Kauli Yake (Ta´ala):*

إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَىٰ نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِن بَعْدِهِ

*"Hakika Tumekuletea* Wahy *kama Tulivyomletea Nuwh na Manabii baada yake." (an-Nisaa 04 : 163)*

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amebainisha kuwa Mtume wa kwanza alikuwa ni Nuuh (´alayhis-Swalaatu was-Salaam). Ametumia dalili juu ya hilo kwa Kauli Yake (Ta´ala):

إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَىٰ نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِن بَعْدِهِ

**"Hakika Tumekuletea *Wahy* kama Tulivyomletea Nuwh na Manabii baada yake." (an-Nisaa 04 : 163)**

Imethibiti katika Swahiyh kwenye Hadiyth ya Uombezi:

**"Watu watamwendea Nuuh na kumwambia: "Wewe ndio Mtume wa kwanza ambaye Allaah Amekutuma katika ardhi."**[50]

Nuuh ndio Mtume wa kwanza. Kutokana na hili tunapata kujua kosa la baadhi ya wanahistoria ambao wamesema kuwa Idriys (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) alikuwa kabla ya Nuuh. Lililo la dhahiri ni kwamba Idriys alikuwa ni katika Mitume wa Banuu Israaiyl.

Mtume wa mwisho alikuwa ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Amesema (Ta´ala):

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا

**"Hakuwa Muhammad baba wa mmoja yeyote miongoni mwa wanaume wenu, lakini ni Mtume wa Allaah na ni mwisho wa Manabii. Na Allaah daima kwa kila kitu ni *'Aliymaa* (Mjuzi)." (al-Ahzaab 33 : 40)**

Hakuna Nabii mwingine baada yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mwenye kudai utume baada yake ni muongo na ni mwenye kuritadi katika Uislamu.

[50] al-Bukhaariy (7510) na Muslim (193).

## 84- Mitume wote wametumwa kwa kazi moja

*Allaah Ameutumia kila Ummah Mtume, kuanzia kwa Nuuh mpaka kwa Muhammad, ili kuwaamrisha kumuabudu Allaah Peke Yake na Akiwakataza na shirki. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

*"Na kwa yakini Tulituma katika kila ummah Mtume (awaamrishe watu wake) kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuwt (miungu ya uongo)." (an-Nahl 16 : 36)*

**Allaah Ameutumia kila Ummah Mtume –** Allaah Ameutumia kila Ummah Mtume akiwaita wamuabudu Allaah Mmoja na akiwakataza na shirki. Dalili ya hilo ni Kauli Yake Allaah (Ta´ala):

وَإِن مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ

**"Na hakuna Ummah wowote (ule) isipokuwa amepita humo mwonyaji." (Faatwir 35 : 24)**

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

**"Na kwa yakini Tulituma katika kila ummah Mtume (awaamrishe watu wake) kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuwt (miungu ya uongo)." (an-Nahl 16 : 36)**

**"Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuwt (miungu ya uongo)" –** Hii ndio maana ya "hapana mola mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah".

## 85- Maana ya Twaaghuut

*Allaah Amewafaradhishia viumbe vyote kukanusha Twaaghuut na badala yake kumuamini Allaah. Ibn Qayyim (Rahimahu Allaah) amesema:*

*"Twaaghuut ni kila chenye kuabudiwa, kinachofuatwa au kutiiwa ambacho mja anapindukia mipaka yake."*

Hapa Shaykh-ul-Islaam (Rahimahu Allaah) anataka kuonesha kuwa Tawhiyd haiwezi kutimia isipokuwa kwa kumuabudu Allaah peke Yake na kujitenga mbali na shirki. Allaah Amefaradhisha hili kwa waja Wake.

Twaaghuut asli yake linatokamana na neno "Twugyaan" na maana yake ni "kupindukia mipaka". Amesema (Ta´ala):

إِنَّا لَمَّا طَغَى الْمَاءُ حَمَلْنَاكُمْ فِي الْجَارِيَةِ

**"Maji yalipofurika, hakika Sisi Tulikubebeni katika (chombo) kinachokwenda (katika maji)." (al-Haaqqah 69 : 11)**

Bi maana wakati maji yalipozidi juu ya kipimo chake cha kawaida, Tulikubebeni katika kinachokwenda.

Kuhusiana na maana ya ki-Shari´ah, maana ya Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah) ni bora zaidi:

"Twaaghuut ni kila chenye kuabudiwa, kinachofuatwa au kutiiwa ambacho mja anapindukia mipaka yake."

Wenye kuabudiwa hawa, kufuatwa na kutiiwa hawahusiani hata hivyo na watu wema. Watu wema hawazingatiwi kuwa ni Twaaghuut wakiabudiwa, kufuatwa au kutiiwa. Masanamu yanayoabudiwa badala ya Allaah ni Twaaghuut. Kadhalika wanatheologia wanaolingania katika upotevu, kufuru, Bid´ah, kuhalalisha Aliyoharamisha Allaah na kuharamisha Aliyohalalisha Allaah. Wao pia ni Twaaghuut. Wale wanaowapendezeshea watawala ili kuacha kuhukumu kwa hukumu ya Allaah na badala yake kuchukua sheria za binaadamu ni Twaaghuut pia. Watu hawa wamepindukia mipaka yao. Mpaka wa mwanachuoni ni yeye kufuata yale aliyokuja nayo Mtume (Swalla Allaahu

´alayhi wa sallam). Kwa sababu mwanachuoni wa kihakika ni mrithi wa Mitume. Wanarithi elimu yao, matendo yao, tabia, Da´wah na kuwafundisha Ummah wao. Wakivuka mpaka huu na kuanza kuwapambia watawala kuacha kuhukumu na Shari´ah ya Kiislamu, wanazingatiwa kuwa ni Twaaghuut. Hili linatokana na kwamba wamevuka mipaka ambayo ni wajibu kwao kufuata.

Kuhusiana na kauli yake "kutiiwa", anachomaanisha ni watawala ambao wanatiiwa utiifu wa Kishari´ah au wa kidunia. Watawala wanatiiwa utiifu wa Kishari´ah pale ambapo wanaamrisha kitu kisichoenda kinyume na maamrisho ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Katika hali hii si sawa kuwachukulia kuwa ni Twaaghuut. Badala yake ni wajibu kwa rai kusikiliza na kutii. Watawala kutiiwa katika hali kama hii na kwa mpaka kama huu ina maana ya kumtii Allaah (´Azza wa Jalla). Kwa ajili hiyo inatakiwa kwetu kumuabudu Allaah (Ta´ala) na kujikurubisha Kwake pindi tunapomtii mtawala katika yale ambayo ni wajibu kumtii. Ni wajibu kwetu kufanya hivo kwa sababu Allaah (Ta´ala) Anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ

**"Enyi mlioamini! Mtiini Allaah na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi." (an-Nisaa 04 : 59)**

Ama kuhusu kuwatii watawala utiifu wa kidunia watu wawatii ikiwa wana nguvu katika utawala wao kwa sababu wana nguvu na sio kwa sababu ya imani. Mtawala anatakiwa kutiiwa kwa ajili ya imani. Aina hii ya utiifu ni yenye manufaa. Inawanufaisha watawala na inawanufaisha raia. Vilevile wanaweza kutiiwa kwa sababu raia wanakhofia nguvu za mtawala. Katika suala hili hali za raia na watawala zimegawanyika aina mbali mbali:

**Ya kwanza:** Kule kutiiwa kwa mtawala kwa sababu ya imani kunakuwa na nguvu. Hii ndio aina iliyo juu kabisa.

**Ya pili:** Kule kutiiwa kwa mtawala kwa sababu ya imani kunakuwa ni dhaifu. Hii ndio aina ya chini kabisa na aina ya khatari, sawa kwa jamii, mtawala na raia. Ikiwa mambo ya kiimani na vizuizi vya mtawala ni dhaifu, kunakuwa na ghasia katika mawazo, tabia na matendo.

**Ya tatu:** Kule kutiiwa kwa mtawala kwa sababu ya imani kunakuwa ni dhaifu na kunakuwa na nguvu kwa sababu ya utawala. Aina hii iko kati na kati. Itakuwa ni bora kwa jamii ikiwa watamtii mtawala kwa sababu ya utawala

wake. Ikiwa kinga hii pia itakuwa dhaifu, basi usiulize hali ya unyonge itayokuwa nayo jamii na matendo yake mabaya.

**Ya nne:** Kule kutiiwa kwa mtawala kwa sababu ya imani kunakuwa na nguvu na kunakuwa ni dhaifu kwa sababu ya utawala. Katika hali hii muonekano wa jamii hautoonekana mzuri kama ulivo ule wa tatu. Hata hivyo mafungamano kati ya watu na Mola Wao yanakuwa ni kamilifu na ni yenye nguvu.

## 86- Twawaaghiyt wakubwa watano

*Twawaaghiyt ni wengi. Wakubwa wao ni watano:*

*1. Ibliys, Allaah Amlaani.*

*2. Yule mwenye kuabudiwa hali ya kuwa yuko radhi kwa hilo.*

*3. Yule mwenye kuwaita watu katika kumuabudu.*

*4. Yule mwenye kudai kujua kitu katika elimu ya ghaibu.*

*5. Yule asiyehukumu kwa yale Aliyoteremsha Allaah.*

**Twawaaghiyt –** Ni wingi wa "Twaaghuut" na tafsiri yake imeshatangulia.

**Wakubwa wao ni watano –** Bi maana viongozi wao ni watano.

**Ibliys –** Ibliys ni yule Shaytwaan aliyewekwa mbali na rehema za Allaah na kulaaniwa ambaye Allaah Amesema juu yake:

وَإِنَّ عَلَيْكَ لَعْنَتِي إِلَىٰ يَوْمِ الدِّينِ

**"Na hakika laana Yangu iko juu yako mpaka Siku ya malipo." (Swaad 38 : 78)**

Hapo kabla Ibliys alikuwa pamoja na Malaika na akifanya yale wanayoyafanya. Lakini pale ambapo alipoamrishwa kumsujudia Aadam, ndipo kulipodhihirika kwake yeye uovu, kukataa na kiburi. Hivyo akawa amekataa, akawa na kiburi, na hivyo akawa ni katika makafiri. Akafukuzwa kuwekwa mbali na rehema za Allaah (´Azza wa Jalla). Allaah (Ta´ala) Amesema:

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَىٰ وَاسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ الْكَافِرِينَ

**"Na (taja) Tulipowaambia Malaika: "Msujudieni Aadam." Wakasujudu isipokuwa Ibliys alikataa na akatakabari na**

**akawa miongoni mwa makafiri." (al-Baqarah 02 : 34)**

**Yule mwenye kuabudiwa hali ya kuwa yuko radhi kwa hilo –** Bi maana akaabudiwa badala ya Allaah hali ya kuwa yuko radhi kwa hilo. Mtu kama huyu atakuwa ni katika viongozi wa Twawaaghiyt – na tunamuomba Allaah Atulinde. Sawa ikiwa mtu huyu ataabudiwa katika uhai wake au baada ya kufa kwake na akiridhia hilo.

**Yule mwenye kuwaita watu katika kumuabudu –** Yule mwenye kuwaita watu katika kumuabudu yeye hata kama hawatomuabudu. Mtu huyu ni katika viongozi wa Twawaaghiyt. Sawa ikiwa atakubaliwa au asiitikiwe [wito wake].

**Yule mwenye kudai kujua kitu katika elimu ya ghaibu –** Ghaibu ni kile kitu ambacho kimefichikamana kwa mwanaadamu. Kuna aina mbili:

**Ya kwanza:** Ya sasa. Ya sasa inatofautiana kutoka kwa mtu na kwenda kwa mwingine. Baadhi ya watu wanaijua na wengine wakawa hawaijui.

**Ya pili:** Huko mbeleni. Aina hii hakuna yeyote anayeijua isipokuwa Allaah peke Yake au Mitume ambao Amewajulisha nayo. Mwenye kudai kuijua ghaibu hii ni kafiri kwa kuwa amemkadhibisha Allaah (´Azza wa Jalla) na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

قُل لَّا يَعْلَمُ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ الْغَيْبَ إِلَّا اللَّهُ ۚ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ

**"Sema: "Hakuna (yeyote yule miongoni mwa) waliomo katika mbingu na ardhi ajuaye ghayb isipokuwa Allaah (Pekee). Na wala hawatambui (ni) lini watafufuliwa." (an-Naml 27 : 65)**

Allaah (´Azza wa Jalla) Amemuamrisha Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuwawekea wazi watu ya kwamba hakuna yeyote aliyeko mbinguni wala ardhini anayeijua ghaibu isipokuwa Allaah. Hii ina maana yule mwenye kudai kujua elimu ya ghaibu basi amemkadhibisha Allaah (´Azza wa Jalla) na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Vipi mtaweza kujua ghaibu hali ya kuwa Mtume mwenyewe (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa hajui ghaibu? Je, nyinyi ni watukufu kuliko Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)? Wakisema kuwa wao ni watukufu kuliko Mtume, wamekufuru. Na wakisema kuwa yeye ndio mtukufu, tunawauliza:

"Kwa nini yeye hakuijua ghaibu na nyinyi mkawa mnaijua?"

Allaah (´Azza wa Jalla) Amesema:

عَالِمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا لَّا مَنِ ارْتَضَىٰ مِن رَّسُولٍ فَإِنَّهُ يَسْلُكُ مِن بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ رَصَدًا

**"*'Aalimu* (Mjuzi) wa ghayb na wala Hamdhihirishii yeyote *ghayb* Yake. Isipokuwa yule Aliyemridhia miongoni mwa Mitume basi hakika Yeye Anamwekea mlinzi mbele yake na nyuma yake." (al-Jinn 72 : 26-27)**

Hii ni Aayah ya pili inayoonesha kuwa mwenye kusema kuwa anajua elimu ya ghaibu ni kafiri. Allaah (Ta´ala) Amemuamrisha Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kusema kuwaambia watu:

قُل لَّا أَقُولُ لَكُمْ عِندِي خَزَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ الْغَيْبَ وَلَا أَقُولُ لَكُمْ إِنِّي مَلَكٌ ۖ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ

**"Sema: "Sikuambieni kuwa mimi nina hazina ya Allaah wala (sikuambieni) kwamba naelewa (mambo ya) ghayb na wala sikuambieni kuwa mimi ni Malaika. Sifuati ila yale niloletewa *Wahy*." (al-An´aam 06 : 50)**

**Yule asiyehukumu kwa yale Aliyoteremsha Allaah –** Kuhukumu kwa Aliyoteremsha Allaah (Ta´ala) ni katika Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah. Kwa sababu inahusiana na kuitekeleza hukumu ya Allaah, jambo ambalo linakwenda na uola Wake na ukamilifu wa ufalme Wake na uendeshaji Wake. Kwa ajili hii Allaah (Ta´ala) Amewaita wale wenye kufuatwa katika mambo mengine yasiyokuwa yale Aliyoteremsha Allaah "miungu" ya wale wenye kuwafuata. Amesema (Ta´ala):

اتَّخَذُوا أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَٰهًا وَاحِدًا ۖ لَّا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۚ سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ

**"Wamewafanya *Ahbaar* wao (wanavyuoni wa dini) na *Ruhbaan* wao (wanavyuoni watawa) kuwa ni miungu badala ya Allaah, na (pia wamemfanya) *Al-Masiyh* mwana wa Maryam (kuwa ni mungu); na hali hawakuamrishwa isipokuwa kumwabudu *Ilaahan Waahidaa* (Mungu Mmoja Pekee). Hapana mola wa haki ila Yeye. Utakasifu ni Wake!**

**kutokana na yale yote wanayomshirkisha nayo.” (at-Tawbah 09 : 31)**

Allaah Amewaita wale wenye kufuatwa “miungu” kwa sababu wamewafanya wao ni wenye kuweka Shari´ah pamoja na Allaah (Ta´ala). Vilevile amewaita wenye kufuata “waja” kwa sababu wamewanyenyekea na kuwatii katika yale yanayoenda kinyume na hukumu ya Allaah (Subhanaahu wa Ta´ala). ´Adiyy bin Haatim alisema kumwambia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**“Hawakuwaabudu.” Akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam): “Ndio. Waliwaharamishia ya halali na kuwahalalishia ya haramu. Wakawafuata. Hivyo ndivyo walivyowaabudu.”**[51]

Utakapofahamu hilo, basi jua ya kwamba kuna Aayah zinazokataa imani ya yule asiyehukumu kwa yale Aliyoteremsha Allaah na badala yake anataka mtu mwengine asiyekuwa Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wahukumu. Vilevile kuna Aayah zinazohukumu kufuru ya mtu huyu, dhuluma na ufasiki wake.

**Kigawanyo cha kwanza:** Amesema (Ta´ala):

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَن يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ وَقَدْ أُمِرُوا أَن يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَن يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنزَلَ اللَّهُ وَإِلَى الرَّسُولِ رَأَيْتَ الْمُنَافِقِينَ يَصُدُّونَ عَنكَ صُدُودًا فَكَيْفَ إِذَا أَصَابَتْهُم مُّصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ ثُمَّ جَاءُوكَ يَحْلِفُونَ بِاللَّهِ إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا إِحْسَانًا وَتَوْفِيقًا أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يَعْلَمُ اللَّهُ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ وَعِظْهُمْ وَقُل لَّهُمْ فِي أَنفُسِهِمْ قَوْلًا بَلِيغًا وَمَا أَرْسَلْنَا مِن رَّسُولٍ إِلَّا لِيُطَاعَ بِإِذْنِ اللَّهِ ۚ وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذ ظَّلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّابًا رَّحِيمًا فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

**“Je, huoni wale ambao wanadai kwamba wao wameamini yaliyoteremshwa kwako na yale yaliyoteremshwa kabla yako; wanataka wahukumiane kwa *twaaghuwt* na hali wameamrishwa wakanushe hiyo. Na shaytwaan anataka awapoteze upotofu wa mbali. Na wanapoambiwa: “Njooni kwenye yale Aliyoyateremsha Allaah na kwa Mtume; utawaona wanafiki wanakugeuka kwa upinzani. Basi**

[51] at-Tirmidhiy (5/262).

**itakuwaje utakapowafika msiba kwa sababu ya yale iliyotanguliza mikono yao? Kisha wakakujia wakiapa: "Wa-Allaahi hatukutaka ila wema na mapatano." Hao ndio ambao Allaah Anayajua yaliyomo ndani ya nyoyo zao. Basi waachilie mbali na wape mawaidha na uwaambie maneno yatakayowaathiri na kuingia katika nafsi zao. Na Hatukutuma Mtume yeyote ila atiiwe kwa idhini ya Allaah. Na lau wao pale walipojidhulumu nafsi zao wangelikujia wakamwomba Allaah msamaha na Mtume akawaombea msamaha, basi wangelimkuta Allaah ni *Tawwaabar-Rahiymaa* (Mwingi wa kupokea tawbah – Mwenye kurehemu). Basi Naapa kwa Mola wako, hawatoamini mpaka wakufanye wewe ni hakimu (mwamuzi) katika yale wanayozozana baina yao, kisha wasione katika nyoyo zao uzito katika yale uliyohukumu na wajisalimishe kwa unyenyekevu." (an-Nisaa 04 : 60-65)**

Allaah (Ta´ala) Amewasifu watu hawa wanaodai kuwa wanaamini, hali ya kuwa ni wanafiki, kwa sifa zifuatazo:

**Ya kwanza:** Wanataka Twaaghuut ihukumu na Twaaghuut ni kila kile kinachoenda kinyume na hukumu ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kila kinachoenda kinyume na hukumu ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni kupindukia na mashambulizi kwa Yule mwenye hukumu na ambaye mambo yote yanarejea Kwake, Naye ni Allaah. Allaah (Ta´ala) Amesema:

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Tanabahi! Ni Vyake Pekee Uumbaji na Amri. Amebarikika Allaah Mola wa walimwengu." (al-A´raaf 07 : 54)**

**Ya pili:** Wanapoitwa katika yale Aliyoteremsha Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), hugeuka na kupinga kikamilifu.

**Ya tatu:** Wanapopatwa na msiba kutokana na yale yaliyochumwa na mikono yao, huapa kwamba hawakukusudia isipokuwa wema na upatanishi. Mfano wa hao ni kama wale wanaopinga leo hukumu za Kiislamu na badala yake wanahukumiana kwa kanuni. Wanadai kuwa hawakukusudia jengine isipokuwa wema na kwamba ni jambo ambalo linaendana na hali ya sasa.

Kisha Akatahadharisha (Subhanaahu) watu hawa ambao wanadai kuwa ni waumini hali ya kuwa wanasifika kwa sifa kama hizi. Yeye (Subhaanahu) Anajua yale yaliyomo kwenye nyoyo zao na yale wanayoyaficha, mambo yanayoenda kinyume na yale wanayoyasema. Akamuamrisha Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) awape mawaidha na awaambie maneno yatakayowaathiri na kuingia katika nafsi zao. Halafu Akabainisha hekima ya kutumwa Mtume, nayo ni asiye mwingine zaidi yake atayetiiwa na kufuatwa, pasina kujali ni nadharia yenye nguvu iliyoje walo nayo na ufahamu wao mpana walo nao. Akaapa (Ta´ala) kwa uola Wake juu ya Mtume Wake, jambo ambalo ni katika aina maalum ya uola na inayoashiria ukweli wa ujumbe wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ameapa kuwa imani ya mtu haisihi isipokuwa kwa kutimia sharti tatu:

**Ya kwanza:** Kurejea kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika kila ugomvi wa kitu.

**Ya pili:** Mtu akunjue kifua chake kwa hukumu yake na baada ya hapo kusipatikane pingamizi yoyote dhidi yake.

**Ya tatu:** Mtu akubali hukumu hii na ajisalimishe kwayo kikamilifu na kuitekeleza bila ya kuirudisha.

**Kigawanyo cha pili:** Amesema (Ta´ala):

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ

**“Na yeyote asiyehukumu kwa yale Aliyoyateremsha Allaah, basi hao ndio makafiri.” (al-Maaidah 05 : 44)**

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

**“Na yeyote asiyehukumu kwa yale Aliyoyateremsha Allaah, basi hao ndio madhalimu.” (al-Maaidah 05 : 45)**

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

**“Na yeyote asiyehukumu kwa yale Aliyoyateremsha Allaah, basi hao ndio mafasiki.” (al-Maaidah 05 : 47)**

Je, sifa zote hizi tatu zinamuhusu mtu mmoja? Kila asiyehukumu kwa yale Aliyoteremsha Allaah ni kafiri, dhalimu na faasiq? Hakika ya (Ta´ala) Amesema:

وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ

**"Na makafiri wao ndio madhalimu." (al-Baqarah 02 : 254)**

إِنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَمَاتُوا وَهُمْ فَاسِقُونَ

**"Hakika wao wamemkanusha Allaah na Mtume Wake na wakafa hali wao ni mafasiki." (at-Tawbah 09 : 84)**

Kila kafiri ni dhalimu na ni faasiq.

Au sifa hizi zinamuhusu kwa mujibu wa ni kwa sababu gani iliyompelekea yeye kuhukumu kinyume na Aliyoteremsha Allaah? Chaguo hili ndio ninaloonelea kuwa liko karibu na haki – na Allaah ndiye Anajua zaidi.

Yule asiyehukumu kwa yale Aliyoteremsha Allaah kwa kuwa anayadharau au kwa kuwa anaonelea hukumu zingine ni bora zaidi na zinaendana na viumbe au zinalingana nao, ni kafiri na ameritadi. Miongoni mwa watu hawa kunaingia pia wale wenye kuwatungia watu kanuni na katiba zinazoenda kinyume na Shari´ah ya Kiislamu. Wamefanya hivi ili iwe ni mfumo utakaofuatwa na watu. Hawakufanya hivyo isipokuwa ni kwa sababu wanaitakidi kuwa sheria zao ndio bora zaidi na zinazoendana na viumbe. Ni jambo linalojulikana kidharurah kwa akili na kimaumbile ya kwamba mwanaadamu haachi mfumo na kwenda katika mwingine isipokuwa ni kwa sababu anaonelea kuwa ule aliyobadilisha nao ndio bora zaidi.

Yule asiyehukumu kwa yale Aliyoteremsha Allaah, pasina kuyadharau na kuonelea kuwa hukumu zingine ni bora zaidi kuliko yenyewe au mfano wa hayo, ni dhalimu. Sio kafiri. Dhuluma zake zinatofautiana kihukumu na njia zake.

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema kuwa wale waliowafanya wanazuoni wao na wamonaki miungu badala ya Allaah wamegawanyika katika makundi mawili:

**La kwanza:** Wanajua kuwa wamebadilisha Dini ya Allaah. Pamoja na hivyo wakawafuata katika mabadilisho haya na kuonelea ya haramu kuwa halali na ya halali kuwa haramu. Wanawafuata viongozi wao pamoja na kwamba wanajua kuwa wanaenda kinyume na Dini ya Mtume. Hii ni kufuru na inachukuliwa amemshirikisha Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

**La pili:** Wanaonelea ya haramu kuwa halali na ya halali kuwa haramu – namna hii ndivyo maneno haya yalivyopokelewa kutoka kwake – lakini wakawatii katika maasi. Hili ni kama wale Waislamu ambao wanafanya maasi na huku wanaonelea kuwa ni maasi. Watu hawa na watu mfano wao wanazingatiwa kuwa ni wafanya madhambi.

Hata hivyo kuna tofauti kati ya hukumu ya kijumla na kutohukumu kwa yale Aliyoteremsha Allaah katika qadhiya fulani. Hukumu ya kijumla inaingia tu katika lile kundi la kwanza. Kwa kuwa aina ya hukumu hii inayoenda kinyume na Uislamu imetungwa kwa sababu tu ameonelea kuwa ni bora na inawafaa watu zaidi kuliko Uislamu.

Suala hili kuhusu kuhukumu kinyume na Aliyoteremsha Allaah ni katika masuala makubwa. Viongozi wengi wa leo wamepewa mtihani kwalo. Hivyo basi, mtu asiwe na haraka ya kuwahukumu kwa kitu wasichostahiki mpaka pale watakapobainishiwa haki. Suala hili ni khatari. Tunamuomba Allaah (Ta´ala) Azintengeneze hali za Waislamu, watawala wao na nchi zao.

Vilevile ni wajibu kwa wale watu ambao Allaah Amewapa elimu kuwaonesha watawala hawa haki ili wasiwe na udhuru wowote. Yule atayekufa, awe amekufa na dalili, na yule atayeishi, awe ameishi na dalili. Mtu asijidharua na kumuogopa yeyote. Hakika ya utukufu ni wa Allaah, Mtume Wake na waumini.

# 87- Ni wajibu kuhukumu kwa Aliyoteremsha Allaah

*Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):*

لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ ۖ قَد تَّبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ ۚ فَمَن يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِن بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ لَهَا ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

*"Hapana kulazimisha katika (kuingia) Dini, kwani imekwishabainika kati ya Uongofu na upotofu. Basi atakayemkanusha twaaghuwt (miungu ya uongo) na akamwamini Allaah kwa hakika atakuwa ameshikilia imara kishikilio madhubuti kisichovunjika, na Allaah ni Samiy'un-'Aliym (Mwenye kusikia yote daima - Mjuzi wa yote daima)." (al-Baqarah 02 : 256)*

*Hii ndio maana ya "hapana mola mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah".*

**Dalili –** Bi maana dalili kuwa ni wajibu kuhukumu kwa yale Aliyoteremsha Allaah na kukanusha kufuru.

**"Hapana kulazimisha katika (kuingia) Dini… –** Hairuhusiwi kumlazimsiha mtu kuamini Dini, kwa dalili na ubainifu wake kuwa wazi. Kwa ajili hii ndio maana Akasema baada yake:

قَد تَّبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ

**"Kwani imekwishabainika kati ya Uongofu na upotofu." (al-Baqarah 02 : 256)**

Ikiwa uongofu umekwishabainika kutokana na upotofu, basi hakika ya kila nafsi iliyosalama itachagua uongofu badala ya upotofu.

**"Basi atakayemkanusha twaaghuwt na akamwamini Allaah… –** Allaah (´Azza wa Jalla) Ametaja mtu kuanza kwa kukanusha shirki kabla ya kumuamini. Kwa sababu kutimia kwa mambo kunakuwa pale ambapo vizuizi vyote vinaondoshwa kabla ya kupatikana kinachothibishwa.

**“kwa hakika atakuwa ameshikilia imara kishikilio madhubuti” –** Bi maana atakuwa ameshikilia imara kishikilio madhubuti. Kishikilio madhubuti ni Uislamu.

## 88- Kichwa cha mambo ni Uislamu

*Katika Hadiyth:*

*"Kichwa cha mambo ni Uislamu, nguzo yake ni Swalah na Jihaad katika njia ya Allaah ndio nundu yake ya juu."*[52]

Mwandishi (Rahimahu Allaah) anachokusudia kwa Hadiyth hii ni kuonesha kuwa kila kitu kina kichwa cha mambo. Kichwa cha mambo alichokuja nacho Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni Uislamu.

**... nguzo yake ni Swalah –** Kwa kuwa Uislamu hausimami isipokuwa kwayo. Kwa ajili hii kauli yenye nguvu ni kwamba yule mwenye kuacha Swalah ni kafiri na hana Uislamu wowote.

**Jihaad katika njia ya Allaah ndio nundu yake ya juu –** Bi maana mambo yake ya juu na kamilifu zaidi ni Jihaad katika njia ya Allaah. Hili ni kutokana na kwamba yule mwenye kuitengeneza nafsi yake ajaribu pia kuwatengeneza wengine kupitia Jihaad katika njia ya Allaah. Hili hufanywa ili Uislamu uweze kusimamishwa na ili neno la Allaah liweze kuwa juu. Yule mwenye kupigana ili neno la Allaah liweze kuwa juu, ndio mwenye kupigana katika njia ya Allaah. Kwa hivyo ndio hufikiwa nundu hii ya juu kwa sababu ni kupitia yenyewe ndio Uislamu unakuwa juu ya dini nyinginezo.

[52] Ahmad (5/231-237), at-Tirmidhiy (5/13) na Ibn Maajah (2/1394).

# 89- Mwisho wa kitabu

*Allaah ndiye Anajua zaidi. Swalah na salaam ziwe juu ya Muhammad, familia yake na Maswahabah zake.*

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amemalizia kitabu chake kwa kurudisha elimu kwa Allaah (´Azza wa Jalla) na kumtumia swalah na salaam Mtume wake Muhammad (Swalla Allahu ´alayhi wa sallam).

Hapa ndio mwisho wa "al-Usuwl ath-Thalaathah". Tunamuomba Allaah Amlipe mwandishi kwa njia iliyokuwa nzuri kabisa, Atujaalie kuweza kupata sehemu katika ujira wake na Atukutanishe naye Peponi – hakika Yeye ndiye Mwingi wa kutoa.

Himdi zote ni Zake Allaah, Mola wa walimwengu. Swalah na salaam zimwendee Mtume wetu Muhammad.